Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

# BUNGE LA TANZANIA

# MAJADILIANO YA BUNGE

## MKUTANO WA ISHIRINI

**Kikao cha Kumi na Nne - Tarehe 23 Juni, 2010**

*(Mkutano Ulianza Saa Tatu Asubuhi)*

## D U A

*Spika (Mhe. Samuel J. Sitta Makinda) Alisoma Dua*

## HATI ZILIZOWASILISHWA MEZANI

Hati zifuatazo ziliwasilishwa Mezani na:-

**NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI:**

Hotuba ya Bajeti ya Waziri wa Maji na Umwagiliaji kwa Mwaka wa Fedha 2010/2011.

**MHE. JANET Z. MBENE (K.n.y. MWENYEKITI WA KAMATI YA KILIMO, MIFUGO NA MAJI):**

Taarifa ya Kamati ya Kilimo, Mifugo na Maji Kuhusu utekelezaji wa majukumu ya Wizara ya Maji na Umwagiliaji kwa Mwaka wa Fedha 2009/2010 pamoja na maoni ya Kamati Kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha wa 2010/2011.

**MHE. MHONGA S. RUHWANYA - MSEMAJI MKUU WA KAMBI YA UPINZANI KUHUSU WIZARA YA MAJI NA UMWAGILIAJI:**

Taarifa ya Msemaji Mkuu wa Kambi ya Upinzani Kuhusu Makadirio ya Matumizi ya Wizara ya Maji na Umwagiliaji kwa Mwaka wa Fedha 2011/2011.

**NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA MIFUGO NA UVUVI:**

Randama za Makadirio ya Matumizi ya Wizara ya Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi kwa Mwaka wa Fedha 2010/2011.

## MASWALI NA MAJIBU

Na. 96

**Njia Mbadala kwa Wakazi wa Ubungo Kibangu**

**MHE. HALIMA J. MDEE** aliuliza:-

Kwa kuwa ni muda mrefu sana umepita tangu Serikali ilipoahidi kuweka njia mbadala kwa wakazi wa mitaa ya Ubungo Kibangu na Mwongozo kufuatia njia iliyokuwa ikitumika kuzolewa maji kwa sababu ya kuwa pembezoni mwa Mto Gide.

Kwa kuwa, Kamati ya Bunge ya Hesabu za Serikali za Mitaa ilitembelea eneo hilo katika kipindi cha miaka minne iliyopita na kuahidi kuishauri Serikali kuchukua hatua za Haraka kutengeneza njia kwenye eneo husika, ushauri ambao waliutekeleza kikamilifu.

(a) Je, ni lini sasa ahadi hiyo itatekelezwa?

(b) Je, Serikali ina mpango wowote wa kukarabati eneo lililomegwa karibu na Daraja la Mto Gide, ambalo ndio kiunganishi kati ya Ubungo, Tabata na Buguruni ili kuepuka maafa kwa wakazi wa maeneo hayo na kama mpango huo upo utaanza kutekelezwa lini?

(c) Je, kulikuwa na makubaliano yoyote baina ya Serikali na wananchi wa maeneo husika juu ya kukubali nyumba zao zibomolewe walipwe fidia ili ipitishwe njia?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri Mkuu, kabla sijajibu swali la Mheshimiwa Mbunge, naomba kutoa maelezo yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali kupitia Halmashauri ya Manispaa ya Kinondoni iliahidi kuweka njia mbadala kwa wakazi wa Mitaa ya Ubungo – Kibangu na mwongozo katika Kata ya Makuburi , kufuatia njia iliyokuwa ikitumika kuzolewa na maji kwani ilikuwa pembezoni mwa Mto Gide. Njia hii ni muhimu sana kwani ni kiunganishi kati ya wakazi wa maeneo ya Ubungo, Tabata na Buguruni.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo mafupi naomba kujibu swali la Mheshimiwa Halima Mdee, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, Serikali kupitia Halmashauri ya Manispaa ya Kinondoni imeshatekeleza ahadi ya Kamati ya Bunge ya Hesabu za Serikali za Mitaa, kwa kutenga kiasi cha shilingi 96,435,571 kwa mwaka wa fedha 2009/2010 kwa ajili ya kulipa fidia wananchi tisa (9) watakaoathirika na matengenezo ya barabara hii mbadala.

(b)Mheshimiwa Spika, Serikali kupitia Halmashauri ya Manispaa ya Kinondoni imeshaanza mpango wa kukarabati eneo lililomegwa karibu na kingo za Daraja la Mto Gide, kwa kufanya tathmini ya gharama za ukarabati huo ambao utahusisha kazi za kujenga kingo za mto kwa kutumia *Gabions* kujaza kifusi na kushindilia. Kwa ujumla wake gharama hizo zimekadiriwa kufikia kiasi cha shilingi 836,458,000/=.

(c) Mheshimiwa Spika, ni kweli kulikuwepo na makubaliano ya Serikali na wananchi wa maeneo husika juu ya kuruhusu nyumba zao zibomolewe na walipwe fidia. Baadhi ya nyumba za wananchi katika eneo lililopendekezwa kupita barabara mbadala zilifanyiwa tathimini na kiasi cha shilingi 96,435,571/= zilihitajika kwa ajili ya fidia. Mpaka kufikia kipindi hiki malipo ya nyumba nne yameshafanywa ambayo yamegharimu shilingi 16,240,262/= yako tayari na wananchi (2) wameshalipwa fidia zao.

Aidha, utaratibu wa malipo ya fidia nyingine zinazofikia shilingi 80,195,307/= unaendelea kwa wananchi waliobaki ili kuwezesha kupata barabara hiyo mbadala.

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Mheshimiwa Spika, kujiaminisha anachosema Waziri wa TAMISEMI ni kweli kwa sababu zile nyumba bado zipo na kwa mujibu wa watu zoezi la fidia linaonekana kwamba haliendi vizuri. Lakini kama amesema hivyo mimi nashukuru Mungu. *(Makofi)*

Katika kipengele (b) cha swali lake amezungumzia juu ya Serikali kufanya tathimini kwa ajili ya kulikarabati ule uwigo wa Mto Gide. Sasa nina tatizo la kutaka kujua hili zoezi litaanza lini kwa sababu miaka minne iliyopita Serikali ilifanya tathimini na gharama zilikuwa milioni 250 haikutekelezeka. Sasa hivi gharama zinaonekana zime-*shoot* hadi milioni 836.

(a) Sasa ili kuepuka gharama kuendelea kuwa kubwa hili zoezi la kuanza sasa kukarabati pale kwa kutumia kiasi hiki cha fedha kilichotengwa hapa zoezi hili litaanza lini na kama kiasi kipo ama tunategemea Bajeti ya mwaka ujao?

(b) Kwa kuwa Manispaa imekuwa ijitahidi kwa kiasi kuweka kokoto lakini zoezi linakuwa siyo endelevu kwa sababu kunakuwa hakuna mifereji ambayo wakati wa mvua zinanyesha sasa inasaidia maji yapite pembezoni badala ya maji kupita katikati ya barabara matokeo yake ni kwamba barabara zinakuwa zinatengenezwa kila mwaka kwa sababu mvua zikinyesha zinaharibika. Nilitaka kujua katika Bajeti ya mwaka huu kuna

mipango yoyote ya kutengeneza mifereji katika njia hizi ili ziweze kuwa endelevu? (*Makofi*)

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Spika, ni kweli Serikali ina mpango mzuri tu wa kuhakikisha kwamba barabara hii mbadala inafanyiwa kazi. Kama tulivyosema tulianza kwanza na ushirikishwaji wa wananchi. Wananchi wenyewe kwanza wakubali kwamba wako tayari kuhamisha au kulipwa fidia nyumba zao.

Mnajua ni tatizo kubwa sana sana, usipowashirikisha wananchi siku hizi inakuwa ni tatizo wakati wa utekelezaji. Hili tumefanikiwa kwa kiasi kikubwa. Mnaona wananchi migogoro mingi inatokana na fidia.

Kwa hiyo, tulikuwa muda wote huu tuna-*negotiate* na wananchi kuhakikisha kwamba wanakubali kwamba watapisha barabara hiyo. Kwa hiyo, kilichotuchelewesha kwenye fidia kwanza ilikuwa ni kazi ngumu kuwashawishi wananchi.

Kuhusu ukarabati huu utaanza lini, mimi nasema kwamba kwa kuwa tumeshafahamu kiasi halisi cha fedha zinazohitajika sisi tutahakikisha kwamba kwa mwaka huu wa fedha tutaanza kukarabati barabara hii.

Kuhusu mifereji katika barabara hili nalijibu kwa ujumla katika barabara nyingi za Manispaa kwa kweli tatizo hilo ni kubwa kwenye Manispaa nyingi. Mara nyingi tunapoteza fedha nyingi kwa ajili ya ujenzi wa barabara.

Lakini mara nyingi inakosa mifereji , kwa hiyo, matokeo yake kila baada ya mwaka barabara hizo zinaharibika. Niziagize tu Manispaa kwamba tunapojenga barabara katika Manispaa zetu katika Majiji/Halmashauri tuhakikishe kwamba tunaweka mifereji ili ziweze kudumu kwa muda mrefu zaidi.

Kwa hiyo, nakubaliana na ushauri huo na tutauchukua na tutahakikisha kwamba tuna washauri Halmashauri kufanyakazi hiyo. (*Makofi*)

Na. 97

**Kujenga Sekondari Tarafa za Rulenge na Murusagamba**

**MHE. ELIZABETH N. BATENGA (K.n.y. MHE. PROF. FEETHAM F. BANYIKWA)** aliuliza:-

Kwa kuwa, Wilaya ya Ngara imepata Sekondari mbili za Kidato cha Tano na Sita ambazo ni Kabanga na Lukole zilizoko karibu na Makao Makuu ya Wilaya ya Ngara:-

Je, ni lini Sekondari kama hizo zitajengwa katika Tarafa za Rulenge na Murusagamba ili wananchi wa Tarafa hizo waweze kuhamasika na kupeleka watoto wao katika Shule za Sekondari za Kata? *(Makofi)*

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, naomba kujibu swalil la Mheshimiwa Prof. Feetham F. Banyikwa, Mbunge wa Ngara, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Halmashauri ya Wilaya ya Ngara, katika mwaka wa fedha 2008/2009 ilikuwa na lengo la kupanua Shule ya Sekondari ya Kabanga ili iweze kupokea wanafunzi wa Kidato cha Tano kwa mwaka 2009 kutokana na ongezeko kubwa la shule za Sekondari Wilayani hiyo.

Hadi sasa Halmashauri ya Wilaya ya Ngara ina shule za sekondari za Serikali 22, na tatu (3) ni za binafsi. Mpango huu ulilenga kuongeza nafasi za kidato cha tano kwa wanafunzi wanaomaliza kidato cha nne na kufaulu lakini wakakosa nafasi za kuendelea na masomo ya Kidato cha Tano kwa sababu ya uchache wa shule.

Mheshimiwa Spika, kwa mwaka 2009/2010 Halmashauri ya Wilaya ya Ngara imefanya upanuzi katika shule ya sekondari Muyenzi iliyoko katika Tarafa ya Rulenge ili kupokea wanafunzi wa kidato cha tano. Kwa sasa Halmashauri katika Bajeti mwaka 2010/2011 imetenga jumla shilingi 155,000,000/= kwa ajili ya ujenzi wa madarasa na hosteli kwa wanafunzi. Hadi sasa ni madarasa manne yapo hatua ya kuezekwa.

Baada ya kukamilisha ujenzi katika Tarafa ya Rulenge mpango wa Halmashauri ni kuanzisha kidato cha tano kwa kupanua shule ya sekondari Murusagamba iliyopo katika Tarafa ya Murusagamba ambapo upanuzi umepangwa kuanza rasmi mwaka 2911 ili iweze kupokea wanafunzi wa kidato cha tano.

**MHE. ELIZABETH N. BATENGA:** Mheshimiwa Spika, kwa kuwa lengo la kujenga shule za sekondari kila kata limefanikiwa sana na hata kuzidi kwamba kila kata iwe na shule ya sekondari.

(a)Je, Serikali ina mpango gani sasa wa kufanya kila tarafa iwe na shule ya Sekondari ili kupokea watoto watakaofanikiwa kushinda katika shule hizi za Sekondari za Kata?

(b) Mheshimiwa Waziri ameeleza kwamba Halmashauri ya Wilaya ya Ngara imejiandaa na imetenga fedha kwa ajili ya kupanua shule sekondari za Murusagamba ili ziweze kuchukua watoto wa kidato cha tano.

Je, Serikali Kuu ni fungu gani itakalotoa ili kuwasaidia kufanikisha lengo hili Halmashauri ya Wilaya ya Ngara? (*Makofi*)

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**: Mheshimiwa Spika, lengo la Serikali kwa sasa ni kuhakikisha kwamba kila tarafa inaanzisha kidato cha tano ili kuchukua watoto wa kidato cha tano katika Kata zote ambazo ziko kwenye tarafa husika. Kwa hiyo, huo ni mpango wa Serikali ambao tunaufanya sasa hivi na ambao tunaendelea kuufanya sasa hivi. Kwa hiyo, Tanzania nzima kila tarafa tunataka waanzishe kidato cha tano kwa ajili ya shule hizi za sekondari tulizozianzisha.

Kuhusu msaada kutoka Serikali Kuu jamani fedha hizo zote zinatafutwa na Serikali Kuu zinapelekwa kwenye Serikali za Mitaa. Kwa hiyo, katika mpango wa MMES II fedha za MMES ambazo zinatoka Serikali Kuu zitapelekwa kwenye Serikali za Mitaa na zimepangwa moja kwa moja kwenye Bajeti ya Serikali za Mitaa kuhakikisha kwamba zinajenga shule za Sekondari ikiwa pamoja na upanuzi wa miundombinu mbalimbali.

Kwa hiyo, fedha hizi mtaziona kwenye Halmashauri mbalimbali katika Bajeti yake na ufafanuzi zaidi utatolewa na Mheshimiwa Waziri wa Elimu na Mafunzo, wakati wa Bajeti yake tarehe 8 Julai, 2010.

Na. 98

**Ubovu wa Barabara ya Buzilasoga – Libanga**

**MHE. ERNEST G. MABINA** aliuliza:-

Kwa kuwa barabara ya kutoka Buzilasoga hadi Lubanga haipitiki kwa miaka mingi sasa:-

Je, ni lini Serikali itatengeneza barabara hiyo?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu naomba kujibu swali la Mheshimiwa Ernest Gakaya Mabina, Mbunge wa Geita, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, barabara ya Buzilasoga – Lubanga ina jumla ya urefu wa kilomita 7 ambazo zote ni za udongo. Barabara hii ni sehemu ya barabara ndefu ijulikanayo kama Sungusira – Misri – Lubanga – Buzilasoga yenye urefu wa jumla ya kilomita 52 ambazo kwa mwaka 2009/2010 ilitengewa kiasi cha shilingi 19,000,000/=.

Mheshimkwa ajili ya matengenezo ya kawaida na shilingi 8,000,000/= kwa ajili ya matengenezo ya sehemu korofi na hivyo jumla ya shilingi 27,000,000/= zilizotengwa kati barabara yote ya Sungusira – Misri – Lubanga – Buzilasoga. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, ingawa kiasi hiki ni kidogo lakini Halmashauri ya Wilaya ya Geita imejitahidi kuipa kipaumbele barabara ya Buzilasoga – Lubanga ambapo kilomita zote 7 za barabara hii zimetengenezwa kwa greda na kuweka changarawe kwa baadhi ya sehemu.

Halmshauri imeomba kiasi cha shilingi milioni 32,000,000/= katika mwaka wa fedha 2010/2011 ambapo sehemu ya fedha hizi itatumika kuweka karavati na moramu katika maeneo korofi.

Kwa hiyo, katika Bajeti ya mwaka huu fedha zimetengwa kwa ajili ya ukarabati wa barabara hiyo.

**MHE. ERNEST G. MABINA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kwa kunipa nafasi niulize maswali mawili ya nyongeza. Kama alivyoeleza kwamba barabara hii ni ndefu ina kilomita 52. Lakini katika maeneo yale sehemu za Kapira na Ivisagaveni pamoja na Ikoni kuna tatizo la madaraja namwomba Mheshimiwa Waziri katika Mfuko wake wa Maendeleo wa Barabara basi atoe shilingi milioni 100 ili aweze kutengenezwa maeneo yale.

Mheshimiwa Spika, la pili, barabara ni ndefu ina kilomita 52 ambayo inaunganisha mkoa wa Mwanza na Geita. Katika mchakato wa kuendeleza mkoa wa Geita anaonaje kuipandisha barabara hii iwe hadhi ya mkoa?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Spika, sisi tunafahamu sana kwamba barabara hii kiuchumi kwa kweli inasaidia sana usafirishaji wa wananchi, mazao pamoja na mifugo kutoka vijijini na kwenda Wilayani Geita.

Tunafahamu kabisa kwamba barabara hii ni kiungo muhimu kati ya Wilaya ya Sengerema na Wilaya ya Geita ambayo yeye anasema kwamba inaunganisha mikoa miwili tofauti. Kwa umuhimu huo, mimi nasema kwamba tutashauriana na Halmashauri ya Wilaya ya Geita kuhakikisha kwamba sehemu zile korofi zinawekewa *culvert* na sehemu nyingine madaraja madogo madogo sio madaraja makubwa.

Kwa hiyo, hilo tutaliangalia na suala la kupandisha hadhi linaanzia kwenye Halmashauri yenyewe linakwenda kwenye Mfuko wa Barabara wa Mkoa na baadaye linazungumziwa kwenye *RCC* linapelekwa Miundombinu. Kwa hiyo, naomba wafuate hizo taratibu ili kama barabara hii imewashinda Halmashauri iweze kupandishwa hadhi kuwa barabara ya miundombinu.

Na. 99

**Ujenzi wa Ununuzi wa Kivuko cha Kinesi - Rorya**

**MHE. PROF. PHILEMON M. SARUNGI** aliuliza:-

Tangu mwaka 2004 Serikali aliwaahidi wananchi wa Rorya pamoja na Mbunge wao kujenga kivuko cha Kinesi katika Tarafa ya Suba ili kumaliza kero hiyo ambayo ilidumu kwa muda wa miaka 30.

(a) Je, ujenzi na ununuzi wa kivuko hicho utaanza lini?

(b) Je, kivuko hicho kitaanza kutoa huduma lini?

**NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA MIUNDOMBINU** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Maendeleo ya Miundombinu, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Philemon Mikol Sarungi, Mbunge wa Rorya, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, naomba nimtaarifu Mheshimiwa Mbunge kwamba Wizara ya Miundombinu tayari imekamilisha taratibu za ununuzi wa kivuko kipya cha Kinesi chenye uwezo wa kubeba tani 85. Vifaa vya ujenzi wa kivuko hicho

vimekwishawasili mkoani Mwanza na ujenzi tayari umeanza. Taarifa hizi ni za kufurahisha sana tunampongeza sana Mheshimiwa Mbunge.

(b) Mheshimiwa Spika, ujenzi wa kivuko unatarajia kukamilika mwezi Oktoba 2010 na kivuko kitaanza kutoa huduma kati ya Kinesi na Musoma mwezi Novemba 2010.

**MHE. PROF. PHILEMON M. SARUNGI:** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya wapiga kura na wananchi wa Rorya, kwa moyo wa dhati kabisa nataka nichukue nafasi hii kuipongeza Serikali ya awamu ya 4 ya Chama cha Mapinduzi hususan Wizara inayohusika chini ya uongozi wa Waziri na Naibu Waziri kwa kutekeleza ahadi ya Serikali, ahadi za Chama cha Mapinduzi zinatekelezeka. Baada ya pongezi hizo nina maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa tatizo hilo ni kero la usafiri kwa kivuko kiliathiri sana wananchi wa Tarafa ya Suba hususan mji mdogo wa Kinesi. Je, Serikali itakubali baada ya ujenzi kukamilika kivuko hicho kiweze kuegeshwa Kinesi badala ya Musoma?

Je, Wizara itakubali kuwafikishia shukrani za dhati kabisa na pongezi kwa Rais wa Jamhuri ya Muungano Dr. Jakaya Mrisho Kikwete na kumwomba aje azindue kivuko hicho mwezi Novemba?

**NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA MIUNDOMBINU:** Mheshimiwa Spika, kwanza napenda kwa niaba ya Serikali nipokee shukrani zake na pongezi alizitoa kwa utekelezaji wa ahadi na Ilani ya Chama cha Mapinduzi na sisi tumezipokea shukrani hizo zinatupa faraja tutaendelea kutekeleza ipasavyo.

Mheshimiwa Spika, swali la kivuko hiki kiegeshwe Kinesi badala ya Musoma tunalipokea na tutaangalia katika utekelezaji ili kivuko hicho kiweze kuegeshwa Kinesi badala ya Musoma na kusema kweli tunazingatia ushauri wake kwa vile yeye amekuwa mfuatiliaji wa karibu sana wa suala hili na sisi tunadhani tukiungana naye wananchi watafarijika zaidi.

Mheshimiwa Spika, juu ya shukrani kwa Mheshimiwa Rais, ni wajibu wetu na kusema kweli tutamfikishia salam hizi Mheshimiwa Rais na kumwomba aridhie ombi hili la kwenda kukifungua kivuko hicho kama ratiba yake itaruhusu na sisi tutasisitiza sana iwe hivyo kwa sababu Mheshimiwa Mbunge amekuwa karibu sana kufuatilia shughuli za kivuko hiki na tunampongeza kwa ajili ya kufuatilia kero za wananchi wa jimbo lake.

**MHE. SAVELINA S. MWIJAGE**: Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Kwa kuwa matatizo ya Rorya ni sawa sawa na matatizo ya Bukoba Vijijini, kivuko cha

Kishogo pamoja na Kashalu. Tangu nimeingia kwenye Bunge hili huwa najaribu kuomba hilo tatizo kile kivuko wanavuka kwa kuvutwa na mkono.

Kivuko kilikuwa kinavusha magari mawili (2) sasa hivi ni gari moja tu na watu 3. Ni lini Serikali itawaonea huruma hawa watu wa Bukoba Vijijini kuwawekea kivuko cha Kenyaba ili na wenyewe wakafurahia Serikali yake hiyo ya awamu ya 4? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA MIUNDOMBINU:** Mheshimiwa Spika, jitihada za Serikali katika kushughulikia vivuko katika nchi nzima zinaendelea vizuri.

Kwa hiyo, katika suala hili alilolileta hapa Mheshimiwa Mbunge tunaomba tu tuwasiliane naye kwa sababu kusema kweli sisi hatuna ubaguzi wa aina yoyote katika kuwahudumia wananchi litawekwa kwenye mipango yetu ambayo tunaiandaa sasa hivi ili wananchi wa Bukoba nao waweze wakanufaika na vivuko hivi kwa ajili ya kuwaondolea kero ya usafiri.

Na. 100

**Mabilioni ya JK Kwa Wajasiriamali**

**MHE. MHONGA S. RUHWANYA** aliuliza:-

Katika Mkutano wa 18 wakati Serikali ikijibu swali kuhusu fedha za mkopo kwa wajasiriamali ilisema kwamba hakukuwa na fedha kutoka kwenye Bajeti ya Serikali, ila Serikali kupitia Benki Kuu *(BOT)* iliingia Mkataba na Benki za *NMB* na *CRDB* na kudhaminiwa bilioni 10.5/=.

(a) Je, iwapo wajasiriamali hao wameshindwa kurudisha fedha hizo, Serikali kupitia *BOT* italipa fedha hizo kutoka fungu gani ikiwa udhamini huo haukupitishwa na Bunge?

(b) Je, kwa nini Serikali ipange kutumia fedha za walipa kodi bila idhini ya Bunge?

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA UCHUMI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Fedha na Uchumi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Mhonga Said Ruhwanya, Mbunge Viti Maalum, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a)Mheshimiwa Spika, ni kweli Serikali kupitia Benki Kuu *(BOT)* iliingia Mkataba na Benki ya *NMB* na *CRDB* wa kudhaminiwa bilioni 10.5 kwa ajili ya kuwakopesha wajasiriamali. Mpango wa kudhamini kupitia Benki Kuu siyo mpya ni

mpango endelevu kwani Benki Kuu tayari inasimamia mifuko miwili (2) ya udhamini ambayo ni:-

(i) Mfuko wa Udhamini wa Mikopo ya Mauzo Nje ya Nchi; na

(ii) Mfuko wa Udhamini wa Mikopo ya Wajasiriamali wadogo na wa kati.

Mheshimiwa Spika, hali ya urejeshaji wa mikopo kwa wajasiriamali waliokopeshwa sio mbaya na inapotokea wajasiriamali kushindwa kurejesha mikopo yao kwa sababu mbalimbali, Serikali itatumia taratibu zilizopo za kulipa fedha hizo.

Taratibu hizo ni pamoja na kuliarifu Bunge kupitia taarifa zake mbalimbali na pili kuliomba Bunge lako Tukufu kuidhinisha fedha hizo kupitia Bajeti ya Wizara ya Fedha fungu la Madeni ya Serikali.

(b) Mheshimiwa Spika, napenda kulikumbusha Bunge lako Tukufu kuwa kupitia Sheria ya Mikopo, Misaada na Dhamana, Waziri wa Fedha na Uchumi amepewa mamlaka na Bunge lako Tukufu kutoa dhamana kwa niaba ya Serikali. Kwa maana hiyo, Waziri wa Fedha amepewa idhini na Bunge na Serikali haitatumia fedha za walipa kodi bila ya idhini ya Bunge, kwani kufanya hivyo ni kosa kwa mujibu wa sheria.

**MHE. MHONGA S. RUHWANYA:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza maswali mawili madogo ya nyongeza.

Mheshimiwa Spika, katika Mkutano wa 18 nilijibiwa swali hili hili Serikali kupitia Naibu Waziri wa Kazi aliahidi kuleta mchanganuo wa jinsi mtu mmoja mmoja na *SACCOS* katika majimbo mbalimbali walivyopata fedha hizo baada ya Wabunge wengi humu ndani kulalamika kwamba fedha hizo watu wao hawajapata. Je, anaweza kutimiza ahadi hiyo kabla ya Bunge hili kuvunjwa?

Je, ni lini sasa Ofisi ya *CAG* itakagua mabilioni hayo ukizingatia kwamba zilianza kutolewa toka mwaka 2006?

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA UCHUMI:** Mheshimiwa Spika, kwanza nataka nimwarifu ni kweli Mheshimiwa Naibu Waziri wa Kazi alitoa ahadi hiyo na wao kama ni wasimamizi kwa sababu Wizara ya Fedha ni watoaji wa dhamana wao wenzetu ni wasimamizi wa suala zima la utekelezaji. Bado nitamfikishia Mheshimiwa Waziri ahadi ile na nitamwomba aifikishe kwako ikiwezekana kabla ya Bunge hili kuvunjwa.

Mheshimiwa Spika, lakini la pili, suala la *CAG* kukagua nataka nimwarifu tu Mheshimiwa Mhonga Said Ruhwanya sasa hivi toka tumetoa hizo fedha ni kipindi kidogo na sasa hivi ni taimu muafaka wa kumwamuru *CAG* aanze kukagua matumizi ili kuweza kuona kwamba fedha hizo zimetumika kwa mujibu wa matumizi tuliyoyakusudia. Tutafanya hivyo na wakati ukifika Mheshimiwa Mhonga na yeye katika eneo lake ataona watu wa *CAG* wakikagua mahesabu ya fedha hizi. *(Makofi)*

**MHE. SHALLY J. RAYMOND:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana.

Kwa kuwa kutokurejeshwa fedha hizo ni pamoja na wajasiriamali hao kukosa elimu ya kuendesha mikopo na kwa kuwa wengi wao ni kinamama na hawana nia mbaya kabisa kutokurejesha. Je, Serikali ina mpango gani sasa kuwa na mkakati pamoja na hizo Benki nyingine zikiwemo hiyo *CRDB, NMB, EXIM* na Mabenki yote yaliyo nchini kutoa elimu kwa kinamama hao na wajasiriamali hao ili waweze kurejesha mikopo hiyo?

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA UCHUMI:** Mheshimiwa Spika, ni kweli elimu ni muhimu sana katika suala zima la ujasiriamali pamoja na urejeshaji wa mikopo. Tayari Wizara yangu imeshaziarifu Benki zote ambazo zinafanya kazi ya kutoa mikopo kwa ajili ya wajasiriamali wadogo wadogo na wa kati kuandaa Bajeti kwa ajili ya kutoa elimu na tayari baadhi ya Benki hizi zimeshaanza kutoa elimu kwa kupitia *SACCOS* na *VIKOBA* na tutaendelea kuzishawishi Benki wafanye hivyo kwa sababu kufanya hivyo ni faida kwao na kwetu sote kwa ujumla.

Na. 101

**Bajeti ya Serikali Kusomwa Aprili Hadi Juni**

**MHE. ARCHT. FUYA G. KIMBITA** aliuliza:-

Zipo kasoro za dhati za usomaji wa Bajeti ya Serikali kipindi cha Juni hadi Agosti katikati:-

Je, Serikali iko tayari kushauriana na nchi zingine wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki ili Bajeti zetu zote ziwe zinasomwa kipindi cha Aprili, hadi Juni katikati ili mwaka mpya wa Serikali yaani tarehe 1 Julai, usiwe unaingiliwa?

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA UCHUMI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Fedha na Uchumi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Fuya Godwin Kimbita, Mbunge wa Jimbo la Hai, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, usomaji wa Bajeti ya Serikali, ndani ya Bunge lako Tukufu ni hatua moja na ni ya mwisho katika mchakato mzima wa maandalizi ya Bajeti.

Bajeti mpaka kufikia hatua ya kusomwa huwa imepitia taratibu mbalimbali na baadhi ya taratibu hizo ziko kwa mujibu wa sheria na kanuni. Taratibu hizo ni kama zifuatazo:-

(i) Kuandaa mwongozo kwa kuwashirikisha wadau mbalimbali na kuutoa kwa Wizara na Taasisi mbalimbali. Shughuli hii hufanywa mnamo mwezi wa Septemba.

(ii) Wizara na Taasisi zinazojitegemea kuwasilisha HAZINA mpango na mahitaji yao ya fedha. Mpango wao ni kwa mujibu wa Ilani ya Uchaguzi

na Mwongozo uliotolewa na HAZINA. Kazi hii inatakiwa kukamilika kabla ya Desemba.

(iii) Bunge lako Tukufun hupokea Taarifa ya Mpango wa Serikali, katika Kikao cha Bunge cha mwezi wa Januari.

(iv) Wataalam wa Kodi kupitia mapendekezo mbalimbali ya kodi mnamo mwezi Machi na Kikao cha Wahisani wa Maendeleo hufanyika baada tu ya kazi hiyo.

(v) Kikao cha Makatibu Wakuu cha kupitia Bajeti na Mpango wa Maendeleo hufanyika kati ya mwezi Aprili na Mei.

(vi) Baraza la Mawaziri hupitia Bajeti na Mpango wa Maendeleo, shughuli hii hufanyika mwezi Mei.

(vii) Kamati ya Fedha na Uchumi ya Bunge kupitia Mpango na Bajeti ya Serikali pamoja na Kamati za Sekta pia hupitia Bajeti za Sekta mbalimbali kazi hii hufanyika mwezi Mei na Juni.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa Mheshimiwa Mbunge katika suala lake hajazitoa kwa kina dosari za usomaji, hata hivyo napenda kumfahamisha kuwa nchi wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki baada ya uchambuzi zimefanya maamuzi ya pamoja ya kuteua siku ya Alhamisi ya pili ya mwezi Juni, kila mwaka iwe ndiyo siku ya kusoma Bajeti kwa nchi zote za Afrika Mashariki. Licha ya uamuzi huo bado ipo nafasi ya kushauriana zaidi na nchi wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki juu ya kusoma Bajeti mwezi Aprili hadi Juni badala ya utaratibu wa sasa wa kusoma Bajeti mnamo mwezi Juni hadi Agosti. Ninachomwomba Mheshimiwa Mbunge atusaidie ni kutupatia hoja za msingi ambazo yeye anaziita dosari dhahiri za usomaji wa Bajeti ya Serikali kwa lengo na kuzifanyia kazi kabla ya kufanya mashauriano na nchi nyingine. *(Makofi)*

**MHE. ARCHT. FUYA G. KIMBITA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru. Mheshimiwa Naibu Waziri kwa maelezo yake nampongeza kwa ufafanuzi alioutoa. Lakini ninayo maswali mawili madogo ya nyongeza.

Mheshimiwa Spika, swali la kwanza je, Mheshimiwa Waziri haoni hayo matatizo zaidi tutakuja kuongea baadaye vizuri, lakini la kwanza niulize tu kwamba haoni kwamba kuna matatizo pale ambako tunasoma Bajeti wakati huu na mafungu mengine katika taasisi zetu wanapopelekewa mafungu mwisho wa mwezi wa Juni ambapo matumizi saa zingine hayawi mazuri na wakati mwingine tunapofikia katika mwaka wa Uchaguzi kwa mfano mwaka huu tulionao mambo mengine inabidi tuyaharakishe harakishe.

Mheshimiwa Spika, swali la pili, na kwa sababu ni Wizara moja hiyo hiyo inayoshughulika na mambo ya fedha hapa nchini ningeomba kumwuliza Mheshimiwa Waziri. Je, Wizara yake au Serikali kwa ujumla mpaka sasa hivi imeshachukua hatua

gani au ina mpango wa kuchukua hatua zipi katika kudhibiti matumizi ya fedha za kigeni holela hapa nchini?

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA UCHUMI:** Mheshimiwa Spika, kwanza nataka nimweleze Mheshimiwa Archt. Fuya Kimbita katika jibu langu la msingi nimesema kwamba atuchambulie haya matatizo ambayo yeye anayoyaona ya kutufanya sisi kama Serikali tuwaombe wenzetu nchi wanachama tubadilishe kipindi cha kusoma Bajeti ili tuweze kuzifanyia kazi na hatimaye tuweze kuwashawishi wenzetu.

Mheshimiwa Spika, lakini nataka niseme tu kwamba nilieleza jana matumizi yanategemeana na *action plan* ya Wizara na Taasisi yalivyo. Kama fedha zile katika *quota* za awali hazijapatikana umepata katika *quota* inayofuata ni wajibu wa Taasisi ile kutekeleza ile *activity* ambayo wameipanga. Kwa hivyo nataka nimwambie Archt. Fuya Kimbita kufanya hivyo si kosa, kosa ni kama ile *activity* haikuwepo, kwa hivyo wewe umeilazimisha ndiyo kosa.

Mheshimiwa Spika, sasa Mheshimiwa Archt. Fuya Kimbita anazungumzia kwamba huu uchaguzi katika kipindi hiki tumekuwa na matatizo kusoma Bajeti. Nataka nimwambie Mheshimiwa Kimbita kwamba nchi wanachama nao vilevile wana Uchaguzi na chaguzi zao lazima tuangalie kalenda zao sina kalenda za chaguzi za nchi wanachama. Inawezekana nchi wanachama nao ikawa wanafanya Uchaguzi mwezi huo wa Aprili – Juni anaoutaka yeye na inawezekana na wao wakawa na tatizo kama la kwetu.

Kwa hiyo, nasema kwamba atupe hizi hoja ili sisi tuzifanyie kazi tukae na wenzetu, tuweze kuona kwamba hakuna *effect* yoyote inayoweza kutokea katika nchi wanachama halafu kwa umoja wetu tuta-*block* siku ya kusoma Bajeti kama hizo hoja zitaturidhisha nchi wanachama sote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, swali lake la pili sikulisikia vizuri naomba alirudie tena.

**SPIKA:** Nadhani umeshalijibu kwenye jibu lako la kwanza. Tunaendelea na swali linalofuata linaulizwa na Mheshimiwa Siraju Juma Kaboyonga, Mbunge wa Tabora Mjini.

Na. 102

**Tatizo la Majisafi na Salama Tabora**

**MHE. SIRAJU JUMA KABOYONGA** aliuliza:-

Kwa kuwa Mji wa Tabora unakabiliwa na upungufu wa maji safi na salama kutokana na ukongwe wa vyanzo vya maji vya mabwawa ya Igombe (1958) na Kazima

(1949) na pia kushindwa kwa miradi ya Serikali ya Uswisi *(SECO)* na Tanzania kuonyesha maendeleo ya kuridhisha:-

Je, Serikali inatoa kauli gani kuhusu namna ya kukabiliana na tatizo hilo kwa haraka?

**NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Siraju Juma Kaboyonga, Mbunge wa Tabora Mjini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, vyanzo vikuu vya maji kwa ajili Manispaa ya Tabora ni mabwawa mawili ya Igombe na Kazima. Bwawa la Igombe lilijengwa na kuanza kufanya kazi mwaka 1958. Pamoja na kupungua kwa maji chanzo hiki kinakabiliwa na tatizo la ubora wa maji kwa sababu yanahitaji kutibiwa kwa kiwango kikubwa ili kufikia kiwango kinachofaa kwa matumizi ya binadamu. Bwawa la Kazima ni chanzo kingine cha maji katika Mji wa Tabora, bwawa hili nalo lilijengwa mwaka 1948, hivi sasa kina chake kimepungua sana kutokana na kuongezeka kwa tope.

Aidha kutokana na hali ya ukame iliyojitokeza mwaka 2009 kina cha maji kilipungua sana na kusababisha bwawa kutokufanya kazi kabisa kuanzia mwezi Julai, 2009 hadi Februari, 2010 na hata sasa ujazo wa maji maji haukidhi mahitaji.

Mheshimiwa Spika, mwezi Februari, 2010 mimi mwenyewe nilifuatana na Mheshimiwa Mizengo Pinda, Waziri Mkuu katika ziara yake Mkoani Tabora. Katika ziara hiyo Mheshimiwa Waziri Mkuu aliagiza Mamlaka ya Majisafi na Majitaka Tabora TUWASA kufanya makisio ya gharama zinazotakiwa kuboresha upatikanaji wa maji katika muda mfupi wakati Serikali inaendelea kutekeleza mradi wa muda mrefu wa kutatua tatizo la maji. Mwezi Aprili, 2010 Wizara yangu ilipeleka Tabora shilingi milioni 230/- kwa ajili ya ununuzi wa pampu mbili za maji ili zisaidie kusukuma maji kutoka kituo cha Igombe. Hata hivyo, bado zinahitajika pampu nyingine mbili ili kupunguza tatizo kwa kiwango kizuri. Wizara yangu inaangalia uwezekano wa kukamilisha ahadi hiyo.

Mheshimiwa Spika, katika mpango wa muda mrefu Wizara yangu inafanya mazungumzo na Serikali ya Uswiss kwa lengo la kukubaliana kutumia fedha za Serikali ya Tanzania na zile za Uswiss kupitia *SECO* kupanua chujio la maji la Igombe ambalo ni muhimu sana katika kuboresha ubora wa maji. Matarajio yangu ni kwamba tutafikia makubaliano ifikapo Julai, 2010 na kuendelea na utekelezaji. Aidha Wizara yangu inaendelea kutafuta fedha za ziada katika programu ya kuendeleza sekta ya maji ili kukamilisha mradi mzima kwa maana ya kuzalisha, kutibu na kusambaza maji mjini.

Mheshimiwa Spika, eneo jingine linaloonekana linaweza kuleta matokeo ya haraka ni uchimbaji wavisima vifupi na virefu ambavyo vinaelekea kuwa na ufanisi katika Manispaa ya Tabora. Napenda kutumia fursa hii kumpongeza sana Mheshimiwa Kaboyonga ambaye kwa jitihada zake mwenyewe tayari amewezesha visima vitano

kuchimbwa na kuwekewa pampu za mkono na hivi sasa wananchi kadhaa wanapata maji katika Manispaa hiyo. Huu ni mfano mzuri wa kuigwa na mimi nataka nimhakikishie Mheshimiwa Kaboyonga kwamba Wizara yangu itaungwa mkono jitihada zake kwa kuangalia uwezekano wa kuongeza visima vingine.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Jakaya Mirisho Kikwete Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania alipokuwa Tabora kwenye siku ya wanawake duniani mwezi Machi, 2010 aliagiza tuangalie uwezekano wa kufikisha maji ya Ziwa Victoria katika miji ya Igunga, Nzega na Tabora. Hatua iliyokwishafikiwa katika kutekeleza agizo hili ni kwamba hadidu za rejea za mtaalam mshauri atakayefanya upembuzi yakinifu wa mradi huo ziliandaliwa na kazi hiyo inatarajiwa kuanza katika mwaka 2010/2011. Nawaomba wananchi wa Tabora na Mheshimiwa Mbunge Kaboyonga kuendelea kuwa na subira kidogo wakati Serikali inaendelea kutatua tatizo lao la maji.

**MHE. SIRAJU JUMA KABOYONGA:** Mheshimiwa Spika, awali ya yote na mimi napenda nimshukuru Naibu Waziri kwa majibu mazuri sana yanayotiwa moyo. Lakini pamoja na hivyo nina maswali mawili ya nyongeza, la kwanza ni kuhusu azma ya Serikali kushirikiana na mimi katika kuchimba visima vya ziada Mjini Tabora. Napenda kwa uhakika kabisa nijue ni lini hasa Serikali itatoa pesa kuiwezesha TUWASA kuchimba visima hivi na hususan kama inawezekana kabla ya Uchaguzi Mkuu?

Swali la pili linahusu azma ya Serikali kushirikiana na *SECO* kuweza kutatua tatizo hili la maji. Hili ndiyo tatizo kubwa. Mradi mzima unahitaji Dola milioni 25, *SECO* mpaka sasa hivi wanazo Dola milioni 5. Kwa hiyo, pengo lililopo ni Dola milioni 20. Je, Serikali inaweza kuwahakikishia wana Tabora kwamba katika Bajeti hii zitatengwa Dola milioni 20 ziunganike na zile za *SECO* ili tupate milioni 25 kumaliza tatizo la maji Mjini Tabora.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI**: Mheshimiwa Spika, kwanza nimhakikishie kwamba tutatenga fedha kwa ajili ya kuunga mkono jitihada ambazo yeye mwenyewe amekwishaanzisha kwa kuchimba visima vile na kwa kuwa wakati Mheshimiwa Waziri Mkuu alipoagiza kwamba TUWASA iandae Makadirio ya gharama za pampu waliandaa Makadirio ya gharama ya pampu nne na sisi tukapeleka fedha za pampu mbili. Basi nataka nimhakikishie fedha hizi za pampu mbili zitakwenda pale.

Lakini pia tutashirikiana na wenzetu wa TUWASA na Tabora kuangalia, yawezekana kabisa fedha hizi za pampu mbili kama haziwezi kuzaa matunda ya haraka tukazitumia kuchimba visima ili wananchi waweze kupata maji haraka iwezekanavyo wakati tunatekeleza ule mradi mkubwa.

Mheshimiwa Spika, kuhusu swali la pili la Serikali kushirikiana na *SECO,* najua kabisa kwamba Serikali ya Uswiss kwa kupitia *SECO* imetenga Dola za Kimarekani takribani milioni 5.7 na sisi katika programu ya kuendeleza sekta ya maji tunazo takribani Dola za Kimarekani milioni 4. Ukitizama hapo utakuta tuna Dola milioni 9.7 sasa pale pana kazi kubwa ambayo ni ya msingi sana ya kutengeneza *treament plant* kwa ajili ya kutibu maji ambayo inahitaji Dola za Kimarekani kama milioni 6.6 au 7.

Sasa ukitizama vizuri utakuta tuna ziada ya takribani Dola za Kimarekani milioni 2.8. Nataka nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge tutafanya hivyo baada ya kukubaliana na Serikali ya Uswiss tutaangalia uwezekano sasa wa kutafuta fedha za ziada ili angalau hatua hiyo ya pili nayo iweze kutekelezeka. *(Makofi)*

Na. 103

**Sera ya Umwagiliaji na Mfumo wa Chakula Duniani**

**MHE. MOSSY SULEIMAN MUSA** aliuliza:-

Kwa kuwa hivi sasa duniani kote sera ya chakula ina umuhimu wake katika kujitosheleza na pia kuuza kile cha ziada na kwa kuwa Serikali yetu iliandaa sera ya umwagiliaji kwa makusudi ya kukidhi azma hiyo:-

Je, Serikali iko tayari kuanza mpango huo mapema katika mwaka wa Bajeti wa 2009/2010?

**NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Mossy Suleiman Musa, Mbunge wa Mfenesini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2009/2010, Serikali ilipitisha Sera ya Taifa ya Umwagiliaji mwezi Februari, 2010. Lengo la sera hiyo ni kuboresha miongozo na maelengo yaliyoanishwa katika sera ya kilimo na mifugo ya mwaka 1997.

Sera ya umwagiliaji inalenga kukidhi mahitaji ya kilimo endelevu cha umwagiliaji ikiwa ni pamoja na kutoa mwelekeo sahihi wa matumizi ya rasilimali za maji kwa umwagiliaji. Hivi sasa Wizara yangu inaandaa Mkakati wa Taifa wa kuendeleza Kilimo cha umwagiliaji na kuandaa Sheria ya umwagiliaji. Hatua hizi zinachukuliwa kwa sababu kilimo cha umwagiliaji kinahitaji nidhamu ya kipekee katika kukiendesha.

Aidha Serikali imeandaa sera ya umwagiliaji ili kuweka mazingira yatakayowavutia wakulima wadogo wa kati na wakubwa kuwekeza katika kilimo cha umwagiliaji kuchangia katika kuongeza uzalishaji wa mazao na usalama wa cha umwagiliaji, kuchangia katika kuongeza uzalishaji wa mazao na usalama wa chakula na kupunguza umaskini.

Mheshimiwa Spika, Serikali ilianza kutekeleza sera ya taifa ya Umwagiliaji baada ya kupitishwa mwezi Februari, 2010 ili kwenda sambamba na kaulimbiu ya Kilimo

Kwanza. Katika utekelezaji huo maeneo yanayaoendelea kupewa kipaumbele ni pamoja na yafuatayo:-

(i) Ukarabati wa miundombinu ya umwagiliaji iliyochakaa na kujenga miundombinu mipya.

(ii) Uvunaji wa maji kwa kukarabati na kujenga mabwana na malambo hasa katika maeneo kame.

(iii) Kuhimiza matumizi ya maji chini ya ardhi hasa kwa ajili ya mazao ya bustani, matunda na mazao ya biashara hususan pamba, zabibu chai na kahawa.

(iv) Matumizi ya teknolojia za umwagiliaji zinazolenga katika matumizi bora ya maji katika kilimo.

Mheshimiwa Spika, katika kutekeleza Sera ya Umwagiliaji na kaulimbiu ya Kilimo Kwanza, Serikali imedhamiria kuongeza Bajeti yake kwa ajili ya kugharamia Kilimo Kwanza ikiwa ni pamoja na kuongeza Bajeti ya Umwagiliaji kwa lengo la kufikia hekta milioni saba (7) ifikapo mwaka 2015. Aidha, kipaumbele katika uwekezaji kinawekwa katika Mikoa Sita yenye uwezekano mkubwa kuongeza mazao ya chakula ambayo ni Kigoma, Morogoro, Mbeya, Iringa, Rukwa na Ruvuma.

Mheshimiwa Spika, Serikali pia imedhamiria kuongeza mbinu ya umwagiliaji katika uzalishaji wa zao la pamba hasa katika Mikoa inayolima pamba zao ambalo lina mchango mkubwa katika uchumi wetu.

**MHE. MOSSY SULEIMAN MUSA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali moja la nyongeza. Pamoja na majibu mazuri kwa kuwa Serikali itatumia kiasi kikubwa cha fedha ili kukamilisha sera hii, Mheshimiwa Naibu Waziri anaweza kutueleza kwamba wana Makadirio yoyote ili sera hiyo iweze kukamilika.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI**: Mheshimiwa Spika, naomba nijibu kwa kufupi tu kwamba asubiri kidogo muda mfupi ujao Mheshimiwa Waziri atatoa hotuba yake ya Makadirio.

Na. 104

**Wanafunzi Wanaohamia Tanzania Bara**
**Kuendelea na Masomo**

**MHE. MASOLWA COSMAS MASOLWA** aliuliza:-

Kwa kuwa, Serikali kupitia Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi huwakataa wanafunzi wanaohamia Tanzania Bara wakatokea Tanzania Visiwani kuendelea na masomo hasa kwa wale ambao wazazi/walezi wao hawafanyi kazi katika taasisi za Muungano katika vile JWTZ, Polisi, Uhamiaji na *TRA* au kwa wale wanaofiwa na walezi/wazazi, hali inayosababisha wanafunzi hao kushindwa kuendelea na masomo.

Je, ni sababu zipi zinazosababisha Serikali kuwakana wanafunzi wasiendelee na masomo yao huku Tanzania Bara.

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI (MHE. MWANTUMU B. MAHIZA)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Masolwa Cosmas Masolwa, Mbunge wa Bububu, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, wanafunzi wote wanaosoma shule za Tanzania Visiwani hupatiwa nafasi za kuhamia katika shule za Tanzania Bara wakiwasilisha taarifa kamili zinazohitajika kuhusiana na maombi ya uhamisho. Taarifa zinazohitajika ni kadi ya maendeleo au taarifa za ufaulu wa mitihani kutoka shule walizokuwa wanasoma na barua kutoka kwa Katibu Mkuu Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali.

Mheshimiwa Spika, fomu za uhamisho kwa wanafunzi wa shule za msingi na sekondari kutoka Tanzania Visiwani hazionyeshi wadhifa au kazi ya mzazi. Aidha waombaji uhamisho hupeleka maombi yao kwa Katibu Mkuu Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali ambaye huleta taarifa kwa Katibu Mkuu Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi. Hivyo Kazi au wadhifa wa mzazi si kigezo cha uhamisho.

Mheshimiwa Spika, mwaka 2008 wanafunzi 162 wa shule za msingi na sekondari walihamia Tanzania Bara kutoka Tanzania Visiwani. Mwaka 2009 wanafunzi 165 walihamia Tanzania Bara. Hadi kufika mwezi Mei, 2010 jumla ya wanafunzi 78 wameshahamia Tanzania Bara kutoka Tanzania Visiwani.

**MHE. MASOLWA COSMAS MASOLWA:** Mheshimiwa Spika, kwanza niishukuru Serikali kwamba swali langu amelifanyia kazi nasema hivyo kwa sababu swali langu ni la mwaka 2007 na takwimu hapa zimeanzia mwaka 2008 kwa maana amelifanyia kazi.

Lakini nina swali moja la nyongeza. Maswali mengi ya Waheshimiwa Wabunge yanakaa muda mrefu bila kujibiwa. Hivi kuna matatizo gani hasa yanayosababisha haya maswali mpaka yanaonekana yanapita muda wake?

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI (MHE. MWANTUMU B. MAHIZA):** Mheshimiwa Spika, Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi hujibu maswali yale tu ambayo yameelekezwa kwao kutoka Ofisi ya Katibu wa Bunge.

Kwa hiyo, kuchelewa kujibiwa si kosa la Wizara ya Elimu na pengine kama lilikuwa na muhimu sana angetufuata tungeweza kumpa majibu kwa wakati muafaka.

Na. 105

**Serikali Kutembelea Vituo vya Walemavu**

**MHE. SAVELINA S. MWIJAGE** aliuliza:-

Kwa kuwa, mara kwa mara Serikali hutenga fedha na kutafuta wafadhili kwa ajili ya kusaidia watu wenye ulemavu ili nao wajione sehemu ya jamii, kwa kuwa walemavu wengi familia zao hazina uwezo mkubwa:-

Je, ni lini Serikali itakuwa na mpango wa kuvitembelea vituo na shule zenye walemavu Mkoani Kagera ili kuona matatizo yao?

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI (MHE. MWANTUMU B. MAHIZA K.n.y. WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Savelina Silvanus Mwijage, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Tanzania ni nchi inayoongozwa kwa kufuata misingi ya usawa na haki kwa wananchi wote. Kila Mwanachi ana haki sawa Kisheria kushiriki kikamilifu katika mambo muhimu yanayomhusu yeye mwenyewe na jamii nzima kwa ujumla. Watu wenye ulemavu wana haki ya kupata mahitaji ya msingi sawa sawa na wananchi wengine wasio walemavu.

Kwa kutambua umuhimu huu, Serikali inafanya kila juhudi kuhakikisha kwamba kundi hili linatambulika na kupewa kila msaada unaostahili.

Mheshimiwa Spika, Wizara yangu pamoja na Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi ina utaratibu wa kuzitembelea shule na vituo vinavyotoa huduma kwa watu wenye ulemavu, kwa lengo la kubaini na kuchukua hatua za kurekebisha kasoro ambazo zinazojitokeza katika utaratibu mzima wa utoaji wa huduma kwa wanafunzi hao.

Katika kutekeleza dhana ya kusogeza huduma mbalimbali karibu na wananchi, Serikali Kuu imekasimu madaraka na majukumu mbalimbali kwa Halmashauri ikiwa ni pamoja na masuala ya watu wenye ulemavu.

Kwa mtazamo huo vituo hivyo vinapaswa kutembelewa na viongozi wa Halmashauri Mbalimbali kwa kuwahusisha Maafisa Ustawi wa Jamii katika Halmashauri hizo.

Mheshimiwa Spika, shule za wanafunzi wenye ulemavu zilizoko Mkoani Kagera ni mbili, ambazo ni Shule ya Mugeza (Mseto), shule ya viziwi Mugeza na shule ya Tumaini. Uongozi wa Halmashauri ya Manispaa ya Bukoba uko karibu na shule hizi na unazitembelea shule hizi mara kwa mara na imekuwa ikichangia nauli za watoto wanaporejea makwao wakati wa likizo.

Mheshimiwa Spika, hadi sasa Serikali haijapokea tatizo lolote la kawaida ambalo limeshindikana kutatuliwa katika ngazi ya Halmashauri. *(Makofi)*

**MHE. SAVELINA S. MWIJAGE:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Kwa kuwa mimi mara kwa mara napenda kutembelea shule hizo na matatizo waliyonayo hawa watoto nayaona.

Kwanza wana matatizo ya matibabu, wakipata magonjwa pale mpaka wapelekwe Bukoba Mjini na wakati huo wanakuwa wana matatizo ya kukosa gari ya kuwapeleka Bukoba Mjini. Aidha, palepale kuna Zahanati na ile zahanati huwa haina madawa. Niliomba hapa mara kwa mara kwamba Serikali iwasaidie kuwasogezea zahanati iliyopo karibu na kituo kile mpaka leo sijaona utekelezaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa spika, suala la pili, kuna shule moja tu ya Mugeza Viziwi inapewa msaada na Dayosisi ya KKKT ndiyo wanaowasaidia. Ni lini Serikali itapanga bajeti ya kuweza kuwasaidi hao viziwi na hawa walemavu waweze kufaidika na Serikali yao kupitia katika shule hizo kuweza kuwasaidia waweze kuwapa magari au madawa?

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI:** Mheshimiwa Spika, naomba kumthibitishia Mheshimiwa Mwijage kwamba, vituo vyote vinavyotoa Elimu Maalumu viko chini ya Halmashauri. Kwa hiyo, naomba kutoa agizo kwa Mkrugenzi pamoja na Afisa Elimu wa Wilaya husika, waende kwenye shule hiyo, wakaitembelee wakaone dosari zilizotajwa na Mheshimiwa Mbunge na pia nimwombe

Mganga Mkuu wa Wilaya, ahakikishe anaongeza dawa katika Zahanati iliyopo karibu na shule hiyo.

Mheshimiwa Spika, naomba nimthibitishie Mheshimiwa Mbunge kwamba, Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi, ndiyo yenye dhamana ya kutoa vifaa. Kwa taarifa yako Mheshimiwa Mbunge, shule hiyo unayoizungumza, katika Mwaka wa Fedha 2009/2010, imepelekewa vifaa kadhaa vya kitaalamu. Nikivitaja vinaweza vikachukua muda lakini viko hapa nitampatia, wamekwishapelekewa vipimo kwa ajili ya kupima uwezo wa masikio, uwezo wa kusikia, mapigo ya moyo, vifaa vya kutengenezea kwa maana ya *repair kits,* wamepewa shime sikio na vifaa vingine vingi tu. Ninaomba nikuthibitishie kwamba, tunayo Bajeti Maalumu kwa ajili ya vifaa hivyo na kwa bahati mbaya sana, naomba niseme idadi ya walemavu viziwi inaongezeka na hii ni changamoto kwetu na tatizo kubwa ni ugonjwa wa malaria; tupambane na malaria tuepushe ulemavu huu kuendelea.

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri wa TAMISEMI kwa maelezo ya ziada.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (TAMISEMI):** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Afya, naomba kuongezea majibu mazuri ya Mheshimiwa Mwantumu Mahiza, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, mimi nimekwishafika katika shule hii, ninafahamu matatizo yake. Tangu shule hizi zilivyogatuliwa kwenye Halmashauri mbalimbali, sasa hivi maombi maalumu ya shule hizo tumeanza kuyashughulikia na kwenye bajeti karibu kila shule yenye matatizo ya walemavu tumepeleka fedha na tumetenga fedha hizo kwa ajili ya huduma maalumu. Kwa hiyo, hilo tumelitekeleza kwa vitendo katika bajeti yetu.

**MHE. OSCAR R. MUKASA:** Mheshimiwa Spika, ninakushukuru. Kwa kuwa suala la kuwatembelea walemavu kwenye shule hizi ni sehemu moja tu ya wajibu wetu kama jamii kwa ndugu zetu wenye ulemavu; na kwa kuwa mahitaji ya walemavu ni mtambuka kwenye Wizara zote na sekta zote: Je, Serikali inatuambia nini kuhusu kuwepo kwa mkakati ambao utahakikisha kwamba utekelezaji wa Sheria mpya ya Walemavu tuliyoipitisha hivi karibuni utahakikisha kwamba Wizara zote na Sekta zote zinawahudumia ipasavyo kwa namna ambayo inaondoa ile dhana kwamba mahitaji yao yanashugulikiwa zaidi kama Afya na Elimu?

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI:** Mheshimiwa Spika, suala la walemavu ni suala linalohusu jamii nzima kwa ujumla. Serikali yetu kwa kuzingatia hilo na kwa kutambua umuhimu na haki wanayostahili kupatiwa, imeweka mikakati na mwongozo kwa kila Wizara namna ya kutoa huduma kwa walemavu. Ninamwomba Mheshimiwa kama ana hoja mahususi atuletee tutaifanyia kazi.

**MHE. MAGDALENA H. SAKAYA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi hii niulize swali dogo la nyongeza. Kwa kuwa upatikanaji wa vyombo vya usafiri kwa walemavu wa viungo kwa sehemu kubwa limeachwa kwenye Mashirika ya

Dini, Mashirika Yasiyokuwa ya Kiserikali, Watu Binafsi na Waheshimiwa Wabunge; na kwa kuwa wapo walemavu wa viungo ambao wanaweza kujitafutia riziki na kuendesha maisha yao ikiwa tu watapatiwa vyombo vya usafiri: Je, Serikali ina utaratibu gani wa kuhakikisha kwamba wale walemavu ambao hawana usafiri ikiwemo baiskeli za kutoka sehemu moja kwenda sehemu nyingine wanapatiwa usafiri kwa kushirikiana na hivi vyombo vingine?

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI:** Mheshimiwa Spika, walemavu katika aina zote, kwa makundi yote, wanapohitaji visaidizi au vifaa ambavyo vitawawezesha kuendesha maisha yao, husaidiwa ama kwenye Wizara husika ya Afya na Maendeleo ya Jamii. Nitoe mfano kwenye Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi, tuna utaratibu wa kutoa baiskeli za miguu mitatu na pia tunawawezesha kwa vitendea kazi vingine ambavyo vinawawezesha kusogea.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, niseme Wizara na Serikali kiujumla, hutoa baiskeli hizi za miguu mitatu kwa kadiri uwezo wa pesa unavyopatikana. Ninaomba Waheshimiwa Wabunge tushirikiane, kama unae mlemavu wa aina hiyo, baiskeli hizi gharama yake ni shilingi 300,000 hadi 6,000,000 na sisi pia tunaweza kuwasaidia walemavu walioko kwenye maeneo yetu kwa sababu ni sehemu ya jamii na ni wapiga kura wetu. *(Makofi)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, ninampongeza Mheshimiwa Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi, kwa umahiri wake wa kujibu maswali. Siyo rahisi kushughulikia Wizara nyingine ambayo haimuhusu moja kwa moja, lakini Mungu anawapa watu vipaji vyao kadiri anavyokadiria. Ninamtakia mema katika Bunge la Kumi. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, maswali yamekwisha na muda wa maswali umekwisha. Kabla sijatoa matangazo, kuna hii Kanuni ya 66(3)(b) inasema; wakati wa Vikao vya Bunge, Mbunge aliyeko Bungeni atatakiwa kutulia na kukaa kwa heshima mahali pake na hatatangatanga kwenye Ukumbi wa Mkutano bila sababu. Sasa naomba mtambue kwamba, kuna watu ambao wanazo sababu na mmojawapo ni Mheshimiwa Haroun Ali Suleiman, ambaye mkimwona anatembeatembea humu ndani msidhani anatangatanga, eti anajifanya hanisikii! Basi mambo mengine mtayajua hivi punde. *(Kicheko)*

Waheshimiwa Wabunge, matangazo; kwanza ni wageni: Mheshimiwa Profesa Mark James Mwandosya, Waziri wetu wa Maji na Umwagiliaji, anao wageni wake kama ifuatavyo:-

Kwanza ni Ndugu Lucy Mwandosya, Mke wa Mheshimiwa Waziri, naomba asimame yule pale asante sana na hongera sana kwa kazi nzuri unayoifanya kuhusu watoto wanaokuwa katika mazingira magumu kule Wilaya ya Rungwe, natambua kazi yako. Wapo pia wageni wa Mheshimiwa Waziri wa Maji na Umwagiliaji Jimbo lile la Rungwe Mashariki, ambao ni Ndugu Bisile Jackob; sijui yuko wapi ninaomba asimame; Bwana na Bibi Mwambungu; Bwana na Bibi Mwaipopo; Mama Manase; Bwana na Bibi Mwakibibi; na Mzee Odira Ongara wa hapa Dodoma; karibuni sana.

Waheshimiwa Wabunge, pamoja na hao wapo wageni 26 wa Wizara ya Maji kama ifuatavyo: Mhandisi Christopher Sai, ambaye ni Katibu Mkuu wa Wizara ya Maji na Umwagiliaji; karibu sana Ndugu Sai, tunakupongeza sana kwa kazi kubwa unayoifanya katika Wizara hiyo; umekulia humo humo na sasa unaiongoza. Tunakutakia mema, usisahau tu kuuimarisha ule Mradi wa Maji pale Urambo Mjini. *(Kicheko)*

Waheshimiwa Wabunge, wapo wageni 26 ambao ni Wakurugenzi, Mamlaka za Maji Mijini na Miradi ya Kitaifa. Wale wageni wetu 26 ambao ni Wakurugezi wa Maji; wale pale upande wa kushoto karibuni sana mna jukumu kubwa sana kwa nchi, kwa sababu maji ni moja ya shida tulizonazo kubwa sana.

Wapo Maafisa 9 wa Maji ya Mabonde; wale pale karibuni sana. Wapo Wakurugenzi 7 wa Kanda za Umwagiliaji, wako mkono wa kulia karibuni sana. Wajumbe 7 wa Bodi ya Maji Dodoma (DUWASA); karibuni sana. Kwa ujumla, ninadhani kwenye *Basement* wako Watumishi 105 kutoka Wizara ya Maji na Umwagiliaji, ninafikiri Mheshimiwa Waziri ameamua wote wasikie michango ya Wabunge katika suala hili zito sana la maji; tunashukuru sana kwa utaratibu huo.

Wapo wageni wa Naibu Waziri, Mheshimiwa Christopher Chiza kama ifuatavyo: Ndugu Germanico Ntezidio kutoka kule Buyungu na Ndugu Milton Mbahere naye kutoka Buyungu; karibuni sana. Kuna Ndugu Yusuph Mwahu kutoka Bonite Bottlers Moshi; karibu sana. Mwalimu Joseph Kamau Gakinya kutoka Kenya; karibu sana ndugu yetu kutoka Kenya; tunafurahi sana kuwepo hapa jisikie uko nyumbani kwa sababu sote tuko katika Jumuiya ya Afrika ya Mashariki. Yupo pia Mchungaji Amos Masadu wa Kanisa la Anglikana Dodoma; karibu sana.

Wageni wa Mheshimiwa Savelina Mwijage ni wanae; ndugu Ashira Rutu na NduguAmiri Mustapha.

Waheshimiwa Wabunge, kuna wageni wa Mheshimiwa Al-Shymaa John Kwegyir, ambao ni Sheikh Abdulmalik Khofu ni shemeji yake kutoka *Dauhil Development Network;* karibu sana Sheikh, tunafurahi kukuona. Pia yupo Ndugu Mbambile Kisanjo, Mwenyekiti wa Kijiji cha Chamakweza.

Ninafurahi kuwatambulisha kwenu wanafuzi 41 na walimu 5 kutoka shule ya *Ignatius Prep and Primary School;* wanafunzi na walimu tafadhali simameni, asanteni sana. Mmependeza sana *sister* pamoja na vijana, tunawaombea Mungu na tunawatakia mema muweze kuja kuwa raia wenye tija na maadili mema katika nchi yetu na tunawatakia safari njema.

Waheshimiwa Wabunge, wapo wageni wangu kama ifuatavyo: Kwanza ni Ndugu Mark Minja, Meneja wa Mauzo wa VODACOM Kanda ya Kati; yule pale ahsante sana. Kuna Louise Maro, Msimamizi wa Mradi wa VODACOM na Wabunge leo tutakuwa na mazungumzo na Watu wa VODACOM, ambayo yatakuwa na manufaa kwa Wabunge wote, kwa hiyo, hawa ni wageni wangu kwa sababu hiyo.

Wapo wageni wangu wengine kutoka Tabora ambao ni Wanachama wa *Tabora Press Club;* naomba wasimame pale walipo wale pale, karibuni sana Ndugu Robert Kakwesi, Juma Kapipi, Salma Abdul, Paul Christian, Thomas Mlugwa, Chuma Shomari, Vivian Pyuza, Simon Kabendera, Nicholas Kagusa, Iddi Juma Ndudu na Lucas Ndanga na baadae mchana tutapata nafasi ya kuongea.

Waheshimiwa Wabunge, mwisho lakini siyo kwa umuhimu ni wageni wangu wengine, ambao walikuwa wanaelekea Dar es Salaam kwa ajili ya shughuli maalumu. Hao ni wanakwaya 37 wa Kanisa la Anglikana la Mtakatifu Martin Urambo, wakiongozwa na Reverent Zefania Magaba, mlezi. Naomba mlezi asimame Mchungaji Zefania huyo, Mwenyekiti wa kwaya Ndugu Richard Chihamba yule pale. Sasa naomba wanakwaya wote wa Saint Martin Urambo muweze kusimama; ahsante ninawashukuru sana kwa kuja na kukubali kusitisha safari yenu kidogo tuweze kusalimiana wakati mkielekea Dar es Salaam kwenda kurekodi nyimbo. Ninatazamia mafanikio na ninyi ni nguvu yangu, ninawashangaa tu hawa vijana wanaofanya fujo huko Urambo Mashariki, lakini nadhani hata ninyi mnashangaa. Katiba imeruhusu, kwa hiyo, acha waendelee tu lakini majibu mtawapa na yatakuwa mazuri; ahsante sana na mbarikiwe sana.

Waheshimiwa Wabunge, Mheshimiwa William Shellukindo, Mwenyekiti wa Kamati ya Nishati na Madini, ameomba niwatangazie kwamba, saa saba mchana leo katika Ukumbi wa *Basement* kutakuwa na Kikao cha Kamati ya Nishati na Madini; ni muhimu sana mnaombwa Wajumbe wote muweze kuhudhuria.

Waheshimiwa Wabunge, leo Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano, anatoa Nishani kwa baadhi ya Watumishi ambao wamechomoza kwa kufanya mambo mazuri sana kwa nchi yetu. Hafla hiyo itakuwa saa kumi, sasa kidogo inaleta shida kwa sababu saa kumi na moja tunaingia Bungeni, lakini kuna hafla ya kupewa nishani, halafu baadae tumealikwa Wabunge wote kwa chakula cha jioni saa kumi na mbili na nusu. Sasa yote kidogo ni magumu, nitawaachieni wenyewe mtazame labda Wenyeviti wa Kamati wanaweza kutengeneza utaratibu ili Bungeni baadhi yetu tuwemo na kwa kuwa hafla hizo ni mbili na zinaendelea, ninadhani hasa ile ya jioni kama hamtakuwa na ubishi sana katika Wizara ya Maji tunaweza tukajikuta tunawahi hafla ya Mheshimiwa Rais.

Waheshimiwa Wabunge, tukitoka kama saa moja, moja na robo, siyo mbaya sana, nitawaarifu Ikulu kuwa Waheshimiwa Wabunge wanakuja saa hizo; lakini sasa mkitaka kuwa eeh! Sasa hiyo itakuwa shida tena lakini matangazo ni hayo, saa kumi ni kutunukiwa Nishani ambayo nadhani tunaweza kabisa tukawepo na baada ya dakika 45 tukatoka tukawahi Bunge, halafu saa kumi na mbili na nusu baadhi yetu ambao tutaweza basi tuweze kufika Ikulu Ndogo Dodoma kwa ajili ya viburudisho na chakula kama hitimisho ya hiyo shughuli ya mchana.

Baada ya hapo, ninakabiliwa na majukumu mengine kwa hiyo, ninamwomba Mheshimiwa Job Ndugai, Mwenyekiti, aje kuendeleza shughuli zilizosalia.

*Hapa Mwenyekiti (Mhe. Job Y. Ndugai) Alikalia Kiti*

## HOJA ZA SERIKALI

### Makadirio ya Matumizi ya Serikali kwa Mwaka 2010/2011 - Wizara ya Maji na Umwagiliaji

**WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kupokea Taarifa ya Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Kilimo, Mifugo na Maji iliyowasilishwa leo hapa Bungeni, naomba kutoa hoja kwamba, Bunge lako Tukufu sasa likubali kujadili na kupitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Maji na Umwagiliaji kwa mwaka 2010/2011.

Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote, napenda kutumia fursa hii kuishukuru Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Kilimo, Mifugo na Maji, chini ya Mwenyekiti wake, Mheshimiwa Gideon Asimulike Cheyo, Mbunge wa Ileje, kwa ushirikiano inaoendelea kutoa kwa Wizara yangu. Nachukua nafasi hii pia, kuishukuru Kamati hiyo kwa ushauri, maoni na maelekezo waliyoyatoa wakati nilipowasilisha taarifa ya kazi zilizotekelezwa mwaka 2009/2010 na Mpango na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Fedha ya Wizara yangu kwa mwaka 2010/2011. Maoni na mapendekezo hayo, yameboresha kwa kiwango kikubwa maandalizi ya Mpango na Bajeti ya Wizara yangu kwa mwaka 2010/2011.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara yangu ilipokea kwa masikitiko makubwa, taarifa ya kifo cha Mheshimiwa Mzee Rashid Mfaume Kawawa, aliyekuwa Waziri Mkuu Mstaafu, Makamu wa Rais Mstaafu, Mbunge wa miaka mingi na mmoja wa Waasisi wa Taifa letu. Mheshimiwa Kawawa, aliwahi kuwa Katibu Mkuu na Makamu Mwenyekiti wa TANU na CCM. Mheshimiwa Kawawa hata baada ya kustaafu aliendelea kuwa mhimili mkubwa wa Taifa letu na tegemeo kubwa la uongozi na wananchi wa Tanzania. Nampa pole Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Vita Rashid Kawawa, Mbunge wa Namtumbo, familia yake, ndugu, jamaa, marafiki na wananchi kwa ujumla. Vilevile, tulipokea kwa masikitiko taarifa za kifo cha Mbunge mwenzetu, Mheshimiwa Sigfrid Selemani Ng’itu, aliyekuwa Mbunge wa Jimbo la Ruangwa. Tunawapa pole Wananchi wa Jimbo hilo, familia yake, ndugu, jamaa na marafiki. Tunamwomba Mwenyezi Mungu, aziweke roho za marehemu mahali pema peponi. Amin.

Mheshimiwa Mwenyekiti, natumia fursa hii kuwapongeza kwa dhati kabisa Wabunge wapya waliojiunga na Bunge lako Tukufu katika kipindi cha mwaka 2009/2010. Wabunge hao ni Mheshimiwa Jaji Frederick Mwita Werema, aliyeteuliwa kuwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali na hivyo kuwa Mbunge kwa wadhifa wake, Mheshimiwa Janet Zebedayo Mbene (CCM) na Mheshimiwa Ismail Jussa Ladhu (CUF), ambao ni Wabunge wa Kuteuliwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitumie fursa hii kumpongeza Mhandisi Christopher Nestory Sayi, kwa kuteuliwa na Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kuwa Katibu Mkuu wa Wizara ya Maji na Umwagiliaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kwa namna ya pekee, kumpongeza Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa kuwa mwenyeji wa Mkutano wa kiuchumi Duniani (*World Economic Forum*), uliofanyika kwa mafanikio makubwa kuanzia tarehe 5 hadi 7 Mei 2010, Jijini Dar es Salaam. Pamoja na masuala mengine, Mkutano huo ulichambua kwa kina changamoto za kijamii, kiuchumi na kimazingira zinazolikabili Bara la Afrika na kuainisha mikakati mbalimbali inayopaswa kutekelezwa ili kukabiliana na changamoto hizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nawashukuru na kuwapongeza Mheshimiwa Mizengo Kayanza Peter Pinda, Waziri Mkuu na Mheshimiwa Mustafa Haidi Mkulo, Waziri wa Fedha na Uchumi, kwa hotuba zao ambazo zimetoa dira na mwelekeo wa bajeti, uchumi na utekelezaji wa kazi za Serikali kwa mwaka 2010/2011. Nawapongeza pia, Waheshimiwa Mawaziri wengine wote walionitangulia kuwasilisha hoja zao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sekta ya Maji: Serikali ya Awamu ya Nne imedhamiria kupunguza umaskini kama ilivyoainishwa katika Dira ya Taifa ya Maendeleo 2025, Mkakati wa Taifa wa Kuondoa Umaskini na Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi (CCM) ya Mwaka 2005. Katika Sekta ya Maji, Ilani inaelekeza Serikali kuendeleza utoaji wa huduma ya maji kwa lengo la kuboresha maisha ya wananchi na kuwapunguzia umaskini. Maelekezo ya Ilani yanalenga utekelezaji wa maeneo makuu yafuatayo:-

(i) Kuwawezesha wananchi mijini na vijijini kupata maji safi, salama na ya kutosha kwa matumizi yao ya kawaida karibu na sehemu wanazoishi na kwa mahitaji ya kiuchumi. Lengo ni kuwafikishia huduma hiyo asilimia 90 ya wakazi wa mijini na asilimia 65 ya wakazi wa vijijini ifikapo mwaka 2010

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali, katika kipindi cha mwaka 2005 hadi 2010 imeendelea kuboresha huduma za maji vijijini kwa kujenga miradi mipya, kukarabati miradi iliyopo, kuchimba visima virefu na vifupi na kufufua vilivyopo na kushirikisha wananchi katika hatua mbalimbali ikiwa ni pamoja na kupanga, kujenga na kuendesha miradi ya maji. Kutokana na utekelezaji huo, idadi ya wananchi vijijini wanaopata huduma ya majisafi na salama imeongezeka kutoka asilimia 53.7 mwaka 2005 hadi asilimia 58.7 mwaka 2009. Kwa upande wa mijini, Serikali iliendelea kuboresha huduma za maji mijini kwa kujenga na kukarabati mifumo ya maji katika Miji Mikuu ya Mikoa 19 ambapo kiwango cha upatikanaji wa maji kwa wakazi wa miji hiyo kimeongezeka kutoka asilimia 78 mwaka 2005 hadi asilimia 84 mwaka 2009. Katika Jiji la Dar es Salaam na Miji ya Kibaha na Bagamoyo inayohudumiwa na DAWASA, kiwango cha utoaji wa huduma ya majisafi kimebaki kuwa kati ya asilimia 50 na asilimia 60.

(ii) Kuhimiza utekelezaji wa ujenzi wa malambo na mabwawa mapya, ukarabati na kufufua malambo ya zamani ili maji mengi zaidi yaweze kupatikana kwa ajili ya matumizi ya wananchi na mifugo

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kipindi cha mwaka 2005 hadi 2010, Serikali ilipanga kujenga na kukarabati mabwawa 26 ya ukubwa wa kati. Hadi kufikia mwezi Juni 2010, Wizara yangu imekamilisha ujenzi na ukarabati wa mabwawa 15 ya Ugunga

(Urambo), Kinyambwiga (Bunda), Moita, Mti Mmoja na Ingamuriak (Monduli), Emboret (Simanjiro), Amasatwa (Kiteto), Katoro (Geita), New Sola (Maswa), Bulenya (Igunga), Masuguru (Bagamoyo), Mugumu (Serengeti), Ingodin (Longido), Nyambele (Bunda), na Nyashitanda (Misungwi).

Ujenzi wa mabwawa ya Kawa (Nkasi), Sasajila (Chamwino), Matwiga (Chunya), Nyambori (Rorya), Wegero (Musoma), Habiya (Bariadi), Iguluba (Iringa), na Seke Ididi (Kishapu) unaendelea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali pia, iliendelea kuimarisha Wakala wa Uchimbaji Visima na Ujenzi wa Mabwawa kwa lengo la kuuwezesha kutoa huduma kwa wateja kwa gharama nafuu. Kazi zilizotekelezwa ni pamoja na kukarabati mitambo chakavu, kununua mitambo mipya minne ya kujenga mabwawa na kununua vifaa vipya vya kisasa vya kutafiti maji chini ya ardhi. Wakala ulichunguza kwa kina maeneo 318 yanayofaa kujengwa mabwawa nchini. Kati ya maeneo yaliyochunguzwa, mabwawa 21 ya ukubwa wa kati yanaendelea kusanifiwa na kujengwa na Wakala na kwa kutumia makampuni binafsi. Mabwawa makubwa mawili ya Manchira (Serengeti) na Kinyambwiga (Bunda) yalijengwa na mabwawa mawili ya ukubwa wa kati ya Sola na Lalago (Maswa) yalikarabatiwa.

(iii) Kushirikisha kwa ukamilifu nguvu za wananchi katika hatua zake zote za kutoa huduma ya maji ikiwa ni pamoja na kupanga, kujenga, kuendesha na kumiliki miradi yenyewe kwa njia ya kueneza kamati za maji za vijiji sambamba na kuimarisha mifuko ya maji ambayo imeanzishwa na wananchi

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sera ya Maji inasisitiza ushirikishwaji wa wananchi katika kupanga na kutekeleza miradi ya maji nchini. Katika kipindi cha mwaka 2005 hadi 2009, Serikali iliendelea kuhamasisha wananchi kushiriki kikamilifu katika kupanga, kujenga na kuendesha miradi ya maji katika maeneo yao, ikiwa ni pamoja na kuunda na kuimarisha vyombo vya watumiaji maji. Lengo la kuunda na kuimarisha vyombo hivyo ni kuhakikisha kuwa huduma ya maji inakuwa endelevu. Uhamasishaji huo umeleta mafanikio na mwamko wa wananchi kumiliki na kugharamia uendeshaji wa miradi ya maji vijijini kama ifuatavyo:-

(a) Kamati za maji zimeongezeka kutoka 10,701 mwaka 2005/2006 na kufikia 12,820 mwezi Desemba 2009;

(b) Fedha zilizo kwenye akaunti za mifuko ya maji zimeongezeka kutoka shilingi bilioni 1.386 mwaka 2005/2006 hadi shilingi bilioni 1.8 mwezi Desemba 2009;

(c) Bodi za mamlaka za maji ngazi ya wilaya zimeongezeka kutoka 67 mwaka 2005/2006 na kufikia 86 mwaka 2008/2009;

(d) Vyombo vya watumiaji maji vilivyoanzishwa kisheria vimeongezeka kutoka 121 mwaka 2005/2006 hadi kufikia 338 mwezi Desemba 2009;

(e) Vikundi vya watumiaji maji ngazi ya vijiji vimeongezeka kutoka 7,239 mwaka 2005/2006 hadi kufikia vikundi 11,662 mwaka 2008/2009.

(iv) Kukamilisha miradi mikubwa ya maji ambayo ni pamoja na Mradi wa Maji toka Ziwa Victoria kwenda Wilaya za Shinyanga Mjini, Kahama, Nzega na Igunga. Mradi wa Maji wa Chalinze katika Mkoa wa Pwani ambao umeenezwa katika vijiji vingine 14 vya Mkoa huo pamoja na Mradi Kabambe wa Kufufua Mifumo ya Maji Safi na Maji Taka katika Jiji la Dar es Salaam

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mradi wa Maji wa Kahama na Shinyanga; kama nilivyolieleza Bunge lako Tukufu mwaka jana, Serikali katika kipindi cha mwaka 2005 hadi 2009, ilikamilisha kazi za ujenzi wa mradi mkubwa wa kutoa maji kutoka Ziwa Victoria hadi Miji ya Kahama na Shinyanga kwa gharama ya shilingi bilioni 252. Mradi huo ulizinduliwa rasmi tarehe 30 Mei, 2009 na Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Mradi umesanifiwa kuhudumia wananchi 1,000,000 ifikapo 2015. Hadi Juni 2010, mradi huo unahudumia wananchi 430,000 katika Miji ya Kahama na Shinyanga na vijiji 39 ambavyo tayari vimeunganishwa kati ya lengo la vijiji 76 katika Mikoa ya Mwanza na Shinyanga. Katika mwaka 2010/2011, Wizara yangu itakamilisha kazi ya kumpata mtaalam mwelekezi atakayefanya upembuzi yakinifu na usanifu wa kufikisha huduma ya maji katika Miji ya Nzega, Igunga na Tabora.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imekamilisha usanifu wa awamu ya pili ya Mradi wa Maji wa Chalinze itakayohusisha vijiji 48 vilivyo katika Wilaya za Bagamoyo na Morogoro (vijijini). Mkandarasi wa mradi katika vijiji nane unaotekelezwa kwa kushirikiana na Benki ya Kiarabu ya Maendeleo ya Afrika *(BADEA)*, ameanza ujenzi mwishoni mwa mwezi Septemba 2009. Vijiji hivyo ni Msolwa, Mdaula, Matuli, Kaloleni, Mwidu, Visakazi, Tukamisasa na Ubenazomozi. Mkandarasi kwa ajili ya vijiji vingine sita vya Ngerengere, Sangasanga, Kinonko, Kidugalo, Sinyaulime na Kizuka amepatikana na ameanza ujenzi. Ujenzi huo unatekelezwa kwa kushirikiana na Serikali ya Jamhuri ya Watu wa China. Utekelezaji wa mradi katika vijiji 34 vilivyosalia utafanyika kwa kugharamiwa na Mfuko wa Pamoja wa Sekta ya Maji, ambapo taratibu za kutangaza zabuni ya ujenzi na kumpata mtaalam mwelekezi wa kusimamia ujenzi huo zinaendelea. Lengo ni kuwa mikataba itasainiwa na kazi kuanza mwezi Agosti 2010.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara kupitia vyombo vya watumiaji maji ilihamasisha wateja kujiunga na mtandao uliopo. Kwa kipindi cha miaka minne ya utekelezaji idadi ya wananchi wanaofaidika moja kwa moja na mradi huu imefikia 76,923.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali ilikamilisha awamu ya kwanza ya kuboresha huduma ya maji katika Jiji la Dar es Salaam kwa kukarabati vyanzo vya maji vya Ruvu Juu, Ruvu Chini na Mtoni. Ukarabati huo umeongeza kiwango cha maji yanayozalishwa kutoka wastani wa mita za ujazo 249,200 kwa siku mwaka 2007/2008 hadi kufikia wastani wa mita za ujazo 273,000 kwa siku mwaka 2008/2009. Ukarabati wa jumla ya kilomita 1,132.5 za mabomba makuu ya kusambaza maji umekamilika. Kwa lengo la kuboresha upatikanaji wa maji katika Jiji la Dar es Salaam, Serikali itatekeleza miradi ya

kuongeza wingi wa maji kwa kujenga Bwawa la Kidunda, kuchimba visima virefu katika maeneo ya Kimbiji na Mpera, kupanua mitambo ya Ruvu Chini na Ruvu Juu na kujenga mabomba makuu ya kufikisha maji Jijini kutoka kituo cha Ruvu Chini na Ruvu Juu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhimiza, kuimarisha na kupanua teknolojia nyepesi na rahisi ya kukinga, kutunza na kutumia maji ya mvua; katika kipindi cha mwaka 2005 hadi 2010, Serikali imeendelea kuhamasisha wananchi kutumia teknolojia ya kuvuna maji ya mvua kwa kujenga matanki ya mfano katika taasisi za umma, shule, zahanati na vituo vya afya. Jumla ya matanki tisa yenye ukubwa mbalimbali yalikarabatiwa. Matanki mapya 313 yalijegwa katika Wilaya za Karatu, Karagwe, Kasulu, Rombo, Siha, Serengeti, Geita, Kwimba, Sengerema, Ukerewe, Bariadi, Bukombe, Kishapu, Maswa, Uyui, Iramba, Sikonge, Urambo, Bukoba Mjini, Lindi Mjini, Shinyanga Mjini na Jiji la Mwanza. Mafundi 18 kutoka Kasulu, Karatu, Bunda, Lushoto, Kigoma, Shinyanga, Lindi, Liwale, Mtwara na Kilosa walipewa mafunzo ya uvunaji wa maji ya mvua yaliyoendeshwa na Chuo cha Maendeleo na Usimamizi wa Maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uhamasishaji wa uvunaji wa maji ya mvua kwa kutumia mapaa ya nyumba umo katika Programu ya Maji na Usafi wa Mazingira Vijijini. Wataalam washauri watazisaidia Halmashauri kujenga matanki matatu ya mfano na kutoa mafunzo kwa mafundi wawili katika kila kijiji. Watatoa elimu kuhusu uvunaji wa maji ya mvua kwa kutumia mapaa ya nyumba katika vijiji vyote 10 vyenye miradi katika kila Halmashauri. Halmashauri za wilaya na miji zinashauriwa kutunga sheria ndogo kwa ajili ya kuzitaka taasisi na kaya kuvuna maji ya mvua kutoka kwenye mapaa ya nyumba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuandaa mazingira mazuri ya kisheria kuhusu rasilimali za maji na kubaini vyombo na muundo utakaomudu majukumu; mipango na menejimenti ya rasilimali ya maji nchini; Serikali katika kuhakikisha rasilimali za maji nchini zinasimamiwa na kuendelezwa ipasavyo, imeweka muundo utakaosimamia rasilimali za maji kama ifuatavyo: Vikundi vya Watumiaji Maji, Vyama vya Watumiaji Maji, Kamati za Maji za Mabonde Madogo ya Maji, Bodi za Maji za Mabonde na Bodi ya Ushauri ya Kitaifa ya Maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Muundo huo umepewa nguvu ya kisheria katika kusimamia na kuendeleza matumizi ya rasilimali za maji kulingana na Sheria ya Usimamizi wa Rasilimali za Maji, Sheria Na. 11 ya Mwaka 2009 na Sheria ya Huduma za Maji na Usafi wa Mazingira, Sheria Na. 12 ya Mwaka 2009, ambazo zilipitishwa na Mkutano wa 15 wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania mwezi Aprili 2009. Mheshimiwa Rais, aliweka saini sheria hizo tarehe 12 Mei 2009 na zilianza kutumika rasmi tarehe 1 Agosti 2009 baada ya kutangazwa katika Gazeti la Serikali. Kwa mujibu wa sheria mpya za maji, jukumu la kusajili vyombo vya watumiaji maji limepewa Halmashauri na Bodi za Maji za Mabonde badala ya Waziri mwenye dhamana ya maji. Hivi sasa Wizara yangu inaendelea kuandaa kanuni za kutekeleza sheria hizo mpya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sheria ya Usimamizi wa Rasilimali za Maji, Sheria Na. 11 ya Mwaka 2009, ina maeneo 41 yanayohitaji Kanuni na Sheria ya Huduma za Maji na

Usafi wa Mazingira, Sheria Na. 12 ya Mwaka 2009, ina maeneo 11 yanayohitaji Kanuni. Katika maandalizi ya kanuni hizo hatua zifuatazo zimefikiwa:-

(a) Kanuni mbili tayari zimechapishwa, kutangazwa na zinatumika. Kanuni hizo ni *Water Resources Management (Registration of Water Users Associations) Regulations 2009 GN. 22* ya tarehe 22 Januari 2010 na *Water Supply and Sanitation (Registration of Community Owned Water Supply Organizations) Regulations* 2009 *GN. 21* ya tarehe 22 Januari 2010;

(b) Kanuni mbili zimesainiwa kwa ajili ya kuchapishwa na kuanza kutumika. Kanuni hizo ni *The Water Resources Management (Procedure for Nomination of Board Members) Regulations 2010* na *The Water Resources Management (Water Abstraction, Use and Discharge) Regulations 2010;*

(c) Kanuni mbili za *Clustering of Water Utilities* na *Water Supply Regulations* zinaandaliwa na zitawasilishwa kwa majadiliano kwenye vikao ngazi ya Wizara; na

(d) Kanuni mbili za *Water Resources Classification and Reserve* na *Water Abstraction Charges* zinafanyiwa utafiti ili kubaini mahitaji ya kitaalam.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Sekta ya Umwagiliaji, maelekezo ya Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya Mwaka 2005 yameweka bayana maeneo ya kipaumbele katika kuendeleza kilimo cha umwagiliaji. Utekelezaji wake ni kama ifuatavyo:-

(i) Maji yakingwe kwenye visima, malambo na mabwawa kwa matumizi ya watu, mifugo na umwagiliaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kipindi cha mwaka 2005 hadi 2010, Serikali imeendelea na ujenzi wa mabwawa kwa ajili ya umwagiliaji. Mabwawa 24 ya umwagiliaji yamejengwa na kukarabatiwa. Mabwawa hayo ni Kiserian (Longido), Quash (Babati), Mangisa (Mbulu) Buigiri (Chamwino), Ikowa (Chamwino), Nkiniziwa (Nzega), Itobela (Uyui), Isikizya (Uyui), Ulyanyama (Sikonge), Budushi (Nzega), Mibono (Nzega), Ngobore (Kilindi), Kisangwa (Bunda), Itumbiko (Kibondo), Msoga (Bagamoyo), Masinono (Musoma Vijijini), Usunga (Sikonge), Magiri (Uyui), Msimba (Uyui), Ibelamilundi (Uyui), Imalampaka (Sikonge), Udogo (Sikonge), Nyamilangano (Kahama) na Nsololo (Uyui). Katika kuhakikisha matumizi endelevu ya mabwawa, Wizara kwa kutumia miongozo iliyoandaliwa imewapa mafunzo wataalam ngazi ya wilaya juu ya kuzingatia hifadhi na ulinzi wa vyanzo vya maji.

(ii) Kipaumbele kiwe katika kuendeleza miradi midogo na ya kati, ikiwa ni pamoja na kuandaa mifumo ya uvunaji wa maji ya mvua na kuchimba mabwawa ili kuimarisha kilimo cha umwagiliaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kipindi cha mwaka 2005 hadi mwaka 2010, Serikali iliendeleza jitihada mbalimbali katika kuboresha kilimo cha umwagiliaji hapa nchini kama ifuatavyo:-

(a) Kuongeza eneo la umwagiliaji kutoka hekta 264,388 mwaka 2005 hadi kufikia hekta 331,490 mwezi Mei 2010. Eneo lililoendelezwa hadi sasa linahusisha hekta 276,261 za mashamba ya wakulima wadogo na hekta 55,229 za mashamba ya wakulima wakubwa wa mazao ya biashara ya chai, kahawa, miwa, maua, mbogamboga na mpunga;

(b) Katika skimu za umwagiliaji, uzalishaji kwa mazao ya chakula na mbogamboga hususan mpunga, vitunguu na nyanya umeongezeka kama ifuatavyo: mpunga ni wastani wa tani 6 kwa hekta kutoka tani 1.8; vitunguu tani 26 kwa hekta kutoka tani 13; na nyanya tani 18 kwa hekta kutoka tani 5;

(c) Kukamilisha na kupitisha Sera ya Umwagiliaji mwezi Februari 2010 na kuanza utayarishaji wa Mkakati wa Taifa wa Kuendeleza Umwagiliaji na Sheria ya Umwagiliaji;

(d) Kukamilisha na kusambaza miongozo ya kitaalam ya kuanzisha, kuendeleza na kuendesha skimu za umwagiliaji ngazi ya wilaya. Kutokana na matumizi ya miongozo hiyo, skimu zilizoibuliwa na kufuzu kupata fedha za nyongeza kutoka Mfuko wa Kuendeleza Umwagiliaji ngazi ya Wilaya *(District Irrigation Development Fund - DIDF)* zimeongezeka kama ifuatavyo: mwaka 2006/2007 (5), mwaka 2007/2008 (39), mwaka 2008/2009 (41), mwaka 2009/2010 (94) na mwaka 2010/2011 (113); na

(e) Kutoa mafunzo kwa wakulima 2,800 na wataalam 250 kuhusu teknolojia sahihi za kuendeleza kilimo cha umwagiliaji na usimamizi bora wa maji kwa ajili ya kilimo endelevu cha umwagiliaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Vikundi 210 vya umwagiliaji viliundwa na kusajiliwa ili kuhakikisha skimu za umwagiliaji zinakuwa endelevu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara ya Maji na Umwagiliaji kwa mwaka 2010/2011 itaendelea kutekeleza majukumu yake kulingana na Sera ya Maji; Sera ya Umwagiliaji; Mkakati wa Maendeleo ya Sekta ya Maji; Mkakati wa Maendeleo ya Sekta ya Kilimo; Programu ya Maendeleo ya Sekta ya Maji (*WSDP*); na Programu ya Maendeleo ya Sekta ya Kilimo (*ASDP*). Kwa kuzingatia sera na mikakati hiyo, dira na dhamira ya Wizara ni kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Dira: Kuwa na mfumo endelevu wa kusimamia na kuendeleza rasilimali za maji utakaoleta manufaa ya kijamii na kiuchumi ikiwa ni pamoja na kuimarisha kilimo cha umwagiliaji kwa lengo la kuongeza Pato la Taifa ili kupunguza umaskini na kuwa na chakula cha uhakika nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Dhamira: Kuhakikisha rasilimali za maji zinasimamiwa, zinaendelezwa na zinatumika kwa njia endelevu na shirikishi ili kukidhi mahitaji ya sekta mbalimbali kwa kuweka mfumo madhubuti wa kitaasisi wa kusimamia

rasilimali za maji, kuendeleza na kuboresha miundombinu ya usambazaji majisafi, uondoaji wa majitaka na miundombinu ya umwagiliaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kutekeleza majukumu yake, Wizara inazingatia ahadi zilizotolewa na Serikali, malengo ya Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya Mwaka 2005, Mkakati wa Kukuza Uchumi na Kupunguza Umaskini Tanzania (MKUKUTA), Malengo ya Milenia, na Dira ya Taifa ya Maendeleo 2025. Majukumu hayo ni pamoja na:-

(i) kutayarisha na kusimamia utekelezaji wa sera, mikakati na programu za kuendeleza sekta ya maji na sekta ya umwagiliaji;

(ii) kutayarisha na kusimamia sheria, kanuni na taratibu zinazosimamia sekta ya maji na sekta ya umwagiliaji;

(iii) kutafuta vyanzo mbalimbali vya fedha kwa ajili ya kutekeleza miradi ya maji na miradi ya umwagiliaji;

(iv) kukusanya, kuchambua, kutafsiri na kuhifadhi takwimu muhimu za sekta ya maji na sekta ya umwagiliaji;

(v) kutoa miongozo ya kusimamia matumizi endelevu ya rasilimali za maji;

(vi) kutoa miongozo kuhusu utoaji wa huduma za maji na usafi wa mazingira mijini na vijijini;

(vii) kutoa mafunzo kwa wataalam wa sekta ya maji na sekta ya umwagiliaji katika ngazi na kada mbalimbali za utekelezaji;

(viii) kuendeleza tafiti kuhusu teknolojia zinazotumika katika kutoa huduma za maji na kilimo cha umwagiliaji;

(ix) kutoa miongozo ya matumizi ya teknolojia bora za umwagiliaji; na

(x) kuratibu majukumu na kutekeleza ushauri wa Bodi ya Taifa ya Maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kutekeleza majukumu yake, Wizara inaongozwa na Sera ya Maji kwa Sekta ya Maji. Kwa Sekta ya Umwagiliaji, Wizara imekuwa ikiongozwa na Sera ya Kilimo na Mifugo. Sera ya Maji inatoa mwongozo unaolenga kuhakikisha kuwa, rasilimali za maji nchini zinalindwa, zinahifadhiwa na zinatumiwa kwa uwiano kwa kuzingatia mahitaji ya sekta za kiuchumi, kijamii na hifadhi ya mazingira. Wizara imetafsiri Sera ya Maji katika lugha nyepesi ili jamii nzima iweze kuielewa vizuri na hivyo kushiriki kikamilifu katika kuitekeleza. Sera ya Kilimo na Mifugo inatoa kipaumbele katika kuendeleza skimu za asili za umwagiliaji za wakulima wadogo ikiwa ni pamoja na kuandaa mifumo ya uvunaji wa maji ya mvua na kujenga mabwawa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka wa 2009/2010, Wizara ilikamilisha maandalizi ya Sera ya Umwagiliaji iliyopitishwa na Serikali mwezi Februari 2010. Sera hiyo inaboresha miongozo na malengo yaliyoainishwa katika Sera ya Kilimo na Mifugo. Sera ya Umwagiliaji inalenga katika kukidhi mahitaji ya kilimo endelevu cha umwagiliaji ikiwa ni pamoja na kutoa mwelekeo sahihi wa matumizi endelevu ya rasilimali za maji kwa umwagiliaji. Hivi sasa, Wizara inaandaa Sheria ya Umwagiliaji na Mkakati wa Taifa wa Kuendeleza Umwagiliaji. Hatua hizi zinachukuliwa ili kwenda sambamba na kaulimbiu ya Kilimo Kwanza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuzingatia makubaliano kati ya Serikali na washirika wa maendeleo yaliyofikiwa wakati wa maandalizi ya Programu ya Maendeleo ya Sekta ya Maji, Wizara yangu hutathmini utekelezaji wa Programu hiyo kila mwaka. Kwa mwaka 2009/2010, tathmini ilifanyika mwezi Novemba 2009, ambapo Serikali iliwakilishwa na Wizara yangu, Wizara ya Fedha na Uchumi, Ofisi ya Waziri Mkuu - Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii, Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi na wadau wengine. Tulikubaliana yafuatayo:-

(i) kusanifu na kutekeleza mfumo wa taarifa za kimenejimenti kwa Programu ya Maendeleo ya Sekta ya Maji ili kuwezesha maandalizi ya kisekta ya mipango, bajeti na utoaji wa taarifa;

(ii) mpango kazi kwa mwaka 2010/2011 uzingatie kikamilifu malengo yaliyopangwa kulingana na Mkakati wa Taifa wa Maendeleo ya Sekta ya Maji;

(iii) kuhakikisha bajeti ya Programu inaandaliwa kwa uwazi kulingana na utekelezaji wa kazi, mahitaji na katika hali ya uwiano;

(iv) kuhakikisha Washirika wa Maendeleo wanatimiza majukumu ya uchangiaji wa fedha kulingana na makubaliano yaliyopo kati ya Serikali na Washirika wa Maendeleo;

(v) kuhakikisha kuwa mfumo wa mawasiliano wa kufuatilia utekelezaji unakuwepo na unatekelezwa ipasavyo;

(vi) kuhakikisha kwamba taarifa za awali kutoka kwa watekelezaji wa Programu zinaingizwa kwenye benki ya kitaifa ya taarifa kwa sekta ya maji;

(vii) kuhakikisha kuwa taarifa za utekelezaji zinasambazwa kwa wadau;

(viii) kuhakikisha kunakuwa na utaratibu mzuri na unaoeleweka wa kuwajengea uwezo watumishi wa sekta ya maji;

(ix) kuhakikisha kwamba mipango ya rasilimali watu kwa sekta ya maji inatayarishwa kwa pamoja kati ya Wizara ya Maji na Umwagiliaji na TAMISEMI;

(x) kutafiti njia bora za kuimarisha utekelezaji wa masuala ya usafi wa mazingira;

(xi) kuwezesha masuala yanayohusu usafi wa mazingira kutekelezwa katika vijiji 1,320 vilivyo chini ya Programu ya Maji Vijijini na Usafi wa Mazingira; na

(xii) kushiriki katika kuandaa na kutekeleza Sera ya Usafi wa Mazingira na mfumo wa uratibu wa masuala hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Bonde la Mto Nile linajumuisha Nchi za Tanzania, Uganda, Kenya, Rwanda, Burundi, Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo, Sudan, Misri, Eritrea na Ethiopia. Kwa kutambua umuhimu wa kushirikiana katika matumizi endelevu ya rasilimali za maji, nchi hizo zilianzisha chombo cha mpito cha ushirikiano *(Nile Basin Initiative*) mwezi Februari 1999 kwa ajili ya usimamizi wa rasilimali za maji zilizo katika Bonde hilo. Maadhimisho ya miaka 10 ya ushirikiano huo yalifanyika mwezi Desemba 2009 ambapo Tanzania ilikuwa mwenyeji.

Nchi washirika zilijadili mafanikio, fursa na changamoto mbalimbali zilizojitokeza katika kutekeleza miradi mbalimbali ya ushirikiano. Jumla ya washiriki wapatao 500 kutoka nchi zote za Bonde la Mto Nile na Washirika wa Maendeleo walihudhuria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mkutano wa tatu wa Mawaziri wa Maji wa Nchi za Bonde la Mto Zambezi linalojumuisha Angola, Botswana, Malawi, Msumbiji, Namibia, Tanzania, Zimbabwe na Zambia ulifanyika mwezi Mei 2010 katika Jiji la Bulawayo, Zimbabwe. Mkutano huo ulihudhuriwa na nchi zote za Bonde.

Pamoja na masuala mengine, mkutano ulijadili taarifa ya kuridhia kwa Mkataba wa kuanzisha Kamisheni ya Bonde la Mto Zambezi (*ZAMCOM*). Hadi mkutano huo ulipokuwa ukifanyika, nchi tano (Angola, Botswana, Msumbiji, Namibia na Tanzania) kati ya nane tayari zilikuwa zimesharidhia mkataba huo. Mkutano uliazimia yafuatayo:-

(i) Malawi na Zimbambwe zikamilishe taratibu za kuridhia Mkataba huo kabla ya mwisho wa mwaka 2010;

(ii) Zambia isaini Mkataba wa *ZAMCOM* hatimaye iridhie Mkataba huo mapema iwezekanavyo mara baada ya sheria yao mpya ya maji kupitishwa na Bunge; na

(iii) Botswana isaini makubaliano na Sekretarieti ya *SADC* (*MoU*) na ikubali kuwa Makao Makuu ya muda ya Kamisheni ya *ZAMCOM.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mkutano wa mwaka wa Mawaziri wa Maji wa Jumuiya ya Maendeleo ya Nchi za Kusini mwa Afrika (*SADC*), ulifanyika tarehe 17 - 21 Mei 2010 katika Jiji la Bulawayo, Zimbabwe. Mkutano huo ulihudhuriwa na Mawaziri toka Angola, Botswana, Lesotho, Tanzania, Zambia, Zimbabwe, Malawi na Msumbiji.

Pamoja na masuala mengine, mkutano ulipata taarifa ya mapitio ya mpango mkakati wa utekelezaji wa miradi ya programu ya maji ya *SADC* (Awamu ya Pili). Mkutano huo ulifikia maamuzi yafuatayo:-

(i) Sekretarieti ya *SADC* iandae kwa haraka mpango mkakati wa utekelezaji wa miradi ya awamu ya tatu; na

(ii) nchi wanachama wa Bonde la Mto Zambezi zikamilishe taratibu zote za kuridhia Mkataba wa kuanzisha *ZAMCOM* kabla ya mwisho wa mwaka 2010.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika ushirikiano huo, Tanzania imenufaika kwa kuanzishwa mfumo wa usimamizi wa rasilimali za maji kwa kujenga vituo 11 vya kufuatilia mwenendo wa rasilimali za maji wakati wa utekelezaji wa Mradi wa *Southern African Development Community – Hydrological Cycle Observing System (SADC HYCOS)* unaotekelezwa chini ya Progamu ya Maji ya nchi za *SADC*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kila mwaka, nchi yetu huadhimisha Wiki ya Maji kuanzia tarehe 16 hadi 22 Machi, ambayo ni Siku ya Maji Duniani. Maadhimisho ya 22 ya mwaka 2010 yalilenga katika kutoa fursa kwa wadau wa sekta za maji na umwagiliaji kushiriki kwa pamoja katika kuhamasisha utekelezaji wa Sera ya Maji na Sera ya Umwagiliaji, mikakati na mipango ya maendeleo ya sekta hizo, ikiwa ni pamoja na kupima mafanikio na changamoto zilizopo. Maadhimisho yalihusisha uendeshaji wa warsha, mafunzo kupitia semina na maonesho ya vifaa, teknolojia na huduma za maji na umwagiliaji.

Vilevile, Maadhimisho ya Wiki ya Maji yalitumika katika kuhamasisha wananchi kushiriki katika kupanga, kujenga, kusimamia na kuendesha miradi ya maji na umwagiliaji na kutunza vyanzo vya maji na mazingira. Maadhimisho hayo, yalitumika pia kuweka mawe ya msingi na kuzindua miradi ya maji na umwagiliaji na uhamasishaji wa jamii kushiriki katika utunzaji, uendelezaji na usimamizi wa rasilimali za maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mwaka 2010, Maadhimisho ya 22 ya Wiki ya Maji yalifanyika Kitaifa Mkoa wa Pwani. Kaulimbiu ya Maadhimisho hayo ilikuwa “Maji Safi na Salama kwa Afya Bora”. Mheshimiwa Shamsi Vuai Nahodha, Waziri Kiongozi wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, alikuwa Mgeni Rasmi kwenye kilele cha Maadhimisho. Kupitia Bunge lako Tukufu, naomba kutoa shukrani zangu za dhati kwa Mheshimiwa Shamsi Vuai Nahodha, kwa kukubali kuwa mgeni rasmi. Napenda kutumia fursa hii, kuwashukuru wananchi wote walioshiriki katika Maadhimisho hayo. Nawashukuru viongozi wote kuanzia ngazi ya kijiji, wilaya hadi mkoa, kwa kuratibu na kusimamia vizuri maadhimisho hayo. Nawashukuru kwa namna ya kipekee, Viongozi wa Mkoa wa Pwani, wananchi na washiriki wote wa maonesho yaliyofanyika kwa wiki nzima Uwanja wa Mwendapole, Kibaha. Mwisho, napenda kuwapongeza sana washindi wote waliotunukiwa zawadi katika maonesho ya mwaka huu na kuwaomba washiriki tena mwakani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kufanikisha utekelezaji wa Programu ya Maji na Usafi wa Mazingira Vijijini, Serikali iliamua kuwe na Mkutano Mkuu wa Mwaka wa Programu hiyo kwa ajili ya kubadilishana uzoefu na kujadili mafanikio na changamoto katika utekelezaji. Mkutano wa kwanza ulifanyika Arusha tarehe 14 hadi 15 mwezi Desemba 2009, ambapo jumla ya washiriki 389 walihudhuria. Mkutano huo ulihusisha Viongozi na Maafisa kutoka Wizara ya Maji na Umwagiliaji, TAMISEMI, Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii, Wizara ya Fedha na Uchumi, Wahandisi wa maji katika Sekretarieti za Mikoa, Wakurugenzi wa Halmashauri, Wahandisi wa Maji wa Halmashauri, Washirika wa Maendeleo, Mashirika yasiyo ya Kiserikali, Wataalam Washauri na Maafisa kutoka Wizara na taasisi nyingine zinazohusika na masuala ya maji. Mkutano huo uliazimia yafuatayo:-

(i) Taarifa za utekelezaji za kila robo mwaka ziandaliwe kwa wakati na umakini na ziwasilishwe TAMISEMI na Wizara ya Maji na Umwagiliaji;

(ii) Halmashauri ziweke kipaumbele kwenye masuala ya usafi wa mazingira na usafi wa mtu binafsi katika mipango na bajeti zao;

(iii) Halmashauri na Sekretarieti za Mikoa ziwajibike kikamilifu katika kusimamia Wataalam washauri katika kuainisha vyanzo vya maji, upimaji, usanifu, kuandaa zabuni na kusimamia ujenzi wa miradi ya maji;

(iv) Wizara ya Maji na Umwagiliaji kwa kushirikiana na TAMISEMI na Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma iweke utaratibu wa kuwahamisha watumishi wa maji walio katika katika Ofisi za Mabonde kwenda katika Halmashauri kwa kuzingatia mwongozo wa mahitaji ya watumishi wanaotakiwa katika Idara ya Maji kwenye Halmashauri na Sekretarieti za Mikoa;

(v) Halmashauri ziandae mpango wa kuhamasisha wananchi kuhusu uanzishaji na usajili wa vyombo huru vya watumiaji maji;

(vi) Idara za Maji na Ujenzi katika Halmashauri zisiunganishwe na pale ambapo zimeunganishwa, zitenganishwe ili kila idara ijitegemee kama idara kamili; na

(vii) Halmashauri zisimamie uagizaji na ufungaji wa mitambo ya maji ili kuhakikisha viwango na ubora unaotakiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mamlaka za Majisafi na Majitaka Mijini katika Miji Mikuu ya Mikoa, Miji Mikuu ya Wilaya na Miji Midogo ni Taasisi za Serikali zinazojitegemea. Taasisi hizo hutoa huduma ya majisafi na majitaka katika miji hiyo kulingana na Sheria ya Huduma za Maji na Usafi wa Mazingira, Sheria Na. 12 ya Mwaka 2009 na Sheria ya DAWASA, Sheria Na. 20 ya Mwaka 2001. Kwa mujibu wa taratibu za uendeshaji, kila mwaka mamlaka hizo hufanya mkutano mkuu kujadili hali ya utendaji kazi na mapato na matumizi ya mwaka kwa lengo la kuongeza ufanisi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mkutano wa 12 ulifanyika tarehe 27 hadi 29 Aprili 2010 Mjini Musoma, Mkoa wa Mara. Mkutano ulifikia maazimio yaliyolenga kuboresha utendaji katika maeneo yafuatayo:-

(i) kutoa taarifa za hesabu za mapato na matumizi ya Mamlaka ambazo ni sahihi;

(ii) kudhibiti upotevu wa maji;

(iii) kutoa taarifa sahihi za viwango vya utendaji;
(iv) kujenga uwezo wa rasilimali watu;

(v) kuhakikisha watumishi wanapewa motisha;

(vi) kuharakisha uwekezaji kwenye Mamlaka;

(vii) kuwasiliana na Mamlaka ya Mapato Tanzania ili kupata msamaha wa kodi ya ongezeko la thamani kwenye dawa za kusafisha na kutibu maji;

(viii) kuzingatia Sera ya Menejimenti ya Tahadhari (*Risk Management Policy*) katika utendaji kazi wa kila siku katika Mamlaka;

(ix) kuzipandisha daraja Mamlaka 10 za miji mikuu ya wilaya, miji midogo na miradi mitatu ya Kitaifa kutoka daraja C kwenda B. Mamlaka hizo ni Kondoa, Makambako, Ngara, Kahama, Liwale, Kyela, Itumba, Tukuyu, Nzega, Pangani na miradi ya kitaifa ni Wanging'ombe, Chalinze na *Kahama-Shinyanga Water Supply Authority (KASHWASA)*; na

(x) kusimamia ipasavyo matumizi ya fedha za Mamlaka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuzingatia makubaliano kati ya Serikali na Washirika wa Maendeleo yaliyofikiwa wakati wa maandalizi ya Programu ya Maendeleo ya Sekta ya Kilimo, Wizara yangu kila mwaka hutathmini kwa pamoja na Washirika wa Maendeleo, utekelezaji wa Programu hiyo, ikiwa ni pamoja na sehemu ya umwagiliaji. Kwa mwaka 2009/2010, tathmini ilifanyika kuanzia mwezi Septemba hadi Oktoba 2009 ambapo Serikali iliwakilishwa na Wizara yangu, Wizara ya Kilimo Chakula na Ushirika, Wizara ya Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi, Wizara ya Viwanda, Biashara na Masoko, Wizara ya Fedha na Uchumi, TAMISEMI na wadau wengine. Katika tathmini hiyo mambo yafuatayo yalijitokeza:-

(i) uchangiaji wa Halmashauri na wakulima katika usimamizi na uendeshaji wa skimu za umwagiliaji ni mdogo hivyo kuhatarisha uendelevu wa skimu hizo;

(ii) uwekezaji katika kuendeleza skimu za umwagiliaji ni mdogo na unasababisha skimu kutokamilika kwa wakati;

(iii) ushiriki wa sekta binafsi katika kuwekeza kwenye uendelezaji wa kilimo cha umwagiliaji ni mdogo;

(iv) Kiwango cha juu ambacho skimu moja inaweza kupata kutoka Mfuko wa Kuendeleza Umwagiliaji ngazi ya Wilaya *(DIDF)* kimeongezeka kutoka shilingi milioni 500 hadi shilingi milioni 800. Hatua hii itasaidia kuongeza kasi ya utekelezaji wa miradi;

(v) uhaba wa wataalam na vitendea kazi kuanzia ngazi ya taifa hadi wilaya katika kuendeleza umwagiliaji;

(vi) utekelezaji wa miradi ya umwagiliaji chini ya *ASDP* uzingatie masuala ya mazingira; na

(vii) mapitio ya Mpango Kabambe wa Taifa wa Umwagiliaji (*NIMP-2002*) yafanyike haraka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Maadhimisho ya Siku ya Wakulima Nane Nane yalifanyika Kitaifa Mjini Dodoma mwezi Agosti 2009. Kikanda yalifanyika Arusha, Morogoro, Mbeya na Mwanza. Kaulimbiu ilikuwa ni "Mapinduzi ya Kijani – Uhakika wa Chakula na Kipato." Wizara ilitumia fursa ya maadhimisho hayo kuhamasisha matumizi bora na endelevu ya maji na kuonesha umuhimu wa miundombinu ya umwagiliaji zikiwemo aina mbalimbali za mifumo ya umwagiliaji na tija inayotokana na miundombinu hiyo. Fursa za kutumia nishati mbadala kama vile upepo na jua za kuendesha pampu za kusukuma maji kwa ajili ya umwagiliaji zilioneshwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Maadhimisho ya Siku ya Chakula Duniani (*World Food Day*), yalifanyika kitaifa Sumbawanga mwezi Oktoba 2009. Ushiriki wa Wizara katika maadhimisho hayo ulitoa fursa ya kuonesha teknolojia mbalimbali za umwagiliaji zenye ufanisi wa matumizi ya maji zinazochangia katika kuongeza usalama wa chakula na kipato cha wakulima. Vipeperushi vinavyoelezea masuala ya umwagiliaji viligawiwa kwa wadau.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mkutano wa Kamati ya Uratibu wa Mfuko wa Kuendeleza Umwagiliaji ngazi ya Wilaya *(DIDF)*, ulifanyika Morogoro Mei 2010. Mkutano huo ulilenga kutathmini na kuidhinisha maombi ya Halmashauri ya kupewa fedha za nyongeza kwa ajili ya miradi ya umwagiliaji iliyopata fedha pungufu katika bajeti zao za kutekeleza Mipango ya Maendeleo ya Kilimo ya Wilaya *(DADPs)*. Mkutano huo ulibaini kuwa, maandiko ya Halmashauri ya kuomba fedha za nyongeza kutoka Mfuko wa *DIDF*, yamekuwa bora zaidi kuliko miaka ya nyuma kutokana na mafunzo yaliyotolewa kwa kutumia miongozo iliyoandaliwa na Wizara.

Mhehsimiwa Mwenyekiti, Mikutano ya Maafisa wa Kanda za Umwagiliaji nchini ilifanyika Dodoma Julai 2009, Dar es Salaam Februari 2010 na Morogoro Mei 2010 ili kujadili utekelezaji wa majukumu ya wadau wa sekta ya umwagiliaji. Maazimio yaliyofikiwa katika mikutano hiyo ni pamoja na:-

(i) kuratibu na kuwezesha utekelezaji wa majukumu ya wadau wa sekta ya umwagiliaji;

(ii) kutoa ushauri wa kitaalam ili kuziwezesha Halmashauri kuibua miradi na kutumia miongozo iliyotayarishwa kwa ajili ya utekelezaji wa *DADPs* na uendeshaji wa Mfuko wa *DIDF* kwa ajili ya kuendeleza skimu za umwagiliaji; na

(iii) kupitia muundo wa sekta ya umwagiliaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mkutano wa 139 wa Baraza la Shirika la Chakula na Kilimo la Umoja wa Mataifa (*FAO*) ulifanyika Rome, Italia kuanzia tarehe 17 hadi 21 Mei 2010. Mkutano huo uliohudhuriwa na nchi wanachama, ulipokea taarifa kutoka kamati mbalimbali ikiwa ni pamoja na Kamati ya Usalama wa Chakula na ile inayoratibu maendeleo ya Miradi ya Ushirikiano wa Kitaalam *(Technical Cooperation Projects).*

Mheshimiwa Mwenyekiti, madhumuni ya mkutano huo yalikuwa ni pamoja na kutoa tamko la kukabiliana na njaa (*petition against hunger*), ambayo imewakumba watu wapatao bilioni moja na kuhakikisha utendaji wa Shirika unaboreshwa. Maazimio yaliyofikiwa ni pamoja na:-

(i) kuongeza ushirikiano wa Shirika na Taasisi nyingine za Umoja wa Mataifa kama vile Programu ya Chakula Duniani (*World Food Programme - WFP*) na Mfuko wa Kimataifa wa Maendeleo ya Kilimo (*International Fund for Agricultural Development – IFAD*) ili huduma kwa nchi wanachama ziwe bora;

(ii) ofisi za kanda za shirika zipewe madaraka zaidi ya kupanga na kuamua katika masuala yanayohusu miradi ya ushirikiano wa kitaalamu; na

(iii) kutoa umuhimu kwa matumizi ya maji katika dhana nzima ya kuongeza uzalishaji wa mazao na kuwa na usalama wa chakula.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mkutano wa Wadau wa Matumizi ya Maji kwa Kilimo *(Agricultural Water Partners),* ulifanyika Tunis, Tunisia kuanzia tarehe 23 hadi 24 Machi 2010. Mkutano huo ulikuwa chini ya Uenyekiti wa pamoja wa Tanzania na Benki ya Dunia. Madhumuni ya mkutano yalikuwa ni kuangalia utekelezaji wa Nguzo ya Kwanza *(Pillar No. 1)* ya *Comprehensive Africa Agriculture Development Programme (CAADP)* katika Nchi za Afrika. Nguzo hii inahusu kuongeza eneo la ardhi lenye usimamizi na matumizi endelevu *(extending the area under sustainable land management).* Mkutano ulibainisha kwamba, katika nguzo ya kwanza, suala la matumizi ya maji kwa kilimo halikuwa limepewa kipaumbele ikilinganishwa na masuala ya ardhi na utunzaji wake.

Hivyo, kutokana na umuhimu wa kujitosheleza kwa chakula na kuwa na ziada, matumizi ya maji katika umwagiliaji yanahitajika kupewa kipaumbele.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Maazimio ya mkutano huo yaliyofikiwa ni pamoja na:-

(i) kuboresha utekelezaji wa *CAADP* na kuhakikisha nchi za Afrika zinaweka saini makubaliano ya *CAADP*;

(ii) kusimamia uanzishwaji wa umoja wa wadau wa matumizi ya maji kwa kilimo;

(iii) kubadilishana utaalam na uzoefu katika masuala ya maji na taasisi nyingine za kikanda;

(iv) kuifanya taasisi ya *Agricultural Water (AgWA)* kuwa na benki ya wataalam (*Experts Pool*); na

(v) kutayarisha mpango-kazi wa taasisi hiyo ili kupata fedha kutoka kwa wafadhili mbalimbali.

(vi) Mkutano wa Kamati ya Uendeshaji kuhusu Tathmini ya Kimkakati ya Mazingira na Jamii

Mheshimiwa Mwenyekiti, mkutano wa Kamati ya uendeshaji kuhusu tathmini ya kimkakati ya mazingira na jamii (*Steering Committee for Strategic Environmental and Social Assessment-SESA*) juu ya Sera ya Umwagiliaji na Mpango Kabambe wa Taifa wa Umwagiliaji ulifanyika Kibaha mwezi Machi 2010. Lengo la mkutano huo lilikuwa kujadili Rasimu ya Awali (*Inception Report*) ya Mtaalam Mshauri kuhusu tathmini ya kimkakati iliyoandaliwa. Pamoja na masuala mengine, mkutano huo uliazimia kwamba, mtaalam huyo azingatie muda wa kukamilisha tathmini ya kimkakati husika kulingana na mkataba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nchi yetu imebahatika kuwa na rasilimali nyingi za maji ingawa rasilimali hizo hazipatikani kwa uwiano ulio sawa katika maeneo yote. Rasilimali za maji zilizopo ni pamoja na Maziwa Makuu ya Victoria, Nyasa, Rukwa na Tanganyika na Mito ya Rufiji, Kilombero, Ruvuma, Ruhuhu, Malagarasi, Pangani, Ruvu, Wami, Mara na Kagera. Rasilimali hizo zinakadiriwa kuwa na kilomita za ujazo 89. Nchi yetu pia inakadiriwa kuwa na hifadhi ya rasilimali za maji chini ya ardhi zipatazo kilomita za ujazo 40.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na kuwa na rasilimali nyingi za maji, maeneo mengi ya nchi yetu yameendelea kuwa na uhaba wa maji yanayofaa kwa matumizi mbalimbali. Uhaba huo unasababishwa na mabadiliko ya tabia nchi ambayo kwa kiwango kikubwa yameathiri mwenendo wa upatikanaji wa mvua za kutosha, uchafuzi wa vyanzo vya maji unaosababishwa na shughuli za kibinadamu kwenye vyanzo na ongezeko la watu na matumizi ya maji kwa shughuli za kiuchumi na kijamii. Takwimu zinaonesha kuwa, pamoja na nchi yetu kuwa na maji mengi kwa sasa, mahitaji ya maji nchini yanaongezeka na hivyo kiwango cha maji yaliyopo kwa mtu kwa mwaka kimeendelea kupungua kutoka wastani wa mita za ujazo 2,700 mwaka 1999 hadi kufikia mita za ujazo 2,150 mwaka 2010.

Mheshimiwa Mwenyekiti, inakadiriwa kuwa, kiwango cha maji kwa mtu kitaendelea kushuka hadi kufikia mita za ujazo 1,950 kwa mtu kwa mwaka ifikapo mwaka 2015 na mita za ujazo 1,500 kwa mtu kwa mwaka ifikapo mwaka 2025, kiwango ambacho kikifikiwa nchi inatambulika kama yenye uhaba wa maji *(water stress).* Serikali itaendelea kuhakikisha rasilimali hizo zinatunzwa na kuendelezwa kwa njia endelevu kwa manufaa ya kizazi cha sasa na vizazi vijavyo kwa kuzingatia mfumo wa mabonde. Yapo Mabonde 9 nchini ambayo ni Pangani, Wami/Ruvu, Rufiji, Ruvuma na Mito ya Pwani ya Kusini, Ziwa Nyasa, Bonde la Kati, Ziwa Rukwa, Ziwa Tanganyika na Ziwa Victoria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, yapo matatizo yanayosababisha upungufu wa maji katika baadhi ya maeneo, ikiwa ni pamoja na yafuatayo:-

(i) ukame wa mara kwa mara unaotokana na mabadiliko ya tabianchi;

(ii) matumizi ya maji yasiyozingatia ufanisi;

(iii) upangaji wa matumizi ya maji bila ya kuoanisha mipango ya sekta nyingine;

(iv) uharibifu wa mazingira na uchafuzi wa vyanzo vya majii unaotokana na kukua kwa shughuli za kijamii na kiuchumi; na

(v) gharama kubwa za uwekezaji katika ujenzi wa miundombinu ya uvunaji na usambazaji wa maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mabadiliko ya tabianchi yana athari kubwa kwa vyanzo vya maji. Kutokana na tathmini iliyofanywa hapa nchini, katika miaka 60 iliyopita, kumekuwepo na ongezeko la joto la wastani wa nyuzi joto moja ikiambatana na uhaba wa mvua na kupungua kwa kina cha maji katika maziwa na mabwawa. Tathmini hiyo pia, inaonesha kwamba, kati ya miaka 50 hadi 100 ijayo, kutakuwa na ongezeko la joto la wastani wa nyuzi joto moja hadi tatu katika nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na mabadiliko hayo, ni muhimu tuendelee kuliweka suala hili katika mipango yetu, ili tubaini njia za kukabiliana na mabadiliko hayo. Inatupasa tuainishe suala la mabadiliko ya tabianchi katika mipango ya Ofisi za Mabonde na utekelezaji wake, ikiwa ni pamoja na kutekeleza yafuatayo:-

(i) kuimarisha ukusanyaji wa takwimu zinazohusu rasilimali za maji na mabadiliko ya tabianchi;

(ii) kuendeleza mafunzo ya wataalam ili kuongeza uelewa na weledi kuhusu mabadiliko ya tabianchi;

(iii) kushirikisha wananchi ili kujifunza na kuimarisha utaalam wa jadi (*Indigenous knowledge*) katika kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi; na

(iv) kushirikiana na taasisi za kiserikali na zisizo za kiserikali zinazofanya utafiti kuhusu mabadiliko ya tabianchi kwa lengo la kufanya utafiti wa pamoja na kutathmini matokeo ya tafiti mbalimbali ili kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2009/2010, Serikali iliendelea kuboresha huduma za maji vijijini. Uboreshaji huo ulihusu ujenzi, upanuzi na ukarabati wa miundombinu ya miradi ya maji vijijini ikiwa ni pamoja na kujenga miradi ya visima virefu na vifupi na kujenga mabwawa katika maeneo kame. Wizara imetekeleza hayo kwa kushirikisha wananchi katika hatua mbalimbali ikiwa ni pamoja na kupanga, kujenga, kusimamia na kuendesha miradi ya maji. Kutokana na juhudi hizo, idadi ya wananchi vijijini wanaopata huduma ya majisafi na salama imeongezeka kutoka asilimia 53.7 mwaka 2005 hadi asilimia 58.7 ilipofika Desemba 2009.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kuboresha huduma za majisafi na uondoaji majitaka mijini, kwa mwaka 2009/2010, Wizara yangu, kupitia Mamlaka za Maji Mijini iliendelea na ujenzi, ukarabati na upanuzi wa mitandao ya majisafi katika miji mikuu ya mikoa, miji mikuu ya wilaya, miji midogo na miradi ya maji ya kitaifa. Kutokana na juhudi hizo, kiwango cha idadi ya wakazi wanaopata huduma ya maji katika miji mikuu ya mikoa 19 kimeongezeka kutoka wastani wa asilimia 78 mwaka 2005 hadi kufikia asilimia 84 mwezi Aprili 2010. Utoaji wa huduma ya maji katika miji mikuu ya wilaya, miji midogo na maeneo yanayohudumiwa na miradi ya kitaifa kwa sasa ni wastani wa asilimia 53.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa Jiji la Dar es Salaam na Miji ya Kibaha na Bagamoyo inayohudumiwa na DAWASA, kiwango cha utoaji wa huduma ya majisafi ni kati ya asilimia 50 na 60 kwa wastani wa saa 7 kwa siku. Kiwango hicho ni kidogo ikilinganishwa na miji mingine kutokana na kukua kwa kasi kwa jiji la Dar es Salaam, ikiwa ni pamoja na ongezeko kubwa la watu ambalo linakadiriwa kuwa asilimia 8 kwa mwaka tofauti na wastani wa asilimia 4.5 mijini kitaifa. Ili kubaini kiwango halisi cha sasa cha utoaji wa huduma, zoezi la uchunguzi linategemea kuanza Julai 2010.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nchi yetu inazo rasilimali nyingi ambazo ni pamoja na ardhi na maji zinazoweza kutumiwa katika kuongeza uzalishaji wa mazao ya kilimo. Mpango Kabambe wa Taifa wa Umwagiliaji wa Mwaka 2002, ulibaini eneo la jumla ya hekta milioni 29.4 zinazoweza kuendelezwa kwa kilimo cha umwagiliaji. Kati ya eneo hilo, hekta milioni 2.3 zina uwezekano mkubwa wa kuendelezwa *(high irrigation potential),* hekta milioni 4.8 uwezekano wa kati (*medium irrigation potential*) na hekta milioni 22.3 zina uwezekano wa chini wa kuendelezwa *(low irrigation potential)*. Vigezo na viashiria vya tathmini hiyo vimebadilika. Tathmini mpya inafanyika kubaini maeneo mapya ya uwezekano wa maeneo ya umwagiliaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mafanikio yaliyopatikana kutokana na uboreshaji wa miundombinu ya umwagiliaji katika skimu za umwagiliaji ni pamoja na:-

(i) kuongezaka kwa uzalishaji wa mazao kutoka viwango vya chini kabla ya uboreshaji na kuwa na viwango vya juu baada ya kuboreshwa kwa skimu. Kwa mfano, uzalishaji wa mazao mbalimbali umeongezeka kwa wastani wa tani kwa hekta kama ifuatavyo; mpunga kutoka tani 2 hadi 5 katika skimu ya Igomelo (Mbarali), nyanya kutoka tani 5 hadi 18 katika skimu ya Igomelo (Mbarali), mahindi kutoka tani 1.5 hadi 4 katika skimu ya Mombo (Korogwe), na vitunguu kutoka tani 13 hadi 26 katika skimu ya Mang'ola (Karatu);

(ii) kuongezeka kwa misimu ya kilimo kutoka msimu mmoja hadi misimu miwili au mitatu kwa mwaka; na

(iii) kuongezeka kwa kipato na kuboreshwa kwa hali ya maisha ya wakulima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kipindi cha mwaka 2005 hadi Juni, 2010 eneo la umwagiliaji lililoendelezwa limeongezeka kutoka hekta 264,388 hadi kufikia hekta 331,490. Eneo hilo limehusisha jumla ya skimu 244. Eneo lililoendelezwa hadi sasa linahusisha hekta 276,261 za mashamba ya wakulima wadogo na hekta 55,229 za mashamba ya wakulima wakubwa wa mazao ya biashara ya chai, kahawa, miwa, maua, mbogamboga na mpunga.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara yangu itaendelea kuhimiza uendelezaji wa miundombinu ya umwagiliaji katika mashamba ya wakulima wadogo, wa kati na wakubwa. Hii itachangia katika kuongeza uzalishaji wa mazao na uhakika na usalama wa chakula na kupunguza umaskini kama inavyosisitizwa katika Mkakati wa Kukuza Uchumi na Kupunguza Umaskini Tanzania (MKUKUTA). Miundombinu hiyo ni pamoja na ujenzi wa mabwawa, matumizi ya teknolojia ya kuvuna maji ya mvua kwa ajili ya umwagiliaji hasa kwenye maeneo kame, matumizi ya maji chini ya ardhi kwa kuchimba visima virefu na vifupi ili kuongeza upatikanaji wa maji kwa ajili ya umwagiliaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sekta za maji na umwagiliaji zinakabiliwa na changamoto mbalimbali ambazo zimechangia kutokufikia kikamilifu malengo yaliyowekwa. Changamoto hizo ni:-

(i) mabadiliko ya tabianchi yanayosababisha ukame, mafuriko na kutotabirika kwa mtawanyiko wa mvua;

(ii) uhaba wa wataalam na vitendea kazi katika ngazi ya Halmashauri;

(iii) ushiriki mdogo wa sekta binafsi katika uendelezaji, uwekezaji, usimamizi na uendeshaji wa skimu za umwagiliaji na miradi ya maji;

(iv) ufinyu wa bajeti katika uwekezaji na uendelezaji wa sekta za maji na umwagiliaji; na

(v) kuchelewa kupata fedha zilizokasimiwa hali inayosababisha kuchelewa kwa utekelezaji wa miradi na wakati mwingine kuangukia katika kipindi cha mvua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mapitio ya Utekelezaji wa Bajeti ya Mwaka 2009/2010 na Mpango wa Mwaka 2010/2011: Sehemu hii inahusu utekelezaji wa mpango wa mwaka 2009/2010 na malengo ya mwaka 2010/2011 katika maeneo ya rasilimali za maji, huduma ya maji na usafi wa mazingira vijijini, huduma ya majisafi na uondoaji wa majitaka mijini, umwagiliaji na huduma za ufundi, na masuala mtambuka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara yangu iliendelea kuimarisha usimamizi wa rasilimali za maji kwa madhumuni ya kuhakikisha rasilimali hizo katika kila bonde, zinatumika kwa uwiano kwa sekta zote na kwa njia endelevu. Miongoni mwa hatua zilizochukuliwa ni kuchunguza na kutathmini rasilimali za maji nchini; kuimarisha ufuatiliaji wa rasilimali za maji; kuimarisha Ofisi za Mabonde ya Maji ili zisimamie kikamilifu rasilimali hizo; kuandaa mipango shirikishi ya usimamizi na uendelezaji wa rasilimali za maji katika Mabonde; na kuweka misingi ya kuwezesha ujenzi wa miundombinu ya kuhifadhi rasilimali za maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2009/2010, Wizara iliendelea kusimamia utekelezaji wa Programu ya Usimamizi wa Rasilimali za Maji kwa kutekeleza kazi katika maeneo yafuatayo: ufuatiliaji wa mwenendo wa rasilimali za maji, utafutaji wa vyanzo vipya vya maji na uchimbaji wa visima, matumizi bora ya rasilimali za maji, utayarishaji wa mipango shirikishi ya kusimamia na kuendeleza rasilimali za maji, kuimarisha Ofisi za Maji za Mabonde, kukusanya maduhuli, kudhibiti migogoro baina ya watumia maji, na usimamizi wa rasilimali za majishirikishi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara yangu huchunguza wingi na ubora wa rasilimali za maji juu na chini ya ardhi kwa kutumia mtandao wa vituo vya kufuatilia mwenendo wa rasilimali hizo. Takwimu na taarifa zinazopatikana kutoka vituo hivyo, huchambuliwa na matokeo yake huiwezesha Serikali kuchukua hatua za tahadhari dhidi ya majanga ya ukame na mafuriko na hutumika katika kubuni na kusanifu miradi mbalimbali ikiwa ni pamoja na ujenzi wa miradi ya maji. Katika mwaka 2009/2010, Wizara yangu ilinunua vifaa vya kukusanya takwimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2009/2010, Wizara yangu imenunua jumla ya vifaa 3,114 vya kupimia maji (*water level loggers, staff gauges, figure plates, remote data transfer instruments, field computers, portable contact gauge dippers, acoustic doppler profile instruments for discharge measurement, portable contact gauges),* mitumbwi na injini zake na suti ya kupimia maji mtoni *(wading suits)* kwa ajili ya Ofisi za Mabonde ya Maji. Vilevile, Wizara imekamilisha upembuzi yakinifu na michoro kwa ajili ya ujenzi na ukarabati wa vituo 292 vinavyohitajika ili kukusanya kikamilifu takwimu za kihaidrolojia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2009/2010, Wizara yangu imeendelea na ujenzi na ukarabati wa vituo 23 vya kupima wingi wa maji katika mito na mabwawa katika Mabonde ya Pangani (1), Wami/Ruvu (2), Rufiji (3), Ruvuma (2), Ziwa Rukwa (2) na Ziwa Victoria (13). Vituo 6 vimejengwa na kukamilika katika Mabonde ya Ruvuma (2), Ziwa Nyasa (1), Ziwa Tanganyika (2) na Ziwa Victoria (1) chini ya Mradi wa

*Southern African Development Community – Hydrological Cycle Observing System (SADC HYCOS).*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mwaka 2010/2011, Wizara yangu itaendelea kuimarisha mtandao wa kufuatilia mwenendo wa rasilimali za maji juu na chini ya ardhi kwa kujenga na kukarabati vituo ikiwa ni pamoja na kufunga vifaa vya kupimia wingi na ubora wa maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maji chini ya ardhi ni chanzo cha uhakika cha kuwapatia wananchi maji hasa katika maeneo kame. Ili kuboresha huduma za maji nchini, Wizara yangu kupitia Ofisi za Mabonde ya Maji, katika mwaka 2009/2010, iliendelea na utafiti wa kubaini maeneo yanayofaa kuchimba visima vya maji. Maeneo yaliyobainishwa ni 796 kama ifuatavyo: Bonde la Pangani (117), Bonde la Wami/Ruvu (30), Bonde la Rufiji (33), Bonde la Ruvuma (147), Bonde la Kati (168), Bonde la Ziwa Rukwa (134), Bonde la Ziwa Nyasa (11), Bonde la Ziwa Tanganyika (63) na Bonde la Ziwa Victoria (93). Katika mwaka 2010/2011, Wizara itachunguza na kubaini maeneo 800 yenye maji chini ya ardhi kwa ajili ya kuchimba visima virefu vya maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara yangu ina jukumu la kuratibu uchimbaji wa visima vya maji unaotekelezwa na Wakala wa Uchimbaji Visima na Ujenzi wa Mabwawa na kampuni binafsi. Lengo la uratibu huo ni kuhakikisha kwamba, taratibu za kitaalam zilizowekwa zinafuatwa na udhibiti wa uchimbaji holela wa visima unaoweza kusababisha athari za kiafya na uharibifu wa mazingira unatekelezwa. Kwa mwaka 2009/2010, Wizara ilihakiki uchimbaji na kusajili visima 1,043. Kati ya visima hivyo, 267 vilichimbwa na Wakala wa Uchimbaji Visima na Ujenzi wa Mabwawa na 776 vilichimbwa na kampuni binafsi . Kampuni binafsi 19 za uchimbaji wa visima zilisajiliwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2010/2011, Wizara yangu itaendelea kuratibu uchimbaji wa visima vya maji kwa kuimarisha usimamizi na udhibiti kupitia Ofisi za Mabonde ya Maji. Wizara itaendelea kutoa elimu kwa wadau kuhusu taratibu zinazotakiwa kufuatwa katika uchimbaji wa visima ikiwa ni pamoja na kuwa na hati za haki ya kutumia maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kuimarisha huduma ya maji safi na salama kwenye maeneo kame, katika mwaka 2009/2010, Wizara yangu kwa kushirikiana na Serikali ya Misri, ilikamilisha uchimbaji wa visima 39 ambapo visima 30 vilikuwa na maji. Visima hivyo vilichimbwa katika Wilaya za Same (6), Kiteto (8), Maswa (7), Magu (6), Bunda (6) na Tarime (6). Visima ambavyo vina maji vipo katika maeneo yafuatayo; vitano maeneo ya Majengo, Karamba, Hedaru, Mwembe-Baraza na Majevu (Same), vitano maeneo ya Enguseroengine, Partimbo, Makami, Mbigili na Osteti (Kiteto), vinne vimechimbwa kwenye maeneo ya Sangamwampuya, Shinyangamwenge, Mandangong'ombe na Mbaragane (Maswa), vitano katika maeneo ya Nyashimba, Ilungu, Mayenga, Kinango na Manala (Magu), vitano katika maeneo ya Igundu, Kunzungu, Namalama, Kiwasi na Bitaraguru (Bunda) na vitano katika maeneo ya Kisumwa, Rebu (2), Magene na Gamasara (Tarime). Visima vyote 30 vilivyopata maji vimewekewa

pampu. Visima 26 vimewekewa pampu za kuendeshwa kwa umeme na kuwekewa jenereta na visima vinne vimewekewa pampu za mkono.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mkataba wa kuendelea na hatua ya pili ya Mradi huo, ulitiwa saini mwezi Desemba 2009, ambapo jumla ya visima 70 vitachimbwa katika maeneo kame kwa mwaka 2010/2011. Maeneo hayo ni Shishiyu, Mwabulimbu, Mwang'honoli, Kadoto, Mwamanege, Mwabomba na Sangamwalugesha (Maswa); Sunzula, Kabale, Lagangabilili, Gambasingu, Mwanunui, Nanga, Bumera, Nkoma, Laini, Kilulu, Nkololo,Kidinda (Bariadi); Lutale, Kitumba, Shighala, Ng'hanya, Mwamigongwa, Lwangwe, Mwakiloba, Mwamgoba, Badugu na Kinango (Magu); Nyasincha na Kibaso (Tarime); Minigo, Omoche, Nyamasanda na Nyambori (Rorya); Karukekere, Buzimbwe, Buguma, Nyangere, Kitaramanka, Nyang'aranga na Marambeka (Bunda); Namelock, Ilera, Chapakazi, Kijungu, Loitepasi, Dongo, Engongangare na Katikati (Kiteto); Mwembe, Makanya, Mgwasi, Same mjini, Mvure, Kongei na Mheza (Same); na Mwanga Mjini (Mwanga).

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2009/2010, Wizara yangu iliendelea kusimamia matumizi bora ya rasilimali za maji kwa kutoa hati za haki ya kutumia maji 29. Lengo ni kuimarisha matumizi endelevu na kuhakikisha kuwa rasilimali za maji zinagawanywa kwa uwiano kulingana na mahitaji ya sekta mbalimbali za kiuchumi na kijamii. Jumla ya matoleo 939 yalikaguliwa kulingana na masharti ya haki ya kutumia maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2010/2011, Wizara yangu kupitia Ofisi na Bodi za Maji za Mabonde, itaendelea kutoa elimu kwa wadau juu ya umuhimu wa kuwa na hati za haki ya kutumia maji na kuendelea kubaini matoleo mengine zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2009/2010, Wizara yangu iliendelea na taratibu za kutayarisha Mipango Shirikishi ya Usimamizi na Uendelezaji wa Rasilimali za Maji katika Mabonde ya Maji kwa awamu tatu. Awamu ya kwanza, inahusisha Bonde la Rufiji na Bonde la Kati, awamu ya pili inahusisha Mabonde ya Ziwa Victoria na Wami/Ruvu na awamu ya tatu inahusisha Mabonde ya Pangani, Ruvuma, Ziwa Nyasa, Ziwa Tanganyika na Ziwa Rukwa. Katika awamu ya kwanza, wataalam washauri wamepatikana na wanaendelea na hatua mbalimbali za utekelezaji. Kwa awamu ya pili, hadidu za rejea za kuwapata wataalam washauri zimeandaliwa. Utekelezaji wake utafanyika chini ya Kamisheni ya Mradi wa Usimamizi wa Mazingira ya Ziwa Victoria kwa Bonde la Ziwa Victoria na Shirika la Misaada la Japan *(JICA)* kwa Bonde la Wami/Ruvu. Kwa awamu ya tatu, tathmini kwa ajili ya kuwapata wataalam washauri imefanyika. Katika mwaka 2010/2011, Wizara yangu itaendelea na kazi ya kuwasimamia wataalam washauri ili kupata mipango shirikishi inayokidhi matarajio yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2009/2010, Wizara yangu imeendelea kuimarisha Ofisi na Bodi za Mabonde kwa kuzijengea uwezo ili ziweze kuchangia kukua kwa sekta za maji na umwagiliaji. Hatua zilizochukuliwa ni pamoja na kutoa mafunzo kwa watumishi, kuajiri wataalam na kuzipatia nyenzo na vifaa vya kazi kama ifuatavyo:-

(i) Wataalam wapya 100 wa fani mbalimbali wameajiriwa na kupelekwa katika Ofisi za Mabonde. Wataalam hao ni wahaidrolojia (10), wahaidrojiolojia (22), wahandisi wa mazingira (7), maafisa maendeleo ya jamii (13), maafisa wa ugavi (8), mafundi sanifu wa haidrolojia (16) na mafundi sanifu wa haidrojiolojia (24);

(ii) Vifaa vya ofisi, mawasiliano na usafiri ikiwa ni pamoja na kompyuta (42), *Scanners (*15*), power point projectors (*7*), printers (*5*) na digital cameras (*22*),* pikipiki (35) na magari (36) vilipelekwa katika Ofisi za Mabonde ya Maji;

(iii) Wataalam 72 na wajumbe watano wa Bodi ya Maji ya Bonde la Wami/Ruvu walipatiwa mafunzo juu ya utekelezaji wa Programu ya Maendeleo ya Sekta ya Maji;

(iv) Wataalam 201 walipatiwa mafunzo katika nyanja za uandaaji wa mipango shirikishi ya usimamizi na uendelezaji wa rasilimali za maji (20); uandaaji wa taarifa za kijiografia kwa kutumia mtandao wa kompyuta (18); uendeshaji wa benki ya takwimu (6); usuluhishi wa migogoro katika matumizi ya maji na mbinu za kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi (16); Sheria za kazi (1); usimamizi wa matumizi ya fedha za umma (48); mafunzo ya sheria mpya ya usimamizi wa rasilimali za maji (65); na matumizi ya programu mbalimbali za kompyuta (27); na

(v) Wizara iliviimarisha vitengo vya ununuzi katika Ofisi za Mabonde ya maji kwa kuvipatia wataalam wa ugavi wanane. Vitengo hivyo vitarahisisha taratibu za ununuzi katika ofisi hizo na hivyo kusaidia katika jitihada za kuzifanya Ofisi za Mabonde zijitegemee. Wataalam hao wamepelekwa katika Ofisi za Mabonde ya Pangani (1), Wami/Ruvu (1), Rufiji (1), Ziwa Victoria (1), Ruvuma (1), Ziwa Rukwa (1), Ziwa Tanganyika (1) na Bonde la Kati (1). Kwa mwaka 2010/2011, Wizara yangu itaendelea kuziimarisha Ofisi za Mabonde kwa kuzipatia wataalam, vitendea kazi na mafunzo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2009/2010, Wizara yangu iliendelea na usanifu wa majengo ya ofisi na maabara za maji katika Mabonde ya Maji ya Rufiji, Ruvuma, Ziwa Nyasa, Ziwa Rukwa, Pangani na Wami/Ruvu. Usanifu wa jengo la Ofisi ya Bonde la Ziwa Nyasa umekamilika na tathmini ya kumpata mkandarasi imekamilika. Kwa Mabonde mengine, usanifu utakamilika ifikapo mwisho wa mwezi Juni 2010. Kwa mwaka 2010/2011, Wizara yangu itaanza ujenzi na ukarabati wa Ofisi za Mabonde.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka 2009/2010, Wizara yangu iliendelea kuimarisha usimamizi shirikishi wa rasilimali za maji unaolenga kupunguza migogoro baina ya watumiaji maji na kuongeza ukusanyaji wa ada za matumizi ya maji. Hatua zilizochukuliwa ni kubaini maeneo ya vyanzo vya maji ya mito *(catchments)* na mabonde madogo ya vyanzo vya maji ya mito *(sub-catchments).* Utambuzi wa maeneo hayo ni hatua muhimu ili kuanzisha kamati za mabonde madogo *(Sub-catchment Committees)* na vyama vya watumiaji maji *(Water Users Association)* katika mabonde yote ya maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara yangu iliendelea na zoezi la kutambua vyanzo vipya vya maji katika mabonde ya maji vikiwemo vijito, chemichemi na visima. Katika

mwaka 2009/2010, jumla ya vyanzo 41 vilitambuliwa katika Mabonde ya Pangani (8), Wami/Ruvu (3), Rufiji (5), Ruvuma (5), Ziwa Nyasa (4), Bonde la Kati (4), Ziwa Rukwa (6), Ziwa Tanganyika (2) na Ziwa Victoria (4). Maeneo ya mabonde madogo 86 yametambuliwa katika mabonde ya Pangani (12), Wami/Ruvu (7), Rufiji (18), Ruvuma (10), Ziwa Nyasa (10), Ziwa Rukwa (15), Ziwa Tanganyika (4) na Ziwa Victoria (10).

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2009/2010, Wizara yangu ilianzisha timu 8 za uwezeshaji (*catchment and district facilitation teams*), kutoa elimu ya uundaji wa vikundi vya watumia maji, pamoja na vyama vya watumia maji katika Mabonde ya Maji ya Rufiji (4), Wami/Ruvu (3) na Ziwa Nyasa (1). Jumla ya vyama vya watumiaji maji *(Water Users Association)* 39 vimeundwa kwenye Mabonde ya Pangani (4), Wami/Ruvu (7), Rufiji (24), Ruvuma (1) na Ziwa Victoria (3) ili kuimarisha usimamizi shirikishi wa rasilimali za maji unaolenga kupunguza migogoro baina ya watumia maji na kurahisisha ukusanyaji wa ada za matumizi ya maji. Vilevile jumla ya vikundi vya watumia maji 168 vilianzishwa katika Mabonde ya Ruvuma (61), Ziwa Tanganyika (34), Ziwa Victoria (29) na Bonde la Kati (44). Kwa mwaka 2010/2011, Wizara itaanzisha timu 10 za kutoa elimu katika ngazi za wilaya na mabonde madogo na kuimarisha nyingine 23 zilizopo. Kulingana na Sheria ya Usimamizi wa Rasilimali za Maji, Sheria Na. 11 ya Mwaka 2009, Ofisi za Mabonde zitaanzisha na kuimarisha vikundi na vyama vya watumiaji maji katika Mabonde yote 9 ikiwa ni pamoja na kuvisajili kisheria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mwaka 2010/2011, Wizara yangu itaendelea kubaini maeneo yanayofaa kutengwa ili kuyakinga na uchafuzi wa mazingira na kutoa elimu ya kusaidia uanzishwaji wa kamati za mabonde madogo, vikundi na jumuiya za watumia maji katika Mabonde yote 9 ya maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara yangu iliendelea kuzihimiza Bodi za Maji za Mabonde kuweka mikakati ya kuimarisha ukusanyaji wa maduhuli kutoka kwa watumia maji na kuyatumia mapato hayo kwa malengo yaliyokusudiwa kulingana na taratibu zinazotawala matumizi ya fedha za umma. Lengo ni kuziwezesha Ofisi za Maji za Mabonde kujitegemea katika uendeshaji. Makusanyo ya maduhuli yamekuwa yakiongezeka mwaka hadi mwaka kuanzia 2005/2006 hadi 2009/2010. Kwa mfano, makusanyo yalikuwa shilingi 717,731,424 mwaka 2005/2006, shilingi 834,673,731 mwaka 2006/2007, shilingi 1,691,720,349 mwaka 2007/2008 na shilingi 1,040,710,592 mwaka 2008/2009. Ilipofika Machi 2010, jumla ya shilingi 806,301,151 zilikuwa zimekusanywa kati ya lengo la shilingi 1,202,461,000.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2010/2011, Ofisi za Mabonde zinakadiria kukusanya kiasi cha shilingi 1,198,690,517 kutokana na ada za matumizi ya maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka 2009/2010, Wizara yangu ilishughulikia migogoro 15 baina ya watumia maji kutoka Ofisi ya Bonde la Kati (8) na Mabonde ya Pangani (2) na Wami/Ruvu (5). Kati ya migogoro hiyo, 12 ilitatuliwa na kusuluhishwa. Migogoro hiyo ilitokana na ushindani wa matumizi ya rasilimali za maji baina ya watumiaji katika mito, maziwa, mabwawa na vyanzo vingine vya maji. Ili kupunguza

migogoro hiyo inayojitokeza mara kwa mara, Ofisi za Maji za Mabonde zimeelekezwa na Wizara kutoa elimu kwa wananchi, kuhamasisha wananchi kuunda kamati za pamoja za kusuluhisha migogoro katika maeneo yao, kuhamasisha uundaji wa vyama vya watumiaji maji na pale inapobidi, kutumia vyombo vya sheria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, usimamizi wa rasilimali za majishirikishi ni moja ya maeneo muhimu katika ushirikiano wa kimataifa. Lengo ni kuhakikisha kuwa rasilimali hizo zinatumika kwa njia endelevu na kwa manufaa ya nchi shiriki. Wizara yangu imeendelea kushirikiana na nchi zilizo katika Mabonde hayo kwa kuunda vyombo vya pamoja ili kusimamia matumizi endelevu ya rasilimali hizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nchi zinazoshirikiana katika Bonde la Mto Nile ni Burundi, Eritrea, Ethiopia, Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC), Kenya, Misri, Rwanda, Sudan, Tanzania na Uganda. Nchi hizo zinakabiliwa na changamoto za maendeleo ya kijamii na kiuchumi ambazo ni ongezeko la watu, uharibifu wa mazingira na katika baadhi ya nchi, umaskini uliokithiri. Hali hiyo imeleta msukumo kwa kila nchi kubuni mikakati ya kukabiliana na changamoto hizo kwa kutumia maji ya Mto Nile katika kuendeleza kilimo cha umwagiliaji, kuzalisha umeme, kuendeleza uvuvi na kuhakikisha wananchi wake wanapata maji ya kutosha kwa matumizi ya nyumbani na viwandani. Ili kuwepo kwa matumizi endelevu ya rasilimali hiyo, nchi hizo zimeunda vyombo mbalimbali vya ushirikiano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushirikiano wa Nchi za Bonde la Mto Nile ulianza katika Mradi wa *Hydromet Survey* uliotekelezwa kuanzia mwaka 1967 hadi 1992 kwa kushirikisha Nchi za Burundi, Zaire (Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo), Misri, Kenya, Rwanda, Sudan, Tanzania na Uganda. Ethiopia ilikuwa mtazamaji *(observer).* Mradi huo ulilenga katika kuweka misingi ya ushirikiano katika matumizi endelevu ya maji ya Bonde la Mto Nile.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya Mradi wa *Hydromet Survey* kumalizika na ili kuendeleza jitihada za ushirikiano katika matumizi bora ya maji kwenye Bonde la Mto Nile, Nchi za Zaire (Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo), Misri, Rwanda, Sudan, Tanzania na Uganda mwezi Desemba 1992 zilianzisha Kamati ya Ushirikiano ya Kiufundi ya Kusaidia Maendeleo na Hifadhi ya Mazingira ya Bonde la Mto Nile *(Technical Cooperation for the Promotion of the Development and Environmental Protection of the Nile Basin-TECCONILE).* Burundi, Eritrea, Ethiopia na Kenya zilikuwa watazamaji *(observers)*. Madhumuni ya *TECCONILE* yalikuwa ni kuzisaidia nchi zinazohusika kuweka utaratibu mzuri wa kuendeleza, kutumia na kuhifadhi maji ya Bonde la Mto Nile kwa uwiano endelevu katika Bonde lote na kuwezesha kila nchi kutumia kiwango stahiki *(equitable entitlement).*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwezi Februari 1999, nchi zote katika Bonde kwa kutambua umuhimu wa kushirikiana katika matumizi endelevu ya rasilimali ya maji, zilichukua hatua ya kihistoria ya kuanzisha chombo cha mpito cha usimamizi wa rasilimali hiyo kijulikanacho kama Umoja wa Ushirikiano wa Bonde la Mto Nile *(Nile Basin Initiative - NBI).* Madhumuni makubwa ya Umoja wa Ushirikiano katika Bonde la

Mto Nile ni kufanikisha maendeleo ya kudumu ya kiuchumi na kijamii kwa kutumia na kugawana rasilimali za maji kwa stahili na mlingano pamoja na faida zote zitokanazo na matumizi endelevu ya rasilimali za maji ya Bonde la Mto Nile.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Umoja wa Ushirikiano wa Nchi za Bonde la Mto Nile *(NBI)* umesimamia utekelezaji wa miradi ya maji, mazingira, nishati, kilimo, mafunzo na kujenga uwezo katika Bonde zima. Vilevile, umesimamia utekelezaji wa miradi kama hiyo katika kila nchi chini ya Programu mbili tanzu za Nchi za Maziwa Makuu *(Nile Equatorial Lakes Subsidiary Action Program)* na Nchi za Bonde la Mashariki la Nile *(Eastern Nile Subsidiary Action Program). NBI* pia imeratibu majadiliano ya Mkataba wa Kudumu wa Ushirikiano wa Nchi za Bonde la Mto Nile utakaoanzisha Kamisheni ya Bonde la Mto Nile. Katika Mkutano wa dharura uliofanyika Kinshasa tarehe 22 Mei 2009, Baraza la Mawaziri wa Maji wa Nchi za Bonde la Mto Nile liliamua kuhitimisha majadiliano na kuweka utaratibu wa kusaini Mkataba huo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mkataba wa Ushirikiano umekuwa wazi kwa Nchi Wanachama wa Bonde la Mto Nile kuanza kusaini kuanzia tarehe 14 Mei 2010 mpaka tarehe 13 Mei 2011. Tayari nchi tano za Umoja huo ambazo ni Ethiopia, Tanzania, Uganda, Rwanda na Kenya zimesaini Mkataba utakaoanzisha chombo cha kudumu cha ushirikiano katika Bonde la Mto Nile - Kamisheni ya Bonde la Mto Nile. Burundi na Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo *(DRC)* zinaendelea na utaratibu wa kuweka saini mkataba huo. Misri na Sudan bado zingependa matumizi ya maji ya Mto Nile yawe kama yalivyo sasa na haki zao za sasa zitambuliwe. Maana yake ni kuwataka wanachama wengine watambue mikataba ya mwaka 1929 na 1959. Mikataba hiyo inazipa nchi hizo mbili mgao mkubwa wa maji na haki zaidi kuliko nchi nyingine wanachama. Licha ya msimamo wa nchi hizo, juhudi za mazungumzo zinaendelea kuzishawishi Misri na Sudan kuridhia mkataba huo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mradi wa Usimamizi wa Mazingira ya Ziwa Victoria, Mradi wa Kuhifadhi Mazingira ya Ziwa Victoria Awamu ya Pili ulianza rasmi tarehe 20 Agosti 2009. Mradi unalenga katika kuchangia mafanikio ya dira ya bonde la ziwa yenye dhamira ya kuona *"Jamii inayozunguka Bonde la Ziwa Victoria inaishi maisha bora katika mazingira yaliyo endelevu kuzingatia mgawanyo wa fursa sawa kwa jamii kati ya nchi zote za Jumuiya ya Afrika Mashariki."*

Mheshimiwa Mwenyekiti, madhumuni ya mradi ni kuboresha ushirikiano wa Nchi za Afrika Mashariki katika kusimamia rasilimali zinazozunguka Bonde la Ziwa Victoria kwa manufaa ya pamoja; na kupunguza uharibifu wa mazingira katika maeneo ya mradi ili kuboresha maisha bora ya jamii ambazo hutegemea rasilimali za Ziwa Victoria. Kwa upande wa Tanzania, walengwa katika awamu ya pili ni Halmashauri za Wilaya ya Maswa, Bariadi, Magu, Meatu, Bunda na Kwimba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa Tanzania, kuanzia mwezi Oktoba 2009, mradi umepokea Dola za Marekani 187,969 kutoka vyanzo vya ndani na mwezi Januari 2010, umepokea jumla ya Dola za Marekani 2,779,330 kutoka Benki ya Dunia.

Hadi kufikia tarehe 25 Mei 2010 mradi ulikuwa umetumia jumla ya Dola za Marekani 308,233 (fedha za ndani na nje) katika kutekeleza shughuli zifuatazo:-

(i) kukamilisha uundaji wa timu ya kitaifa ya wataalam ya uendeshaji wa mradi ambayo ilianza kazi rasmi mwezi Septemba 2009;

(ii) kuelimisha wadau na wananchi mbalimbali kuhusu dira, dhima, malengo na shughuli zitakazofanyika kwa kupitia semina, mikutano, kongamano na maonesho;

(iii) kuboresha uwezo wa kitaasisi katika kusimamia rasilimali za maji na uvuvi katika Ziwa Victoria ili kuzijengea uwezo taasisi katika kuhuisha sera, sheria na kanuni zinazosimamia uendelezaji wa bonde la Ziwa Victoria;

(iv) kutoa mafunzo ya ukusanyaji taarifa za awali;

(v) kufuatilia ubora wa maji katika ziwa na takwimu kuwekwa kwenye benki ya takwimu (*Database)* tayari kwa uchambuzi;

(vi) kutayarisha mpango wa utekelezaji wa kazi za Mradi; na

(vii) kuandaa mfumo wa ufuatiliaji, tathmini na usimamizi wa taarifa kwa kutumia mfumo wa kompyuta wa kuandaa taarifa za kijiografia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2009/2010, timu ya kitaifa ya wataalam ya uendeshaji wa mradi imeteuliwa. Timu hiyo inajumuisha mratibu wa mradi, mtaalam wa ufuatiliaji na tathmini, mhasibu, wataalam wa uvuvi, rasilimali za maji, magugu maji, ununuzi, misitu na uhifadhi wa matumizi ya ardhi. Imeanza kazi rasmi mwezi Septemba 2009.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka 2010/2011, Wizara yangu itaendelea na uratibu na utekelezaji wa awamu ya pili ya mradi kulingana na kazi zilizopangwa. Wizara itaendelea kuelimisha umma kuhusu matumizi bora ya ardhi na hifadhi ya mazingira ili kulinda vyanzo vya maji. Wizara itasimamia sheria za maji na mazingira na kuendelea kufuatilia mwenendo wa ubora wa maji ya Ziwa Victoria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2009/2010, Serikali iliendelea na taratibu za kuridhia Mkataba wa Kuanzisha Kamisheni ya Bonde la Mto Zambezi *(Zambezi Watercourse Commission - ZAMCOM*). Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania liliridhia Mkataba huo tarehe 8 Februari 2010. Taarifa rasmi ya nchi kuridhia imewasilishwa kwenye Sekretarieti ya Jumuiya ya Maendeleo ya Nchi za Kusini mwa Afrika *(SADC)*, mwezi Mei 2010. Kwa mwaka 2010/2011, Wizara yangu itaendelea na uratibu wa shughuli za Kamisheni ya Pamoja ya Bonde la Mto Zambezi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Bonde la Mto Ruvuma; Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania liliridhia Mkataba wa kuanzisha Kamisheni ya Pamoja ya Maji

kati ya Tanzania na Msumbiji mwezi Novemba 2009. Sekretarieti ya *SADC* tayari imejulishwa rasmi kuhusu Bunge letu Tukufu kuridhia Mkataba huo. Makubaliano hayo ni utekelezaji wa Itifaki ya *SADC* kuhusu Majishirikishi *(Revised SADC Protocol on Shared Watercourses).* Kwa mwaka 2010/2011, Wizara yangu itaendelea na uratibu wa shughuli za Kamisheni ya Pamoja ya Maji kati ya Tanzania na Msumbiji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Programu ya Maendeleo ya Bonde la Mto Songwe; Mto Songwe una tabia ya kuhama wakati wa mafuriko katika ukanda wa chini wa tambarare unapoelekea kuingia Ziwa Nyasa. Hali hiyo huathiri karibu hekta 15,000 za mazao mbalimbali pamoja na maisha na mali za wananchi wanaoishi kwenye maeneo tambarare.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kukabiliana na kuhama kwa Mto Songwe na athari zitokanazo na tatizo hilo, Serikali ya Tanzania na Serikali ya Malawi, ziliamua kufanya uchunguzi utakaowezesha kutekeleza mradi wa kudhibiti kingo za mto huo. Matokeo ya uchunguzi huo yameziwezesha Serikali hizo mbili kuwa na Programu ya Maendeleo ya Bonde la Mto Songwe yenye miradi mitano ifuatayo ambayo inahitaji kufanyiwa usanifu wa kina:-

(i) uendelezaji na usimamizi wa rasilimali za maji;

(ii) uendelezaji wa miundombinu;

(iii) uendelezaji na usimamizi wa rasilimali ardhi;

(iv) udhibiti wa mazingira; na

(v) uendelezaji wa taasisi zitakazosimamia utekelezaji na uendeshaji wa programu hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, usanifu wa kina wa miradi husika utachukua miezi 32 na utagharimu Euro 5,779,515. Kati ya hizo Euro 1,004,220 sawa na asilimia 18 zitachangiwa na Tanzania na Malawi (Tanzania Euro 596,610, Malawi Euro 407,610). Kiasi cha Euro 4,775,295 sawa na asilimia 82 ya fedha zote zinazohitajika kitachangiwa na Benki ya Maendeleo ya Afrika *(AfDB).* Tanzania na Malawi zimekubaliana kuwa Makao Makuu ya Programu yatakuwa Kyela. Katika mchango wake, Tanzania itatoa ofisi na vifaa vya ofisi vya gharama ya Euro 189,000.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukarabati wa OFisi ya Programu umekamilika na Serikali inaendelea na mchakato wa kujenga ofisi mpya. *AfDB* imepitia na kuridhia makubaliano ya ushirikiano *(Memorandum of Understanding - MoU)* kati ya Tanzania na Malawi ambao unatakiwa kusainiwa na Serikali hizi mbili kama sehemu ya mchakato wa Benki kuingia mkataba wa kutoa fedha (*Grant Agreement*). Bodi ya *AfDB* imeridhia awamu hii ya programu tarehe 25 Mei 2010 na mkataba (*Grant Agreement*) unaandaliwa. Baada ya usanifu, ujenzi wa miradi utachukua miaka 10 kwa gharama ya Dola za Marekani milioni 400. Uratibu wa ushiriki katika Programu ya Maendeleo ya Bonde la

Mto Songwe umehamishiwa Wizara ya Maji na Umwagiliaji kutoka Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi. Kwa mwaka 2010/2011, Wizara itakamilisha ujenzi wa ofisi mpya Kyela na itaendelea kushiriki katika uratibu wa miradi itakayotekelezwa chini ya Programu ya Maendeleo ya Mto Songwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hatua mbalimbali zimeendelea kuchukuliwa ili kudhibiti uchafuzi wa vyanzo vya maji katika maeneo yote ya Mabonde. Ukaguzi wa watumiaji maji wenye uwezekano mkubwa wa kuchafua vyanzo vya maji umeendelea kufanyika katika viwanda, migodi na taasisi mbalimbali. Migodi ya Geita, Buzwagi, North Mara, Resolute, El-hilal, Mwadui na Shanta ilikaguliwa. Wameshauriwa watekeleze vyema mipango ya udhibiti wa uvujaji wa maji kutoka kwenye migodi kwa kuimarisha mabwawa ya majitaka. Hadi sasa sampuli 1,086 za maji zimekusanywa na kupimwa ubora wake. Wahusika wamepewa maelekezo ili kudhibiti uchafuzi katika maeneo yaliyoonekana kuwa na ubora wa maji usiokidhi viwango vinavyokubalika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara yangu imeandaa miongozo itakayotumika kuchagua maeneo maalum ya kuanzisha vituo vya ufuatiliaji wa ubora wa rasilimali za maji juu na chini ya ardhi ili kudhibiti uchafuzi wa vyanzo vya maji. Ofisi za Mabonde yote ya maji ziko katika hatua za kubaini maeneo hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara yangu inaendelea kufanya sensa ya kupata idadi na mahali vilipo visima vilivyochimbwa katika Mabonde. Hadi mwezi Mei 2010 jumla ya visima 1,020 vimehesabiwa. Katika mwaka 2010/11, Wizara yangu itaendelea kukagua matumizi mbalimbali ya maji ili kudhibiti ubora wake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mwaka 2009/2010, Wizara yangu iliendelea na udhibiti wa uchafuzi wa vyanzo vya maji, ambapo jumla ya sampuli 243 kati ya 300 za majitaka kutoka viwandani na mabwawa ya kusafisha majitaka Dar es Salaam, Mwanza, Tanga, Morogoro, Dodoma, Bukoba na Iringa zilichunguzwa kabla ya kutupwa kwenye mazingira. Matokeo yalionesha sampuli 225 sawa na asilimia 92.6 majitaka yake yanasafishwa kufikia viwango vinavyokubalika kwa majitaka hayo kutupwa kwenye mazingira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara yangu ina jukumu la kuhakiki ubora na usafi wa maji kwa lengo la kulinda afya za wananchi. Katika kutimiza azma hiyo, mwaka 2009/2010 Wizara ilipanga kukagua vyanzo vya maji 1,750 ambapo sampuli 3,500 za maji zingekusanywa na kuhakikiwa ubora wake kwa kutumia mtandao wa maabara za maji zilizopo nchini. Ilipofika mwezi Aprili 2010, jumla ya sampuli 3,223 zilikusanywa katika maeneo ya mijini na vijijjni na kuchunguzwa viwango vya kemikali na uwepo wa vijidudu. Kati ya sampuli hizo, 3,043 zilikuwa kwenye viwango vinavyokubalika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maji yanayosambazwa yanapaswa kusafishwa na kutibiwa ili yawe na viwango vinavyokubalika. Dawa za kusafisha na kutibu maji zinatakiwa kuhakikiwa ubora wake. Jumla ya sampuli 29 za dawa zikiwemo 14 aina ya shabu – *Aluminium Sulphate* na 15 aina ya *Calcium Hypochlorite* ambazo hutumika kuua vijidudu katika maji, zilihakikiwa ubora wake. Matokeo yalionesha kuwa dawa hizo zipo

katika viwango vinavyokubalika na ushauri ulitolewa kuhusu matumizi yake. Katika mwaka 2010/2011, Wizara yangu itaendelea kuhakiki ubora na usafi wa maji ili kulinda afya za wananchi na kulinda mazingira. Vyanzo vya maji vitatathminiwa ubora wake na inakadiriwa kupima sampuli 3,500 kutoka vyanzo mbalimbali vitakavyokaguliwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara kila mwaka inashiriki katika zoezi la Kimataifa la kupima uwezo wa kiutendaji wa maabara za maji (*Water Laboratories Performance Evaluation)* hasa katika kutoa takwimu sahihi ikiwa ni pamoja na kukidhi matakwa ya kutambulika kimataifa. Mwaka 2009/2010 maabara nne ambazo ni Maabara Kuu iliyopo Dar es Salaam, Maabara za Iringa, Mwanza na Tanga, zimeshiriki katika zoezi hili chini ya Mpango wa *Global Environmental Monitoring System* (*GEMS/WATER*). Sampuli za zoezi hilo zilipokelewa mwezi Aprili 2010 na zinafanyiwa uchunguzi. Taarifa ya uchunguzi wa viashiria (*parameters*) 40 itatumwa kwa waratibu nchini Marekani mwezi Agosti 2010. Katika mwaka 2010/2011, Wizara yangu itashiriki katika zoezi la aina hii chini ya Mpango wa *Southern African Development Community Measurement Traceability (SADCMET)* linaloratibiwa na Shirika la Maji la Namibia (*NAMWATER)*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwezi Julai 2007 Wizara yangu kwa kushirikiana na TAMISEMI ilianza utekelezaji wa Programu ya Maji na Usafi wa Mazingira Vijijini kwa kutekeleza miradi inayoleta matokeo ya haraka kulingana na mipango na vipaumbele vya kila Halmashauri. Katika mwaka 2009/2010, jumla ya miradi 352 ilijengwa ikihusisha visima virefu na vifupi (259), miradi ya bomba (32), miradi ya uvunaji wa maji ya mvua (42) na chemchemi (19). Vilevile, jumla ya miradi 353 ilikarabatiwa ikihusisha visima virefu/vifupi (281), miradi ya bomba 59, malambo 11, mradi wa uvunaji wa maji ya mvua mmoja na chemchemi moja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2009/2010, utekelezaji wa miradi katika vijiji 10 kwa kila Halmashauri uliendelea. Tarehe 24 Juni 2009 na tarehe 10 Februari 2010 nilitoa taarifa hapa Bungeni kuhusu hatua iliyofikiwa na kila Halmashauri katika utekelezaji. Halmashauri 123 kati ya Halmashauri 132 sasa zimepata ridhaa kutoka Benki ya Dunia kuhusu kusaini mikataba kati yake na wataalam washauri. Halmashauri zote 123 zimeajiri wataalam washauri na wameanza kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa Halmashauri sita za Manispaa ya Kigoma/Ujiji, Kibondo, Kilosa, Morogoro, Manispaa ya Morogoro na Bariadi kampuni zilizokuwa zimeshinda gharama za kufanya kazi zilikuwa za juu kuliko kiwango kinachokubalika. Halmashauri hizo zimetakiwa kuandaa orodha nyingine fupi ya kampuni za wataalam washauri kwa ajili ya kupitishwa kwenye Vikao vya Bodi za Zabuni za Halmashauri ili zipelekwe Benki ya Dunia kupata ridhaa ya kuendelea na hatua inayofuata. Halmashauri hizo zimepitisha orodha kwenye Bodi zao na zimepelekwa Benki ya Dunia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Halmashauri ya Manispaa ya Singida haikupata ridhaa ya Benki ya Dunia kumwajiri mtaalam mshauri kwa kuwa kampuni iliyoidhinishwa na Halmashauri hiyo siyo kampuni ya ushauri katika kazi za kiufundi bali ni Shirika lisilokuwa la Kiserikali *(NGO)*. Halmashauri tayari imepitisha orodha nyingine kwenye

Bodi ya Zabuni na imepelekwa Benki ya Dunia. Halmashauri ya Manispaa ya Musoma imejumuisha vijiji vyake katika Mpango wa Mamlaka ya Majisafi na Majitaka ya Manispaa ya Musoma. Utekelezaji wa miradi katika vijiji hivyo utafanyika kupitia Mamlaka hiyo. Halmashauri ya Simanjiro ilirudia matangazo lakini hakuna wataalam washauri waliojitokeza kuomba kufanya kazi hiyo. Orodha fupi ya wataalam washauri imeandaliwa na kutumwa Benki ya Dunia kwa ajili ya kupata ridhaa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Halmashauri ambazo zimesaini mikataba baina yake na wataalam washauri, wataalam hao wanaendelea na uchunguzi na tathmini ya vyanzo vya maji, usanifu wa miradi ya maji, uhamasishaji wa jamii kuhusu usafi wa mazingira, kuunda vyombo vya watumiaji maji na kuandaa zabuni za ujenzi wa miradi. Hadi mwezi Mei 2010, utekelezaji ulikuwa umefikia hatua mbalimbali. Halmashauri sita za Temeke, Ilala, Rombo, Kiteto, Kisarawe na Mvomero zipo kwenye hatua ya ukusanyaji wa takwimu za awali, utafutaji wa vyanzo vya maji na uchaguzi wa teknolojia inayoafikiwa na wananchi wenyewe na ambayo wataimudu katika kuendesha miradi yake. Halmashauri 12 za Rorya, Chunya, Ileje, Kyela, Mbarali, Mbozi, Rungwe, Bagamoyo, Maswa, Mji wa Babati, Manispaa ya Songea na Jiji la Mbeya zimepokea taarifa za awali *(inception report)* kutoka kwa wataalam washauri ikielezea namna kazi ya usanifu, usimamizi wa ujenzi wa miradi ya maji na uelimishaji wa wananchi itakavyotekelezwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Halmashauri 45 za Meru, Ngorongoro, Njombe, Iringa, Kilolo, Ludewa, Makete, Mufindi, Bukoba, Ngara, Muleba, Biharamulo, Kigoma, Kasulu, Moshi, Mbinga, Tunduru, Kahama, Nzega, Korogwe, Handeni, Bukombe, Meatu, Igunga, Urambo, Sikonge, Tabora, Ulanga, Kilindi, Lushoto, Kilombero, Kwimba, Misungwi, Ukerewe, Sumbawanga, Mji wa Njombe, Mji wa Korogwe, Manispaa ya Dodoma, Manispaa ya Kinondoni, Manispaa ya Moshi, Manispaa ya Bukoba, Manispaa ya Iringa, Manispaa ya Sumbawanga, Manispaa ya Tabora na Jiji la Tanga, wataalam washauri wameandaa taarifa za awali na kuainisha kazi zitakazofanyika *(scoping study).*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Halmashauri 19 za Kondoa, Mpwapwa, Bahi, Chamwino, Tarime, Mafia, Misenyi, Karagwe, Siha, Musoma, Serengeti, Namtumbo, Songea, Nkasi, Mpanda, Mji wa Mpanda, Muheza, Mkinga na Pangani wataalam washauri wameandaa zabuni. Halmashauri zinatangaza zabuni za kuwapata wakandarasi watakaochimba visima vya majaribio na baadaye kuviendeleza kama visima hivyo vitakuwa na maji ya kutosha na yenye ubora unaofaa. Halmashauri 17 zimetangaza zabuni za kuwapata wakandarasi. Halmashauri hizo ni Arusha, Manispaa ya Arusha, Karatu, Longido, Monduli, Kongwa, Mji wa Lindi, Bunda, Manispaa ya Mtwara, Masasi, Jiji la Mwanza, Kibaha, Mji wa Kibaha, Mkuranga, Shinyanga, Manispaa ya Shinyanga na Kishapu. Halmashauri 13 za Chato, Mwanga, Same, Kilwa, Nachingwea, Mbulu, Hanang', Mbeya, Tandahimba, Geita, Magu, Sengerema na Manyoni, zimefanya tathmini ya kuwapata wakandarasi watakaochimba visima vya majaribio.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Halmashauri tisa za Lindi, Liwale, Ruangwa, Nanyumbu, Newala, Mtwara, Rufiji, Iramba na Singida zimeajiri wakandarasi wa

kuchimba visima vya majaribio. Katika Halmashauri za Hai na Babati, wataalam washauri wamefanya usanifu wa miradi ya maji ya mtiririko na kuandaa rasimu ya taarifa za usanifu wa awali *(draft design reports)* pamoja na kuandaa zabuni za kuwatafuta wakandarasi wa kujenga miradi hiyo. Halmashauri hizo tayari zimetangaza zabuni za kuwatafuta wakandarasi wa kujenga miundombinu ya maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2009/2010, Wizara yangu kupitia Wizara ya Fedha na Uchumi ilipeleka jumla ya shilingi bilioni 49.12 kwenye Halmashauri zote kwa ajili ya kuendelea kuzijengea uwezo na kutekeleza miradi kwenye vijiji vilivyoainishwa kwenye Programu ya Maji na Usafi wa Mazingira Vijijini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuanzia mwaka 2010/2011, Halmashauri zinatarajiwa kuanza ujenzi wa miundombinu ya maji kwenye vijiji 10 vya kila Halmashauri. Gharama zinazohitajika katika ujenzi wa miundombinu ya maji, kujenga uwezo wa watekelezaji wa programu, uhamasishaji, kutoa elimu ya usafi binafsi na ya mazingira, usimamiaji, ufuatiliaji na kulipa wataalam washauri kwa ajili ya usimamizi wa wakandarasi wa ujenzi, zinakadiriwa kuwa Dola za Marekani milioni 415.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kuziwezesha Halmashauri na Sekretarieti za Mikoa kutekeleza majukumu yao, Wizara yangu imetoa nyenzo za kufanyia kazi kwa ajili ya Halmashauri na Sekretarieti za Mikoa yote. Mwaka 2009/2010, Halmashauri zilipata pikipiki (252), *printers* (132) na magari (61). Sekretarieti zote za mikoa zimepatiwa magari 21. Matarajio ni kuwa ifikapo mwisho wa mwezi Juni 2010, kila Halmashauri itakuwa na gari moja, mashine ya *fax* moja, *photocopier* moja na kompyuta moja. Wizara yangu iliendelea na ujenzi na ukarabati wa ofisi. Ofisi 22 zilijengwa na Ofisi ya Sekretarieti ya Mkoa wa Rukwa ilikarabatiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka 2009/2010, nililitaarifu Bunge lako Tukufu kwamba, Wizara yangu ingeendelea kuzisaidia baadhi ya Halmashauri kusanifu na kuandaa zabuni kwa ajili ya utekelezaji wa miradi mbalimbali ya maji vijijini. Katika mwaka wa 2010/2011, Wizara yangu itashirikiana na Halmashauri husika katika kutekeleza miradi hiyo ikiwa ni pamoja na Ingri Juu, Masoko, Iwungilo, Mwakaleli, Kakonko, Ngeleka, Matema, Kabembe, Chiwambo, Ilamba na Lukululu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2009/2010, Wizara yangu kwa kushirikiana na Benki ya Maendeleo ya Ujerumani (*KfW*), iliendelea na utekelezaji wa Mradi wa Maji katika Wilaya za Moshi Vijijini na Hai. Mradi wa Maji wa Moshi Vijijini ulihusisha ujenzi wa vyanzo vitatu vya maji vya Monyo, Kineng’ena na Mue, ujenzi wa matanki 25 yenye mita za ujazo kati ya 50 na 150, ujenzi wa matanki 148 ya kupunguza msukumo wa maji, uchimbaji wa visima 14, uchimbaji wa mitaro na ulazaji wa bomba urefu wa kilomita 188, ujenzi wa vituo 212 vya kuchotea maji na uunganishaji wa maji katika nyumba 2,107 za watu binafsi. Mwaka 2010/2011 ujenzi wa mradi utaendelea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2009/2010, Mradi wa Maji wa Hai ulihusisha ujenzi wa Miradi ya Maji ya Levishi, Machame, Mkalama na North West Kilimanjaro. Mradi wa Levishi umekamilika na umekabidhiwa kwa wananchi mwanzoni

mwa mwezi Januari 2010. Katika mwaka wa fedha 2010/2011, ujenzi wa mradi utaendelea Vijiji vya Machame, Mkalama na North West.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2009/2010, Serikali kwa kushirikiana na Serikali ya Japan, ilikamilisha ujenzi wa Mradi wa Maji katika Mikoa ya Pwani na Dar es Salaam. Mradi ulikabidhiwa kwa wananchi mwezi Machi 2010. Mradi huo unawahudumia watu 24,500. Visima tisa vimejengwa na kufungwa pampu za mikono katika Vijiji vya Kitunda Kivule, Kitunda Mzinga na Pugu Stesheni. Miradi saba ya maji ya bomba imejengwa, chanzo kimoja cha maji kimejengwa, nyumba tisa za mitambo zimejengwa, matanki mawili ya juu ya ardhi yamejengwa, matanki matano ya juu ya mnara yamejengwa, mabomba yenye urefu wa km 63 yamelazwa na vituo vya kuchotea maji 93 vimejengwa. Mradi umegharimu shilingi bilioni 10.68.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2009/2010, Wizara yangu iliendelea na maandalizi ya Mradi wa Maji wa Wilaya za Same, Mwanga na Korogwe. Taarifa ya usanifu wa mradi imeandaliwa. Katika mwaka 2010/2011, Wizara itaajiri mtaalam mshauri ambaye atafanya mapitio ya usanifu na kusimamia kazi za ujenzi wa mradi. Taratibu za kumpata mkandarasi zitafanyika. Ujenzi unatarajiwa kuanza katika mwaka wa 2010/2011. Mradi huu umegawanywa katika awamu mbili. Awamu ya kwanza itatekelezwa kwa ushirikiano kati ya Serikali ya Tanzania kupitia Programu ya Maji na Usafi wa Mazingira Vijijini *(BADEA)* na Mfuko wa Maendeleo wa nchi zinazozalisha Mafuta *(OPEC Fund for International Development-OFID)*. Awamu hiyo ya mradi italenga katika kusambaza majisafi na salama katika vijiji saba (Kirya, Kiti cha Mungu, Njia Panda, Handeni, Kagongo, Bora, Nyabinda) vya Wilaya ya Mwanga na vijiji viwili (Ruvu Mferejini na Ruvu Jiungeni) vya Wilaya ya Same. Kazi zitakazotekelezwa katika awamu ya kwanza ni ujenzi wa miundombinu, kama ifuatavyo:-

(a) chanzo cha maji katika Bwawa la Nyumba ya Mungu;

(b) mtambo wa kusukuma maji toka chanzo cha maji;

(c) mtambo wa kusafisha maji eneo la Kijiji cha Njia Panda (Mwanga);

(d) mtambo wa kusukuma maji safi eneo la Kijiji cha Njia Panda;

(e) tanki kuu la kuhifadhi na kusambaza maji katika Kijiji cha Kisangara;

(f) matanki ya kuhifadhi maji katika vijiji vya awamu ya kwanza;

(g) bomba kuu na mabomba ya kusambaza maji katika vijiji vya awamu ya kwanza; na

(h) njia ya umeme kwenda mitambo ya kusukuma maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, awamu ya pili itahusu ujenzi wa miundombinu kama ifuatavyo:-

(a)mtambo wa pili wa kusukuma maji safi eneo la tanki la Kisangara (Mwanga);

(b)tanki kubwa la kuhifadhia maji katika kilima cha Kiverenge (Mwanga);
(c)matanki ya kuhifadhia maji katika vijiji vya awamu ya pili;

(d)bomba kuu la maji kutoka tanki la Kiverenge hadi vijiji vyote vya awamu ya pili vya Kileo, Kivulini, Kituli, Kifaru, Lembeni, Mgagao, Kisangara, Kiruru, Ibwejewa, Mbambua na Kiverenge (Mwanga); Njoro, Ishinde, Chajo, Bangalala, Mwembe, Mgwasi, Makanya, Hedaru, Gavao, Mabilioni, Bendera, Majengo, Mgandu na Mkonga Ijinyu (Same); Bwiko, Mkombozi, Manga Mtindiro, Manga Mikocheni na Nanyogie (Korogwe) na Miji ya Mwanga na Same;na

(e)mabomba ya kusambaza maji katika vijiji hivyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, awamu ya kwanza itagharimu Dola za Marekani milioni 35.76. Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania itachangia Dola za Marekani milioni 13.76, *OPEC-Fund* itachangia Dola za Marekani milioni 12 na *BADEA* itachangia Dola za Marekani milioni 10. Mradi katika awamu zote mbili unakadiriwa kugharimu shilingi bilioni 147.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mradi wa Maji Vijijini katika Mikoa ya Mwanza na Mara unatekelezwa kwa ushirikiano kati ya Wizara yangu na Serikali ya Japan. Mradi huo unalenga kuwapatia huduma ya maji wananchi katika vijiji 45 vya Mikoa ya Mwanza (26) na Mara (19). Jumla ya visima 177 vitachimbwa na kufungwa pampu za mkono. Hadi mwezi Mei 2010 jumla ya visima 65 katika Wilaya za Sengerema na Kwimba Mkoa wa Mwanza vilikuwa vimechimbwa na 34 kati ya hivyo vilikuwa na maji ya kutosha. Kazi ya ujenzi wa visima itaendelea kwa mwaka 2010/2011.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mradi wa Maji Vijijini Mkoa wa Tabora unatekelezwa kwa ushirikiano kati ya Serikali za Tanzania na Japan. Tathmini ya athari za kimazingira na kijamii na ubora wa maji chini ya ardhi ilifanyika katika Halmashauri zote za Mkoa wa Tabora kwa ajili ya kuanza utekelezaji wa mradi huo. Katika mwaka 2010/2011, usanifu wa awali wa miradi utafanyika. Hadi kukamilika kwake, mradi huo utagharimu shilingi bilioni 9.6.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2009/2010, Wizara iliendelea kusimamia ujenzi wa mabwawa mapya 13 ya Habiya (Bariadi), Nyambori (Rorya), Salama Kati (Bunda), Seke Ididi (Kishapu), Wegero (Musoma Vijijini), Iguluba (Iringa), Masuguru (Bagamoyo), Ingodin (Longido), Kawa (Nkasi), Mti Mmoja (Monduli), Sasajila (Chamwino), Matwiga (Chunya), Nyambele (Bunda) na ukarabati wa bwawa la Bulenya (Igunga). Utekelezaji wa ujenzi wa mabwawa hayo upo katika hatua mbalimbali za ujenzi. Mabwawa matano ya Bulenya, Mti Mmoja, Masuguru, Ingodin na Nyambele yamekamilika. Katika mwaka 2010/2011, ujenzi wa mabwawa ya Kawa (Nkasi), Sasajila (Chamwino), Matwiga (Chunya), Nyambori (Rorya), Wegero (Musoma), Habiya

(Bariadi), Iguluba (Iringa) na Seke Ididi (Kishapu) utaendelea. Shilingi bilioni 9.878 zimekasimiwa kwa mwaka 2010/2011.
Uendelevu wa miradi ya maji vijijini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na juhudi kubwa zinazofanywa na Serikali kuhakikisha idadi kubwa ya wananchi waishio vijijini wanapata majisafi na salama ifikapo mwaka 2025, ni muhimu kuweka taratibu zitakazohakikisha kuwa miradi iliyojengwa na inayoendelea kujengwa inakuwa endelevu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uundaji na usajili wa vyombo vya watumiaji maji; katika kuhakikisha kuwa uendeshaji na usimamiaji wa miradi ya maji unafanyika ipasavyo ni lazima kuunda vyombo vya watumiaji maji na kuvisajili kwa mujibu wa sheria. Aina ya vyombo vya watumiaji maji vilivyoundwa na kusajiliwa na idadi yake hadi mwezi Desemba 2009 ni kama ifuatavyo: Jumuiya za Watumiaji Maji (*Water Users Association*) 263 kwa mchanganuo ufuatao kimkoa: Arusha (28), Iringa (13), Mbeya (5), Dodoma (10), Ruvuma (3), Kilimanjaro (10), Kagera (12), Shinyanga (14), Lindi (2), Morogoro (5), Tabora (5), Manyara (30), Mara (48), Singida (35), Kigoma (2), Dar es Salaam (37), Pwani (1), Tanga (1) na Mtwara (2); Kampuni 22 za Morogoro (21) na Kilimanjaro (1); na Udhamini *(Foundation of Registered Trustees)* tano zilizo Kilimanjaro (3), Mtwara (Mbuo) (1) na Dodoma (Kibaigwa) (1).

Kulingana na takwimu hizo ni dhahiri kwamba, juhudi zaidi za kuhamasisha uundaji na usajili wa vyombo vya watumiaji maji inabidi zifanywe na Halmashauri na Mikoa. Hali hii inachangia kwa kiasi kikubwa kwa baadhi ya miradi kutofanya kazi na juhudi zetu kutokuwa endelevu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kukuarifu kwamba, kamati za maji zilizopo ni ngazi tu ya muda ya kuelekea kwenye uundaji wa vyombo huru vya kuendesha miradi. Halmashauri na wananchi wasiishie kwenye uundaji wa kamati za maji za vijiji. Kamati ya Maji si chombo huru kwani ni sehemu ya serikali ya kijiji. Halmashauri inabidi zisaidie Kamati za Maji zifanye kazi ya kuunda vyombo huru vitakavyosajiliwa kisheria kwenye Halmashauri. Kwa vile uundaji na usajili wa vyombo vya watumiaji maji sasa unafanyika katika ngazi ya Halmashauri, Halmashauri zote zihakikishe kwamba, miradi iliyopo na mingine itakayojengwa, ikiwa ni pamoja na ile itakayojengwa kupitia Programu ya Maji Vijijini, inaundiwa vyombo huru vya watumiaji maji. Kanuni za usajili wa vyombo vya watumiaji maji tayari zimetolewa kisheria kupitia Gazeti la Serikali GN. 21 la tarehe 22 Januari 2010. Katika mwaka 2010/2011, Halmashauri zinatakiwa ziandae mipango kazi ya kutoa elimu kwa wananchi kuhusu kuanzisha na kusajili vyombo vya watumiaji maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara yangu imetoa matangazo ya kutafuta mtaalam mshauri atayefanya kazi ya kuainisha vituo vya kuchotea maji nchi nzima. Kuainishwa kwa vituo hivyo kutawezesha kufahamu vizuri zaidi na kwa kutumia teknolojia ya kisasa ya kuandaa ramani ya vituo vya maji (*water point mapping*), mahali vilipo, vinavyofanya kazi, visivyofanya kazi na idadi ya watu wanaohudumiwa na vituo hivyo.

Taarifa zitakazopatikana na ufahamu wa mtandao wa vituo vya kuchotea maji zitawezesha Halmashauri kufahamu upatikanaji wa maji katika vijiji na kata. Taarifa hizo pia zitasaidia katika ufuatiliaji wa uendelevu wa miradi ya maji nchini. Kazi hiyo itafanyika chini ya programu kuanzia mwaka 2010/2011.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2009/2010, Wizara yangu iliendelea kutekeleza Programu ya Majisafi na Uondoaji wa Majitaka Mijini kwa kukarabati, kujenga na kupanua mifumo ya majisafi na majitaka pamoja na kuzijengea uwezo Mamlaka za Maji na Miradi ya Kitaifa kwa lengo la kuwapatia wananchi wengi zaidi majisafi na kuziwezesha kujiendesha kibiashara. Utekelezaji huo uliendelea katika Mamlaka za Majisafi na Majitaka katika miji mikuu ya mikoa, miji mikuu ya wilaya, miji midogo na miradi ya maji ya kitaifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika miji mikuu ya mikoa 19 kiwango cha utoaji wa huduma ya majisafi mijini kimefika wastani wa asilimia 84 mwaka 2010 kutoka asilimia 83 mwaka 2009. Ilipofika Mei 2010, wastani wa muda wa upatikanaji wa maji mijini kwa uhakika katika miji hiyo ulikuwa saa 18 kwa siku. Kwa Jiji la Dar es Salaam na Miji ya Kibaha na Bagamoyo upatikanaji wa maji ni asilimia 50 hadi 60 na wastani wa upatikanaji wa maji ni saa 7 kwa siku. Huduma ya uondoaji majitaka imebakia katika asilimia 18 kwa miji mikuu ya mikoa 19.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2009/2010, Wizara yangu iliendelea kuziimarisha kwa kuzijengea uwezo Mamlaka za Maji katika ngazi za Makao Makuu ya Mikoa, Miji Mikuu ya Wilaya na Miradi ya Kitaifa ili kuboresha ufanisi katika utoaji wa huduma katika miji hiyo kama ifuatavyo:-

(i) kusanifu majengo ya ofisi katika Miji ya Babati na Sumbawanga. Ujenzi wa majengo hayo utaanza mwaka 2010/2011;

(ii) kuzipatia Mamlaka za maji za miji ya wilaya, miji midogo na miradi ya kitaifa *printers* (42), kompyuta (42), pikipiki (120) na magari 10;

(iii) kukamilisha taratibu za kumpata mtaalam mshauri wa kufanya upembuzi yakinifu, usanifu na kuandaa zabuni kwa ajili ya ukarabati na upanuzi wa miundombinu katika miradi ya kitaifa ya Makonde na *Handeni Trunk Main (HTM)*. Mtaalam mshauri ataanza kazi mwaka 2010/2011;

(iv) kutoa mafunzo ya usimamizi wa Mamlaka kwa Bodi za Mamlaka ndogo 35; na

(v) kuandaa Mkataba wa makubaliano kati ya Wizara, Halmashauri na Mamlaka za Miji midogo na Miradi ya Kitaifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2009/2010, Wizara yangu iliendelea kutekeleza miradi inayotoa matokeo ya haraka katika Miji Mikuu ya Wilaya, Miji

Midogo na Miradi ya Kitaifa. Wizara ilitoa kiasi cha shilingi bilioni 3.24 kwa ajili ya miradi hiyo. Fedha hiyo ilitumika kukarabati miundombinu, kununua dira na kununua mitambo ya kusukuma maji. Ujenzi wa miundombinu ya maji ulifanyika katika miji ifuatavyo:-

Mji wa Mugumu: ujenzi wa mradi wa maji katika mji huu uliendelea kutekelezwa kwa kukamilisha ujenzi wa kitekeo cha maji, ulazaji wa mabomba, kujenga vituo 12 vya kuchotea maji, kununua na kufunga pampu bwawani, kuvuta umeme toka msongo mkuu wa Taifa kwenda kwenye chanzo cha maji (bwawani) na kununua na kufunga jenereta. Kazi zilizobaki ambazo zitaendelea kutekelezwa mwaka 2010/2011 ni kukamilisha ujenzi wa mbauti mbili za mifugo (*cattle trough*). Mugumu sasa ina uhakika wa kupata maji.

Mji wa Misungwi: kazi zilizotekelezwa ni pamoja na kusanifu mtandao wa maji, ulazaji wa mabomba umbali wa kilomita 13 kutoka Ziwa Victoria mpaka Mjini, ufungaji wa pampu na ujenzi wa njia ya umeme wa kV 3 umbali wa kilomita 12 kutoka laini kuu kwenda ziwani. Mradi upo katika hatua za mwisho za utekelezaji.

Mji wa Lamadi: kazi zilizofanyika ni usanifu wa kitekeo cha maji kwenye chanzo cha maji Ziwa Victoria, bomba kuu kutoka Ziwani hadi eneo litakapojengwa tanki la kuhifadhia maji umbali wa kilomita 6.5 na usanifu wa tanki lenye ukubwa wa mita za ujazo 90 na bomba la kupeleka maji mjini umbali wa kilomita 4.3. Ujenzi wa mradi utaanza mwaka 2010/2011.

Mji wa Mlowo: kazi zilizokamilika ni ujenzi wa kitekeo cha maji, ukarabati wa nyumba ya mitambo, ujenzi wa chujio la maji, ununuzi wa mabomba kwa ajili ya bomba kuu na mabomba ya usambazaji na kulaza bomba kuu kutoka kwenye kitekeo cha maji hadi kwenye tanki. Kazi zilizobaki ni kufunga pampu, kulaza mabomba ya kusambaza maji yenye urefu wa kilomita 4.7 na kujenga vituo vya kuchotea maji 20.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Miji mingine iliyopata fedha ni pamoja na Handeni; miji midogo ya Kasumulu, Himo, Mwanga, Sengerema, Kibondo, Kasulu, Manyoni, Mahenge, Pangani, Itumba-Isongole, Chiwambo, Monduli, Ngudu, Urambo, Chunya, Kilindi, Tunduma, Muheza, Mikumi na Miradi ya Kitaifa ya HTM, Makonde, Maswa, Wanging'ombe, Mugango-Kiabakari na Kahama-Shinyanga. Kazi zilizofanyika ni pamoja na ununuzi wa mabomba, pampu, dira za maji, uchimbaji wa visima vya majaribio na mbauti za mifugo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara yangu iliendelea kuchangia gharama za uendeshaji kwa kulipia ankara za umeme wa miradi ya kitaifa na Mamlaka za Majisafi na Majitaka Daraja B na C. Hadi kufikia Juni 2010, jumla ya shilingi bilioni 1.88 zilitumika. Katika mwaka 2010/2011, Wizara yangu itaendelea kuchangia gharama za umeme katika miradi 7 ya kitaifa na kuchangia gharama za umeme za Mamlaka za Majisafi na Majitaka za Daraja B na C ngazi ya mkoa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2009/2010, Wizara yangu kwa kushirikiana na Shirika la Maendeleo la Ujerumani (*GTZ*), iliendelea kuandaa utaratibu

wa kuziweka Mamlaka za Majisafi na Majitaka za Miji katika makundi (*clustering*). Madhumuni makubwa ni kupunguza gharama za uendeshaji na kuongeza ufanisi. Miji iliyo katika Mikoa ya Tanga na Morogoro imechaguliwa kuwa ya majaribio na utekelezaji wake utaanza mwaka 2010/2011.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2009/2010, Wizara yangu ilianza ujenzi, ukarabati na upanuzi wa vyanzo vya maji ikiwa ni pamoja na uchimbaji wa visima, upanuzi wa mitandao ya usambazaji maji na ujenzi wa matanki katika Miji ya Mtwara, Babati, Lindi na Sumbawanga. Utekelezaji ulikuwa kama ifuatavyo:-

(a) Mtwara Mjini: mabomba ya kusambaza maji yenye urefu wa kilomita 13 yamelazwa na ujenzi wa jengo la Mhandisi Mshauri umekamilika. Kazi zinazoendelea ni kulaza bomba kuu la umbali wa kilomita 4, kuendelea kulaza mabomba ya kusambaza maji, kununua na kuweka pampu kubwa kwenye visima 5, *booster pumps* 7, kati ya hizo kubwa ni 4 na ndogo 3 kwenye mtandao wa majisafi;

(b) Babati Mjini: ujenzi wa matanki matatu ya kuhifadhia maji yenye ujazo wa mita za ujazo 150 na uchimbaji wa visima 10 umekamilika. Kazi zinazoendelea ni ujenzi wa chujio la maji na ulazaji wa bomba kuu na yale ya usambazaji;

(c) Lindi Mjini: ukarabati wa mfumo wa majisafi unaendelea ambapo hadi sasa bomba zenye urefu wa kilomita 32 kati ya 47 zimebadilishwa. Ujenzi wa nyumba ya Mhandisi umekamilika. Uagizaji wa pampu 10 kwa ajili ya visima vya Kitunda umefanyika. Kazi zinazoendelea ni kukarabati visima 10 katika eneo la Kitunda na ujenzi wa matanki ya kuhifadhia maji; na

(d) Sumbawanga Mjini: visima vitatu vimechimbwa na mabomba ya kusambazia maji yenye urefu wa kilomita 25.4 kati ya 46.2 yamelazwa. Nyumba 251 zimeunganishwa kwenye mtandao wa maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha 2010/2011, Wizara yangu itaendelea na ujenzi wa mitandao ya usambazaji maji na kukamilisha kazi hiyo mwishoni mwa mwaka 2010 katika Miji ya Mtwara, Babati, Lindi na Sumbawanga. Mtaalam mshauri ataendelea kufanya upembuzi yakinifu, usanifu na uandaaji wa zabuni za ujenzi wa miundombinu ya majisafi na majitaka ya kukidhi mahitaji ya maji ya miji hiyo hadi mwaka 2030. Mradi huo utatekelezwa kwa ushirikiano kati ya Serikali na Umoja wa Ulaya chini ya Mpango wa *ACP-EU Water Facility*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali kwa kushirikiana na Serikali ya Ufaransa kupitia Shirika lake la Maendeleo la *AFD*, inatekeleza mradi wa kuboresha huduma za majisafi katika mpango wa muda wa kati katika Miji ya Musoma na Bukoba. Katika kipindi cha 2009/2010, kazi ya kusanifu mradi wa majisafi katika miji hiyo na kuandaa zabuni zilitekelezwa. Rasimu ya zabuni imewasilishwa na inapitiwa na Mamlaka za Bukoba na Musoma. Lengo ni kuanza ujenzi mwaka 2010/2011. Mtaalam mshauri ataendelea kufanya upembuzi yakinifu, usanifu na uandaaji wa zabuni za ujenzi wa miundombinu ya majisafi na majitaka ya kukidhi mahitaji ya maji ya miji hiyo hadi

mwaka 2030. Mradi huo utatekelezwa kwa ushirikiano kati ya Serikali na Umoja wa Ulaya chini ya mpango wa *ACP-EU Water Facility*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2009/2010, Wizara yangu iliendelea kuboresha huduma za maji katika Mji wa Kigoma/Ujiji kwa kuchukua hatua za dharura baada ya kina cha maji kuendelea kushuka kwenye Ziwa Tanganyika na tatizo la umeme usio wa uhakika. Hatua zilizochukuliwa ni kwa kutekeleza kazi za dharura kwa gharama ya shilingi milioni 517 kama ifuatavyo:-

(i) kununua pampu mbili za kuzamisha ziwani;

(ii) kununua pampu mbili za kupokea maji kutoka pampu mbili zilizoko ziwani ambazo zitasukuma maji hadi kwenye matanki;

(iii) kukarabati mabomba kwenye vituo vya kusukuma maji na kununua viungio; na

(iv) kukarabati *transformer* ya kVA 800 na kununua transfoma mpya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara yangu katika mwaka 2009/2010 ilianza mpango wa muda wa kati wa kuhakisha huduma zinaboreshwa katika Mji wa Kigoma/Ujiji hadi mwaka 2015. Mtaalam mshauri amekamilisha kazi ya usanifu wa Mradi wa Majisafi wa Mji wa Kigoma/Ujiji na kuandaa zabuni. Zabuni hiyo itatangazwa ili kumpata mkandarasi kabla ya Desemba 2010. Kazi ya ujenzi itaanza katika mwaka 2010/2011. Mtaalam mshauri huyo pia anasanifu mradi wa maji katika Mji wa Kasulu. Mji wa Kibondo utafanyiwa usanifu na mtaalam mshauri atakayefanya usanifu wa Miradi ya Maji Biharamulo, Muleba, Bunazi, Ngara, Karagwe na Chato. Katika mwaka 2010/2011 mtaalam mshauri ataendelea kufanya upembuzi yakinifu, usanifu na uandaaji wa zabuni za ujenzi wa miundombinu ya majisafi na majitaka ya kukidhi mahitaji ya maji ya Kigoma hadi mwaka 2030. Mradi huo utatekelezwa kwa ushirikiano kati ya Serikali na Umoja wa Ulaya chini ya Mpango wa *ACP-EU Water Facility*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara yangu kwa kushirikiana na Serikali ya Uswisi kupitia Shirika lake la Maendeleo la *SECO*, inaendelea na utekelezaji wa mradi wa kupanua na kukarabati mifumo ya majisafi na majitaka ya Manispaa za Tabora na Dodoma. Kwa upande wa Dodoma, kazi ya kujenga mfumo wa majitaka wenye urefu wa kilometa 8.2 eneo la Hazina imekamilika. Jumla ya wateja 127 wameunganishwa kwenye mtandao huo. Serikali ilitoa kiasi cha shilingi 830,519,823 ambazo zilitumika kwa ujenzi na ukarabati wa mfumo wa majitaka na shilingi 200,000,000 kwa ununuzi wa pampu tatu kwa ajili ya visima vya Mzakwe. Kwa upande wa Tabora, Serikali ilitoa shilingi milioni 230 na *SECO* ilitoa Dola za Marekani 350,000 ambazo zilitumika kukarabati na kupanua miundombinu ya majisafi na majitaka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara yangu katika mwaka 2009/2010 ilikamilisha kazi ya uchunguzi, usanifu na utayarishaji wa zabuni ili kukidhi mahitaji ya maji Tabora na Dodoma hadi mwaka 2020. Kazi hiyo pia, inahusisha Urambo na Sikonge kwa upande

wa Tabora. Kwa Dodoma kazi ya kumpata mkandarasi kwa ajili ya ujenzi wa miundombinu ya majisafi na majitaka imeanza na ujenzi unatarajiwa kuanza mwaka 2010/2011.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2009/2010, Wizara yangu iliendelea kuboresha huduma za maji Morogoro. Katika kutekeleza mpango wa muda wa kati wa kuwa na mifumo ya maji ya kukidhi mahitaji hadi 2020, mtaalam mshauri anakamilisha kazi ya usanifu na uandaaji wa zabuni. Kwa Miji Midogo ya Mahenge, Mikumi na Ifakara, taratibu za kumpata mtaalam mshauri atakayeanza kazi hizo zitafanyika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mradi wa Uboreshaji wa Miundombinu ya Majisafi na Majitaka Singida unatekelezwa kwa pamoja kati ya Wizara yangu, *BADEA* na Mfuko wa Maendeleo wa nchi zinazozalisha mafuta (*OPEC Fund)*. Kazi za ujenzi wa mradi wa kupanua mfumo wa majisafi Singida zinazohusu uchimbaji wa visima 10 na ujenzi wa miundombinu ya maji zimeanza mwezi Novemba 2009. Kazi hizo zitaendelea kutekelezwa katika mwaka 2010/2011 na zitachukua miezi 24. Katika kutekeleza mpango wa muda wa kati wa kuhakikisha Singida inakuwa na mfumo wa majitaka na miji ya Kiomboi na Manyoni inakuwa na mifumo ya maji ya kukidhi mahitaji hadi 2020, Wizara yangu, katika mwaka 2010/2011 itakamilisha utaratibu wa kumpata mtaalam mshauri atakayeanza kazi ya usanifu na utayarishaji wa zabuni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara yangu kwa kushirikiana na Umoja wa Ulaya pamoja na Benki ya Maendeleo ya Ujerumani (*KfW*) katika mwaka 2009/2010, iliendelea kuboresha huduma za majisafi na majitaka Mwanza, Mbeya na Iringa chini ya Programu ya *Regional Centres* (Awamu ya Pili), kwa lengo la kukidhi mahitaji ya majisafi na uondoaji majitaka. Kwa Mji wa Mbeya utekelezaji uliendelea kwa kujenga mitambo ya kutibu maji maeneo ya Sisimba, Sawaya na Imeta, ujenzi wa matanki 8 ya kuhifadhia majisafi, kupanua mtandao wa majisafi na majitaka katika maeneo ya Uyole, Iyunga na kujenga mabwawa ya majitaka eneo la Kalobe. Kazi hizo zitaendelea katika mwaka 2010/2011.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Jiji la Mwanza, kazi za ujenzi, ukarabati na upanuzi wa miundombinu ya majitaka katika makazi yasiyo rasmi, uunganishaji wa wateja kwenye mtandao wa majisafi na majitaka na ujenzi wa mitambo ya kusukuma majitaka ziliendelea kutekelezwa katika mwaka 2009/2010. Kazi hizo zitaendelea katika mwaka 2010/2011. Kwa Iringa, katika mwaka 2009/2010, kazi za ujenzi wa miundombinu ya majisafi na majitaka ziliendelea. Zimehusu ujenzi wa matanki ya kuhifadhia maji na mtambo wa kusafisha maji. Kazi hizo zitaendelea mwaka 2010/2011.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mpango wa muda wa kati na muda mrefu ni kuhakikisha Miji ya Mbeya, Iringa na Mwanza na Miji Midogo ya Rujewa, Vwawa, Chunya, Kyela, Kasumulu, Tunduma, Mbalizi, Itumba na Tukuyu kwa Mkoa wa Mbeya na Miji Midogo ya Njombe, Kilolo, Ilula, Mafinga, Ludewa, Makete, Makambako na Mradi wa Kitaifa Wanging’ombe kwa Mkoa wa Iringa na Miji Midogo ya Magu, Nansio, Geita, Misungwi, Ngudu, na Sengerema Mkoa wa Mwanza inakuwa na mifumo ya maji

ya kukidhi mahitaji mpaka mwaka 2025. Mkataba umesainiwa na wataalam washauri watakaoanza kazi ya usanifu na utayarishaji wa zabuni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kuboresha huduma ya majisafi na majitaka, katika mwaka 2009/2010, Wizara yangu iliendelea na usanifu na utayarishaji wa zabuni za ujenzi wa miundombinu Arusha, Moshi, Shinyanga, Songea na Tanga. Usanifu huo pia, ulihusisha Miji ya Loliondo, Mwanga na Same, Maswa, Kishapu, Ushirombo, Mbinga, Tunduru, Namtumbo, Muheza na Pangani. Kazi hizo zitakamilika mwaka 2010/2011.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyolitaarifu Bunge lako Tukufu mwaka jana, Wizara yangu katika kipindi cha mwaka 2005 hadi 2009, ilikamilisha kazi za ujenzi wa Mradi Mkubwa wa Maji kutoka Ziwa Victoria hadi Miji ya Kahama na Shinyanga kwa gharama ya shilingi bilioni 252. Mradi huo ulizinduliwa rasmi na Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania tarehe 30 Mei 2009.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2009/2010, Wizara yangu iliendelea kutekeleza kazi mbalimbali kuhusiana na mradi huo. Kazi zilizotekelezwa baada ya uzinduzi ni kama ifuatavyo:-

(i) kuimarisha Mamlaka ya kuendesha mradi wa maji inayojulikana kama *Kahama Shinyanga Water Supply Authority* (KASHWASA) inayosimamiwa na Bodi ya Wakurugenzi. Mamlaka ya kusimamia maji mjini Kahama pia imeimarishwa;

(ii) kuendelea na zoezi la kuunganisha wateja ambapo hadi kufikia Juni 2010 wateja 11,129 katika mji wa Shinyanga na wateja 7,552 katika mji wa Kahama waliunganishwa na kuanza kupata huduma ya majisafi na salama; na

(iii) ujenzi wa matoleo ya maji katika vijiji 40 na tanki moja la Mhalo umekamilika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2010/2011, Wizara yangu itaendelea kufanya usanifu katika vijiji vilivyobaki ikiwa ni pamoja na kuongeza vituo vya kuchotea maji. Jumla ya vijiji 76 vinatarajiwa kupata maji toka mradi huo. Usanifu wa kuunganisha miji midogo ya Isaka, Munhunze, Kagongwa na Tinde utafanyika. Upembuzi yakinifu na usanifu wa kupeleka maji hayo Nzega, Igunga na Tabora utatekelezwa mwaka 2010/2011.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kipindi cha 2009/2010, Wizara yangu iliendelea na ukarabati, ujenzi na upanuzi wa Miradi ya Maji ya Miji Mikuu ya Wilaya, Miji Midogo na Miradi ya Kitaifa. Utekelezaji wa kazi hizo ni kama ifuatavyo:-

Ujenzi wa mradi wa maji wa Chalinze: Mradi wa maji wa Chalinze (Awamu ya Pili), unajumuisha usambazaji wa majisafi katika vijiji 48 vilivyogawanywa katika makundi tisa ya utekelezaji. Utekelezaji katika Wilaya ya Bagamoyo, Mkoa wa Pwani, unahusu Vijiji vya Mdaula, Msolwa, Ubenazomozi, Kaloleni, Mwidu, Visakazi, Matuli na Tukamisasa. Ujenzi ulianza mwezi Septemba 2009 na utaendelea kutekelezwa katika mwaka 2010/2011. Katika vijiji sita vya Kinonko, Kizuka, Sinyaulime, Sangasanga,

Kidugalo na Ngerengere, Mkoa wa Morogoro ujenzi umeanza mwezi Desemba 2009 na utaendelea kutekelezwa mwaka 2010/2011. Taratibu za kuwapata wakandarasi kwa ajili ya utekelezaji katika maeneo yaliyobaki zimekamilika na ujenzi wa miradi utaanza mwaka 2010/2011. Vijiji vitakavyohusika ni Mihuga, Kwekonje, Mkange, Masimbani, Mandamazingara; Kiwangwa/Mwavi, Fukayosi, Makurunge, Mkenge Kidomole, Masunguru/Mwetemo, Msinune, Pongwe, Msungura, Madesa, Kisanga, Malivundo, Mindukeni, Kinzagu, Makombe, Talawanda, Msigi, Vigwaza, Chamakweza, Buyuni, Visezi, Magindu, Lukenge, Chahua, Gwata, Gumba, Kwaruhombo, Kwang'andu, Pongwe, Kiona na Kifuleta.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2009/2010, Wizara yangu kwa kushirikiana na Shirika la Maendeleo la Ufaransa (*AFD*) iliendelea na kukamilisha ujenzi wa miradi ya maji katika miji ya Mpwapwa na Utete. Mradi wa Mpwapwa umekamilika mwezi Juni 2010 na ule wa Utete utakamilika mwezi Julai 2010. Idadi ya watu watakaonufaika na miradi hiyo ni 9,335 kwa Mji wa Utete na 27,900 kwa Mji wa Mpwapwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2009/2010, Wizara yangu iliendelea kuboresha huduma za maji katika Miji ya Ikwiriri, Kibaigwa, Kilosa, Turiani, Mvomero, Kibiti na Gairo kwa kutekeleza miradi ya maji katika miji hiyo. Utekelezaji wa miradi upo katika hatua mbalimbali kama ifuatavyo:-

(i) Ujenzi wa miradi ya maji Ikwiriri na Kibiti ulianza mwezi Agosti 2009 na utakamilika mwezi Julai 2010;

(ii) Mkataba wa ujenzi wa Mradi wa Maji Kibaigwa umesainiwa mwezi Mei 2010 na ujenzi utaanza mwezi Juni 2010; na

(iii) Mikataba ya ujenzi wa Miradi ya Maji Kilosa, Turiani, Mvomero na Gairo itasainiwa mapema mwaka 2010/2011.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2009/2010, Wizara yangu iliendelea kuboresha huduma za maji katika Miji ya Igunga, Bunda, Nachingwea na Masasi. Utekelezaji wa miradi ya maji katika miji hiyo upo katika hatua mbalimbali kama ifuatavyo:-

Nachingwea na Masasi: Taratibu za kumpata mkandarasi wa kujenga Mradi wa Maji wa Mbwinji, Masasi na Nachingwea zinaendelea. Mkandarasi anatarajiwa kupatikana kabla ya Septemba 2010 na kazi ya ujenzi itaanza mwezi Oktoba 2010. Hadidu za rejea kwa ajili ya kumpata mtaalam mshauri atakayetathmini vyanzo vipya vya maji zimeandaliwa. Vyanzo hivyo ni pamoja na:-

(i) Maji chini ya ardhi katika mabonde madogo ya Mkumba-Shamba na Mkumba-Pacha mjini Nachingwea ambayo yana uwezo wa kutoa kiasi cha mita za ujazo 6,300 kwa siku;

(ii) Maji chini ya ardhi katika bonde dogo la Mnero Mjini Masasi ambalo lina uwezo wa kutoa mita za ujazo 13,700 kwa siku; na

(iii) Bwawa la Mchema ambalo likikarabatiwa linaweza kujaa kwa msimu mmoja wa mvua na kuhifadhi mita za ujazo 110,000. Pia kuna uwezekano wa kujenga bwawa eneo la Miesi.

Bunda: Kazi ya ujenzi wa matanki mawili, nyumba ya pampu, nyumba ya mlinzi na ujenzi wa barabara (*access road*) umekamilika. Kazi zitakazoendelea mwaka 2010/2011 ni pamoja na usanifu na ujenzi wa chanzo, ujenzi wa bomba kuu kutoka ziwani hadi kwenye matanki ya maji, ujenzi wa chujio pamoja na kupeleka umeme.

Igunga: Kazi za ujenzi na ukarabati wa mtandao wa maji, matanki, mbauti za mifugo na vituo vya maji pamoja na ufungaji wa dira za maji zilitekelezwa. Ujenzi wa chujio umeanza mwezi Mei 2010 na utachukua muda wa miezi 6 kukamilika. Mradi utakapokamilika unakadiriwa kuhudumia watu 32,695 na mifugo 24,507.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2009/2010, Serikali kwa kushirikiana na Shirika la Marekani la *Millenium Challenge Corporation (MCC),* iliendelea na utekelezaji wa miradi ya majisafi katika Jiji la Dar es Salaam na Manispaa ya Morogoro. Mapitio ya utekelezaji na mpango wa mwaka 2010/2011 ni kama ifuatavyo:-

(i) Upanuzi wa mtambo wa Ruvu Chini; Mtaalam mshauri wa kusanifu na kupanua mtambo wa kusafisha maji wa Ruvu Chini amekamilisha usanifu na kutayarisha zabuni kwa ajili ya mkandarasi wa kupanua mtambo wa Ruvu Chini. Ujenzi wa mradi huo utaanza mwaka 2010/2011. Kazi hiyo itaongeza uwezo wa uzalishaji wa maji kutoka mita za ujazo 180,000 hadi mita za ujazo 270,000 kwa siku;

(ii) Kupunguza maji yanayopotea; Katika mwaka 2009/2010 mtaalam mshauri amekamilisha kazi ya usanifu wa mradi wa kupunguza maji yanayopotea unaohusisha maeneo ya Tegeta, Bunju na Bagamoyo. Kazi ya ulazaji wa mabomba katika maeneo hayo yenye urefu wa kilomita 470 na kuunganisha wateja 17,000 itaanza mwaka 2010/2011; na

(iii) Upanuzi wa mfumo wa majisafi Morogoro; Kwa kushirikiana na Shirika la *MCC* taratibu za kumpata mkandarasi wa kukarabati mtambo wa kusafisha maji wa Mafiga na ujenzi wa mtambo mpya eneo la Mambogo pamoja na ukarabati wa matanki ya maji zinaendela. Ujenzi wa mradi huo utaanza katika mwaka 2010/2011.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Huduma ya majisafi na uondoaji wa majitaka Dar es Salaam, Kibaha na Bagamoyo; Wizara kupitia DAWASA inaendelea kutekeleza mradi wa uboreshaji wa miundombinu ya majisafi na majitaka Jijini Dar es Salaam. Mradi huo unakamilika mwezi Juni 2010. Kazi zilizotekelezwa mwaka 2009/2010 chini ya mradi huo hadi kufikia mwezi Juni 2010 ni zifuatazo:-

(i) Kukarabati mitambo mitatu ya kuchuja maji ya Ruvu Juu, Ruvu Chini na Mtoni;

(ii) Kukarabati mabwawa ya kusafisha majitaka katika maeneo ya Msasani, Mabibo, Kurasini, Lugalo, Vingunguti, Ukonga, Buguruni na Mikocheni;

(iii) Ulazaji wa mabomba mapya ya majitaka yenye urefu wa kilomita 45.7;

(iv) Kukarabati mabomba ya majitaka yenye urefu wa kilomita 76;

(v) Kujenga chemba *(manholes)* 576 za kupokea majitaka na kununua vifaa kwa ajili ya kusafisha na kufanyia matengenezo mabomba ya majitaka;

(vi) Kuboresha mfumo wa umeme mkubwa pamoja na kujenga njia mpya ya umeme yenye urefu wa kilomita sita kwenda kituo cha maji Ruvu Darajani na kufunga transfoma mpya tano katika vituo vya Ruvu Juu na Ruvu Chini kwa lengo la kuongeza ufanisi na kuwa na uwezo wa akiba pale dharura inapotokea; na

(vii) Kukarabati jumla ya kilomita 110 za mabomba makuu ya kusafirisha maji kutoka kwenye mitambo ya Ruvu Juu na Ruvu Chini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara kupitia *DAWASA* imeendelea kukamilisha miradi ya kulaza mabomba madogo *(Infill secondary and tertiary mains)* na kuunganisha maji kwa wateja. Hadi kufikia Juni 2010, kazi zifuatazo zilitekelezwa:-

(i) Kulaza mabomba yenye urefu wa kilomita 241.5 katika maeneo ya Kunduchi, Mtongani, Kilongawima, Mbezi Beach na kuunganisha wateja 7,507 kati ya wateja 10,500 waliolengwa. Kazi ya kuwafungia dira za maji wateja waliobaki inaendelea na itakamilika mwezi Desemba 2010;

(ii) Kulaza mabomba yenye urefu wa kilomita 335 katika maeneo ya Kimara, Changanyikeni na Makongo na kuunganisha wateja 16,808 na kuwafungia dira za maji;

(iii) Kulaza mabomba yenye urefu wa kilomita 303 na kuunganisha wateja 8,800 katika maeneo ya Kiluvya, Kibaha na Mlandizi;

(iv) Kulaza mabomba yenye urefu wa kilomita 145 katika maeneo ya Tabata, Segerea na Makuburi na kuunganisha wateja 9,123 na kuwafungia dira za maji;

(v) Kulaza mabomba yenye urefu wa kilomita 118 katika maeneo ya Mikocheni, Msasani, Mabibo, Ubungo na Kurasini na kuunganisha wateja 4,205 na kuwafungia dira za maji; na

(vi) Kukamilisha ujenzi wa magati 294 ya kuchotea maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kazi hizo zilizotajwa hapo juu na zile zilizofanyika kati ya 2005 - 2009 zinafanya jumla ya mabomba mapya ya usambazaji maji yaliyolazwa kufikia urefu wa kilomita 1,282 na wateja waliofungiwa dira kufikia 111,756.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara yangu inaendelea na utekelezaji wa Mradi wa Kuboresha Upatikanaji wa Majisafi na Usafi wa Mazingira katika maeneo ya pembezoni mwa Jiji la Dar es Salaam ambayo hayakuunganishwa na mfumo wa maji wa Jiji. Katika mwaka 2009/2010, Wizara yangu kwa kushirikiana na Shirika la Maendeleo la Ubelgiji (BTC), ilianza utekelezaji wa mradi wa kuboresha huduma ya maji kwa kuchimba visima 20 vya utafiti katika maeneo yaliyochaguliwa katika Wilaya za Ilala, Temeke na Kinondoni pamoja na uhamasishaji wa jamii ili kushiriki katika miradi hiyo. Visima vilivyoonesha hali nzuri ya maji vitaendelezwa mwaka 2010/2011.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara yangu, kwa kushirikiana na asasi zisizo za kiserikali, iliendelea kutekeleza miradi midogo 50 ya maji. Jumla ya miradi 43 iliibuliwa na wananchi. Miradi 39 imekamilika na inafanya kazi. Miradi 11 ipo katika hatua za mwisho za ujenzi na itakamilika mwezi Juni 2010.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imeendelea kulitafutia ufumbuzi wa kudumu tatizo la maji kwa Jiji la Dar es Salaam kwa kutafiti vyanzo vipya vya maji. Kiasi cha maji kinachozalishwa kwa sasa ni mita za ujazo 300,000 kwa siku wakati mahitaji ni mita za ujazo 450,000 kwa siku. Mahitaji yanakadiriwa kufikia mita za ujazo 960,000 kwa siku ifikapo mwaka 2030. Katika kukabiliana na ongezeko hilo la mahitaji, Wizara yangu imeendelea na juhudi za kutafuta vyanzo vipya vya maji vikiwemo Bwawa la Kidunda na uchimbaji wa visima virefu Kimbiji na Mpera. Hatua zilizofikiwa ni kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Bwawa la Kidunda, Mhandisi mwelekezi ameteuliwa Februari 2010 na ameanza kazi za kutengeneza ramani mpya ya eneo la bwawa, kuchunguza athari za mradi kwa jamii na mazingira, kusanifu bwawa na kuandaa zabuni. Kazi hizo zitakamilika Septemba 2010. Ujenzi wa bwawa utaanza rasmi mwaka 2011/2012. Ujenzi utachukua miaka mitatu kukamilika. Bwawa la Kidunda litawezesha maji kupatikana Ruvu Chini na Ruvu Juu kwa uhakika katika majira yote ya mwaka na wakati wa ukame. Bwawa hilo litasaidia kupunguza uwezekano wa mafuriko katika Mto Ruvu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2009/2010, Wizara yangu iliendelea na utekelezaji wa mradi wa uchimbaji wa visima virefu Kimbiji na Mpera. Hatua iliyofikiwa katika utekelezaji ni kama ifuatavyo:-

(i) Taratibu za kumpata mhandisi mshauri wa kusimamia uchimbaji wa visima na ujenzi wa mfumo wa maji zipo katika hatua za mwisho. Mhandisi huyo ataanza kazi mwezi Julai 2010.

(ii) Idhini ya kutangaza zabuni ya kumpata mkandarasi wa ujenzi imeombwa Benki ya Dunia. Zabuni hiyo itatangazwa baada ya kumwajiri mhandisi mshauri.

(iii) Kazi ya kutathmini athari za mradi kwa jamii na mazingira ilianza Januari 2010 na itakamilika Juni 2010.

(iv) Kazi ya kutathmini gharama ya ardhi na mali za wananchi watakaoathirika na mradi huo imekamilika katika eneo la Kimbiji. Inaendelea katika eneo la Mpera na itakamilika Juni 2010; na

(v) Ulipaji wa fidia kwa wananchi watakaoathirika na ujenzi wa mradi utafanyika mara baada ya kupata fedha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mradi huo utaanza kutekelezwa mwaka wa fedha 2010/2011. Wizara ya Fedha na Uchumi imeupa kipaumbele mradi huo kwa kuanzisha kasma ya mradi kwa ajili ya kufanikisha utekelezaji wake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uzalishaji wa majisafi kwa Mamlaka zote 19 za miji mikuu ya mikoa uliongezeka kutoka wastani wa mita za ujazo 300,016 kwa siku kwa mwaka 2008 hadi mita za ujazo 306,700 kwa siku mwaka 2009. Kwa upande wa Jiji la Dar es Salaam, mwaka 2009 uzalishaji maji ulikuwa wastani wa mita za ujazo 300,000 kwa siku ikilinganishwa na mita za ujazo 273,000 kwa siku mwaka 2008. Kiwango hicho cha uzalishaji maji kinajumuisha vyanzo vya Ruvu Juu, Ruvu Chini, Mtoni na visima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, makusanyo ya maduhuli yatokanayo na mauzo ya maji katika Mamlaka za maji za miji mikuu ya mikoa yameongezeka kutoka shilingi bilioni 34.8 mwaka 2008/2009 hadi kufikia shilingi bilioni 41.04 mwaka 2009/2010, sawa na ongezeko la asilimia 18. Katika kipindi hicho DAWASCO imeweza kukusanya shilingi bilioni 26, ikilinganishwa na shilingi bilioni 24 mwaka 2008/2009.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kufikia mwezi Juni 2010, ufungaji wa dira za maji kwenye miji mikuu ya mikoa 19 umeongezeka hadi kufikia dira 226,005 ukilinganishwa na dira 202,227 zilizoripotiwa Juni 2009. Ongezeko hilo limefanya idadi ya wateja waliofungiwa dira katika miji hiyo kufika asilimia 90. Lengo ni kuwafungia dira za maji wateja wote wa maji mijini ifikapo mwaka 2012. Hadi kufikia mwezi Juni 2010, *DAWASCO* ilikuwa na wateja 95,385. Kati ya hao, wateja 74,400 sawa na asilimia 78 wamefungiwa dira za maji. Lengo ni kuwafungia wateja wote (asilimia 100) ifikapo Desemba 2010.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wastani wa upotevu wa maji, kwenye Mamlaka za Majisafi na Majitaka ngazi ya mikoa kwa mwaka 2008/2009 ulikuwa asilimia 37. Kufikia Juni 2010 upotevu wa maji umepungua hadi kufikia asilimia 36. Lengo ni kupunguza upotevu huo hadi asilimia 30 ifikapo mwaka 2015 na hatimaye kufikia asilimia 20, ambacho ni kiwango kinachokubalika kimataifa. Kwa Dar es Salaam lengo ni kupunguza upotevu wa maji kutoka asilimia 53 mwaka 2009 hadi kufikia asilimia 45 mwaka 2015.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2009/2010, Wizara imekamilisha ufungaji wa dira kubwa 70 za maji *(bulk meters)* katika kanda 25 za usambazaji za Dar es Salaam. Dira hizo ambazo zimeunganishwa na mfumo wa mawasiliano (*Telemetry*),

zinasaidia kubaini maji yaliyozalishwa na kutumika katika maeneo tofauti. Utaratibu huo utasaidia kubaini upotevu wa maji ili hatua za haraka zichukuliwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, huduma ya uondoaji wa majitaka bado si ya kuridhisha kutokana na mwamko mdogo wa wananchi kuomba kuunganishwa kwenye mitandao, uchakavu wa miundombinu iliyopo, gharama kubwa za uwekezaji pamoja na ongezeko kubwa la watu mijini. Huduma ya uondoaji majitaka imepanda kutoka asilimia 17 mwaka 2008/2009 hadi asilimia 18 mwaka 2009/2010. Lengo la MKUKUTA ilikuwa asilimia 30 ifikapo 2010. Wateja wa majitaka wameongezeka kutoka 17,208 mwaka 2008/2009 hadi kufikia 17,700 mwaka 2009/2010, sawa na ongezeko la wateja 492.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara yangu imeendelea kusimamia Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji *(EWURA).* Katika mwaka 2009/2010, *EWURA* imeendelea kudhibiti utoaji wa huduma kwenye sekta za umeme, mafuta ya petroli, gesi asilia, majisafi na majitaka nchini ambapo ubora wa huduma husika umeimarika na bei za huduma hizo zimeendelea kuwa wazi zaidi na za kueleweka kwa wadau mbalimbali. Majukumu ya *EWURA* kwa uchumi wa taifa ni makubwa. *EWURA* iliendelea kujenga uwezo wake kwa kuajiri watumishi wapya 16 wa fani mbalimbali, kutoa mafunzo kwa watumishi na kuandaa nyenzo mbalimbali za udhibiti zikiwemo sheria ndogo ili kuboresha utendaji kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa sekta ya maji, *EWURA* inadhibiti jumla ya Mamlaka za Maji 122 ikiwa ni pamoja na Mamlaka 19 za miji mikuu ya mikoa, 95 za miji mikuu ya wilaya na miji midogo, Miradi ya kitaifa saba na *DAWASA* na *DAWASCO*. Hadi Juni 2010, Mamlaka nane kati ya Mamlaka za maji za miji mikuu ya mikoa 19 zilitimiza masharti ya kupewa leseni za kudumu. Mamlaka hizo ni za Dodoma, Tanga, Singida, Mbeya, Moshi, Arusha, Mwanza na Tabora. Kwa mujibu wa Sheria ya Huduma za Maji na Usafi wa Mazingira, Sheria Na. 12 ya Mwaka 2009, Sehemu ya 29(4), leseni zitadumu kwa kipindi kisichopungua miaka 10. *DAWASA* na *DAWASCO* zinaendelea kutumia leseni waliyopewa mwaka 2005 ambayo nayo inadumu kwa miaka 10.

Mamlaka za mikoa zilizobakia zinaendelea kutoa huduma kwa kutumia leseni za muda. Leseni hizo za muda zinatolewa kwa lengo la kutoa fursa kwa Mamlaka kutimiza masharti ya leseni za kudumu. Kuhusu Mamlaka za Miji Mikuu ya Wilaya, Miji Midogo na Miradi ya Kitaifa, *EWURA* imetoa elimu kwa wafanyakazi 155 kutoka menejimenti za Mamlaka hizo kuhusu namna ya kuomba leseni na wajibu na majukumu yao kwa mujibu wa leseni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hadi mwezi Juni 2010, Mamlaka 49 kati ya 102 za Miji Mikuu ya Wilaya, Miji Midogo na Miradi ya Kitaifa zilikuwa zimeomba leseni za muda. Uchambuzi wa *EWURA* unaendelea. Katika mwaka 2010/2011, *EWURA* itaendelea kutoa mafunzo kwa Mamlaka ndogo, kuchambua na kufanya taftishi kwa maombi ya leseni yatakayowasilishwa na hatimaye kutoa leseni za kudumu kwa watoa huduma za majisafi na majitaka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *EWURA* ina jukumu la kufuatilia utendaji wa Mamlaka za Maji kwa kupitia taarifa zinazowasilishwa na ukaguzi unaofanyika mara kwa mara. Katika mwaka 2009/2010, *EWURA* ilipitia na kuchambua taarifa mbalimbali za mwaka 2008/2009 kutoka Mamlaka 19 za Mikoa, *DAWASA*, *DAWASCO* na Mamlaka 67 za Miji Mikuu ya Wilaya, Miji Midogo na Miradi ya Kitaifa. Kwa Mamlaka za Makao Makuu ya Mikoa, uchambuzi ulizingatia malengo yaliyo kwenye Makubaliano ya Utendaji *(Performance Agreement)* yaliyosainiwa kati ya *EWURA* na Mamlaka husika. Kutokana na uchambuzi huo, *EWURA* iliandaa taarifa ya kwanza ya utendaji ya mwaka 2008/2009 inayolinganisha utendaji wa Mamlaka za Maji za Mijini. Taarifa hiyo inapatikana katika tovuti ya EWURA *(www.ewura.go.tz).* Masuala muhimu yaliyojitokeza ni:-

(i) Mahitaji ya maji ni makubwa kuliko kiwango cha maji yanayozalishwa na kusambazwa.

(ii) Pamoja na juhudi za ufungaji wa dira za maji kwa wateja bado kiwango cha upotevu wa maji ni kikubwa; na

(iii) Mifumo ya majitaka bado ni midogo kuweza kukidhi mahitaji yaliyopo kwenye maeneo ya usambazaji wa huduma. Katika mwaka 2010/2011 Wizara yangu itaendelea na utafiti wa vyanzo mbadala vya maji ili kuweza kukidhi mahitaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *EWURA* ina jukumu la kuhakikisha kuwa miundombinu ya majisafi na majitaka inafanya kazi kwa ufanisi unaotakiwa. Katika mwaka 2009/2010, *EWURA* ilifanya ukaguzi wa miundombinu na kuelekeza namna ya kuboresha ufanisi katika Mamlaka 32 za Majisafi na Majitaka. Mamlaka hizo ni za Moshi, Dodoma, Arusha, Shinyanga, KASHWASA, Kahama, Morogoro, Singida, Mbeya, Iringa, Babati, Mwanza, *DAWASA/DAWASCO*, Lindi, Mtwara, Dakawa, Mvomero, Mahenge, Kilosa, Mikumi, Gairo, Ifakara, Nzega, Ushirombo, Bunda, Musoma, Biharamulo, Muleba, Kasumulu, Vwawa na Kilolo. *EWURA* itaendelea kukagua miundombinu ya Mamlaka ili kuhakiki viwango vya huduma za majisafi na majitaka zitolewazo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *EWURA* ina jukumu la kudhibiti bei za huduma za majisafi na majitaka kwa lengo la kulinda maslahi ya watumiaji na wawekezaji kulingana na sera ya maji. Maslahi hayo ni kiwango cha ubora wa huduma unaokubalika. Katika mwaka 2009/2010, *EWURA* ilipokea na kuchambua maombi 15 ya bei za maji. Maombi yote yalipata kibali cha kubadilisha bei. *EWURA* iliidhinisha bei mpya za maji kwa Mamlaka za *DAWASA/DAWASCO*, Nzega, Bunda, Biharamulo, Tunduma, Musoma, Mbalizi, Babati, Dodoma, Muleba, Kilolo, Vwawa, Iringa na Kasumulu. Mwaka 2010/2011, *EWURA* itaendelea kupokea, kuchambua na kuyafanyia maamuzi yanayostahili maombi yatakayowasilishwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara yangu inatekeleza Programu ya Kuendeleza Sekta ya Kilimo *(Agricultural Sector Development Programme – ASDP)* na inatekeleza

Mkakati wa Maendeleo ya Sekta ya Kilimo (*Agricultural Sector Development Strategy – ASDS).* Katika utekelezaji wa *ASDP*, malengo makuu ni pamoja na kuongeza tija katika kilimo na mapato ya wakulima na kuwawezesha wakulima kupata mafunzo na teknolojia za kisasa. Sekta ya Umwagiliaji imepewa kipaumbele katika Programu ya Maendeleo ya Sekta ya Kilimo kwa kuwa inachangia katika ongezeko la uzalishaji wa mazao ya kilimo na uhakika wa chakula.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kilimo cha umwagiliaji kwa kiwango kikubwa kinatekelezwa katika ngazi ya wilaya chini ya Mipango ya Maendeleo ya Kilimo ya Wilaya *(District Agricultural Development Plans – DADPs).* Asilimia 75 ya mahitaji yote ya Programu ya Maendeleo ya Sekta ya Kilimo ni kwa ajili ya kutekeleza maendeleo ya kilimo cha umwagiliaji. Katika Programu hiyo, zipo fedha za nyongeza ambazo miradi inayoanzishwa chini ya *DADPs* inaweza kupatiwa ili kuziba upungufu kwa lengo la kukamilisha utekelezaji. Fedha hizo zinatoka kwenye Mfuko wa Kuendeleza Umwagiliaji katika ngazi ya Wilaya *(District Irrigation Development Fund – DIDF).* Upo pia Mfuko wa Kuendeleza Umwagiliaji katika Ngazi ya Taifa *(National Irrigation Development Fund – NIDF).* Mfuko huo unatumika kugharamia uendelezaji wa skimu za umwagiliaji zenye gharama kubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara yangu kupitia ofisi saba za kanda za umwagiliaji, inatoa utaalam unaohitajika katika kutayarisha miradi ya umwagiliaji ili ijumuishwe katika Mipango ya Maendeleo ya Kilimo ya Wilaya. Utaalam huu unahusisha pia ufafanuzi wa matumizi ya miongozo ya kuanzisha, kuendeleza na kuendesha skimu za umwagiliaji ili kuwezesha skimu hizo ziwe na tija na ziwe endelevu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2009/2010, Sekta ya Umwagiliaji ililenga katika kutekeleza maeneo ya kipaumbele yafuatayo:-

(i) Kukamilisha ujenzi, ukarabati na uboreshaji wa miundombinu ya umwagiliaji kwenye skimu za wakulima wadogo. Hizi ni skimu ambazo hazifanyi kazi kwa viwango vinavyotakiwa kutokana na sababu mbalimbali.

(ii) Kufanya upembuzi yakinifu na usanifu wa miradi kwenye maeneo yanayofaa kwa umwagiliaji.

(iii) Kujenga miradi mipya katika maeneo yenye uwezekano wa kuendelezwa.

(iv) Kujenga mabwawa ya ukubwa mbalimbali kwa ajili ya kuhifadhi maji kwa matumizi ya kijamii na kiuchumi.

(v) Kuhamasisha matumizi ya teknolojia mbalimbali za umwagiliaji zinazotumia maji kwa ufanisi na tija.

(vi) Kuhamasisha matumizi ya maji chini ya ardhi kwa ajili ya umwagiliaji.

(vii) Kuhamasisha matumizi ya teknolojia zinazotumia nishati mbadala.

(viii) Kuimarisha na kuendeleza tafiti mbalimbali ili kuongeza ufanisi na tija katika matumizi ya rasilimali za maji na ardhi bila kuathiri mazingira.

(ix) Kukamilisha utayarishaji wa Sera ya Umwagiliaji, Mkakati wa Umwagiliaji na Sheria ya Umwagiliaji.

(x) Kufanya tathmini ya kimkakati ya mazingira na masuala ya kijamii (*Strategic Environmental and Social Assessment - SESA)* katika Sera ya Umwagiliaji na Mpango Kabambe wa Taifa wa Umwagiliaji kama inavyoelekezwa na Sheria ya Mazingira ya Mwaka 2004.

(xi) Kukamilisha utayarishaji wa miongozo ya kuanzisha, kuendeleza na kuendesha skimu za umwagiliaji katika ngazi ya Wilaya.

(xii) Kufanya mapitio ya Mpango Kabambe wa Taifa wa Umwagiliaji *(National Irrigation Master Plan)*; na

(xiii) Kutoa mafunzo kwa watumishi na wakulima katika maeneo mbalimbali yanayohusu uendelezaji, uendeshaji na utunzaji wa miundombinu ya umwagiliaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imepanga kujenga miundombinu ya umwagiliaji katika mikoa sita iliyopewa kipaumbele kutokana na uwezo wake mkubwa wa kuzalisha mazao ya chakula na biashara. Mikoa hiyo ni Morogoro, Mbeya, Iringa, Ruvuma, Rukwa na Kigoma. Katika mwaka 2010/2011, Wizara yangu imeainisha maeneo ya kipaumbele katika sekta ya umwagiliaji kama yafuatayo:-

(i) Kuboresha kwa kukarabati miundombinu ya umwagiliaji katika skimu za wakulima wadogo, kujenga skimu mpya katika maeneo yanayofaa kuendelezwa na kufanya upembuzi yakinifu na usanifu wa skimu.

(ii) Kujenga mabwawa ya ukubwa mbalimbali ili kuhifadhi maji kwa ajili ya umwagiliaji na kuendeleza teknolojia ya uvunaji wa maji ya mvua katika maeneo kame. Kuhamasisha matumizi ya teknolojia za umwagiliaji zenye ufanisi na tija katika upatikanaji, matumizi ya maji pamoja na matumizi ya maji chini ya ardhi.

(iii) Kuimarisha na kuendeleza tafiti mbalimbali zinazohusu umwagiliaji ili kuongeza ufanisi na tija katika matumizi ya rasilimali za maji na ardhi bila kuathiri mazingira pamoja na kuendelea kufanya tathmini ya kimkakati ya mazingira na masuala ya kijamii *(Strategic Environmental and Social Assessment – SESA).*

(iv) Kusambaza Sera ya Umwagiliaji, kukamilisha uandaaji wa mkakati wa umwagiliaji pamoja na sheria ya umwagiliaji na kuendelea na mapitio ya Mpango Kabambe wa Taifa wa Umwagiliaji *(National Irrigation Master Plan);* na

(v) Kutoa mafunzo kwa wataalam na wakulima katika maeneo mbalimbali yanayohusu uanzishaji, uendelezaji, uendeshaji na utunzaji wa miundombinu ya umwagiliaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2009/2010, Wizara yangu ilipanga kufanya upembuzi yakinifu na usanifu wa skimu za umwagiliaji 80 zenye kuwezesha kumwagilia eneo la jumla ya hekta 160,000. Kati ya lengo hilo jumla ya skimu 65 zenye eneo la hekta 143,040 sawa na asilimia 89.4 ya eneo lililopangwa, zilitekelezwa. Utekelezaji huu ulifanyika katika kanda zote saba za umwagiliaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2010/2011, Wizara yangu itaendelea kufanya upembuzi yakinifu na usanifu wa miradi 30 ya umwagiliaji yenye ukubwa wa eneo la jumla ya hekta 95,000 katika Kanda zote saba za umwagiliaji ili iwepo miradi ya umwagiliaji iliyo tayari kwa uwekezaji.

Maeneo yatakayohusika katika kanda ni kama ifuatavyo: Kanda ya Kati (hekta 5,000), Morogoro (hekta 25,000), Tabora (hekta 15,000), Mwanza (hekta 10,000), Kilimanjaro (hekta 10,000), Mbeya (hekta 20,000) na Mtwara (hekta 10,000).

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika utekelezaji wa Programu ya Maendeleo ya Sekta ya Kilimo, Wizara yangu katika mwaka 2009/2010, ilipanga kuendeleza skimu za umwagiliaji zenye eneo la jumla ya hekta 27,726 kwa kujenga miundombinu ya umwagiliaji. Eneo la jumla ya hekta 20,745 limeendelezwa. Utekelezaji huu ni sawa na asilimia 75 ya lengo lililokusudiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ujenzi wa mabwawa sita kwa ajili ya umwagiliaji uliendelea na upo katika hatua mbalimbali za utekelezaji kama ifuatavyo: Mabwawa ya Msoga (Bagamoyo), Itumbiko (Kibondo) na Budushi (Nzega) yamekamilika. Ujenzi wa Bwawa la Ulyanyama (Sikonge) umekamilika na kazi inayoendelea ni ya kuimarisha matoleo ya maji. Ujenzi wa Bwawa la Misozwe (Muheza) umefikia asilimia 50 na utakamilika mwaka wa fedha 2010/2011. Ujenzi wa Bwawa la Kahama/Nkhalanga (Nzega) umefikia asilimia 30.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2010/2011, Wizara yangu itakarabati na kuendeleza jumla ya skimu 25 zenye eneo la hekta 18,000. Eneo hilo litajumuisha ujenzi na ukarabati wa mabwawa 8 yenye uwezo wa kuhifadhi maji ya kutosha kumwagilia eneo la hekta 3,250. Kwa mwaka 2010/2011, Wizara yangu pia itaendelea kushirikiana na Halmashauri za Wilaya katika kuendeleza teknolojia zinazotumia maji kwa ufanisi hasa katika maeneo yanayozunguka Ziwa Victoria, Ziwa Nyasa na maeneo yenye maji chini ya ardhi. Utekelezaji huu utahusisha uhamasishaji wa matumizi ya pampu zinazoendeshwa kwa miguu, upepo, mionzi ya jua na dizeli kwa ajili ya kusukuma maji kwa matumizi ya umwagiliaji na matumizi mengine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2009/2010 Wizara yangu iliendelea kusimamia utekelezaji wa miradi ya umwagiliaji iliyoibuliwa na wakulima na kujumuishwa katika Mipango ya Maendeleo ya Kilimo ya Wilaya (*DADPs*). Wataalam wa Kanda za Umwagiliaji wameendelea kutoa ushauri wa kitaalam katika utayarishaji,

usanifu na usimamizi wa utekelezaji wa miradi ya umwagiliaji inayojumuishwa kwenye mipango hiyo. Kutokana na ushauri huo, skimu 183 zilipata jumla ya shilingi bilioni 13.54 kupitia *DADPs*. Kati ya skimu hizo, skimu 94 zilipata shilingi bilioni 23 kutoka katika Mfuko wa Kuendeleza Umwagiliaji ngazi ya Wilaya (*DIDF*).

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2010/2011, Wizara yangu kwa kutumia wataalam walio katika Kanda za Umwagiliaji, itaendelea kutoa huduma za kitaalam kwa Halmashauri za Wilaya katika kuandaa na kusimamia utekelezaji na uendeshaji wa miradi ya umwagiliaji. Jumla ya skimu 225 zitaendelezwa kupitia *DADPs* kwa gharama ya shilingi bilioni 19.635. Kati ya skimu hizo, jumla ya skimu 113 zitaendelezwa kupitia *DIDF* kwa gharama ya shilingi bilioni 31.107. Baadhi ya skimu hizo ni Ugalla, Kasyabone, Minepa, Kinyope, Mbambo, Muhwazi, Mang'ola, Kifunda, Mitumbati, Ngana, Mlambalasi, Kimwangamao, Katela/Ntaba, Katuka, Ulongambi, Mongoroma/Serya, Kisegese, Kyota, Kakese, Mbaka, Maliwanda na Chanzuru.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2009/2010, Wizara yangu iliendelea kuhamasisha wadau katika matumizi ya teknolojia za umwagiliaji kwa njia ya matone *(drip irrigation system*) katika maeneo yote yenye maziwa, mito na yenye uwezekano wa kupata maji chini ya ardhi. Kazi hii ilihusisha uhamasishaji, usimamizi wa kutumia pampu zinazoendeshwa kwa miguu, upepo, mionzi ya jua na dizeli kwa ajili ya kusukuma maji kwa matumizi ya umwagiliaji. Wizara iliendeleza mashamba ya mfano 10 katika Kanda ya Mwanza kwa kutumia maji ya Ziwa Victoria ambapo jumla ya hekta 200 ziliendelezwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kuhamasisha matumizi bora ya maji na yenye ufanisi, Wizara yangu imeendelea kusimamia mashamba madogo ya mfano ya umwagiliaji kwa njia ya matone katika maeneo mbalimbali kama vile Halmashauri za Wilaya za Iringa, Chamwino, Moshi Vijijini na Kanda za Umwagiliaji za Kilimanjaro, Morogoro, Mwanza, Mbeya na Mtwara. Maeneo mengine ni Kanda za Maonesho ya Nane Nane za Arusha, Morogoro, Mbeya na Dodoma. Wizara imeendelea kusimamia vituo vya mfano vilivyoanzishwa katika shule za sekondari, vyuo na taasisi kwenye Kanda za Umwagiliaji kama ifuatavyo: Kilimanjaro (6), Morogoro (2), Mbeya (3) na Tabora (5). Katika mwaka 2010/2011, Wizara yangu itaendelea kuhamasisha wadau katika matumizi ya teknolojia za umwagiliaji zenye ufanisi na tija katika matumizi ya maji kama vile umwagiliaji kwa njia ya matone na umwagiliaji wa kunyunyizia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kuwa na kilimo cha umwagiliaji cha kitaalam, chenye tija na endelevu, suala la kuendeleza utafiti wa kuwezesha kutatua changamoto za kitaalam kwa wakulima wa umwagiliaji *(Applied Research)* ni muhimu. Katika mwaka 2010/11, Serikali kwa kushirikiana na Serikali ya Japan itaanza maandalizi ya ujenzi wa kituo cha utafiti na mafunzo ya umwagiliaji katika Mkoa wa Morogoro. Kituo hiki kitatumika kufanya tafiti na mafunzo yenye lengo la kukabiliana na changamoto mbalimbali katika uendelezaji wa umwagiliaji hapa nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2009/2010, Wizara yangu ilikamilisha utayarishaji wa Sera ya Umwagiliaji. Katika mwaka 2010/2011 kazi ya usambazaji wa

Sera hiyo na kuitafsiri kwa lugha ya kiswahili na lugha nyepesi itaendelea. Wizara pia, itaendelea kukamilisha uandaaji wa Mkakati wa Kuendeleza Umwagiliaji, kufanya mapitio ya Mpango Kabambe wa Taifa wa Umwagiliaji pamoja na kuandaa sheria ya umwagiliaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2009/2010 Wizara yangu iliandaa na kutoa mafunzo kwa wakulima 510 ambapo kati ya hao 250 walipewa mafunzo juu ya kuendeleza teknolojia sahihi za umwagiliaji na matumizi bora ya maji na 260 walipatiwa mafunzo ya matumizi ya teknolojia ya kuvuna maji na uendeshaji wa skimu za umwagiliaji. Vilevile, wataalam 30 wa ngazi mbalimbali za umwagiliaji walipewa mafunzo ya kuendeleza teknolojia sahihi za matumizi bora ya maji. Mafunzo haya yalifanyika hapa nchini na nje ya nchi katika Nchi za Misri, Japan, Afrika ya Kusini, China, Ethiopia, Kenya, Korea ya Kusini, Uturuki, Sudan na India.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2010/2011, Wizara yangu itatoa mafunzo kwa watumishi 50 na wakulima 350 katika fani za matumizi bora ya maji, uendeshaji na utunzaji wa miundombinu ya umwagiliaji. Wataalam watapewa mafunzo kuhusu usimamizi wa ujenzi wa miundombinu ya umwagiliaji, utafiti na teknolojia mbalimbali za umwagiliaji. Wizara yangu itaimarisha usimamizi wa utekelezaji wa shughuli za umwagiliaji kwa kushirikiana na Halmashauri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara yangu imeendelea kushirikiana na chuo kinachotoa mafunzo ya umwagiliaji cha Igurusi (Mbarali) katika kutoa mafunzo kwa wakulima wa skimu za umwagiliaji. Mafunzo yalitolewa katika fani za matumizi bora ya maji shambani, usimamizi na uendeshaji wa skimu za umwagiliaji. Wizara pia imetoa fursa za mafunzo kwa vitendo kwa wanafunzi wa chuo hicho. Wizara yangu imeshirikiana na Chuo cha Ufundi cha Arusha kuandaa mitaala ya ufundishaji wa kozi za umwagiliaji ngazi za vyeti, stashahada na shahada. Kupitia Chuo cha Maendeleo na Usimamizi wa Maji, Wizara inaandaa mitaala ya cheti na stashahada.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2010/2011, Wizara yangu itaendelea kushirikiana na vyuo mbalimbali katika kutoa mafunzo katika fani ya umwagiliaji kwa wataalam na wakulima kama ifuatavyo:-

(i) Kuendelea kukijengea uwezo Chuo cha Maendeleo na Usimamizi wa Maji ili kiweze kutoa wataalam wa umwagiliaji wa kutosha na wenye sifa zinazohitajika kusimamia uendeshaji endelevu wa skimu za umwagiliaji. Kwa kushirikiana na Wizara ya Mawasiliano, Sayansi na Teknolojia, Wizara yangu itachangia katika kuandaa mitaala kwa ajili ya fani ya umwagiliaji katika Chuo cha Sayansi na Teknolojia cha Mbeya *(Mbeya Institute of Science and Technology - MIST).* Wizara yangu pia, itashirikiana na Chuo Kikuu cha Kilimo cha Sokoine katika kuboresha mitaala inayohusu mafunzo ya umwagiliaji ili yakidhi changamoto zilizo katika sekta ya umwagiliaji;

(ii) Kuendelea kushirikiana na Wizara ya Kilimo Chakula na Ushirika na Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi katika kuvijengea uwezo Chuo cha Kilimo cha

Igurusi (Mbeya), Chuo cha Mafunzo ya Kilimo (*Kilimanjaro Agricultural Training Centre – KATC)* na Chuo cha Ufundi Arusha ili viweze kutoa wataalam wa umwagiliaji;

(iii) Kushirikiana na Wizara ya Kilimo Chakula na Ushirika katika kukitumia Chuo cha Wakulima cha Mkindo (Mvomero) kutoa mafunzo ya matumizi bora ya maji na uendeshaji wa skimu za umwagiliaji kwa wakulima; na

(iv) Kukamilisha ujenzi wa Chuo cha Wakulima cha Kifunda (Rungwe) kwa ajili ya kutoa mafunzo ya matumizi bora ya maji na uendeshaji wa skimu za umwagiliaji kwa wakulima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2009/2010, Wizara yangu kwa kushirikiana na Serikali ya Japan kupitia JICA, ilikamilisha utayarishaji wa miongozo ya kitaalam ya kutekeleza miradi ya umwagiliaji kupitia Mipango ya Maendeleo ya Kilimo ya Wilaya. Miongozo hiyo imesambazwa katika Halmashauri zote. Wizara imekamilisha makubaliano na Serikali ya Japan ya kuendeleza awamu ya pili ya mradi wa ushirikiano wa kitaalam kati ya Tanzania na Japan *(Tanzania Japan Technical Cooperation Project - TCP)*, baada ya kukamilika kwa awamu ya kwanza iliyowezesha uandaaji wa miongozo hiyo. Utekelezaji utaanza katika mwaka 2010/2011 na utakuwa wa muda wa miaka mitatu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2010/11, nchi yetu imebahatika kupata mradi wa *Agricultural Water Solutions*, utakaofadhiliwa na taasisi ya hiari ya *Bill and Melinda Gates Foundation.* Mradi huu unatokana na jitihada ya Shirika la Chakula la Umoja wa Mataifa *(FAO)* na Mfuko wa Kimataifa wa Maendeleo ya Kilimo *(IFAD)* kuangalia matumizi ya maji kwa watu maskini vijijini. Madhumuni ya mradi huu ni kuangalia jinsi ya kuongeza ufanisi wa matumizi ya maji kwa kilimo na kuainisha fursa za uwekezaji kwa wakulima wadogo ili kupambana na umaskini. Utekelezaji wa mradi huu utafanyika kwa kushirikiana na taasisi zifuatazo*: International Water Management Institute (IWMI), International Food Policy Research Institute (IFPRI), Stockholm Environment Institute (SEI) na International Development Enterprises (IDE).*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika maandalizi ya mradi huu, nchi sita zilipendekezwa baada ya kukidhi vigezo. Vigezo hivyo ni pamoja na uzingatiaji wa matumizi ya maji kwa kilimo, uwepo wa dhana ya kupambana na umaskini vijijini na utekelezaji unaoridhisha wa malengo ya miradi inayopata misaada kutoka kwa wafadhili. Nchi zilizopata mradi huu ni Tanzania, Burkina Faso, Ethiopia, Ghana, Zambia na majimbo mawili ya India ambayo ni Madhya Pradesh na West Bengal.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara yangu kupitia Chuo cha Maendeleo na Usimamizi wa Maji, ina jukumu la kujenga uwezo wa wataalam wa fani za ufundi katika uendelezaji na usimamizi wa matumizi ya maji. Kwa kushirikiana na Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Washirika wa Maendeleo, Wizara ilitekeleza mapendekezo yaliyoainishwa kwenye Mkakati wa Muda wa kati na Mpango wa Uendeshaji wa Wakala wa Chuo cha Maendeleo na Usimamizi wa Maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2009/2010, Chuo kilidahili wanafunzi 122 na kuwa na jumla ya wanafunzi 269 wa stashahada. Kati ya hao, wanafunzi 48 walihitimu mafunzo katika fani mbalimbali mwezi Mei 2010. Fani husika na idadi ya wanafunzi waliohitimu ni kama ifuatavyo: uhandisi wa maji (32), utafutaji wa maji chini ya ardhi na uchimbaji visima (6), sayansi ya maji (*Hydrology*) (5) na teknolojia ya maabara za uchunguzi wa maji (5). Vilevile, mafundi sanifu *(Artisans)* 65 walihitimu mafunzo katika fani mbalimbali zinazohusiana na sekta ya maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kukiboresha Chuo, Wizara ilinunua vifaa na nyenzo muhimu kwa ajili ya kuimarisha mafunzo ikiwa ni pamoja na magari 8 na vitabu. Zabuni kwa ajili ya kuwapata wataalam washauri wa kusanifu mabweni manne, madarasa na karakana kwa ajili ya ukarabati zimeandaliwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2010/2011, Wizara yangu kupitia Chuo cha Maendeleo na Usimamizi wa Maji itaendelea kutoa mafunzo kwa mafundi sanifu na sadifu wa sekta ya maji. Chuo kitaanza kutoa mafunzo katika ngazi ya shahada ya kwanza kwa kudahili wanafunzi wapatao 100. Wanafunzi 135 wapya wa ngazi ya stashahada watadahiliwa ikilinganishwa na 122 kwa mwaka 2009/2010. Chuo kitatoa mafunzo kwa mafundi sadifu 80 katika daraja la kwanza hadi la tatu katika fani mbalimbali zinazohusiana na sekta za maji na umwagiliaji. Chuo kitasajili washiriki 500 wa kozi fupi katika fani mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka 2010/2011, Chuo kitaendelea kutekeleza mapendekezo yaliyoainishwa kwenye Mkakati wa Muda wa Kati na Mpango wa Uendeshaji wa Wakala wa Chuo ikiwa ni pamoja na:-

(i) Kununua vifaa kwa ajili ya mafunzo na kukarabati mabweni sita pamoja na madarasa;

(ii) Kukamilisha mitaala kwa ajili ya stashahada ya umwagiliaji na shahada ya uhandisi wa maji na kuanza kudahili wanafunzi wa mafunzo ngazi ya stashahada ya umwagiliaji na shahada ya uhandisi wa maji;

(iii) Kuboresha mitaala ya stashahada katika fani zote;

(iv) Kuboresha mifumo ya kimenejimenti na teknolojia ya mawasiliano kwa njia ya kompyuta; na

(v) Kuimarisha utafiti na ushauri wa kitaalam katika masuala mbalimbali yanayohusu maendeleo ya sekta za maji na umwagiliaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2009/2010, Wizara iliendelea kuujengea uwezo Wakala wa Uchimbaji wa Visima na Ujenzi wa Mabwawa (DDCA), ili kuuwezesha kutoa huduma ya uchimbaji wa visima na ujenzi wa mabwawa kwa ufanisi. Katika kipindi hicho, Wakala umechimba visima virefu 267 nchini kote na unaendelea na ujenzi wa Bwawa la Misozwe (Muheza). Jumla ya maeneo 236 yamefanyiwa uchunguzi

wa maji chini ya ardhi kwa ajili ya uchimbaji wa visima virefu. Wizara imenunua mitambo miwili *(bulldozer* na *excavator)* ya kujenga mabwawa na vifaa vya kupimia maji chini ya ardhi. Tathmini ya kumpata mzabuni wa kuleta mitambo mitano na vifaa vya uchimbaji wa visima virefu imekamilika. Taratibu za kumpata mzabuni atakayeleta vifaa vya usanifu wa mabwawa na vifaa vya maabara ya udongo zinaendelea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2010/2011, Wizara kupitia Programu ya Maendeleo ya Sekta ya Maji itaendelea kuimarisha Wakala kwa kununua mitambo mitatu mipya ya uchimbaji wa visima na mitambo miwili ya ujenzi wa mabwawa pamoja na vifaa vya usanifu wa mabwawa na vifaa vya maabara ya udongo. Wakala utachimba visima virefu 600 katika maeneo mbalimbali nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Bohari Kuu ya Maji ina jukumu la kununua, kuhifadhi na kusambaza vifaa na nyenzo ikiwa ni pamoja na mabomba na viungio vyake; pampu za kusukuma maji na vipuri vyake; dira za maji na dawa za kutibu na kusafisha maji zenye ubora unaotakiwa, kwa bei nafuu na kwa wakati uliopangwa. Katika mwaka 2009/2010 Bohari Kuu ya Maji iliendelea na shughuli zake za kusambaza vifaa vya maji katika Halmashauri, Mamlaka za Maji na miradi mbalimbali ya maji hapa nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hatua za kuibadili Bohari Kuu ya Maji kuwa Wakala wa Serikali zimeanza. Lengo ni kuiboresha ili iweze kutoa mchango mkubwa zaidi katika upatikanaji wa vifaa vya miradi ya maji. Katika mwaka 2010/2011, Wizara yangu itaendelea na taratibu za kuibadili Bohari hiyo kuwa Wakala wa Serikali. Wizara itatekeleza mpango wa kuhamisha shughuli za Bohari Kuu ya Maji kwenda eneo la Boko, Dar es Salaam, eneo ambalo ni kubwa zaidi kwa kuhifadhi vifaa na dawa za kutibu na kusafisha maji. Mpango huu, utawezesha upanuzi wa shughuli za ugavi wa vifaa na nyenzo za ujenzi wa miradi ya maji na umwagiliaji. Vifaa na nyezo za miradi ya umwagiliaji ni pamoja na pampu za kusukuma maji, matanki ya maji na mabomba kwa ajili ya umwagiliaji wa njia ya matone na unyunyiziaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka jana Bunge lako Tukufu lilipitisha Sheria ya Usimamizi wa Rasilimali za Maji, Sheria Na.11 ya Mwaka 2009 na Sheria ya Huduma za Maji na Usafi wa Mazingira, Sheria Na. 12 ya Mwaka 2009. Nachukua nafasi hii kulitaarifu Bunge lako kuwa, Sheria hizo zimeanza kutumika rasmi tarehe 1 Agosti 2009. Katika mwaka 2009/2010, Wizara yangu iliendelea kusambaza sheria hizo kwa Halmashauri, Ofisi za Mabonde ya Maji, Mamlaka za Maji na wadau wengine wa Sekta ya Maji. Wizara inaendelea na maandalizi ya Kanuni za Sheria hizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sheria ya Usimamizi wa Rasilimali za Maji, Sheria Na.11 ya Mwaka 2009, ina maeneo 41 yanayohitaji Kanuni. Hadi sasa Kanuni mbili zinazohusu usajili wa vyombo vya watumiaji maji *Water Resources Management (Registration of Water Users Association) Regulations, 2009* na *Water Supply and Sanitation (Registration of Community Owned Water Supply Organizations) Regulations, 2009)* zimetangazwa kwenye Gazeti la Serikali kupitia Matangazo ya Serikali GN. 21 na 22 ya tarehe 22 Januari, 2009 na zimeanza kutumika. Kanuni mbili zinazohusu uteuzi wa Wajumbe wa Bodi *(The Water Resources Management (Procedure for Nomination of*

*Board Members) Regulations 2010)* na taratibu za utoaji vibali vya matumizi ya maji na umwagaji majitaka *(The Water Resources Management (Water Abstraction, Use and Discharge) Regulations 2010)* zimesainiwa tayari kwa kutangazwa kwenye Gazeti la Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sheria ya Huduma za Maji na Usafi wa Mazingira, Sheria Na. 12 ya Mwaka 2009, ina maeneo 11 yanayohitaji Kanuni. Rasimu za Kanuni mbili zinazohusu utoaji huduma za maji *(Water Supply Regulations)* na uunganishaji wa Mamlaka za maji *(clustering of water utilities),* zimeandaliwa. Maoni ya wadau yanakusanywa kabla ya kuzikamilisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2010/2011 Wizara yangu itaendelea kukamilisha uandaaji wa Kanuni za Sheria ya Usimamizi wa Rasilimali za Maji na Sheria ya Huduma za Maji na Usafi wa Mazingira. Wizara itaendelea kutoa ushauri wa kisheria kwa wadau wote wa sekta za maji na umwagiliaji pale unapohitajika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara yangu inatambua uhusiano uliopo kati ya athari zinazotokana na uharibifu wa mazingira na uchafuzi wa vyanzo vya maji. Katika mwaka 2009/2010, Wizara yangu kwa kushirikiana na Baraza la Taifa la Usimamizi wa Mazingira *(NEMC),* ilitoa mafunzo ya tahadhari za kimazingira na kijamii katika utekelezaji wa miradi ya maji ili kuwajengea uwezo wataalam 375 kutoka Ofisi za Mabonde (49), Halmashauri (259), Mamlaka za Maji (18), Kanda za Umwagiliaji (11) na Ofisi za Mikoa (18). Kwa mwaka 2010/2011, Wizara yangu itaendelea na jitihada za kutoa elimu ya mazingira kwa wadau wengi zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2009/2010, Wizara yangu iliendelea kuimarisha na kuboresha mawasiliano baina yake na wadau wa sekta za maji na umwagiliaji, kwa kutoa taarifa na kuelimisha wadau wake kupitia vyombo mbalimbali vya habari. Jumla ya vipeperushi 10,000 vilisambazwa, vipindi 93 vya redio na televisheni vilitayarishwa na makala 15 za magazeti zilitolewa. Wizara imeendelea kuboresha tovuti yake kwa kuandaa na kutoa taarifa kwa lugha za kiswahili na kiingereza ili zieleweke kwa wadau wote. Elimu kuhusu sekta ya maji na sekta ya umwagiliaji imeendelea kutolewa kwa wananchi na wadau wengine kupitia Ofisi za Maji za Mabonde, Ofisi za Kanda za Umwagiliaji, Mamlaka za Maji za Miji Mikuu ya Mikoa na Halmashauri ikiwa ni utekelezaji wa Mkakati wa Mawasiliano wa Programu ya Maendeleo ya Sekta ya Maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2010/2011, Wizara yangu itaendelea kuelimisha wananchi juu ya masuala ya sekta za maji na umwagiliaji ikiwa ni pamoja na Sheria Mpya za Maji, Sera ya Umwagiliaji na Utunzaji wa Mazingira. Wizara itaendelea kutoa elimu juu ya Sera ya Maji, Sera ya Umwagiliaji na Mkakati wa Maendeleo ya Sekta ya Maji kwa lugha nyepesi kupitia vyombo vya habari, tovuti na vipeperushi. Jumla ya vipeperushi 10,000 vitasambazwa. Vipindi 50 vya redio na televisheni vitatayarishwa na makala 20 za magazeti zimepangwa kutolewa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kipindi cha 2009/2010 Wizara yangu ilikamilisha mpango mkakati wa matumizi ya teknolojia ya habari na mawasiliano kama

hatua muhimu katika uendelezaji na kujenga uwezo wa usimamizi na matumizi endelevu ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEKNOHAMA) kwa kipindi cha miaka mitano (2010 – 2014). Wizara inaendelea na matengenezo ya mfumo wa kompyuta wa utunzaji na ufuatialiaji wa majalada na kukamilisha utengenezaji wa mfumo wa kompyuta wa ukusanyaji wa takwimu na taarifa zinazohusu utekelezaji wa Programu ya Maendeleo ya Sekta za Maji na Umwagiliaji katika ngazi ya Wizara; Ofisi za Mabonde; Mamlaka za Majisafi na Majitaka; EWURA; Ofisi za Kanda za Umwagiliaji na Halmashauri za Wilaya, Miji na Majiji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2010/2011, Wizara yangu itatekeleza mfumo wa kompyuta wa ukusanyaji na ufuatiliaji wa takwimu na taarifa zinazohusu utekelezaji wa Programu ya Maendeleo ya Sekta za Maji na Umwagiliaji. Wizara itaanzisha benki ya takwimu ya sekta za maji na umwagiliaji na kuunganisha mfumo wa mtandao wa mawasiliano wa Wizara na taasisi zake ili kurahisisha mawasiliano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara yangu pia itaanza kutekeleza mfumo wa kompyuta wa utunzaji na ufuatiliaji wa kumbukumbu na nyaraka mbalimbali *(Records Management and Files Tracking System)* ikiwa ni utekelezaji wa Mpango wa Uboreshaji wa Utumishi wa Umma *(Public Service Reform Programme).* Wizara itaandaa mwongozo wa matumizi ya TEKNOHAMA na kujenga uwezo wa wataalam wanaosimamia uendelezaji wa TEKNOHAMA katika Wizara na taasisi zake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2009/2010, Wizara yangu ilitambua umuhimu wa kutoa fursa sawa kwa jinsia zote katika kutekeleza maazimio ya mkutano wa wanawake wa *Beijing* na malengo ya MKUKUTA. Utekelezaji huo ulihusu uteuzi wa wanawake sita katika nafasi za kutoa maamuzi, ambapo Mkurugenzi mmoja na Wakurugenzi Wasaidizi watano waliteuliwa. Wizara inashiriki katika Maadhimisho ya Siku ya Wanawake Duniani kila mwaka. Mwongozo kuhusu masuala ya jinsia umeandaliwa. Miongozo ya mafunzo inayohusu masuala ya jinsia kwa watumishi na uwakilishi katika Kamati za Kisekta, Bodi za Mamlaka za Maji na Mabonde ya Maji umetolewa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mwaka 2010/2011, Wizara yangu itaendelea kutoa fursa sawa kwa jinsia zote katika ngazi za maamuzi na kukamilisha mwongozo kuhusu masuala ya jinsia. Vilevile, Wizara itaendelea kutoa mafunzo kuhusu uelewa wa masuala ya jinsia kwa watumishi 150.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2009/2010, Wizara yangu imeendelea kutekeleza awamu ya pili ya Mkakati wa Kitaifa wa Kuzuia na Kupambana na Rushwa. Wizara kwa kushirikiana na Ofisi ya Rais, Utawala Bora na Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa, iliendelea kuwaelimisha watumishi umuhimu wa kushiriki katika kuziba mianya ya rushwa. Wajumbe wa Bodi ya Ununuzi ya Wizara walipatiwa mafunzo ya Sheria ya Ununuzi, Sheria Na. 4 ya Mwaka 2004 na Kanuni zake. Lengo likiwa ni kuzingatia taratibu zilizowekwa za ushindani ulio wazi na kuhakikisha kuwa

huduma zinaboreshwa kama ilivyoainishwa na Sheria hiyo. Wizara iliendesha mafunzo ya Huduma Bora kwa Mteja kwa watumishi 280.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mwaka 2010/11, Wizara yangu itaendelea kuimarisha mapambano dhidi ya rushwa katika Sekta za Maji na Umwagiliaji. Mapambano hayo yatahusisha utoaji wa elimu kwa watumishi kuhusu namna ya kuziba mianya ya rushwa na Utawala Bora. Wizara itaendelea kusimamia kikamilifu Sheria za Maji, Ununuzi, Matumizi ya Fedha na Sheria nyingine na Kanuni na taratibu zinazohusu maadili katika utumishi wa umma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2009/2010, Wizara iliendelea kutoa elimu ya kinga dhidi ya maambukizi ya Virusi vya UKIMWI na kuhamasisha upimaji wa hiari ili kutambua hali ya afya ya watumishi. Hadi sasa watumishi wanane wanaoishi na Virusi vya UKIMWI wamejitokeza na wanapewa huduma ya lishe ya mlo kamili na kugharamiwa matibabu. Kati yao wanne ni wanaume na wanne ni wanawake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mwaka 2010/2011, Wizara yangu itaendelea kutoa mafunzo kwa watumishi yanayohusu mbinu mbalimbali za kujikinga na maambukizi ya Virusi vya UKIMWI na umuhimu wa kupima ili kutambua hali ya afya. Vilevile Wizara yangu itaendelea kutoa lishe kamili kwa watumishi waliobainika kuwa na maambukizi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2009/2010, Wizara iliendelea kuboresha mazingira ya kazi kwa watumishi kwa lengo la kuongeza ufanisi, ikiwa ni pamoja na kuboresha muundo wa utumishi katika uendeshaji na usimamizi wa mipango ya kisekta. Wizara ina jumla ya watumishi 2,078, watumishi 365 wamepandishwa vyeo katika nafasi mbalimbali kati yao watumishi 183 ni wanawake na 182 ni wanaume. Watumishi 142 waliajiriwa katika fani mbalimbali. Mkataba wa Huduma kwa Mteja umekamilika na utazinduliwa mwezi Julai 2010. Katika mwaka 2010/2011 Wizara itaajiri watumishi 146 katika lengo la kukidhi ikama ya watumishi 2,224. Jumla ya watumishi 272 watapandishwa vyeo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2009/2010, Wizara kwa kushirikiana na taasisi za utekelezaji *(implementing agencies)* wa Programu ya Maendeleo ya Sekta ya Maji *(WSDP)*, imekamilisha kuandaa mpango wa kuwajengea uwezo watumishi *(capacity development plans).* Mpango huo umebainisha kasoro katika mifumo ya utendaji kazi, nafasi za ajira, mahitaji ya vitendea kazi na mafunzo yanayohitajika kwa watumishi. Mafunzo ya Mfumo wa Wazi wa Mapitio na Upimaji wa Utendaji Kazi (*OPRAS*) yamefanyika kwa watumishi 600 wa Makao Makuu. Utekelezaji wa *OPRAS* utaanza katika mwaka 2010/2011 kwa Watumishi wa Makao Makuu. Katika mwaka 2010/2011, Wizara inatarajia kuendesha mafunzo hayo kwa watumishi walio kwenye Ofisi za Mabonde na Kanda za Umwagiliaji. Jumla ya watumishi 435 wamepatiwa mafunzo mbalimbali ya muda mrefu na mfupi ndani na nje ya nchi ili kuwawezesha kuboresha utendaji wao wa kazi.

Katika mwaka 2010/2011, Wizara itaanza kutekeleza kikamilifu mpango wa kuwajengea uwezo watumishi kwa kutoa mafunzo ya muda mrefu na mfupi, kununua vitendea kazi na kuajiri na kurekebisha mifumo ya utendaji kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa napenda kutumia fursa hii, kuwashukuru wale wote waliochangia kwa namna moja au nyingine katika kuiwezesha Wizara yangu kufanikisha majukumu yake. Nakiri kwamba, mafanikio yaliyopatikana katika mwaka 2009/2010 ni kutokana na jitihada za pamoja, ushirikiano na misaada ya kifedha na kitaalam kutoka kwa washirika wa maendeleo, ikiwa ni pamoja na nchi wahisani, mashirika ya misaada, taasisi zisizo za Kiserikali, mashirika ya kidini na taasisi za kifedha kwa ujumla. Napenda kuzishukuru Serikali za Ujerumani, Japan, Ufaransa, Jamhuri ya Watu wa China, Uholanzi, Uswisi, Ireland, Ubelgiji, Uingereza, Korea ya Kusini, Sweden, Norway, Saudi Arabia, Misri, Israel na Marekani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile, napenda kutoa shukrani kwa taasisi za fedha za kimataifa ikiwa ni pamoja na Benki ya Dunia, Benki ya Maendeleo ya Afrika, Benki ya Kiarabu ya Maendeleo ya Afrika (*BADEA*), Benki ya Uwekezaji ya Umoja wa Ulaya *(EIB)*, Mfuko wa Maendeleo wa nchi zinazozalisha Mafuta *(OPEC Fund)*, Benki ya Maendeleo ya Ujerumani *(KfW)*, Shirika la Maendeleo la Ujerumani *(GTZ)*, Umoja wa Ulaya, Shirika la Maendeleo la Umoja wa Mataifa (*UNDP*), Shirika la Makazi Duniani *(UN Habitat)*, Shirika la Umoja wa Mataifa la Kuhudumia Watoto (*UNICEF*), Shirika la Chakula na Kilimo la Umoja wa Mataifa (*FAO*), Shirika la Kimataifa la Maendeleo ya Kilimo (*IFAD*), Shirika la Mpango wa Chakula Duniani (*WFP*), Shirika la Kimataifa la Nguvu za Atomiki (*IAEA*), Shirika la Marekani la *Millenium Challenge Cooperation (MCC)* na Shirika la Misaada la Marekani (*USAID)*, kwa misaada ya fedha na michango yao ya utaalam katika kufanikisha utekelezaji wa majukumu na malengo ya Wizara yangu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninayashukuru mashirika ya kidini ya *World Islamic League*, Shirika la *Ahmadiya Muslim Jamaat Tanzania*, *Islamic Foundation*, Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania, Kanisa la Kilutheri la Ujerumani, Baraza Kuu la Waislam Tanzania, Kanisa Katoliki Tanzania, Kanisa la Anglikana Tanzania, *Catholic Agency for Overseas Aid and Development (CARITAS)* na *Livingwater International*.

Nashukuru pia, taasisi zisizo za kiserikali za *Tanzania Water and Sanitation Network (TAWASANET)*, Wahamasishaji wa Maji, Maendeleo na Afya *(WAMMA)*, *Southern Highlands Participatory Organization (SHIPO)*, *Water Aid*, *World Vision*, *Concern*, *Netherlands Volunteers Services (SNV)*, Shirika la Kimataifa la Kuhifadhi Uasili *(IUCN)*, *World Wide Fund for Nature (WWF)*, *African Medical Research Foundation (AMREF)*, *Clinton HIV Aids Initiative (CHAI)* na *Bill and Melinda Gates Foundation* na wale wote ambao kwa njia moja au nyingine wameendelea kuzisaidia sekta za maji na umwagiliaji katika kutekeleza majukumu tuliyopewa. Naomba, kwa dhati kabisa, kupitia kwako Mheshimiwa Mwenyekiti, nitumie fursa hii kuwashukuru wote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hotuba hii haitakuwa imekamilika kabla sijatoa shukrani zangu za dhati kwa Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa dhamana na heshima kubwa aliyonipa kuiongoza Wizara ya Maji na Umwagiliaji. Kabla ya hapo, alinipa heshima kubwa ya kuwa Waziri wa Nchi katika Ofisi ya Makamu wa Rais mwenye dhamana ya kusimamia masuala ya mazingira. Naomba nitumie fursa hii kwa namna ya pekee, kutoa shukrani zangu za dhati kwa dhamana na heshima kubwa aliyonipa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, namshukuru pia, Mheshimiwa Dkt. Ali Mohamed Shein, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Nimefanya kazi chini yake kama Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais (Mazingira). Miongozo na misingi aliyoiweka imenisaidia katika kazi zangu kwani Maji na Mazingira ni sehemu mbili za sarafu moja. Natoa shukrani zangu za dhati kwa Mheshimiwa Mizengo Kayanza Peter Pinda, Waziri Mkuu; amekuwa karibu sana na Sekta za Maji na Umwagiliaji. Uongozi wake umetusaidia katika kutekeleza majukumu yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeweza kuyafanya haya yote kutokana na ushirikiano wa wananchi. Nitumie fursa hii kutoa shukrani za pekee kwa Wananchi wote wa Tanzania na wadau wengine ambao sikuweza kuwataja mmoja mmoja kwa kushirikiana na Wizara yangu katika kutekeleza majukumu yake.

Naomba kutoa shukrani za pekee kwako wewe Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Naibu Spika na Waheshimiwa Wenyeviti wa Bunge, kwa kuliongoza Bunge lako Tukufu kwa kasi na viwango na kulijengea heshima ndani na nje ya nchi. Nawashukuru pia, Waheshimiwa Wabunge wote kwa michango yao wanayotoa ndani na nje ya Bunge hili inayolenga kuboresha Sekta za Maji na Umwagiliaji. Wizara yangu itaendelea kushirikiana nao kwa lengo la kuinua hali ya maisha ya wananchi na uchumi wa Taifa kwa ujumla.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hotuba yangu haitakuwa kamili kama sitatoa shukrani za dhati kwa Wananchi wa Jimbo la Rungwe Mashariki, kwa ushirikiano mkubwa wanaonipa na kunivumilia pale ninaposhindwa kuwa nao kutokana na majukumu mengine ya Kitaifa yanayonikabili. Imani yao kwangu ni kubwa. Nami nitaendelea kuwatumikia kwa juhudi na bidii kwa kadiri Mwenyezi Mungu atakavyonijalia. Vilevile, nawashukuru Wananchi wa Jimbo la Buyungu, kwa niaba ya Mheshimiwa Mhandisi Christopher Kajoro Chiza (Mb), Naibu Waziri wa Maji na Umwagiliaji, kwa ushirikiano wanaompatia katika kutekeleza majukumu ya jimbo lake na yale ya Kitaifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kwa njia ya pekee, nitoe shukurani zangu za dhati kwa Mheshimiwa Mhandisi Christopher Kajoro Chiza (Mb), Naibu Waziri wa Maji na Umwagiliaji, kwa msaada na ushirikiano wake kwa kipindi chote tulichofanya kazi pamoja katika kuiongoza Wizara ya Maji na Umwagiliaji. Naomba pia, nitoe shukrani zangu kwa Mhandisi Christopher Nestory Sayi, Katibu Mkuu na Makatibu Wakuu waliomtangulia na ambao wamemsaidia kuisimamia Wizara, Mhandisi Patrick Rutabanzibwa na Ndugu Wilson Chiremeji Mukama, Wakuu wa Idara na Vitengo,

Viongozi wa Mashirika na Taasisi chini ya Wizara yangu, wataalam na watumishi wote kwa kujituma katika kusimamia utekelezaji wa majukumu tuliyopewa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, namshukuru Bwana Mwinyiheri Ndimbo, Katibu wa Waziri, ambaye amekuwa Katibu wangu kwa kipindi chote nilichokuwa nikiiongoza Wizara ya Maji na Umwagiliaji. Nawashukuru Makatibu Mahsusi katika ofisi yangu; Bibi Loice Mwakatundu na Bibi Janeth Petro; na Msaidizi wa Ofisi, Bibi Bevenia Myolla. Namshukuru Bwana Athumani Fernandes, dereva wangu wa miaka mingi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho lakini siyo kwa umuhimu, naishukuru familia yangu, mke wangu Lucy, watoto wetu Max, Sekela na Emmanuel, mkwe wangu Digna na wajukuu Tusekile na Lusekelo. Siku zote hawa wamekuwa nguzo iliyo imara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili Wizara yangu iweze kutekeleza majukumu na malengo yaliyoelezwa katika hotuba hii, naomba kutoa hoja kwamba, Bunge lako Tukufu liidhinishe jumla ya shilingi 251,535,392,000 kwa ajili ya matumizi ya Wizara yangu kwa mwaka 2010/2011. Kati ya fedha hizo, Matumizi ya Kawaida ni shilingi 18,442,785,000 ambapo shilingi 11,892,605,000 ni Mishahara ya Watumishi *(PE)* na shilingi 6,550,180,000 ni fedha za Matumizi Mengine *(OC).* Bajeti ya Maendeleo ni shilingi 233,092,607,000, ambapo kati ya fedha hizo shilingi 41,565,045,000 ni fedha za ndani na shilingi 191,527,562,000 ni fedha za nje.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba tena nitoe shukrani zangu za dhati kwako na kwa Waheshimiwa Wabunge kwa kunisikiliza. Hotuba hii pia inapatikana katika Tovuti ya Wizara kwa anwani *www.maji.go.tz.* Maji ni Uhai na Usafi wa Mazingira ni Utu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa heshima kubwa naomba kutoa hoja. (*Makofi*)

**WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Waziri Maji na Umwagiliaji, Mheshimiwa Profesa Mark Mwandosya, kwa hotuba nzuri sana, inayotia matumaini makubwa kwa Watanzania. Kabla sijamwita Msemaji wa Kamati ya Kilimo, Mifugo na Maji, niwataarifu Waheshimiwa Wabunge walioomba kuchangia hotuba hii mpaka sasa ni Wabunge 30 na kati yao ambao bado hawajachangia hata mara moja ni 16. Tutajitahidi kwenda kadiri tutakavyoweza. Kwa hiyo, kama mtu atachangia chini ya dakika alizonazo basi itakuwa ni vizuri kuwapa nafasi wengine wachangie. Tutakapofika kipindi hicho wa kwanza kuchangia atakuwa Mheshimiwa Madeje, atafuatiwa na Mheshimiwa Peter Serukamba na Mheshimiwa Teddy Kassela-Bantu ataendelea kujiandaa.

**MHE. JANET Z. MBENE (K.n.y. MWENYEKITI WA KAMATI YA KILIMO, MIFUGO NA MAJI):** Mheshimiwa Mwenyekiti, namshukuru Mwenyekiti wa Kamati kwa kunipa heshima ya kuwasilisha Taarifa hii ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Kilimo, Mifugo na Maji kuhusu utekelezaji wa majukumu ya Wizara ya Maji

na Umwagiliaji kwa mwaka wa Fedha 2009/2010 na Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2010/2011.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa Kanuni ya 99(7) ya Kanuni za Bunge, Toleo la 2007, naomba kuwasilisha Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Kilimo, Mifugo na Maji kuhusu utekelezaji wa Majukumu ya Wizara ya Maji na Umwagiliaji kwa Mwaka wa Fedha wa 2009/2010 na Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha wa 2010/2011.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika utekelezaji wa majukumu yake, Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Kilimo, Mifugo na Maji ilikutana na Wizara ya Maji na Umwagiliaji tarehe 28 Mei, 2010 katika Ofisi Ndogo ya Bunge ya Dar es Salaam ili kuchambua Taarifa ya Utekelezaji wa Bajeti, Maoni ya Kamati na Changamoto zilizojitokeza kwa mwaka 2009/2010. Aidha, tarehe 1Juni 2010 Kamati ilikutana tena na Wizara ili kuchambua Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara kwa Mwaka wa Fedha wa 2010/2011.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati wa kupitia na kuchambua Taarifa ya utekelezaji wa Wizara kwa mwaka wa fedha wa 2008/2009 na Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa mwaka wa fedha wa 2009/2010, Kamati ilitoa maoni na ushauri kwa Serikali. Napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa, kwa kiasi kikubwa Serikali imeyafanyia kazi maoni ya Kamati. Ninapenda kutaja baadhi ya maeneo ambayo utekelezaji wake unaonekana ni pamoja na:-

(a) Mradi wa Kimbiji na Mpera ambao tayari fedha zake za awali za utekelezaji kiasi cha shilingi bilioni 5.084 zitaanza kutolewa katika bajeti ya mwaka huu.

(b) Bwawa la Kidunda limetengewa shilingi bilioni tatu za awali za utekelezaji zitatolewa katika bajeti ya mwaka huu.

(c) Maji katika Jiji la Dar es Salaam, DAWASCO imejitahidi kwa kuongeza dira kufikia asilimia 70. Aidha, mgao wa maji ni wa uhakika zaidi kuliko ilivyokuwa katika miaka iliyotangulia.

(d) Kilimo cha umwagiliaji kinaendelea kuongezewa fedha za utekelezaji mwaka hadi mwaka.

(e) Ofisi za maji za mabonde zinaendelea kuboreshwa kwa kupatiwa vifaa muhimu, wataalam na kutoa mafunzo kwa wataalam waliopo.

(f) Katika kuimarisha huduma za maji vijijini, Wizara imeainisha watumishi 198 watakaohamishiwa Halmashauri za Wilaya ili kuzijengea uwezo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na jitihada kubwa zinazofanywa na Wizara katika kutekeleza majukumu yake, bado inakumbana na changamoto mbalimbali ambazo zimekuwa ni kikwazo katika kufikia malengo iliyojiwekea. Baadhi ya changamoto hizo ni:-

(a) Kiasi kidogo cha fedha zinazotengwa na ucheleweshaji wa utoaji fedha hizo na hivyo kuathiri utekelezaji wa baadhi ya Miradi ya Wizara.

(b) Kuongezeka kwa idadi ya watu nchini hususan katika maeneo ya mijini wakati miundombinu ya maji bado ni ya zamani hivyo kusababisha wananchi wengi kutofikiwa na huduma ya maji.

(c) Athari za mabadiliko ya tabia nchi zimesababisha ukame kwa baadhi ya maeneo na mafuriko kwa maeneo mengine ambayo yameleta uharibifu wa miundombinu ya maji na umwagiliaji.

(d) Uchafuzi wa vyanzo vya maji kutokana na matumizi ya kemikali katika maeneo ya uchimbaji wa madini.

(e) Uwezo mdogo wa utekelezaji wa miradi katika ngazi ya Halmashauri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Mwaka wa Fedha wa 2010/2011, Wizara ya Maji na Umwagiliaji chini ya Fungu 49 ili kutekeleza majukumu yake, inaomba jumla ya shilingi 251,535,392,000. Kati ya fedha hizo, shilingi 18,442,785,000 ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida na shilingi 233,092,607,000 ni kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo. Kati ya fedha za matumizi ya kawaida, shilingi 11,892,605,000 ni kwa ajili ya mishahara na shilingi 6,550,180,000 ni kwa ajili ya matumizi mengineyo.

Aidha, kati ya fedha za maendeleo, shilingi 41,565,045,000, sawa na asilimia 17.5 ni fedha za ndani na shilingi 191,527,562,000, sawa na asilimia 82.5 ni fedha za nje.

Mheshimiwa Mwenyekiti, fedha hizi zinazoombwa zitaiwezesha Wizara kutekeleza kazi mbalimbali ilizojipangia. Baadhi ya kazi zitakazotekelezwa ni pamoja na:-

(a) Kuendeleza na kusimamia rasilimali za maji kwa ajili ya maendeleo ya kijamii na kiuchumi.

(b) Kuimarisha utafiti katika usimamizi na uendelezaji wa rasilimali za maji na matumizi ya teknolojia zinazowiana.

(c) Kuratibu na kusimamia utekelezaji wa Programu ya Maendeleo ya Sekta ya Maji.

(d) Kufahamisha umma masuala yanayohusu sekta za maji na umwagiliaji.

(e) Kununua vifaa na nyenzo za kazi za Wizara.

(f) Kuandaa na kusambaza sheria za maji na kanuni zake.

(g) Kujenga, kuendesha na kuboresha benki ya takwimu ya sekta.

(h) Kutathmini miradi ili kuhakikisha inatekelezwa kulingana na fedha zilizotengwa.

(i) Kutoa miongozo kwa Bodi za Maji za Mabonde katika masuala yanayohusu Usimamizi na Uendelezaji wa Rasilimali za Maji.

(j) Kusimamia Benki ya Taifa ya Takwimu ya Rasilimali za Maji na kusambaza taarifa zinazohitajika kwa wadau.

(k) Kuratibu na kufuatilia utunzaji na udhibiti wa rasilimali za maji.

(l) Kuzijengea uwezo Maabara Kuu, Maabara za Mikoa, Kanda na Kituo cha Utafiti cha Ngurdoto.

(m) Kutathmini matokeo ya uwekezaji katika umwagiliaji kwenye skimu 15 za umwagiliaji kwenye kanda saba za umwagiliaji.

(n) Kuendelea kutekeleza Miradi ya maji katika Mamlaka za Maji ili kuongeza upatikanaji wa maji kwa wakazi wa mijini mwaka 2009/2010 hadi mwaka 2010/2015 kutoka asilimia 84.0 hadi asilimia 90 katika miji 19 ya mikoa, asilimia 50 – 60 hadi asilimia 70 kwa Jiji la Dar es Salaam na asilimia 53 hadi asilimia 57 kwa miji midogo ya mikoa na miradi ya kitaifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kuelezea utekelezaji wa maoni ya Kamati, mafanikio, changamoto zilizoikabili Wizara katika utekelezaji wa majukumu yake kwa Mwaka wa Fedha wa 2009/2010, naomba kuwasilisha maoni na ushauri kwa Serikali kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, maoni ya Jumla: Bajeti ya Wizara imekuwa ikipungua wakati mahitaji ya maji kwa matumizi ya binaadam na mifugo yakiongezeka na pia yakihitajika kwa kilimo cha umwagiliaji ili kutekeleza kaulimbiu ya Kilimo Kwanza. Fedha za ndani za maendeleo zimepungua kutoka bilioni 50 mwaka wa 2009/2010 hadi kufikia bilioni 41 kwa mwaka huu wa 2010/2011.

Hali hii itasababisha Miradi mingi kutotekelezeka kama Uboreshaji wa Huduma ya Majisafi na Majitaka kwa Jiji la Dar es Salaam na kushindwa kulipa madeni ya wakandarasi. Kutokana na hali hiyo, Kamati inashauri ifuatavyo:-

- Serikali ihakikishe inatenga fungu la kutosha kwa ajili ya kulipa madeni ya wakandarasi vinginevyo miradi mingi itakwama.

- Serikali iangalie umuhimu wa maji kwa viumbe na kilimo na hivyo kuongeza Bajeti ya Wizara hii kama inavyostahili.

- Kupunguza utegemezi kutoka kwa wafadhili kwa kuainisha na kuongeza vyanzo vingine vya mapato vya ndani ili huduma za maji zigharamiwe kwa kiwango kikubwa kutokana na mapato ya ndani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu uratibu wa Miradi katika Halmashauri. Miradi mingi ya maji na umwagiliaji ipo kwenye Halmashauri ambazo ndizo mamlaka za utekelezaji, lakini Halmashauri hizo hazina wataalam wa kutosha. Kamati bado inashauri, Serikali Kuu bado ni msimamizi wa Miradi yote nchini, hivyo isiziachie Halmashauri pekee na badala yake isimamie kuratibu ili miradi ya maji iweze kuleta matokeo mazuri. Aidha, ihakikishe wataalam zaidi wanapelekwa katika Halmashauri hizo ili kuweza kusimamia vyema miradi hiyo na hatimaye kuleta tija.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu vifaa vya miradi. Kutokana na vifaa vingi vya miradi kutumika tofauti na malengo yaliyokusudiwa, Kamati inashauri vifaa vyote vya miradi kama vile magari, mitambo na kadhalika vitumike kama ilivyokusudiwa ili kuleta ufanisi katika miradi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu Bonde la Mto Nile. Mto Nile unapita katika nchi mbalimbali katika bara letu la Afrika, hivyo basi nchi hizo zote kama Tanzania, Kenya, Uganda, Rwanda, Congo, Ethiopia, Misri, Sudan zina haki ya msingi ya kutumia maji hayo. Katika kuhakikisha kunakuwepo matumizi sahihi ya maji hayo mnamo mwaka 1999 kilianzishwa chombo kinachoitwa *The Nile Basin Initiative* na ilikubalika kusainiwe mkataba wa matumizi ya pamoja ya Mto huo.

Aidha, baadhi ya nchi kama Misri na Sudan zimekataa kusaini kutokana na kutoridhishwa na baadhi ya vipengele ambavyo kimsingi havina madhara kwa nchi yoyote ile. Kamati inaipongeza Serikali kusaini mkataba huo na inafarijika kuona Serikali inafanya maamuzi ya busara na yenye maslahi kwa Taifa hili, kwa kizazi cha leo na cha baadaye.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maji ni hitaji la msingi la maisha na uhai wa viumbe vyote katika nyanja mbalimbali ikiwa ni pamoja na uzalishaji wa umeme na mali viwandani, matumizi ya majumbani na usafi wa mazingira. Katika nchi yetu huduma ya maji bado haijatosheleza mahitaji ndiyo maana maeneo mengi wananchi wengi wanataja ukosefu wa huduma za maji kuwa ndiyo tatizo kubwa linalowasumbua. Kutokana na umuhimu huu Kamati ina ushauri ufuatao:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusiana na hali ya maji katika Jiji la Dar es Salaam. Jiji linakabiliwa na uhaba mkubwa wa maji kutokana na kukua kwake kwa kasi ikiwa ni pamoja na ongezeko kubwa la watu la asilimia nane kwa mwaka tofauti na wastani wa Kitaifa wa ongezeko la watu mijini la asilimia 4.5. Ongezeko lingine ni kukua kwa shughuli za kiuchumi ikiwa ni pamoja na ongezeko kubwa la uzalishaji viwandani na kupanuka kwa ujenzi wa makazi na kibiashara.

Kutokana na ukuaji huo wa kasi kiwango cha upatikanaji wa maji ni kati ya asilimia 50 hadi 60, kiwango ambacho hakiridhishi kabisa. Kamati inatambua na inapongeza jitihada ambazo Wizara inachukua katika kuhakikisha inapunguza tatizo la maji katika Jiji la Dar es Salaam. Mahitaji ya Maji kwa Jiji la Dar es Salaam ni kiasi cha mita za ujazo 450, 000 kwa siku lakini mpaka sasa kiasi cha maji kinachopatikana ni mita za ujazo 300,000 ikiwa ni pungufu ya mita za ujazo 150, 000. Kutokana na hali hiyo, Kamati inashauri yafuatayo:-

- Serikali ihakikishe kuwa Mradi wa Kimbiji na Mpera unafanikiwa kwa kuutengea fedha zilizoombwa hasa fedha za ndani bila ya kutegemea sana fedha za wafadhili kwani Mradi huu utaondoa kabisa tatizo la maji kwa Jiji la Dar es Salaam kutokana na visima vyake kuwa na maji mengi yanayokisiwa kufikia robo ya maji ya Ziwa Viktoria. Tuthubutu kujitegemea kama tulivyofanya kwa mradi wa maji kutoka Ziwa Victoria kwenda Kahama – Shinyanga.

- Mradi wa Bwawa la Kidunda utekelezwe. kama ilivyopangwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu hali ya Maji katika Mji wa Tabora. Huu ni Mji unaokumbwa na tatizo la maji kwa muda mrefu sasa na wananchi wa mji huo wamekuwa wakihangaika na tatizo hilo bila kupatiwa ufumbuzi wa kudumu. Kwa sababu ya hali hii, wanaoathirika zaidi ni akina mama na watoto kiasi cha kushindwa kufanya shughuli nyingine za maendeleo kwa kupoteza muda mwingi katika kutafuta maji. Kamati inashauri Serikali ihakikishe inaweka mikakati madhubuti ya kuondoa tatizo na itekeleze uamuzi wake wa kuunganisha Mji wa Tabora katika Mradi wa Maji kutoka Ziwa Victoria kwenda Kahama – Shinyanga.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu maji katika Mji wa Dodoma. Ingawa hali ya maji kwa Mji wa Dodoma inaridhisha, zipo dalili za kuanza kupungua kwa presha ya maji ikilinganishwa na ilivyokuwa zamani kiasi cha kutishia usalama wa hali ya maji hapo siku za usoni. Hii inatokana na ongezeko kubwa la watu kutokana na ujenzi wa Taasisi nyingi za elimu ya juu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inashauri kwamba, Serikali ichukue tahadhari kwa kuhakikisha kwamba hatua za haraka zinachukuliwa ikiwa ni kuongeza mtandao wa maji ili kuzuia tatizo kubwa la maji safi kuja kutokea hapo baadaye. Aidha, mfumo wa maji taka nao uzingatiwe ili kuendeleza usafi wa Mji huo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inaipongeza Serikali kwa Mpango wa Mradi wa Vijiji kumi ambao unalenga kupunguza tatizo la maji. Kupungua kwa bajeti ya

mwaka huu kutasababisha pia mradi huu nao uathirike. Kamati inaendelea kusisitiza Serikali itafute namna ya kuuendeleza mradi huu ili uwafikie wananchi wengi zaidi. Aidha, kwa mwaka ujao wa fedha bajeti ya mradi iongezwe na ipanue wigo wa mradi kwa vijiji vingi zaidi nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, biashara ya vyuma chakavu imeendelea kuleta madhara kwa miundombinu ya maji kwani tangu biashara hii ishamiri, hujuma za miundo mbinu ya maji nayo imekuwa ikiongezeka. Kamati inashauri Serikali kuchukua hatua za haraka kudhibiti biashara hii. Ipo haja ya kutoa elimu kwa wananchi juu ya athari zitokanazo na hujuma za miundombinu ikiwa ni pamoja na kuanzisha ulinzi shirikishi ili kuwabaini wote wanaojihusisha na hujuma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu upotevu wa maji. Maeneo mengi ya nchi yamekuwa yakipata mvua na hivyo kuwepo kwa maji ya kutosha kwa kipindi hicho, lakini kutokana na mifumo duni tuliyonayo, maji hayo yamekuwa yakipotea kutokana na kutokuvunwa. Aidha, maji mengine mengi ya mabomba yamekuwa yakipotea kutokana na uchakavu wa miundombinu na hivyo kuvuja, kuibiwa kwa miundombinu na wizi wa maji kwa kujiunganishia kinyume cha utaratibu. Inakadiriwa kiasi cha maji ya bomba asilimia 36 kimekuwa kikipotea kila mwaka wakati kiwango kinachokubalika ni cha asilimia 20. Kamati inaamini tukiamua tunaweza kudhibiti upotevu huu na hivyo nchi kuwa na maji yakutosha kwa binaadamu, mifugo na kilimo. Kamati inashauri yafuatayo:-

- Kutokana na Maji ya Mvua kutokuvunwa, ni vyema basi kuwekwe utaratibu wa kuhakikisha kila Ramani ya nyumba au jengo itakayopelekwa kwenye mamlaka husika ili kupata kibali cha kujenga iwe na mfumo wa uvunaji wa maji ya mvua na kuwepo na usimamizi madhubuti. Aidha, mabwawa yachimbwe karibu na mito mikubwa ili wakati wa mafuriko yale maji yaingie katika mabwawa hayo kwa ajili ya matumizi ya baadaye.

- Kutokana na uchakavu wa miundombinu kupoteza maji mengi, Serikali ihakikishe inakarabati miundombinu hiyo mara kwa mara pale inapobidi.

- Kutokana na hujuma kama ilivyoelezwa awali, biashara ya vyuma chakavu ipigwe marufuku na kuwepo ulinzi shirikishi ili kuwabaini wahujumu wa miundombinu ya maji.

- Kutokana na wizi wa maji katika Jiji la Dar es salaam kwa kujiunganishia bila kuzingatia utaratibu, Serikali kupitia *DAWASCO* ifanye msako wa mara kwa mara pia kutumia ulinzi shirikishi ili kuwabaini wezi wote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sekta ndogo ya umwagiliaji inahitaji uwekezaji wa kutosha kuwezesha upanuzi wa kilimo cha umwagiliaji ili kuongeza mazao ya chakula na biashara kwa lengo la kuwa na uhakika wa chakula na pia katika kuongeza pato la Taifa na kupunguza umasikini miongoni mwa wananchi. Kilimo cha umwagiliaji kinazalisha mara tatu zaidi ya kilimo cha kutegemea mvua na kuwezesha kulima mara tatu kwa mwaka.

Kutokana na umuhimu huu, pamoja na jitihada zinazofanywa na Serikali katika kuendeleza kilimo cha umwagiliaji hali bado siyo ya kuridhisha. Kiasi cha fedha kinachotengwa kuendeleza kilimo cha umwagiliaji kimekuwa kikiongezeka kwa kiasi kidogo sana kwa mfano, mwaka 2008/2009 ilikuwa ni shilingi bilioni 13.1, mwaka 2009/2010, shilingi bilioni 17.8 na mwaka 2010/2011 ni shilingi 18.2. Kiasi hiki ni kidogo sana ikilinganishwa na mikakati tuliyonayo ya kuhakikisha kilimo kinakua kwa kiwango kinachotakiwa. Kamati inashauri yafuatayo:-

- Serikali iongeze bajeti ya umwagiliaji kwa kadri itakavyowezekana.

- Skimu za wakulima wadogo za umwagiliaji ziimarishwe na kuenea katika maeneo mengi zaidi na ikiwezekana zifike mpaka katika ngazi ya kaya hasa katika maeneo yenye mito inayotiririka maji mwaka mzima.

- Serikali itumie wataalam wake kuwafundisha wananchi juu ya umuhimu wa umwagiliaji.

- Wananchi waelimishwe juu ya umuhimu wa kuvuna maji ya mvua kwa ajili ya kilimo cha umwagiliaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti,ili kufikia lengo la kutekeleza azma ya Kilimo Kwanza ni lazima tuwekeze katika miradi ya umwagiliaji. Katika bajeti ya Wizara ya mwaka huu haijaonekana dhahiri kuwepo kwa mikakati ya kutekeleza azma hii. Bajeti ya Wizara imeendelea kupungua, hii inadhihirisha bado hatujakipa kilimo kipaumbele kinachostahili. Kamati inashauri yafuatayo:-

- Serikali iainishe waziwazi maeneo itakayoyazingatia katika kutekeleza dhana hii na kutenga rasilimali za kutosha.

- Serikali ishirikishe Sekta Binafsi katika kilimo cha biashara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kukushukuru tena kwa kunipa nafasi hii ili kuwasilisha Taarifa ya Kamati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuwashukuru wajumbe wa Kamati kwa ushirikiano, uvumilivu na michango yao mizuri wakati wa kupitia na kuchambua kwa kina Bajeti ya Wizara hii. Naomba kuwatambua wajumbe wa Kamati kwa majina kama ifuatavyo:-

Mhe Gideon A. Cheyo, Mwenyekiti; Mheshimiwa Kidawa H. Saleh, Makamu Mwenyekiti; Mheshimiwa Kheri K. Ameir, Mjumbe; Mheshimiwa Teddy L. Kasella – Bantu, Mjumbe; Mheshimiwa Charles N. Keenja, Mjumbe; Mheshimiwa Salim H. Khamis, Mjumbe; Mheshimiwa Castor R. Ligallama Mjumbe; Mheshimiwa Joyce N. Machimu, Mjumbe; Mheshimiwa Benson M. Mpesya, Mjumbe; Mheshimiwa Cynthia H. Ngoye, Mjumbe; Mheshimiwa Said J. Nkumba, Mjumbe; Mheshimiwa Juma S. Omary,

Mjumbe; Mheshimiwa Mwanakhamis K. Said, Mjumbe; Mheshimiwa Salum K. Salum, Mjumbe; Mheshimiwa Abdulkarim E. Shah, Mjumbe; Mheshimiwa Kaika S. Telele, Mjumbe na Mheshimiwa Janet Mbene, Mjumbe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kutumia fursa hii kumpongeza na kumshukuru Waziri wa Maji na Umwagiliaji Mheshimiwa Profesa Mark J. Mwandosya; Naibu Waziri, Mheshimiwa Eng. Christopher K. Chiza; Katibu Mkuu Eng. Christopher Sayi pamoja na wataalam wote wa Wizara kwa ushirikiano na juhudi wanazofanya katika kutekeleza majukumu ya Wizara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, napenda kumshukuru Katibu wa Bunge, Dr. Thomas Kashililah, Makatibu wa Kamati hii, Ndugu Pamela Pallangyo na Ndugu Pili Omari kwa kuihudumia vyema Kamati na kuhakikisha Taarifa hii inakamilika kwa wakati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya maelezo hayo sasa nashauri Bunge lako Tukufu lijadili na kuidhinisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Maji na Umwagiliaji kwa mwaka wa fedha wa 2010/2011 jumla ya shilingi 251, 535, 392,000/=

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja hii na naomba kuwasilisha.

**MHE. MHONGA S. RUHWANYA - MSEMAJI WA KAMBI YA UPINZANI KWA WIZARA YA MAJI NA UMWAGILIAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuniwezesha kuwepo hapa, napenda kutumia fursa hii kwa mujibu wa Kanuni za Bunge kifungu cha 99 (7) toleo la 2007 kutoa maoni ya Kambi ya Upinzani kuhusiana na Bajeti ya Wizara ya Maji na Umwagiliaji kwa mwaka 2010/2011.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kwa nafasi ya kipekee kabisa kukishukuru Chama changu cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA) kwa kuendelea kuniunga mkono katika kazi walizonikabidhi katika kipindi cha 2005-2010. Nawaahidi kuwa kwa uwezo wa Mwenyezi Mungu nitajitahidi kutimiza majukumu yangu kwa masilahi ya Taifa langu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia natoa shukurani zangu za dhati kwa Mheshimiwa Hamad Rashid Mohammed, Kiongozi wa Upinzani Bungeni na Naibu wake Mheshimiwa Dr. Willibrod Slaa, kwa kutoa mwongozo sahihi kwa Kambi kwa mujibu wa kanuni za Bunge. Pia napenda kumshukuru Nibu Waziri wangu Kivuli Mheshimiwa Mkiwa Adam Kimwanga kwa ushirikiano wake wakati wote wa kuandaa hotuba hii na hata kuniwezesha leo hii kuwepo hapa na kuzungumza kwa niaba ya Kambi ya Upinzani. Vilevile bila kumsahau ndugu Oliva Mwikila, Mratibu wa Kambi yetu ya Upinzani ambaye anahakikisha hotuba zetu zinaandikwa kwa ufanisi mkubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naishukuru sana familia yangu, wadogo zangu, mtoto wetu Pearl na hasa mama yangu mzazi anayetutunza kutu-*support* na kuendelea kutulea na kuhakikisha tunapata elimu na kuzidi kunishauri kuendelea na masomo ya Shahada ya

Juu (Uzamili) ambayo nayafanya sasa. Mungu ambariki na namwambia nampenda sana na namshukuru sana kwa mwongozo wa maisha na ushauri wa kila siku wa maisha yangu na kuendelea kutukumbusha maneno ya marehemu baba yetu kuwa elimu bora ndio urithi wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na kwamba Mheshimiwa Waziri hakunipongeza wala ku-recognize mchango wa Kambi ya Upinzani juu ya maoni, ushauri na changamoto zinazosaidia ufanisi wa Wizara hii, hivyo nachukua fursa hii kutoa pongezi kwa Mheshimiwa Profesa Mark Mwandosya; Naibu wake, Mheshimiwa Eng. Christopher Chiza, pamoja na timu nzima ya watendaji wa Wizara hiyo kwa juhudi wanazozifanya katika kuhakikisha maji yanapatikana kwa Watanzania na pia kuhakikisha kuwa sekta ya maji inachangia katika pato la Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatizo la maji ndicho kilio kikubwa cha Watanzania mijini na vijijini. Hivyo basi Kambi ya Upinzani katika hotuba hii tutajikita zaidi kuangalia ni kwa vipi Serikali imetimiza jukumu lake katika kulikabili tatizo hili na kuwawezesha wananchi wengi zaidi mijini na vijijini kupata maji safi na salama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maji ni nguzo muhimu sana katika uhai wa binadamu na nchi ili iwe na maendeleo endelevu, msingi mkubwa ni maji. Ilani ya CCM inasema wananchi watapata maji safi na salama umbali wa mita 400 kutoka kwenye makazi yao . Taarifa ya utafiti wa bajeti ya kaya kwa miaka unaonyesha kuwa mwaka 1992 asilimia 46 ya Watanzania walikuwa wanapata maji kutoka kwenye vyanzo salama vya maji, mwaka 2001 ikawa asilimia 55 na mwaka 2007 ikawa asilimia 52. Kushuka huku kwa asilimia tatu kwa watu wanapata maji safi na salama ni dalili kuwa, utendaji wa Serikali unarudi chini kadri muda unavyokwenda badala ya kupanda kama inavyosemwa hapa Bungeni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *Afro barometer* iliyofanyika mwaka 2008 inaonyesha kuwa wananchi hawaridhiki na utendaji wa Serikali katika suala zima la kutoa huduma ya maji mijini na vijijini. Takwimu zinaonyesha kuwa mwaka 2003 asilimia 46 walikuwa wanaridhika, mwaka 2005 asilimia ya wanaoridhika ikashuka hadi 41% na mwaka 2008 ikawa ni asilimia 42.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi ya Upinzani inaliona hili kuwa ni mzaha kwani katika tafiti hizo zote watu wanaoridhika na utendaji wa Serikali haijawahi kufika asilimia 50 kama zilivyo kwenye sekta ya elimu na afya. Je, ni kweli Ilani ya CCM inatekelezwa kwa vitendo? Kutokuridhika kwa wananchi ni kielelezo cha wazi kuwa siyo tu hawaridhiki na utekelezaji wa Ilani, bali pia hawaridhiki na Ilani ya CCM ambayo inatafsiriwa kwa vitendo kwa njia ya huduma zinazotolewa. Huu ni ushahidi wa wazi wa CCM na Serikali yake kushindwa kutekeleza ilani yao wenyewe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu malengo ya MKUKUTA na Ilani ya CCM ukurasa 83 ni kwamba ifikapo mwaka 2010 asilimia 90 ya familia zinazoishi mijini na asilimia 65 ya familia zinazoishi vijijini ziwe na uwezo wa kwenda na kurudi kwenye chanzo cha maji kwa muda wa dakika 30. Lakini taarifa ya maendeleo ya watu na umaskini inaonyesha kuwa ni asilimia 42.1 tu ndio wanaopata maji katika muda huo,

asilimia 9.7 wanapata maji kwa kutumia zaidi ya muda huo na asilimia 48.2 zilizobaki wanatumia maji yasiyo safi na salama. Ni ukweli kwamba muda mwingi wa wananchi vijijini unatumika kutafuta maji badala ya kwenye shughuli nyingine za maendeleo. Kambi ya Upinzani inamtaka Mheshimiwa Waziri alitolee maelezo suala hili. Hili nalo ni ushahidi wa wazi wa kushindwa kwa Serikali ya CCM kutekeleza Ilani yake yenyewe na kushindwa kutoa huduma muhimu kama maji kwa wananchi wake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la maji limekuwa suala ambalo limezidi kuwaongezea umaskini wananchi wa mijini na vijijini. Maeneo mengi ya mijini wananchi wamekuwa wakitumia kati ya shs.3000 hadi 10,000 kwa siku kulingana na ukubwa wa familia kwa ununuzi wa maji. Tukiangalia hali halisi ya kipato cha Mtanzania ni kuwa asilimia 9.8 ya pato la mtu maskini hutumika kwenye ununuzi wa maji. Wakati asilimia 3.0 ya pato la familia yenye uwezo hutumika katika manunuzi ya maji kwa mwezi. Kwa maana ya kwamba mwenye uwezo huweza nunua maji ya jumla kwenye boza au magari ya wauza maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni ukweli kuwa Dodoma ni Mkoa ambao *water table* iko juu lakini ukitoka kidogo nje ya Dodoma Mjini hali ya maji ni tofauti kabisa, kwani maji ni tatizo sugu kwa miaka mingi. Kambi ya Upinzani inauliza ni kwanini Serikali isichimbe visima kwa matumizi ya kawaida kwa wananchi wa Dodoma wakati bajeti inapangiwa kwenye mkoa wao? Pia ipo tabia ya *DUWASA* kukata maji bila kutoa taarifa kwa wananchi ambao ndio watumiaji wajiandae.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nitoe sababu ni kwa nini sekta hii imekuwa nyuma katika utoaji huduma kwa wananchi, wakati fedha zinazotolewa ni nyingi:-

(a) Kumekuwa na utapeli mkubwa kwenye miradi hiyo ya maji, mfano, Mheshimiwa Rais alifungua mradi wa maji Pwaga Wilaya ya Mpwapwa 4.09.2007 akielewa kuwa tanki lile lilikuwa ni jipya lakini ukweli ni kwamba lilijengwa tangu mwaka 1977, ujio wake ulipelekea lipakwe rangi lakini wakasahau kufuta mwaka lilipojengwa. World Bank walitoa Tshs.573 milioni na wananchi walichanga Tshs.27 milioni. Mabwawa mawili yaliyojengwa hayakuwa na thamani halisi ya fedha hizo. Hadi sasa wananchi wa Pwaga hawana maji.

(b) Mradi mkubwa wa maji Newala uliogharimu shilingi millioni 172 lakini hauwezi kutumika kwa miaka mingi ijayo kwa ukosefu wa umeme na wananchi wa vijiji 11 wataendelea kutazama matenki 11 matupu bila manufaa yoyote kwao. Korogwe vijijini nako hali ni hiyo hiyo, mikataba mibovu inayohusu uchimbaji wa visima 16. Kati ya hivyo Miradi mingine haifanyi kazi kabisa na mingine wala haipo kwa mujibu wa Taarifa ya *LAAC* iliyowasilishwa hapa Bungeni. Wilaya ya Kiteto nayo ni hivyo hivyo, kwani miradi mikubwa imejengwa lakini kwa kuwa ujenzi ni hafifu karibu yote haifanyi kazi.

(c) Mkoa wa Tabora una tatizo sugu la maji, vyanzo vyake miundombinu yake ni toka 1958 lile la Igombe na lile la Kazima ni la toka 1949. Serikali ichukue hatua haraka kurekebisha hilo. Vile vile tukiangalia Wilaya ya Urambo tatizo la maji ni kubwa mno, mradi wa visima kwa vijiji kumi, mradi unakwenda taratibu sana, visima

vimechimbwa vifupi mno wakati wa ukame vinakauka. Tatizo la maji linarudi pale pale, fedha tayari zimeliwa. *(Makofi)*

(d) Mheshimiwa Mwenyekiti, matatizo yanayofanana na hayo niliyoyataja hapo juu yameenea katika mikoa mbalimbali na hivyo kusababisha ukosefu wa maji na kuwaacha wananchi wakiwa hawana la kufanya. Kwa mfano, hivi karibuni Serikali iliingia makubaliano na kampuni moja ya kichina ili kusambaza mabomba ya maji katika Jimbo la Ubungo. Cha kushangaza licha ya usambazaji huo kukamilika zaidi ya miezi minne iliyopita maji hayajaanza kutoka. Kambi ya Upinzani inataka maelezo kutoka Serikalini ni lini maji hayo yataanza kutoka? Au ndio Jimbo husika liko kwenye foleni ya kusubiri uzinduzi utakaofanywa na Rais kama ilivyojitokeza katika miradi mingine katika maeneo mbalimbali ya nchi? *(Makofi)*

(e) Mheshimiwa Mwenyekiti, usugu wa tatizo la maji unakikabili pia Kijiji cha Chasimba (kinachojumuisha vitongoji vya Chatembo, Chachui na Chasimba),kilichopo Boko kata ya Bunju. Wanakijiji wamekuwa wakipata usumbufu mkubwa wa kupata maji licha ya kuwa tayari kugharamia gharama za kuvuta maji. Cha kushangaza zaidi ni kuwepo kwa maji kwa upande wa pili wa bara bara unaopakana na kijiji husika. Kambi ya upinzani inataka kupata jibu, ni kwanini kuna urasimu mkubwa wa kupeleka maji kutika kijiji cha Chasimba? Kijiji ambacho kilisajiliwa kihalali mwaka 1975 Licha ya wanakijiji husika kuonyesha dhamira ya kutaka kushirikiana na serikali kuwezesha kuvutwa kwa maji? *(Makofi)*

(f) Uvujaji wa maji mijini umesababisha kiwango kikubwa cha upotevu wa maji kwa maeneo mbalimbali. Hii inatokana kwa kiasi kikubwa na miundombinu iliyochakaa na hivyo kushindwa kuhimili msukumo wa waji unaopita kwenye miundombinu hiyo chakavu. Kiwango cha Kimataifa cha uvujaji ni chini ya 20% wakati kwa Tanzania ni zaidi ya 33%. Dar es Salaam ni zaidi ya 45%.

(g) Mradi wa maji Kahama – Shinyanga ulioigharimu Serikali kiasi cha sh. 252 bilioni. Taarifa iliyotolewa na Mkurugenzi wa Kashwasha (Mamlaka ya Maji Kahama na Shinyanga tarehe 26.10.2009) kuwa mradi umepata hasara ya Sh. 500 milioni. Hasara hii ni mbali ya ile inayopatikana kutokana na hujuma inayotokana na wananchi wanaoona kuwa wana haki ya kutumia maji hayo, kwani bomba kuu la mradi huo linapita katika vijiji 54 vya wilaya za Misungwi, Shinyanga na Kahama, lakini vijiji vyote hivyo havina maji safi na salama. Je, ni kweli wananchi hao walaumiwe kwa kutoboa bomba hilo kwa ajili ya kujipatia maji yao na mifugo? Kambi ya Upinzani inamtaka Waziri awaeleze wananchi hao lini watapata maji safi na salama ili waache kuendelea kufanya uharibifu huo? Ubadhirifu kuhusu Mradi wa Shinyanga/Kahama uliwasilishwa hapa Bungeni, lakini wahusika walilindwa na hatimaye aliyetoa siri ya ubadhirifu huo hata kama yeye mwenyewe alikuwa na madhaifu yake, lakini taarifa yake haikufanyiwa kazi, badala yake kafukuzwa kazi bila utaratibu kufuatwa na hatimaye Serikali ikawajibika kulipa mafao, jambo ambalo ni kuliingizia hasara zaidi Taifa.

(h) Mbali na taarifa hiyo ya mwaka jana, kutokana na kutofanyika kwa utafiti wa kutosha kuhusiana na uwiano wa miundombinu ya maji ya zamani na mipya na *pressure* ya maji imesababisha kupasuka kwa mabomba ya zamani na hivyo kupotea kwa

maji zaidi ya lita 40,000 kwa siku. Wananchi wengi wanaendelea kukosa maji. Hasara kwa mwezi ni takriban Sh. 300 Milioni ikiwa ni gharama za uendeshaji na wananchi kutokulipa Ankara za maji kutokana na kutopata huduma hiyo. Hasara kwa Taifa inaendelea kila kukicha. *(Makofi)*

(i) Hali ya kushangaza ni tatizo sugu la maji katika Mkoa wa Kigoma wakati lipo Ziwa Tanganyika, mbali ya Ziwa hilo ipo mito mingi ukiwemo mto mkubwa wa Malagarasi lakini maji safi na salama hayapatikani. Mabomba ya wananchi yameota kutu kwani matatizo hayo ya ukosefu wa maji ni zaidi ya miaka mitano. Athari ni kubwa kwa wananchi ambao inabidi wanunue maji ya magaloni kwa sh 250 hadi 500. Vivyo hivyo hospitali ya Mkoa wa Kigoma hununua maji hata ya kufanyia usafi. Pamoja na kuhakikishiwa umeme, miundombinu ya maji imechakaa mno. Serikali itueleze ina mpango gani wa kuweka miundombinu mipya ya maji bado haijabadilishwa.

(j) Mheshimiwa Spika, Kambi ya Upinzani inamtaka Mheshimiwa Waziri alieleze Bunge hili ni kwa nini Mkurugenzi Mkuu wa *MOWASA* (Mamlaka ya Maji Safi na Taka-Moshi) ambaye amefunguliwa kesi ya jinai namba 94 ya mwaka 2010 kwa matumizi mabaya ya ofisi bado anaendelea kuwa ofisini kinyume na sheria na kanuni za utumishi, zinazomtaka kusimamishwa kazi ili uchunguzi huru uendelee. Ni nani anamlinda Mkurugenzi huyu kinyume na taratibu za ajira Serikalini? Kambi ya Upinzani inamtaka Mheshimiwa Waziri alitolee hili ufafanuzi wa kina. Je, nchi hii inasheria tofauti za ajira? *(Makofi)*

(k) Kutokana na taarifa nyingi ambazo zimekuwa zikitolewa na asasi mbalimbali za Serikali na binafsi kuhusiana na kemikali za sumu zinazotoka katika Mgodi wa North Mara na kuingia katika Maji ya Mto Tigite na kuingia Mto Mara hadi Ziwa Victoria kuwa za kuwachanganya wananchi. Kambi ya Upinzani inamtaka Waziri atoe tamko rasmi kuhusu usafi na usalama wa maji hayo kwa matumizi ya nyumbani, viwandani, mifugo na mashambani. Kama hayafai, je, Serikali ina mpango gani wa kuhakikisha wananchi wanaotegemea Mto Tegete wanapatiwa maji safi na salama kwa matumizi yao na mifugo yao?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu maji na uchumi. Ilani ya Chama Tawala ya mwaka 2005 inasema kuwa ifikapo mwaka 2010 tutakuwa na eneo la hekta milioni moja za umwagiliaji, lakini hivi sasa sekta ya umwagiliaji ina hekta 331490, lakini hata ifikapo mwaka 2015 eneo la umwagiliaji litakuwa hekta 600,000 tu. Ni wazi Ilani ya CCM sambamba na Serikali pia vimeshindwa hata kufikia malengo ya umwagiliaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaamini kuwa Serikali inaongozwa na Sera katika utendaji kazi wake na sio matamko ya kisiasa ya kutafutia kura kama vile ya Kilimo Kwanza. Kambi ya Upinzani inaelewa umuhimu wa Umwagiliaji, lakini tatizo kubwa ni kwamba Wizara inafanya kazi bila ya kuwa na mwongozo (Sera). Kambi ya Upinzani

inashindwa kuelewa ni kwa vipi Wizara inaundwa bila ya kuwa na Mwongozo wa utendaji kazi wake yaani Sera ya Umwagiliaji? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, takwimu zinaonyesha kuwa eneo la umwagiliaji mwaka 2005 lilikuwa hekta 264,388, mwaka 2008 likafikia hekta 289,245. Sawa na ongezeko la hekta 24,857 ambayo ni asilimia 8.6. Kwa kipindi hicho Bunge lako Tukufu limepitisha jumla ya Sh. 597,301,121,600/- kwa Wizara hii. Je, fedha hizo zinalingana na ongezeko hilo la asilimia 8.6?

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuna imani Watanzania watatoa maamuzi sahihi kwa ulinganisho huo. Je, Serikali imekwisha kufanya ukaguzi wa ufanisi katika miradi yake au inatumia fedha nyingi tu za wananchi, wahisani na hata mikopo ya Benki ya Dunia ambayo Taifa litakuja kulipa wakati tulichopata hakifanani kabisa kwa thamani na tulichokipata? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi ya Upinzani inamtaka Waziri atoe ufafanuzi wa kina mathalan kwa mradi wa vijiji 10 kwa kila kijiji hadi sasa zimetoka kiasi gani kwa kazi ya usanifu, upembuzi, yaani kabla hata maji hayajapatikana na je fedha hizo zinafanana na miradi itakayojengwa, na je fedha kwa ajili ya miradi hiyo yote imepatikana au yote imetumika katika upembuzi yakinifu na kadhalika? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu maji na uchumi. Ili uchumi ukue katika sekta zote, maji ni nyenzo muhimu sana, hivyo basi uchumi unaokuwa sekta ya maji ni muhimu sana, katika kilimo, mifugo, viwanda na katika sekta ya ujenzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sekta ya kilimo ili ifanye vizuri, maji ndio kichocheo kikubwa sana. Serikali kwa takwimu zake imekuwa na program nyingi za kuwekeza kwenye miradi mbalimbali ya kilimo, lakini tija inayotokana na uwekezaji huo kwa mujibu wa takwimu zilizopo bado ni ndogo sana. Maeneo mengine miradi hiyo haitumiwi vizuri na wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni dhahiri kwamba Sera ya maji ya umwagiliaji imechelewa sana, imekamilika mwaka huu 2010. Kwa hiyo tunaishauri Serikali ifanye haraka kuitumia kama walivyotuahidi muda wa sekunde zilizopita. Katika kitabu *Vol. IV* cha bajeti ya maendeleo ya mwaka 2010/2011, bajeti ya maji inaonekana ni bilioni 233,092,607,000. Fedha za ndani ni bilioni 41,565,045,000 na fedha za nje ni bilioni 191,527,562,000. Hii ni hatari sana kwani kiasi kikubwa kinategemewa kutoka nje kwa wenzetu. Je, zisipopatikana maana yake miradi mingi ya maji haitatekelezeka.

Hali hiyo ilijitokeza katika bajeti ya mwaka 2009/2010 ambapo bilioni 36 zilikuwa za ndani, wakati bilioni 195 ambayo ilileta jumla ya bilioni 231 zilikuwa zinategemea kutoka nje. Ufike wakati tutafute vyanzo vipya vya mapato ili tujitegemee katika maendeleo yetu na si vibaya mkifuata ushauri wa Wapinzani wa bajeti mbadala ili

kuongeza vyanzo vingine vya mapato kwani itasaidia kupunguza utegemezi wa wafadhili nje.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Mhonga kwa hotuba kwa niaba ya Kambi na nikupongeze zaidi kwa vazi lako, linaashiria mema Oktoba. Sasa kama nilivyosema wachangiaji ataanza Mheshimiwa Ephraim Madeje na atafuatiwa na Mheshimiwa Peter Serukamba. Mheshimiwa Teddy Kasella-Bantu ajiandae. Mheshimiwa Madeje, Mbunge wa hapa tulipo.

**MHE. EPHRAIM N. MADEJE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, sina budi kumshukuru Mwenyezi Mungu ambaye ameniwezesha kufika siku ya leo. Aidha, namshukuru pia kwa vile alivyonipa afya njema katika miaka mitano iliyopita na ambacho kiliniwezesha kuhudumia wananchi wa Dodoma katika harakati za kuleta maendeleo na nina imani kabisa na namwomba Mwenyezi Mungu azidi kunipa afya njema ili niweze kuendelea kuwatumikia wananchi wa Dodoma kwa ridhaa yao katika miaka mitano ijayo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sina budi kuwashukuru wananchi a Dodoma kwa vile ambavyo waliniheshimu, walivyoweka imani yao kwangu na vile ambavyo walishirikiana na mimi pamoja na Serikali ya CCM katika kutekeleza Ilani ya Uchaguzi ya mwaka 2005. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kipindi hiki cha miaka mitano kwa hakika Wilaya ya Dodoma Mjini imepiga hatua kubwa katika maendeleo. Tukiangalia karibu katika nyanja zote, nyanja za miundombinu, afya na elimu, hiki ni kipindi ambacho kwa kweli tumepiga hatua. Nikizungumzia sehemu ndogo tu au tuseme nyanja ya elimu katika Jimbo hili tulitekeleza vilivyo ujenzi wa shule za Kata. Kwa sasa hivi kwa kweli tumevuka hilo lengo na tumeingia katika kushindana kuwa na shule mbili, tatu au nne katika Kata moja. Kwa hiyo, hiyo ni hatua kubwa sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo ambalo tumepiga hatua zaidi zaidi kuliko katika maeneo mengine yoyote ni katika elimu ya juu. Udahili katika vyuo vyetu vya elimu ya juu umeongezeka sana. Lakini zaidi zaidi ujenzi wa Chuo Kikuu cha Dodoma na pia ufunguzi wa Chuo Kikuu cha St. John’s nacho pia kimeongeza ufanisi katika eneo la elimu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kuanzishwa kwa *UDOM* hatuna budi kumshukuru sana sana Mheshimiwa Rais wetu Mheshimiwa Dr. Jakaya Mrisho Kikwete kwa uamuzi wake ambao kwa kweli umetunufaisha sana katika hilo eneo. Naweza kusema kwamba kama ni kasungura kadogo kwenye upande wa elimu ya juu sisi Dodoma tumemla sungura mzima isipokuwa mkia tukawabakizia watu wengine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa naomba nije kwenye bajeti ya Wizara hii. Kwanza naomba nimpongeze Waziri, Naibu Waziri, Watendaji wote waliohusika katika

kuitayarisha bajeti hii ni bajeti ambayo imefanya mapitio mazuri kwa kazi iliyofanyika katika kipindi kilichopita. Imetuelezea kinagaubaga tutarajie nini katika kipindi kinachokuja. Nawapongeza sana kwa bajeti hiyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia naomba nimpongeze Waziri na Naibu wake kwa jinsi ambavyo wamekuwa wakifuatilia shughuli za utoaji wa huduma za maji katika Wilaya yangu ya Dodoma Mjini. Mheshimiwa Waziri katika kipindi hiki cha miaka minne ameshatembelea shughuli za *DUWASA* na pia shughuli za utoaji huduma za maji vijijini zaidi ya mara tatu. Nampongeza sana kwa hilo. Pia niwapongeze watendaji katika Wizara kwa kazi nzuri ambazo wamefanya katika kufuatilia hasa mradi wa Benki ya Dunia yaani ule mradi wa Vijiji kumi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, huduma ya maji katika jimbo hili iko katika sehemu mbili. Sehemu moja inahusu utoaji wa huduma ya maji hapa mjini kati. Unaweza ukasema Dodoma Mjini *per se* huduma hiyo inatolewa na Shirika la Maji Safi na Maji Taka la *DUWASA* bila upendeleo. Shirika hili naweza kutamka kwamba limekuwa likitoa huduma ambayo inaridhisha kwa kiwango kikubwa. Huduma imeendelea kuridhisha pamoja na kwamba Dodoma au tuseme wakazi wa Dodoma wameongezeka kwa haraka sana. Ujenzi na ujio wa Chuo Kikuu cha *UDOM* umeongeza sana idadi ya watu katika Mji huu. Upanuzi wa vyuo vingine pia umeongeza sana watu. Lakini pia shughuli mbalimbali za biashara na za Serikali na za kijamii zimeongezeka na kuongezeka kwake kumeongeza watu hapa. Lakini pamoja na hayo Shirika hili limeendelea kutoa huduma nzuri. Kwa hiyo tunawapongeza sana kwa hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, huduma za maji vijijini. Kwa sababu Dodoma ina vijiji 40 zimekuwa zikitolewa na Serikali za Mitaa kwa maana ya Halmashauri kwa ushirikiano na Serikali Kuu ambayo ndiyo inatoa fedha na mipango mingine mbalimbali. Kazi ya kuhudumia wananchi huko vijijini imekuwa ikiendelea vizuri. Miradi ambayo ilikuwepo tangu zamani, visima ambavyo vilikuwepo, vimekuwa vikikarabatiwa pale inapobidi. Lakini pia vingine vipya vimekuwa vikijengwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatizo ambalo tumelipata ni katika eneo la ule mradi wa Benki Kuu, ooh, samahani ule mradi wa Benki ya Dunia. Mradi ambao unahusu vijiji 10 katika Wilaya yetu kama ambavyo tumekuwa tukizungumzia katika Bunge lako Tukufu na kama ambavyo hata Waziri mwenyewe amekuwa akikiri kwamba siku za nyuma utekelezaji wa mradi huu ulikuwa ukisuasua kidogo, kwa kweli mradi huu umechelewa sana katika kutekelezwa. Sasa ombi langu kwa Wizara ni kwamba kasi iongezwe katika……

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**MHE. EPHRAIM N. MADEJE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Madeje. Mheshimiwa Peter Serukamba, atafuatiwa na Mheshimiwa Teddy Kasella-Batu, Waheshimiwa ni dakika kumi kumi.

**MHE. PETER J. SERUKAMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti na mimi nikushukuru kwa kunipa nafasi ili niweze kuchangia katika bajeti ya Wizara ya Maji na Umwagiliaji. Kwanza na mimi nianze kwa kuwashukuru wananchi wa Jimbo la Kigoma Mjini kwa heshima waliyonipa na wanaendelea kunipa na ushirikiano wanaonipa katika kutekeleza wajibu wangu. Napenda kuwahakikishia nitaendelea kuifanya kazi hii kwa moyo wangu wote na kwa unyenyekevu mkubwa ili tuweze kufikia yale malengo yetu ya maisha bora kwa Watanzania hasa wale wa Kigoma Mjini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo nami nimpongeze Mheshimiwa Waziri kwa hotuba nzuri ya bajeti yake ya mwaka huu. Baada ya kusema hayo niipongeze Serikali kwa kutekeleza Ilani ya Chama chetu, Kigoma juzi tumefungua mradi mkubwa wa umeme na barabara. Kwa hiyo, naishukuru sana Serikali kwa kusikiliza kilio chetu cha muda mrefu. Wakati huu nikiishukuru Serikali nilitaka nimkumbushe rafiki yangu Profesa Mwandosya kwamba amebakia yeye tu wenzake wamemaliza. Umefika wakati na yeye atumalizie hili tatizo letu la maji na napata shida kidogo inapokuwa Profesa anakuwa wa mwisho wakati wenzake wamemaliza haraka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, namwomba Profesa na yeye atutatulie hili nalo liishe. Maana tatizo la Kigoma kutokuwa na maji halina maelezo ya namna yoyote ile. Kwa sababu Kigoma ndio mji pekee ambao pamoja na miji mingine tunalo Lake Tanganyika ambapo moja ya sita ya maji yote yaliyoko duniani yako Lake Tanganyika *and yet* maji haya hayatumiki. Watu wa Kigoma pale hawana maji. Halina maelezo kwa namna yoyote ile. Lakini haiwezekani akina Ngeleja waje juzi watekeleze mambo, Profesa awe bado. Naomba Profesa naye hili nalo naye alishughulikie, wakati umefika kwa Profesa kuondoa tatizo la maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, niseme, maji ni uhai. Wako wanafalsafa wamesema duniani kama kutatokea vita ya tatu ya dunia basi inawezekana itasababishwa na maji. Kwa hiyo, suala la maji kwangu ni suala la msingi sana. Ningeomba tulipe kipaumbele kwa maana ya bajeti na maana ya utekelezaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naelezea tatizo la maji la Kigoma Mjini. Mji ule wa Kigoma umeendelea kukua lakini miundombinu ya maji imebakia kuwa ile ile toka tumepata uhuru. Najua Serikali imekuwa inafanya hapa na pale. Lakini bado naamini tatizo ni la kibajeti. Kwa hiyo, ningeiomba Serikali tufike wakati sasa tuamue.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mradi huu wa *World Bank* ambao na Kigoma tumo, lakini kwa bahati mbaya tumeambiwa sisi bei za Wakandarasi zimekuwa juu, kwa hiyo, wanarudia tena. Mradi huu ni zaidi ya miaka mitano unaongelewa, naamini kama tungekuwa tuliamua kujitegemea kwamba tutumie pesa zetu za ndani leo hii Manispaa nyingi na Halmashauri nyingi nchini tatizo la maji lingekuwa limeondoka. Lakini kwa

sababu, tunawasubiri hawa ndugu zetu nadhani sasa tubadili mwelekeo katika namna ya kutatua tatizo la maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nchi zote zilizoendelea kuna mambo hawaongei tena. Hauwezi kuwakuta wanaongea habari ya maji, habari ya umeme, wanaongea barabara, kwa sababu ni mambo ambayo mnatakiwa kuwa mnayafanya, yanakwisha, mnakwenda kwenye mambo mengine zaidi. Kwa kweli, hili la maji hasa kwa Manispaa ya Kigoma, bado halielezeki kwa namna yoyote ile. Sasa niiombe Serikali, ifike wakati watusaidie tutenge pesa kwenye bajeti; kama tumeweza kufanya mradi wa Ziwa Viktoria, naamini tunaweza tukaanzisha Maziwa Viktoria mengi kwa namna ile ile.

Baada ya mradi ule kwisha, zile pesa zilizokuwa zinakwenda kule kwa ajili ya mradi ule, sasa zingehamishiwa kwenye mradi mwingine, tukaamua sasa tunaanza kutatua tatizo la maji kutoka Ziwa Tanganyika. Ziwa Tanganyika lina maji mengi sana, tatizo la Tabora na la Kigoma lingekwisha. Lakini hii tunagawa kidogo kidogo ili kila mtu apate, kila siku tutakuwa tunaongelea tatizo la maji. Hata hivi vijiji kumi, kwangu mimi ni vijiji kumi, kwa maana kule ni kuchimba visima. Bado maeneo mengi tatizo la maji litakuwepo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ningeiomba Serikali tuanzishe mkakati kama ambavyo tulianzisha kwenye mambo mengine makubwa, kama vile kwenye shule, tuanzishe mkakati na tutumie pesa za ndani kwamba mwaka huu tunatenga pesa zetu za ndani, hata bilioni 200 labda kwa ajili ya Manispaa 20, Halmshauri 20, ndani ya miaka mitano tatizo hili la maji litakwisha. Lakini bado siamini kama tutaendelea kusubiri wafadhili, tutakuwa tunaongea kila siku, upembuzi yakinifu, upembuzi wa kina, *World Bank* wamesema wanaleta *No objection*, mwaka unakwenda. Nadhani umefika wakati tufanye maamuzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukitatua tatizo la maji tutakuwa tumesaidia sana katika maendeleo. Tunapunguza hata magonjwa kwa 50%, yapo magonjwa mengi sana ambayo yanasabishwa na watu kutokunywa maji safi na salama. Kwa hiyo, nasema tatizo hili la maji *in a long run* lingeweza kutusaidia kibajeti. Ukisha-*solve* tatizo la maji, bajeti ya afya inapungua. Kwa hiyo, nadhani umefika wakati sasa hili eneo nalo tulipe ufuatiliaji unaotakiwa; tuitendee haki hii sekta nayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa niongelee suala la umwagiliaji. Nilikuwa nasoma kitabu hiki, ni kweli tunataka kufanya kilimo Tanzania, lakini naamini, kilimo cha kutegemea mvua, hata tungekuwa tumempa kila Mtanzania trekta, lakini kama tunategemea mvua bado hatutaweza kuleta mapinduzi ya kijani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mapinduzi ya kijani, yataletwa kwa kuanzishwa kwa *scheme* kubwa za umwagiliaji. Pale kwetu Kigoma tunalo bonde la Mo Ruche, wakubwa hawa hata hawalitaji, lakini ni bonde kubwa lina uwezo wa kulisha Mkoa mzima wa Kigoma, bonde moja tu, lakini tunahitaji uwekezaji mkubwa. Kwa hiyo, naomba Mheshimiwa Waziri, tusitapanye pesa kwenye *schemes* ndogondogo nyingi, tukiamua kwamba mwaka huu tunaanzisha *scheme* mbili kubwa, nadhani *impact* itaonekana.

Hizi tunazopeleka kidogo kidogo kila mtu apate, ni kweli ndio maana hata rafiki zangu wa Upinzani hapa wanasema hakuna kilichofanyika ingawaje tumefanya, kumbe ni kwa sababu tunafanya kidogo kidogo lakini kwa maeneo mengi sana. Lakini nasema umefika wakati tu-*concentrate* kwenye maeneo makubwa machache, halafu tukimaliza tunahamia maeneo mengine. Hapa nadhani ni rahisi na tunaweza tuka-*count* maendeleo yetu kwa haraka zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, namwomba Mheshimiwa Waziri, katika mabonde ambayo ni ya msingi sana, naomba aje atembelee bonde la Ruche, aliangalie na aone kile ambacho tunakisema hapa tunamaanisha nini. Naamini tukiweza ku-*invest* kwenye bonde lile, tutaweza kutatua tatizo kubwa tulilonalo la bonde lile ili na sisi tuweze kuchangia kwa kiasi kikubwa kwenye maendeleo ya nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, narudia tena. Serikali imetusaidia kwenye umeme, imetusaidia kwenye barabara, sasa nimwombe kaka yangu, rafiki yangu Profesa, amebakia yeye, tunaomba na yeye atusaidie tulimalize tatizo hili la maji la Mji wa Kigoma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, nikushukuru na nikupongeze kwa Kiti hicho, umekikalia vizuri. Nikuombee Mungu uendelee kukikalia kwa kadri tutakavyozidi kuendelea. Baada ya kusema hayo, naunga mkono hoja hii. *(Makofi)*

**MHE. TEDDY L. KASELLA–BANTU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi ili na mimi nichangie katika hoja iliyoko mbele yetu. Awali ya yote napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipa uhai na kuweza kusimama hapa leo. Pia nawashukuru wapiga kura wangu wa Jimbo la Bukene na kwa ushirikiano na tulivyofanya nao kazi kwa miaka mitano, mpaka maendeleo yameonekana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naweza kusema machache kabla sijaingia katika hoja kamili. Katika Jimbo la Bukene, kabla ya miaka hii mitano kulikuwa na Shule za Sekondari mbili, sasa kuna shule za Sekondari 16, yaani kata 14 na tumeshirikiana na

wananchi kujenga shule za sekondari kwa kila Kata. Mimi mwenyewe nimeshiriki kuweka matofali ya chumba kimoja katika Kata zote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pale nilipolichukua Jimbo kulikuwa hakuna simu; kulikuwa na simu za mkorogo, lakini sasa hivi tuna *Voda, Zain, tiGO,* kila mahali. Kwa hiyo, hayo ni maendeleo ya miaka mitano tuliyoshirikiana na wananchi wa Bukene wakiniambia kwamba wanahitaji kitu gani na mimi nachakarika kuhakikisha kwamba nawatimizia ahadi yao kwa sababu, niliwaambia nataka wanipe sauti ya Bukene ili iweze kusikika kila mahali. Sasa hivi tuna barabara ambayo wanapita watu wote wakitaka kwenda Tabora kutoka Nzega, wanapitia Bukene. Hata Spika, na Mawaziri wote wakienda Urambo na kwingine, wanapita kwenye barabara hiyo. Barabara ya changarawe, ahadi ya Rais, lakini ni nzuri kabisa, imekuwa sawasawa karibu kuwa kama ya lami.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, hayo ni maendeleo. Yote hayo na mengine mengi ambayo siwezi hata kuyataja kwa sababu, sio Wizara yake na dakika zangu zitakwisha, nataka kuwaambia tu kwamba wale wanaopita wanasema kwamba safari hii sitagombea, ili kuwakatisha tamaa wananchi wa Bukene, naomba niseme kwa kutumia Bunge lako Tukufu kwamba Mungu akinijalia wakati muafaka ukifika, nagombea kwa hiyo, tuje tubanane tu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nawapongeza Waziri wa Maji na Umwagiliaji na Naibu wake pamoja na Rais, kwa yale yote waliyoyafanya katika kutekeleza Ilani ya Uchaguzi. Kuhusu maji, kwa kweli, wamefanya kitu kikubwa sana haijapata kutokea. Kwa mfano, nitasemea kwangu siwezi kusema kwingine, maana unaanza pale pale, *charity starts at home.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kulikuwa na vijiji vile kumi ambavyo vilikuwa vinatakiwa vipewe maji siku nyingi, lakini ikwa utekelezaji wa sasa wa awamu ya nne, vijiji kumi kila Wilaya. Sasa wale wanaosema Awamu ya Nne haijafanya kazi, nawashangaa. Vijiji kumi kwa kila Wilaya nchi nzima. Kwangu mimi ambaye tuko pamoja na Mheshimiwa Selelii Wilaya moja na vijiji kumi, nina vijiji sita na Seleli ana vijiji vinne ambavyo sasa hivi watu wanapewa mafunzo na tayari wameshapima maji yako wapi na kazi ya kuchimba visima katika vijiji hivyo itaanza karibuni. Vijiji vya kusema bila kusema uwongo, mtu yeyote anaweza kwenda akaangalie, vya kwangu mimi mwenyewe ni Sigili, Nawa, Buhondo, Itobo, Ikindwa na Mahene. Kwa hiyo, ukienda pale utakuta kazi imeshafanyika; hiyo ndio kusema tunazungumza kama Ilani ya Uchaguzi na utekelezaji unafanyika palepale. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo wengine watasema kwamba vijiji kumi sio vingi kwa sababu tuna vijiji vingi, lakini Roma haikujengwa kwa siku moja. Tumeanza na tutaendelea, kwa hiyo kwa kifupi nawaombea maisha marefu, kaka yangu Profesa

Mwandosya na Naibu wake, waende wakashinde tena. Nawaomba wananchi wao wawachague tena, warudi na wapewe Wizara hizi ili waendelee pale walipomalizia, tusije tukaharibikiwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nakuja kwa Bukene, nimeshasema maji hivyo vijiji sita vimeshapata na ambavyo ni vijiji kumi kwa *District.* Sasa nakuja, pale Bukene Makao Makuu ya Wilaya, maji hayajaonekana kwa miaka 35, Kiingereza au Kinyamwezi wanasema *thirty five years*, hawajaona maji, lakini sasa kuna maji. Ile haikuwemo kwenye vijiji sita, ilikuwa ipo peke yake na nilipopata Ubunge nimepiga kelele nimemwomba Waziri, wakati ule Naibu Waziri wa Maji alikuwa ni Mheshimiwa Shamsa Mwangunga, tukaenda nae mpaka Bukene, akaangalia *system* na sasa ninavyokwambia maji yapo. Hiyo ni hongera kwa Awamu ya Nne. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile naomba nizungumzie bwawa la Kahama ya Alanga, ambalo tulipata pesa kwenye bajeti ambayo inakwisha Juni, lakini mpaka sasa hivi halijakwisha. Lakini hili bwawa, halijakwisha kwa sababu kulikuwa na uzembe fulani, kati kati ya yule aliyepewa tenda. Madiwani wa sehemu hiyo wakamwambia bwana, mvua zikianza hapa mwezi Oktoba, Novemba, huwezi kumaliza.

Yeye akasema mimi naweza, nitafanya hivi, naelewa; basi wakaona wamuache kama ni mtaalam, lakini ikatokea kwamba ilipofika Novemba, hakuweza kutengeneza lile bwawa. Kwa hiyo, sasa hivi katika hotuba ya Mheshimiwa Waziri, imesemwa kwamba liko kwenye bajeti ya mwaka 2010/2011. Kwa hiyo, vilevile niko kwenye Kamati na nimeambiwa kwamba hili bwawa litakwisha na naamini kwamba litakwisha. Leo nimezungumza na watu wa Bukene, wameniambia kwamba watu wanafanya kazi. Kwa hiyo, naamini kwamba litakwisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili bwawa likiisha, maana yake ni kwamba tunakwenda kwenye kilimo cha kisasa. Kama unavyowajua Wanyamwezi, wenyewe ni wafanyakazi, kwa hiyo hili bwawa likiisha tutalima mpunga na vitu vingine. Sisi tunataka tulime mara tatu kama wanavyolima wengine, kwa hiyo, hapo tutaondokana na umaskini. Bahati nzuri tuna mahali pa kuuza mpunga, ambao ni Igembe Nsabo ya Bukene na vilevile tumepata umeme unakuja pale. Kwa hiyo, tutatengeneza mchele, na tutakwenda kuuza ndani ya nchi na nje ya nchi. Kwa hiyo, haya mambo naomba tu yaende kama yalivyo na huyo aliyepewa *contract* hii, atumalizie upesi maana anatucheleweshа kubadilisha maisha yetu ili tuwe matajiri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuna mabwawa mengi ya asilia ambayo yalichimbwa na Machifu, Watemi wakwetu, kwa hiyo tunaomba kama *system* iilivyokuwa inasema kwamba sasa tunakwenda kwenye mabwawa madogo madogo, kwa hiyo sasa naomba yale mabwawa madogo madogo yaanze kufanya kazi. Wale wataalam wa kilimo na umwagiliaji, basi waende wakawaeleze wananchi kule, wawatayarishe ili waweze kuchimba yale mabwawa katika utaalam unaotakiwa ili tuingie katika kilimo cha umwagiliaji ambacho ni kilimo cha kisasa. Kama nilivyosema, watu wa kwetu ni wakulima, kwa hiyo, hamna tatizo, tunachoomba ni tuelezwe tu, tusaidiwe, yale

mabwawa yote madogo madogo yachimbwe ili watu wote waweze kuwa walimaji wa kilimo cha umwagiliaji, kilimo cha kisasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante na naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MHE. DR. IBRAHIM S. MSABAHA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna Mnyamwezi mmoja hapa anasema kwamba wote hawapo, lakini sote tupo. *Alhamdulillah Rabil-Alamiina,* namshukuru Mwenyezi Mungu, Mola wa viumbe wote kwa kuniwezesha kusimama hapa leo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimesimama kumpongeza Waziri wa Maji na Umwagiliaji, nimesimama kuipongeza Wizara ya Maji, nimesimama kuipongeza Serikali inayoongozwa na ndugu yetu Mheshimiwa Dr. Jakaya Mrisho Kikwete, kwa sera nzuri na kwa utekelezaji mzuri haswa kwenye sekta hii ya maji. Hususan, napenda nimshukuru sana Mheshimiwa Waziri, alichukua fursa yeye na watendaji wake wakuu kufika mpaka kwenye Jimbo la Kibaha Vijijini na hususan katika Kata na Kijiji cha Soga, ambako kwa miaka mingi palikuwa na shida kubwa ya maji na kufika kwake kulikuwa ni neema.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kuondoka, watendaji wake walifanya kazi ya ziada na hivi sasa Soga pana maji na maeneo mengine pia ya Jimbo la Kibaha Vijijini, hususan maeneo ya Mlandizi na kadhalika, pia yana maji. Kwa hiyo napenda nimpongeze sana na nimshukuru kwa jitihada zake. Sishangai, kwa miaka mingi ambayo nimemfahamu Profesa Mwandosya, ni mtu shupavu, mkweli na mchapakazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sera ni nzuri na utekelezaji pia ni mzuri, lakini panapotekelezwa sera pia inawezekana utekelezaji ukaibua changamoto ambazo inabidi watendaji wazifuatilie. Nimesimama pengine kuainisha tu kwa ufupi changamoto hizi ili Mheshimiwa Waziri na timu yake waweze kuzifuatilia. Jimbo la Kibaha Vijijini, kwa upande wa maji limekuwa na miradi miwili au mitatu mikubwa.

Kwanza, mradi ambao utafika mpaka kwenye Jimbo la Kibaha kwa upande wa Kata ya Magindu, mradi wa Wami – Chalinze, awamu ya pili. Lakini pia mradi ambao ukandarasi wake ulipewa kampuni ya Kichina na kwa wale wasukuma wanaoishi pale Mlandizi kwa kuwa walikuwa hawaelewi kwamba hawa ni makandarasi tu, wakawa wanauita ni mradi wa Wachina. La tatu, ni mradi huu wa maji kutoka Kongowe hadi Soga. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyosema awali nataka niguse, nimefurahi kusikia asubuhi hii kwamba mradi huu wa Wami – Chalinze utaendelea na kwa hivyo basi nina matumaini makubwa kwamba vile vijiji ambavyo vitapitiwa na mradi huu kwa

upande wa Jimbo la Kibaha Vijijini, hususan Gwata, Gumba, Magindu na vinginevyo vitapata maji. Sasa nikija kwenye mradi huu ambao wasukuma wanauita mradi wa wachina, pale Mlandizi. Mradi huu ambao pia umekwenda kwenye Kata ya Soga, niseme tu kwamba umeibua changamoto. Kama nilivyosema utekelezaji wa sera unaweza ukaibua hoja za kisera, hoja za kisiasa, ambazo watendaji inabidi wazijue lakini sisi viongozi na hususan Mheshimiwa Waziri anapaswa kuzifahamu kama ni changamoto.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano, pale Mlandizi, kuna maeneo ambayo kwanza utekelezaji wenyewe ulikuwa ni kwamba watu wanachimbiwa *line* za mabomba na katika ndani ya mita 50 wanafungiwa maji bila ya kulipia, ni jambo zuri sana. Lakini kama ambavyo inaonekana hivi sasa, tatizo la hili ni kwamba wakati imechangia kuwawezesha watu wengi kupata maji na tunashukuru sana, lakini wale ambao hawakupata wanajiona kama wametengwa na hivyo wanaibua hoja za kwamba kama vile wamepewa upendeleo watu wengine na wengine hawakuwapendelea. Lakini sio tu watu ambao wako nje ya mita 50, hata wale ambao wako ndani ya mita 50 wengine wamerukwa. Unakuta katika utekelezaji, huyu amepata bomba la maji na mwingine hakupata, pamoja na kwamba wote wameorodheshwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini si hivyo tu, kwa utaratibu huo huo wa mita 50 kuna maeneo mengine ambayo yaliorodheshwa hayakuwekewa kabisa. Sasa niliona niliseme hili kwa sababu kama nilivyoeleza awali, linaibua hoja za kisiasa na wakati huu ni wakati wa siasa zaidi na kwa sababu ni wakati wa siasa zaidi, ni vizuri Mheshimiwa Waziri na timu yake ya Wizara wakalifahamu hili. Pengine ingekuwa ni busara wapate muda waende wakaone utekelezaji wa mradi huu. Pia pamekuwa na malalamiko juu ya vifaa, mabomba, koki, na kadhalika, inaonekana kuwa ubora wake sio mzuri. Kwa hiyo, ningetoa wito kwa Wizara na wasimamizi wa mradi huu, kwamba waende wakaone udhaifu au wachunguze waone hali yenyewe jinsi ilivyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mradi huu ambao unaitwa mradi wa Wachina, kama nilivyosema kwa Mlandizi na Soga imekuwa hivyo hivyo, kuna maeneo ambayo watu hawakufikiwa nje ya mita 50, lakini pia hata ndani ya mita 50 kuna maeneo ambayo yameachwa. Lakini baya zaidi kwa pale Soga huku unakoanza mradi kwenye kitongoji cha Dengwa ambako ndiyo naishi pale, Mbunge ana maji, lakini akitoka nje ya uzio wake wananchi wake hawana maji.

Mheshimiwa Waziri ningeomba hili ulitazame kwa jicho la huruma. Najua nimepata maelezo kwamba pengine utekelezaji uko njiani lakini naomba utekelezaji ufanywe haraka basi kwa sababu ni jambo ambalo mimi kama Mbunge linanitia simanzi kidogo, kwamba nikitoka nje ya uzio pale pale kwenye kitongoji ambacho naishi, watu hawapati maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeona niyaseme haya kwa sababu kama nilivyosema awali wakati mwingine utekelezaji wa sera huibua hoja za kisera, hoja za kisiasa kama nilivyosema awali wakati huu ni wakati wa siasa zaidi, nafahamu kwamba watendaji

wako wakuu ndugu Mutalemwa na timu yake na pia wa *DAWASA* na timu yake wanafanya kazi kubwa na wamefanya kazi kubwa. Nawaomba tu waongeze juhudi ili suala hili lifikie tamati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kurejea tu na nisingependa kuwa na maneno mengi kwenye suala hili kwamba naishukuru sana Wizara kwa utekelezaji wa miradi hii. Nimeibua changamoto au utekelezaji wake umeibua changamoto na naomba changamoto hizi zitazamwe kwa karibu zaidi. Nawatakia kila la heri katika utekelezaji wa majukumu yenu katika Wizara. Ahsanteni sana.

**MHE. RAMADHAN A. MANENO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi nami niweze kuchangia hotuba ya Wizara ya Maji na Umwagiliaji. Kwanza, nami nichukue nafasi hii kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujalia heri tumeweza kukutana leo kuweza kuchangia Wizara ya Maji ambayo ni Wizara muhimu sana katika jamii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini niwashukuru wananchi wangu wa Jimbo la Chalinze kwa jinsi wanavyonipa ushirikiano na bado nawaahidi kwamba nitawatumikia ipasavyo kadri siku zinavyozidi kwenda. Nimshukuru Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu, Wakurugenzi, Meneja wetu wa mradi wa maji pale Wami Chalinze ndugu Akonae na watumishi wote jinsi wanavyoshirikiana nami katika kuhakikisha wananchi wa Jimbo la Chalinze wanapata maji ya uhakika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nami nichukue nafasi hii kwanza kuishukuru Wizara na Watumishi wote kwa jinsi wanavyofanya kazi kwa bidii wanavyotaka kuhakikisha mwananchi Mtanzania anapata maji. Lakini tatizo kubwa hapa ni bajeti finyu wanayopewa wenzetu wa Wizara ya Maji hatimaye kutokuweza kukamilisha miradi kwa wakati muafaka. Mimi nishauri Serikali ione jicho la huruma sana kwa upande wa Wizara ya Maji kuiongezea fedha za kutosha ili wananchi waweze kupata maji kwa wote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nishukuru Serikali kwa majibu mazuri au kwa maelezo mazuri waliyonieleza hapa leo kupitia kwenye hotuba ya Mheshimiwa Waziri kwa ukamilishaji wa mradi wa maji awamu ya pili katika Jimbo la Chalinze unaanza mwezi wa nane, niwashukuru sana niwaambie asante sana. Kwani Mheshimiwa Waziri kwangu ilikuwa kilio kikubwa kwa yale maji, kama huu mradi usingeanza mwezi wa nane, kwangu ilikuwa mtihani na katika maelezo yangu hapa ilikuwa nikuulize swali hili mradi wa awamu ya pili ya umaliziaji wa kusambaza maji vijiji vilivyobaki unaanza lini? Ila umenimalizia swali hili umenijibu ifikapo mwezi wa nane, wakandarasi wataanza kupelekwa vijijini hatimaye mambo yanaanza nikushukuru sana na niwahakikishie wananchi wangu wa vijiji vyote vile 48 havikupata maji awamu ya kwanza sasa wakae mkao wa kupata maji safi ya kutoka Wami. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimshukuru Mheshimiwa Waziri na Naibu wake walivyojitahidi kukamilisha mradi ule wa bwawa la umwagiliaji pale Msoga. Bwawa lile sasa limekamilika lina maji mengi na nishukuru Serikali tulishatenga milioni 350 kwa

ajili ya kuanza utekelezaji wa kuwasaidia wakulima wadogo wadogo ili kutumia bwawa lile Msoga ili mambo yaweze kwenda vizuri, nikushukuru sana Mheshimiwa Waziri na timu yako. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini niishukuru Serikali pia kwa kukamilisha bwawa lile la pale Masugulu, lakini pia nishauri kwa sababu mradi wa maji Chalinze Wami ambao utakamilika mwakani ambao utaanza kukamilika awamu ya pili mwezi Agosti, ule umoja wa WAMACHA uliopo pale Chalinze sasa ni vizuri ukaongezewa nguvu ama kupewa bodi ama sasa iwe mamlaka kamili kwani watumiaji watakuwa wengi na wigo utakuwa ni mpana sana kwa sababu mradi utafika mpaka Jimbo la Bagamoyo.

Pia utafika katika Jimbo la Kibaha kama alivyomaliza kusema Mheshimiwa kaka yangu Dr. Ibrahim Msabaha na pia utakwenda Morogoro vijijini. Sasa ni vizuri kukawa na mamlaka ya kuweza kuwasaidia wenzetu WAMACHA ili waweze kufanya kazi yao kwa umahiri na uhakika zaidi hasa kwenye kukusanya mapato. Lakini pia niwasihi wananchi baada ya kukamilika kwa huo mradi waitunze hii miradi na wasiwe wanaihujumu hasa wale ambao wanapenda kujiunganishia maji bila kutumia sheria na taratibu zilizowekwa na mamlaka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri katika kipindi hiki kwenye sekta ya maji mafanikio ni makubwa na mnahitaji kupongezwa na kila Mbunge humu atakayeinuka atasema kwake kunahitaji maji lakini mafanikio yameweza kuonekana. Niwasihi wananchi wangu wa Jimbo la Chalinze, kwa kuwa sasa tunakamilisha upatikanaji wa maji na mimi nataka nichukue nafasi hii kupitia Bunge lako Tukufu maombi yetu ya kutaka Chalinze iwe Wilaya nimeyaweka mezani kwa wahusika na *Inshallah* maji yakipatikana kwa wingi ombi letu hili linaweza likafanikiwa katika kipindi kijacho, wao tu wanipe nguvu, wanipe uwezo, wanipe tena, niweze kuwafuatilia maombi yao hatimaye Chalinze tuweze kupata Wilaya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimshukuru Mheshimiwa Rais ambaye ndiye Mwenyekiti wetu wa Chama cha Mapinduzi kwa kazi kubwa anayoifanya katika utekelezaji wa awamu ya nne katika mtiririko wake ule wa maneno yake ya Ari Mpya, Kasi Mpya na Nguvu Mpya na sisi pia tulitekeleza hiyo Ari Mpya, Nguvu Mpya na Kasi Mpya. Lakini juzi sasa amekuja na mpya amesema hali zaidi, Nguvu Zaidi na Kasi Zaidi. Sasa yule ambaye anayejua Ari Zaidi, Nguvu Zaidi na Kasi Zaidi ni yule aliyeshiriki kwenye Nguvu Mpya, Kasi Mpya na Ari Mpya ambaye ni mimi Mbunge wao Jimbo la Chalinze, sasa wanipe niendeleze hayo maneno aliyosema Mheshimiwa Rais juzi wasiweze kumpa mtu mwingine yoyote ambaye hakushiriki kwenye Kasi Mpya. *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niushukuru mradi wa Awamu ya Pili, kwa Vijiji vya Ubena, Msolwa, Mdaula, Tokamisasa tayari kazi imeanza lakini kubwa tu Mheshimiwa Waziri nimwombe, kwa hivi vijiji vilivyobaki wakandarasi watakaopewa kazi hii wapeni wakandarasi waliokuwa makini wenye uwezo ili miradi hii ikamilike kwa wakati muafaka. Kwa sababu kuwapata wakandarasi ambao hawana uhakika wanaotucheleweshea miradi yetu vijijini ni kuwakatisha tamaa wananchi. Niwaombe

sana wakati mko kwenye mchujo au mchakato wa kuwapata hao wakandarasi basi tuwapate wakandarasi wenye kuletea matumaini ya haraka iwezekanavyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nirudie tena kusema vijiji vile ambavyo sasa vitafaidika na mradi huu kama Pongwe Msungula, Mwatemo, Masuguru huko Kowekonje, Kwa Msanja, Kwa Luhombo, kwa Ng’andu, Mkange basi na wao wasikate tamaa kwani nilipita huko kwenye mwezi wa tatu nikiwaambia Serikali yetu ni sikivu itawahakikishia kuwafikishieni maji na leo uliponiambia mwezi wa nane mambo yataanza *Inshallah* na kwa kuwa na sisi kura za maoni zitaanza tarehe 1 Agosti, 2010 nitawaambia tu wasiwe na shaka mambo yatakuwa mazuri na wao tarehe 1 Agosti, 2010 watimize mazuri kwangu hatimaye mambo yaweze kwenda vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, nimtakie Mheshimiwa Waziri afya njema pamoja na timu yake kwa yale yote waliyodhamiria kuweza kukamilika katika 2010/2011, basi yatimizwe pamoja na ukamilishaji wa maji safi na salama, awamu ya pili katika Jimbo la Chalinze. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja. (*Makofi*)

**MHE. ELIETA N. SWITI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi, kabla sijaingia katika kuchangia hoja iliyoko mbele yetu, naomba kwanza nimshukuru sana Mheshimiwa Rais wa nchi yetu Dr. Jakaya Mrisho Kikwete kwa kufika hivi juzi tu Mkoa wa Rukwa na kufungua ujenzi wa barabara za lami. Lakini pia kwa kuzindua ujenzi wa kituo cha umeme utakaowezesha Manispaa ya Sumbawanga kupata umeme na Namanyele kupata umeme wa uhakika, nasema ahsante sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo naomba sasa nichangie hoja iliyopo mbele yetu, kwa ujumla tunasema hakuna kilimo bila maji. Mkoa wa Rukwa unajulikana kwa kuzalisha chakula na ni kwa sababu tu mvua inayonyesha kule kwa sasa tunasema inatosha lakini ili tuweze kuzalisha zaidi kilimo cha uhakika na endelevu kinategemea umwagiliaji.

Nichukue fursa hii basi kuipongeza sana Serikali ya Jamhuri ya Muungano na hasa ndugu zetu wanaoshughulika na umwagiliaji kuanzia Wizara mpaka kanda zetu za umwagiliaji kwa kutupatia sisi watu wa Rukwa miradi kadhaa ya umwagiliaji ikiwemo Urwila, Katuka na juzi juzi Rukwa tulipewa mradi wa Kkijiji cha Ulumi ambacho mimi Mbunge wa Viti Maalum nimeshirikiana nao katika kupata mradi huo kutoka *Japanes Food Aid*, nasema ahsante sana kwa Waziri mhusika kwa Naibu Waziri *Engineer* wa kweli kweli, Mheshimiwa Chiza na kwa wataalam wote wa umwagiliaji wa Wizara hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mtindo huo nasema sasa Rukwa kweli tutaruka tutaondoa umaskini na kwa kweli tutakwenda kama ambavyo Serikali yetu imepanga. Suala la maji safi na salama katika Mkoa wa Rukwa bado linahitaji kufanyiwa kazi ingawaje katika Mji wa Manispaa ya Sumbawanga kuna mradi mkubwa wa kusambaza maji bado yako maeneo ambayo hayawezi kufikiwa na mradi huu. Kwa hiyo, nachukua

nafasi hii kuiomba Serikali kutafuta namna nyingine ya kuwezesha maeneo hayo yaweze kupata maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mji wa Namanyere ni Mji Mkuu wa Wilaya ya Nkasi, mji huu una matatizo ya maji na tatizo hili ni sugu. Japokuwa labda hatuwezi kupata maji kutoka mahali pengine ambapo wanahitaji kupeleka nguvu nyingi lakini naiomba Serikali iwatume wataalam kusaidiana na Halmashauri ya Namanyele ili mji ule uweze kupata maji ya uhakika, safi na salama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, masuala ya Benki ya Dunia sasa hivi yamebadilika, Benki ya Dunia imekwishaanza kujikita katika kilimo jambo ambalo halikufanyika huko nyuma, nichukue fursa hii kuiomba Serikali yetu kuchukua mikopo ya Benki ya Dunia ili basi na sisi tuweze kupata miradi mikubwa zaidi ya umwagiliaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Benki ya Dunia huko nyuma haikuwa inashughulika na kilimo lakini sasa wamesema watashughulika na kilimo kwa kufuata sera ya nchi ile bila kufanya walivyofanya hapo zamani ambapo walifika ndani ya nchi husika na kusema tuna fedha hizi sasa tunataka ninyi mfanye hili na hili, wao wanasema watafuata sera ya nchi yetu. Kwa hiyo, naiomba Serikali ichukue mikopo hiyo ili nasi tuweze kufaidika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, visima na mabwawa katika Mkoa wa Rukwa ni muhimu sana, Mkoa wa Rukwa una mabonde mengi ambayo yatahitaji mabwawa na ni kwa sababu mahali huko hakuna mito, basi nichukue fursa hii kuiomba Serikali kutupatia mabwawa madogo madogo ambayo yanaweza kutumiwa na wakulima wa Rukwa ili kuweza kulima zaidi na kuzalisha zaidi chakula kwa ajili ya wananchi wa Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nichukue fursa hii kushukuru sana kwa kunipa nafasi ya kuweza kuchangia hoja iliyo mbele yetu. Naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MHE. ENG. BENITO W. MALANGALILA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nikushukuru wewe mwenyewe kwa kunipa nafasi hii, lakini kwanza nianze kumshukuru Mwenyezi Mungu, Mungu aliye hai kwa mapenzi yake ya kunipa uhai mpaka nipate nafasi siku ya leo ya kuzungumzia juu ya Wizara hii ya Maji na Umwagiliaji na pia nimshukuru sana Mheshimiwa Waziri wa Maji na Umwagiliaji pamoja na Naibu wake na Katibu Mkuu wao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia ningependa niishukuru sana Wizara hii ya Maji na Umwagiliaji kwa namna walivyoshughulikia suala la maji katika Jimbo langu la Mufindi Kusini, katika Vijiji vya Sawala, Mtwango, Lufuna, Kibao na pia katika kijiji cha Igoda, Luhunga na Mkonge. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama kumbukumbu zangu zitakuwa sahihi miaka yote takribani zaidi ya kumi nimekuwa nikiulizia maji katika kijiji cha Sawala, Mtwango, Lufuna, Kibao, Mpanga na Kitilu. Lakini Benki ya Dunia katika hivyo vijiji vinne, imetoa zaidi ya shilingi milioni 900 na ikataka sisi wananchi wa hivyo vijiji tuchangie

asilimia 2.5 hapo mwanzo ilionekana kwamba wananchi wale wachangie asilimia tano, ambayo ilikuwa inakuja karibu milioni 48 katika hivyo vijiji vinne.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini baadaye wakarekebisha kwamba tuchangie asilimia 2.5. Kwa hivyo, wananchi wale wanatakiwa kuchangia shilingi 24 milioni na hivyo hivyo kwa Igoda, Luhunga na Mkonge, Benki ya Dunia imetoa zaidi ya shilingi milioni 900 kwa maana hiyo na wananchi wa vile Vijiji vya Igoda, Luhunga na Mkonge nao wanatakiwa kuchangia asilimia 2.5 tu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, mimi binafsi nikiwa kama Mbunge wa lile Jimbo baada ya kuguswa sana katika mradi wa maji katika ule Mfuko wangu wa kuchochea maendeleo ya Jimbo nimechangia shilingi milioni moja, katika vijiji vya Sawala, Mtwango, Lufuna na Kibao. Hata hivyo, nimechangia milioni moja tena nyingine kwa ajili ya Ligonda, Luhunga na Mkonge. Kwa hiyo, lengo langu ni kwamba nipunguze makali ya michango ya wananchi kwa hiyo, namshukuru sana Mheshimiwa Waziri kwa namna kwanza alivyonivumilia nimemsumbua sana kwenye kile kiti chake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sawala, Mtwango, Lufuna na Kibao ulikuwepo mradi wa maji katika Serikali ya Awamu ya Kwanza, basi namwomba Mheshimiwa Waziri aurejeshe ule mradi, namshukuru sana Mheshimiwa Waziri kwamba hatimaye Serikali imenielewa na kwa maana hiyo ule mradi wa awamu ya kwanza umetekelezwa na kwa maana hiyo napenda kuishukuru Serikali ya Awamu ya Nne kwamba imenisikia kilio changu ambacho nimekuwa nikilia kwa miaka mingi sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini nimesema nilikuwa naulizia kijiji cha Mpanga na Kitiru. Mpanga iko chini sana ya Sawala, Kitiru iko chini sana Sawala na mimi nikiwa Mwenyekiti wa *NGO* moja pale Mufindi ilikuwa inaitwa Mdidea, yaani ni *NGO* iliyokuwa inasimamia maendeleo mchanganyiko, tulifanya *survey* na *survey* iko ofisi ya maji pale Mafinga, tuliona kwamba pale Sawala, linaweza kulisha Mpanga, linaweza kulisha Sawala yenyewe, linaweza kulisha Kitiru, linaweza kulisha na Kibao pia.

Kwa hiyo, nadhani Wizara hii ya Maji na Umwagiliaji waone kwamba hili ni jukumu lao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati nilipokuwa nauliza maswali hapa Bungeni, Serikali ilikuwa inasema kwamba Sawala, Mtango na Kibao ni Serikali Kuu, lakini Mpanga, Kitilu na Lufuna ni Halmashauri. Lakini namshukuru Mungu sana kwamba Lufuna kimekuwa ni kijiji cha 11 kati ya vijiji 10, kwa hiyo, Mufundi sasa tuna vijiji 11 na ninamshukuru Mungu zaidi katika vijiji 11, tisa vipo Jimboni kwangu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la mwisho, kuna vijiji vya Visima, kijiji kimoja kinaitwa Nyigo, Nyigo ni kijiji ambacho kiko mpakani mwa Njombe, Halmashauri imejitahidi kupeleka maji pale lakini kwa bahati mbaya kile chanzo ambacho tumechukua maji hakitoshelezi. Kwa hiyo, ninapenda Wizara hii ya Maji na Umwagiliaji, iende ikahakiki kile chanzo, kuna tenki kubwa sana pale Inyigo na tenki lile lilijengwa katika Serikali ya Awamu ya Kwanza, bahati mbaya sana kulikuwa na mashine ya maji

iliibiwa basi ninaomba Wizara iende pale Inyigo ikaongee na wenzetu wa Njombe. Juzi juzi nilikuwa naongea na Mheshimiwa Makwetta, tumeshakubaliana kwamba itabidi yale mabomba tuliyoweka pale tuyafumue ili twende tukaweke kwenye kile chanzo cha awali kabisa ambacho tulikuwa tumekiweka kule Inyigo. Kwa hiyo, huo ndiyo ushauri ambao ninapenda kuishauri Wizara asubuhi ya leo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia…

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa heshima naomba kuunga mkono hoja ya Wizara hii. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Mhandisi Benito Malangalila, sasa ni Mheshimiwa Felister, atafuatiwa na Mheshimiwa Benson Mpesya na baada ya hapo Mheshimiwa Sijapata F. Nkayamba ajiandae.

**MHE. FELISTER A. BURA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia katika Bunge lako Tukufu na kwa sababu ni mara yangu ya kwanza tangu nipate msiba mkubwa wa kufiwa na mume wangu, nianze kwa kutoa shukurani za dhati kwa Mheshimiwa Spika, Waheshimiwa Wabunge wote, Ofisi ya Katibu wa Bunge, Wanawake wote wa Mkoa wa Dodoma na wananchi wote waliojumuika pamoja nami katika msiba mzito ulionipata. Sina cha kuwalipa isipokuwa Mwenyezi Mungu atawalipa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze pia kumpongeza sana Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete, kwa kazi kubwa anayofanya katika kutekeleza Ilani ya Chama cha Mapinduzi ya uchaguzi ya mwaka 2005 kwa umahiri na kwa kudumisha amani katika nchi yetu. Nimpongeze pia kwa kutujengea Chuo Kikuu cha Dodoma, chuo ambacho hakina mfano wa kufananisha katika Afrika Mashariki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mkoa wa Dodoma, ni Mkoa kame, Mkoa ambao tunapata mvua kwa mwaka kwa kipindi cha wiki mbili tu na sana sana mvua zikizidi tunapata mvua kwa kipindi cha wiki tatu tu. Kwa hiyo, Mkoa wa Dodoma ni Mkoa kame sana, mahitaji ya maji ni makubwa sana kwa binadamu na pia kwa wanyama. Kwa hiyo, kwa kupata mvua kwa kipindi kifupi sana tuna mahitaji makubwa sana ya maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kipindi hiki cha miaka mitano, Serikali imejitahidi kutupa maji katika maeneo mbalimbali katika vijiji lakini bado kuna vijiji ambavyo viko kwenye programme ya maji vijijini ambavyo havijaweza kupata maji. Pengine nitaje baadhi ya vijiji hivyo katika Wilaya ya Dodoma mjini kwa mfano kijiji cha Ng’ong’ona, Chididimo, Chilolo, Mkonze na kadhalika. Ninaisihi sana Serikali

kwamba miradi hii inapopangwa kwenye programme basi kwenye maeneo yenye ukame kama Dodoma miradi hii ingetekelezwa kwa kipindi husika kwa sababu wanawake wanapata taabu sana, hawawezi wakafanya miradi mingine kipindi cha ukame. Sisi kipindi cha ukame kinaanza tangu mwezi wa nne mpaka Desemba wananchi hawana maji kwa ajili ya mifugo yao na wao wenyewe. Kwa hiyo, utakuta kutwa nzima wananchi na hasa wanawake wanahangaika kutafuta maji. Kwa hiyo, ninaomba miradi ambayo inapangwa na itekelezwe kwa kipindi husika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini vilevile mji wa Dodoma unakua kwa kasi sana na Serikali inaona, kuna haja ya kuweka mipango madhubuti ya maji katika mji wa Dodoma. Nimesoma katika hotuba ya Mheshimiwa Waziri akionyesha jinsi Serikali ya Tanzania ilivyoingia mkataba na Serikali ya Uswisi kujenga mifumo ya Majisafi na Majitaka yenye urefu wa kilomita 8.2, naipongeza sana Serikali kwa uamuzi huo. Lakini *programme* hii ingeendelea mpaka katika Chuo Kikuu cha Dodoma maana baada ya muda mfupi kutakuwa na wanafunzi 40,000 bado hujawahesabu wafanyakazi, Walimu, wafanyabiashara watakaofanya biashara katika eneo lile na kadhalika. Kwa hiyo, kuna mahitaji makubwa sana ya maji safi na salama na kuna mahitaji makubwa sana ya miundombinu ya maji na hata *system* ya maji machafu. Ninaiomba Serikali kulifikiria hilo na kuwa na mpango mkakati kwa sababu bila maji wanafunzi wale wanaweza wakapata tabu sana, wafanyakazi pia watapata tabu na bado tuna mahitaji makubwa sana ya maji katika Chuo Kikuu cha Dodoma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia kuna upotevu wa maji, katika hotuba ya Waziri, nimeona kuna upotevu mkubwa sana wa maji, upotevu huu unatokana na miundombinu iliyochakaa ya maji katika miji yetu. Mkoa wa Dodoma tu mathalani 44% ya maji yanapotea, ukienda Dar es Salaam 53%, Mkoa wa Lindi 61%, huu ni upotevu mkubwa sana wa maji. Nashauri tunapotekeleza *programme* mbalimbali za maji, hebu tuangalie namna ya kujenga miundombinu ya maji ili maji tunayoyapata kwa tabu basi yasiishie njiani na tunaposema tunachimba visima tunahakikishe kwamba wananchi wamepata maji, ni vizuri pia tukaangalia namna ya kutengeneza miundombinu ya maji ambayo imechakaa ili maji yasiendelee kupotea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Wilaya yetu ya Kongwa, tuna miradi mbalimbali ya maji na ninamshukuru Mungu na ninaishukuru Serikali kwamba miradi ambayo ilikuwa chini ya *World Bank* imeweza kutekelezwa na hata mwaka huu tuna pesa ambazo zimetengwa kwa ajili ya miradi mbalimbali ya maji vijijini. Lakini tuliahidiwa kupata gari kwa ajili ya kufuatilia maji katika vijiji hivyo ambavyo *programme* ya maji inatekelezwa. Ni muda mrefu sasa na tunaomba magari hayo yaje kwa sababu vijiji hivyo viko mbali na kufuatilia utekelezaji wa *programme* ni kazi kubwa. Ninaiomba Serikali yetu ambayo ni sikivu na Mheshimiwa Waziri tangu alipoingia madarakani katika Wizara hii ya Maji ametutembelea sana katika Wilaya ya Kongwa na ninaamini kwamba atatusaidia kupata magari kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nizungumzie pia suala la umwagiliaji katika mto Bubu. Tuliomba sana pesa kwa ajili ya kuanzisha mradi wa umwagiliaji katika mto Bubu katika Wilaya ya Kondoa. Nadhani suala hili la umwagiliaji katika mto Bubu Wilayani Kondoa

tumelizungumza kwa muda mrefu na Mheshimiwa Waziri analijua na tuna ahadi mbalimbali za Serikali kwamba mradi huu ungetekelezwa kabla ya uchaguzi huu ambao uko mbele yetu. Nina imani kwamba hata kama haipo kwenye bajeti hii basi bajeti ijayo Serikali itatusaidia kutuwezesha kuanzisha kilimo cha umwagiliaji kwa kutumia mto Bubu. Mkoa wetu kama nilivyosema, ni kame kwa hiyo tunapopata fursa ya kupata maji kwa ajili ya kilimo hasa cha umwagiliaji, nadhani shida ya chakula itaisha katika Mkoa wa Dodoma na ...

*(Hapa kengele alilia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**MHE. FELISTER A. BURA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Felister Bura lakini ningeweza kukupa dakika mbili au tatu umalizie yale ya Kongwa. *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Benson Mpesya atafuatiwa na Mheshimiwa Sijapata Nkayamba, Mheshimiwa Baba Askofu, karibu.

**MHE. BENSON M. MPESYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza naomba nikushukuru wewe kwa kutambua uwepo wangu katika nyumba hii. Naomba nitumie nafasi hii kwanza kabisa kukupongeza wewe binafsi kwa kukalia Kiti hicho kwa sasa hivi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwanza kwa kuchangia katika hoja hii kwa kuiunga sana mkono hoja hii na Serikali kwa ujumla kwa kuileta hapa. Ninaomba niwashauri wenzangu muungane na mimi kuiunga hoja hii ili fedha alizoomba Mheshimiwa Waziri tumpatie akatekeleze majukumu yaliyopo mbele yake hasa wengi tunavyofahamu jinsi anavyofuatilia, asivyopuuzia na ukiangalia katika bajeti karibu kila mahali pamoja na kwamba ni Sungura mdogo lakini amejitahidi katika nchi nzima kutoa uzito unaolingana katika kila miradi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa njia hii, naomba kwanza nimtakie kila la kheri Prof. Mark Mwandosya, Eng. Christoper K. Chiza, wafanyakazi wote wa Wizara hii ambao kwa muda wa miaka mitano tumefanya nao kazi vizuri, Wakurugenzi wote wa Majisafi na Majitaka Mijini, Wakurugenzi wote wa mabonde yote kwani kazi wanayoifanya ni kazi nzito sana hasa katika rasilimali hii kubwa sana. Mimi nawatakia Mawaziri wote wawili *Professor* pamoja na *Engineer* Mungu awarejeshe tena katika Bunge hili ili muendelee kuwatumikia Watanzania wenzenu kwa kazi nzuri mliyoionyesha na maombi yetu mara zote sisi ni daraja kati ya Mungu na tunaowaombe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nina mambo machache kwanza kwa sababu nafarijika na kazi nzuri inayofanywa kwanza kwenye Jimbo langu la Jiji la Mbeya, shughuli

zinazofanyika za miradi ya maji hasa kupitia kwa wafadhili wetu wa Ulaya pamoja na Shirika la KfW haileti shaka hata kidogo kwamba Serikali iliyopo madarakani na Makamisaa waliopewa majukumu wanayatekeleza majukumu yao vema. Nikianzia kwenye chanzo cha Nzovwe, nikienda kule Iganzo kazi iliyofanyika inaonyesha wazi kwamba tatizo la maji kwa Mbeya Mjini litaondokana kabisa na niwashukuru kwa sababu ya usikivu bonde la Uyole ilikuwa tuchelewe kupata maji lakini sasa maji yameelekezwa kule na miundombinu inatengenezwa kwa ajili ya kuhakikisha kwamba bonde la Uyole hawapati matatizo ya maji tena.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kwa nini nimesema nawaombea mrudi katika Bunge hili? Ni kwa sababu ya jambo moja zito, ninaomba muone kwamba maji ni rasilimali muhimu sana katika nchi hii na pengine hata miaka inayokuja maji itakuwa ni rasilimali muhimu sana. Sasa ni karibu miaka 49 toka tumepata uhuru, wapo ndugu zetu hawajawahi kunywa maji ya bomba, lakini siyo hilo tu, wenzetu katika dunia hii wamefikia mahali wanaita zile *social transfers* Serikali, sasa ifikie mahali kama si kwa kuondoa kabisa gharama za maji na kutoa maji bure kama ruzuku kwa wananchi basi tufikirie namna ya kupunguza kwa sababu maji ni rasilimali ambayo ni muhimu na ni dawa kwa wananchi lakini kwa kweli gharama za maji zimekuwa zikipanda kila wakati na kwa watu wanyonge ambao mnajua karibu 80% watu wetu tulionao ni watu wa kipato cha chini wamekuwa wakilalamikia sana gharama za maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninasema hivi kwa sababu wapo wenzetu ambao katika Serikali zilizoendelea wamefikia mahali wanatoa umeme na maji bure na sisi tufikirie hatuwezi labda tukasema hata umeme tutoe bure lakini tuangalie katika hii rasilimali ya maji, tuangalie ni namna gani tutakavyofika mahali kila Mtanzania apewe maji bure kama dawa. Uwezekano huo upo kwa sababu hizo ndiyo *social transfers*, lakini tukae chini na kukaa chini nawaomba sana wananchi wa Jimbo la Muhambwe kule Rungwe Mashariki waturudishie hawa watu ili tuweze kufanya kazi inayokusudiwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo langu ambalo ninajua kabisa kwamba limepewa uzito unaostahili, nitazungumzia juu ya upatikanaji wa maji katika Kata ya Itagano Mlimani kabisa kule juu unapokwenda Mlima Mbeya. Kata hii inapakana na Kata ya Ihango ya Mbeya Vijijini na watu hawa ni jamii moja, niliwahi kuzungumza hapa Bungeni kwa muda mrefu sana kwamba Kata zote mbili zinategemea chanzo cha Mto Malagala na katika vikao mbalimbali nimetoa ushauri wangu kwamba katika kusanifu mradi wa kuwapatia maji watu wa Itagano na Ihango unatakiwa uwe mradi mmoja tu kwa sababu chanzo ni hicho hicho cha Malagala na wale watu wanatenganishwa na barabara ndogo tu upande huu ni Mbeya Mjini na upande huu ni Mbeya Vijijini. Ninaamini kabisa shughuli za kuwapatia maji watu wa Ihango na Itagano zinaendelea vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nizungumzie jambo dogo tu lakini lina umuhimu wake hasa katika matumizi ya dira yaani dira za maji. Kwa mtu yeyote anayeelewa, unapomuwekea mteja dira ya maji maana yake atalipa kadri dira

itavyoonyesha kwamba ni kiasi gani cha maji amekitumia. Yapo matatizo madogo madogo yanatupata katika mazingira tunayokaa hasa katika matumizi ya maji, kwa mfano, kule kwangu katika Jiji la Mbeya watu wengi wanatumia maji kwa ajili ya kutengenezea matofali, lakini hawa watu wameshaweka dira na kama utatumia maji zaidi dira itaonyesha kwamba huyu ametumia maji kiasi hiki na mtu anapoweka maji nyumbani kwake atatumia kwa matumizi mbalimbali. Kama matofali ni kazi inayoweza kuajiri watu basi hatuwezi kuipuuza kwani ni kazi muhimu lakini unapomwambia mtu atoe faini au alipe achukue kibali cha kutumia maji zaidi, hapana, haiingii akilini kwamba dira imewekwa kwa ajili ya nini, maana utatumia maji na kadri yanavyozidi kutumika ndivyo utakavyolipa zaidi…

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**MHE. BENSON M.MPESYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga sana mkono hoja hii, ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana na sasa ni Mheshimiwa Sijapata F. Nkayamba atafuatiwa na Mheshimiwa Prof. Mwalyosi ambaye atakuwa ndiye mchangiaji wetu wa mwisho asubuhi hii. Sijapata naona hajapatikana, karibu Mheshimiwa Prof. Mwalyosi.

**MHE. PROF. RAPHAEL B. MWALYOSI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana kwa kunipa nafasi hii. Awali ya yote …

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Madgalena H. Sakaya utakuwa mchangiaji wetu wa mwisho.

**MHE. PROF. RAPHAEL B. MWALYOSI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote, nianze kwa kuipongeza na kuishukuru Serikali hususani Mawaziri hawa, Prof. Mark Mwandosya na Mheshimiwa Eng. Christopher K. Chiza, kwa kuwezesha kwa hali ya juu sana sekta ya upatikanaji wa maji pamoja na umwagiliaji katika Jimbo langu la Ludewa, nawashukuru sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, namba mbili, niwashukuru wananchi wa Ludewa kwa uvumilivu wao, hususani pale ambapo miradi yetu hii hasa ya maji, pengine hata ya umwagiliaji inapochelewa, wakati mwingine kukatisha tamaa lakini wameendelea kuwa wavumilivu sana. Nawashukuru na kuwapongeza vilevile kwa uvumilivu wao. Mshikamano waliouonesha, uvumilivu na imani yao kwangu katika kuwawezesha kimaendeleo kupitia sekta ya maji na kilimo hususan umwagiliaji, ninaamini mshikamano huo na uvumilivu vitaendelea endapo watanipa ridhaa yao katika kipindi kijacho na ninaamini watafanya hivyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa kuchangia kwenye sekta hii nitachangia kwenye maeneo yote mawili, maji na umwagiliaji. Kwenye suala la maji, wakati mimi ninaanza kazi katika Wilaya yetu ya Ludewa, chini ya asilimia 50 ya vijiji vyetu vilikuwa na maji

safi na ya uhakika si lazima yawe ya bomba, yanaweza kuwa ya visima lakini hadi hivi leo tunavyoongea tuna vijiji 19 ambavyo vimepita kwenye michakato mbalimbali ya kupata maji, kuna miradi iliyokamilika na miradi ambayo inakaribia kuisha. Lakini vilevile tuna vijiji 15 ambavyo viko chini ya programu hii ya Benki ya Dunia ambavyo vinaendelea na mchakato huu wa kupata maji. Ukijumlisha vijiji hivyo ni karibu vijiji 34 ambavyo ni karibu 44% ya vijiji vyote 77 vya Wilaya ya Ludewa. Kwa hiyo, tumechangia katika kipindi hiki 44% ya upatikanaji wa maji katika Wilaya yetu. Ukifanya hesabu, ukijumlisha na asilimia tuliyokuwa nayo kabla ya 2005 utakuta tunabakiwa na kiasi cha 10% ya vijiji ambavyo vitakuwa bado havina maji. Nakumbuka vijiji hivyo ni pamoja na vile vya Maholomwa, kule Ludende, kuna vijiji vya Mwambao, kule Nkanda na kadhalika na Utilili kule Lupanga lakini ninaamini katika kipindi hiki kutokana na uzoefu na kazi nzuri wanayofanya Mawaziri hawa, Mwandosya na Chiza, lazima tutapata miradi mingine kuwezesha kuhakikisha kwamba, vijiji vilivyobaki vinapata maji ili iwe 100% kwa vijiji vya Wilaya ya Ludewa kuwa na maji safi, ninawashukuru sana kwa hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye upande wa umwangiliaji, nilipoanza kazi tulikuwa hatuna mradi wowote wa umwagiliaji, lakini hivi ninavyozungumza leo tuna skimu tatu ambazo ziko kwenye mchakato wa kufikia hatua ya umwagiliaji. Skimu moja kule Lifua katika Kata ya Lwilo, sehemu kubwa ya miundombinu imekamilika, bwawa limejengwa, mifereji imejengwa kwa shilingi milioni 400 na hivi ninavyozungumza kuna shilingi milioni 230 nyingine ambazo ziko kwa ajili ya kurefusha mfereji kwa ajili ya umwagiliaji. Kazi hiyo ya kurefusha mfereji imeanza na tunategemea katika msimu huu wa kiangazi mfereji ule utaanza kazi na wananchi wataweza kuzalisha chakula, hasa mpunga na ingawaje wanamwagilia tayari lakini umakini katika umwagiliaji utaongezeka na tija itakuwa kubwa zaidi. Eneo lile ni kame, kwa hiyo wananchi wanapata shida ya chakula kila mwaka, tunatarajia katika Kata zile na za jirani watakuwa na chakula cha kutosha na ziada ya kuuza katika maeneo mengine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mradi wa pili kwa umuhimu ni wa Mkiu ambao tuna fedha shilingi milioni 340 zipo na Mkandarasi karibu anaanza kazi ya ujenzi wa miundombinu. Mradi mwingine ambao ni wa muhimu ni ule wa Manda, ambao una hekta karibu 1000 tafiti zake zimekamilika na tunangojea ujenzi wa bwawa, ambalo pia linatakiwa liwe daraja la kuvuta mto Luhuhu na ninajua tafiti zote zinazotakiwa zimekamilika na tunachongojea ni fedha kutoka Serikalini kwa ajili ya ujenzi wa daraja ambalo vilevile litakuwa ni bwawa kwa ajili ya kutiririsha maji kwenda kwenye umwagiliaji. Eneo hili la Manda kama nilivyosema ni sehemu ya Tarafa ya Masasi, ni kame sana ‘*semi arid*’ na kila mwaka wanapata shida ya chakula. Kwa hiyo, wananchi hasa wa Manda nao wameunda ushirika wao, wameandikisha chama chao na wako tayari kwa kazi ya umwagiliaji, wanachongoja ni kukamilika kwa mradi huu ili wakaanze kazi kubwa ya umwagiliaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Rais alipotembelea maeneo yale mwaka jana aliahidi ujenzi wa daraja lile na mimi nimezungumza na Prof. Mwandosya, Waziri wa Miundombinu kwamba kutokana na agizo lile Wizara hizi mbili na kwa kushirikiana pamoja na Wizara ya Kilimo na Mikoa ya Iringa na Ruvuma, tufanye juhudi kuhakikisha kwamba daraja na bwawa lile linajengwa upesi iwezekanavyo ili wananchi hawa waanze kufaidi umwagiliaji katika eneo lile na kujiondoa katika matatizo makubwa ya chakula kila mwaka. Nitapenda kujua Mheshimiwa Waziri, uniambie ushirikiano wenu na Miundombinu pengine na Wizara nyingine ambazo niliwaandikia barua na nikaomba mshirikiane ili fedha zipatikane haraka, nitapenda kujua mmefikia wapi na ni lini mradi huo utaanza kazi hasa baada ya kujenga daraja ambalo vilevile ni bwawa. Nitashukuru na wananchi wale wananisikia na wana hamu sana ya kuanza kazi ya umwagiliaji pale.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niseme tu kwamba wananchi wetu ni waelewa sana, pale wanapoelezwa hatua kwa hatua kazi zinazoendelea na mipango ya Serikali, wanapoelezwa wanaelewa lakini inapochukua muda mrefu sana wanaanza kukata tamaa kwamba mambo tunayoyapata huku Bungeni kutoka kwenye Serikali wanadhania pengine ni porojo tu au ni uongo. Lakini mimi ninataka kuwathibitishia wananchi hawa kwamba, Serikali yetu ni sikivu, inafanya kazi kwa mipangilio mizuri, inaelewa mahitaji ya wananchi na wanaendelea kutusaidia kwa kadri mafungu ya fedha yanapopatikana na sisi Wabunge kazi yetu tunanyang'anyana hapa fedha kidogo 'Sungura mdogo huyu' kila mmoja anapeleka Jimboni kwake kidogo anachopewa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa maneno hayo, ninakushukuru sana kwa kunipa nafasi, ninaunga mkono hoja, ahsante. *(Makofi)*

**MHE. MAGDALENA H. SAKAYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa na mimi nafasi ili niweze kuchangia hoja iliyoko mbele yetu. Awali ya yote, nimpongeze Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri na Watalaamu wote wa Wizara hii kwa kuweza kuandaa hii hotuba na kutuletea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia niipongeze sana hotuba ya Kambi ya Upinzani, nimpongeze Msemaji Mkuu wa Kambi ya Upinzani, ametoa hotuba nzuri sana, ninaomba Serikali iifanyie kazi, iitumie ili iweze kuboresha huduma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niende moja kwa moja kwenye mchango wangu. Kwanza, naenda kwenye kitabu cha Mheshimiwa Waziri, ukurasa wa 70. Nashukuru sana kusikia kwamba, jumuiya nyingi sana zipatazo 263 za watumiaji wa maji zimeundwa Mikoa mbalimbali hapa Tanzania. Kwa kweli, hilo ni faraja kubwa, lakini hoja yangu kubwa ninataka kujua, watumiaji hawa kwa kuunda jumuiya zao hizi ni kwa kiasi gani wanashiriki kutunza vyanzo vya maji? Kwa sababu kuunda jumuiya ni jambo moja lakini kubwa na la msingi ni kwa jinsi gani kila anayetumia maji atashiriki kutunza vyanzo vya maji ili viweze kuwa na maji endelevu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nasema hivyo kwa sababu kwa muda mrefu sana tumeona maeneo mengi, makampuni na viwanda wakiwa watumiaji wakubwa wa maji na wanaweka mpaka mabomba ya kunyonya maji kwenye mito mbalimbali, lakini wanakuwa hawashirikishwi kikamilifu na wengi wao pia wamekuwa hata baada ya kuchukua maji safi kutoka kwenye mito lakini wanamwaga maji machafu kutoka viwandani na kuyaelekeza kwenye maji safi na salama ambayo ni kwa ajili ya matumizi ya wananchi. Kwa hiyo, ninaomba wakati Mheshimiwa Waziri ana-*wind up* ajaribu kutuambia, ni kwa jinsi gani jumuiya zote hizi 263 zimeshiriki kikamilifu kutunza vyanzo vya maji kwenye Mikoa mbalimbali ambayo imetajwa hapa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ni kukosekana kwa umakini mkubwa na utaalamu wa kutosha tunapotekeleza miradi yetu mikubwa. Ni jambo la kusikitisha, utakuta mradi mkubwa unatekelezwa kwa kugharimu mamilioni ya pesa, lakini ndani ya muda mfupi unakuta wananchi wa eneo lile lile wanaanza kulalamika maji. Mfano mzuri ni mradi mkubwa wa maji wa Kahama - Shinyanga. Hapa Bungeni kila mmoja aliona wivu kwamba, wananchi wa Kahama na Shinyanga sasa wameondokana na tatizo la maji. Mradi ambao umegharimu shilingi bilioni 252, lakini kwa taarifa ambazo zipo kwenye Mkoa wa Mwanza, tangia kukamilika kwa mradi mpaka sasa, kila siku iendayo kwa Mungu lita 40,000 zinapotelea ardhini bila kutumika. MUWASA yenyewe inatumia shilingi milioni 300 kusafisha maji kwa kutumia gharama kubwa za umeme, lakini kwa sababu maji hayo yanapotea MUWASA inapata hasara ya shilingi milioni 300 kwa ajili ya kusafisha maji ambayo hayatumiki. Hivi tunakwenda wapi? Gharama kubwa kama hizi zinapotea, huku Watanzania wengi hatuna huduma ya maji, tunalalamika tu. Kambuzi kweli ni kadogo, tunasema tunagawana kasungura, kwa nini tugawane bila kuwa na utaratibu na umakini? Nina wasiwasi kwamba, wataalam waliotumika wakati wa utekelezaji wa mradi huu hawakuwa makini vya kutosha kwa sababu kwa taarifa zilizopo ni kwamba, wameweka *pressure* kubwa ya maji, mabomba mapya yanaunganishwa kwenye mabomba ya wakati wa ukoloni, kwa hiyo, kila siku mabomba yanapasuka. Pamoja na kwamba zipo hujuma za wananchi, lakini ni ndogo sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatizo kubwa ni *pressure* ambayo ni kubwa wakati *diameter* ya mabomba ni ndogo, kwa hiyo maji yanavyokuja kwa *pressure* kubwa, yanapasuka na maji yanaelea ardhini, wakati huo huo hapa tumeshuhudia Waheshimiwa Wabunge kutoka Shinyanga, Nkasi na maeneo mengine wakilalamika kuwa wananchi wao hawana maji. Hiyo ni aibu na tunaomba sana Serikali inapoamua ku-*implement* mradi kwa kujua kwamba fedha ni kidogo kwa mfano kwa kuwa mradi huu wa Shinyanga ulifadhiliwa na fedha kutoka *World Bank,* kwa hiyo ilibidi utekelezwe kwa ukamilifu ili kuhakikisha kwamba angalau kwa miaka 10 ijayo tatizo la Shinyanga na Kahama lingekwisha na tunahama kwenda eneo lingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivyo hivyo kwa maeneo mengine kwa mfano ukiangalia mradi wa Newala umegharimu shilingi milioni 172 lakini hadi leo wananchi

wa Newala wanalalamika kuhusu maji. Ukiangalia mradi wa Pwaga, Mpwapwa, umegharimu shilingi mlioni 600, nguvu za wananchi pamoja na msaada lakini bado wananchi wanalalamika kuhusu kutopata maji. Tukienda hivi hatupigi hatua na tutakuwa tunapiga *mark time*, nenda mbele, rudi nyuma kwa sababu hivi leo hatuketegemea wananchi wa Pwaga walalamike kuhusu maji. Sisi watu wa Urambo ambao tunalalamika kuhusu maji miaka yote tulitegemea Serikali ihamie kule na kutuletea maji, lakini kuendelea kurudi tena huku Pwaga wanalalamika, huku Shinyanga wanalalamika, kilio cha maji Tanzania kitaendelea miaka yote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ni la uchimbaji visima 10 kwa kila Wilaya. Kwanza, niseme tu kwamba, hii programu inakwenda taratibu sana, sijui kwa Wilaya nyingine lakini kwa mfano Wilaya yetu ya Urambo inakwenda taratibu sana. Wananchi tulipata matumaini kwamba, angalau baada ya muda fulani tutakuwa tumeondokana na tatizo sugu la maji, lakini hii programu inakwenda taratibu sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kingine ni kwamba, ninarudi palepale kwenye utaalam, hatuna wataalam wanaokidhi viwango kwa sababu hata vile visima vichache ambavyo vimechimbwa bado wakati wa ukame vinakauka, inawezekana wamekwenda kuchimba kipindi cha mvua wakashindwa kutathmini kwamba wakati wa ukame kutakuwepo na shida. Kwa hiyo, ninaomba sana, hii programu ni nzuri lakini *is very slow* na pia wanapochimba vile visima kwa sababu vinatakiwa kuwa visima virefu basi kweli viwe virefu vya kuweza kukidhi haja kwa matumizi ya leo na kesho, kwa sababu bado, Urambo ni tatizo, akina mama wanatembea kilomita tano kufuata maji na wengine wameamua kujichimbia visima vyao vidogo vidogo jirani na nyumbani, kitu ambacho tunajua kabisa maji yako juu na siyo salama, lakini wafanyaje!

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ni miundombinu ya maji kwa Manispaa ya Tabora. Nashukuru leo asubuhi Serikali imetujibu kwamba, kuna mpango mzuri wa kuhakikisha kwamba Mkoa wa Tabora, hasa Manispaa inapata maji salama, lakini pamoja na taratibu na harakati hizo bado sasa hivi maji yanayotumika pale siyo salama na siyo salama kwa sababu mabwawa yale ni ya muda mrefu na maji ni machafu sana. Manispaa haiwezi kugharamia kusafisha yale maji mpaka yawe katika viwango vya kutumiwa na binadamu. Kwa hiyo, ninaiomba Serikali wakati inaendelea na taratibu hizo za kuhakikisha kwamba Tabora tunapata maji safi na salama, isaidie Manispaa kupata zile dawa za kusafisha maji kwa sababu viongozi wakija Mkoani pale, Manispaa wanajitahidi kweli maji yaonekane ni safi, viongozi hawa wakifungua maji hawawezi kuona kuwa ni machafu, lakini wakiondoka tu ukirudi ukiangalia maji yanayotumiwa na wananchi, ni maji ambayo sura yake inatisha. Kwa kweli, siyo maji safi wala salama na tunaomba sana Serikali itilie mkazo kuhakikisha kwamba, hili linafanyika ili wananchi wale waweze kujikomboa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nadhani yangu ni hayo machache ninakushukuru sana, ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, muda uliobaki kwa kweli haumtoshi mchangiaji yeyote mwingine. Uchangiaji huu utaendelea jioni kabla ya Mheshimiwa Naibu Waziri na Mheshimiwa Waziri, kujibu hoja zetu. Kwa hiyo, tutakaporudi Saa

11.00 jioni, Mheshimiwa Sijapata Nkayamba ataanza, atafuatiwa na Mheshimiwa Dr. Zainab Gama na baadaye Mheshimiwa Nimrod Mkono atafuatia. Kwa hatua hiyo basi, ninaomba kusitisha shughuli za Bunge hadi Saa 11.00 jioni.

*(Saa 6. 59 mchana Bunge lilisitishwa mpaka Saa 11.00 jioni)*

*(Saa 11.00 jioni Bunge lilirudia)*

*Mwenyekiti (Mhe. Zubeir Ali Maulid) Alikalia Kiti*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge tunaendelea. Waheshimiwa Wabunge naomba niwataje wachangiaji kama walivyotajwa watatu wa mwanzo wa jioni hii ni Mheshimiwa Sijapata Nkayamba, atafuatiwa na Mheshimiwa Dr. Zainab Gama, atafuatiwa na Mheshimiwa Nimrod Mkono na Mheshimiwa Christopher Ole Sendeka ajiandae.

Mheshimiwa Sijapata Nkayamba simuoni, sasa namwita Mheshimiwa Dkt. Zainab Gama ambaye naye simuoni, sasa moja kwa moja nampa Mheshimiwa Christopher Ole-Sendeka kwa sababu Mheshimiwa Mkono naye simuoni ili aweze kuchangia.

**MHE. CHRISTOPHER O. OLE-SENDEKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nianze mazungumzo yangu ya jioni ya leo, kukushukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia hoja hii ya Wizara ya Maji na Umwagiliaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwanza kwa kumpongeza Prof. Mark Mwandosya, Waziri wa Maji na Umwagiliaji pamoja na Naibu Waziri Eng. Christopher Chiza, Katibu Mkuu na watendaji wengine wote wa Wizara, kwa kutambua matatizo ya msingi yanayoikabili Wilaya ya Simanjiro katika tatizo kubwa la maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Baba wa Taifa Mwalim Julius Kambarage Nyerere, katika miaka ya 1987 alipokuwa akihutubia Mkutano Mkuu kwa CCM kwenye wosia wake aliwahi kusema maneno haya na kwa ruhusa yako naomba kunukuu:-

*“Mawazo yanaendelea kujengeka miongoni mwa Watanzania kwamba kati ya maneno ya viongozi na matendo yao kuna ufa unaozidi kupanuka. Uzito wa matatizo yetu na ugumu wa kuyatafutia ufumbuzi wa haraka inaendeleza mawazo na mashaka haya”.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Baba wa Taifa Mwalimu Julius Kambarage Nyerere aliyatumia maneno haya katika Kitabu chake cha Wosia wa Mwalimu katika Mkutano wa

mwaka 1987 wakati anang'atuka kuwa Mwenyekiti wa Taifa wa Chama Tawala cha CCM. Makusudi mahsusi ya Mwalimu kueleza ufa uliopo kati ya maneno na vitendo vya viongozi, ililenga makusudi kuwashauri na kuwashawishi Watanzania na hasa viongozi kutembea katika maneno yao kwamba unapotoa ahadi fulani, ni vizuri kwa muungwana ahadi hiyo ukaitekeleza kwa kasi, ari na nguvu na kwa haraka inavyowezekana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, imani yangu ni kwamba Serikali ya Chama cha Mapinduzi ni Serikali sikivu. Nitumie nafasi hii kuwakumbusha tu viongozi wetu, wakati mwingine kwamba ni vizuri yale ambayo wameahidiwa yakatekelezwa kwa nguvu stahiki. Wabunge wote wa Bunge hili na Watanzania kwa ujumla, walishuhudia kauli ya Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Mizengo Kayanza Peter Pinda, alivyosema:-

*"Japokuwa katika Wilaya nyingi za nchi yetu kuna matatizo ya maji lakini Wilaya ya Simanjiro inaongoza kwa tatizo la maji."*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini ni wakati huo ndipo Serikali ilipotenga shilingi milioni moja kwa ajili ya upembuzi wa mradi wa kuyavuta maji kutoka Mto Ruvu na kupeleka Makao Makuu ya Wilaya ya Simanjiro pale Orkesmet. Ni ukweli usiofichika kwamba kutoka Makao Makuu ya Wilaya ya Simanjiro Orkesmet kwenda mahali ambapo wanaweza kupata maji ya mto, ni kilomita zaidi 75 kupitia kijiji cha Lerumo na kwenda mpaka Ruvu-Remiti. Wakati wa kiangazi inapofika mwezi Juni na Julai, vijiji zaidi ya 15 vya Wilaya ya Simanjiro wanalazimika kuhama kutoka kwenye makazi yao ya kudumu kufuata maji katika maeneo mengine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kwa maana hiyo, Madiwani wa Halmashauri ya Wilaya Simanjiro na mimi Mbunge wao tulihakikisha kwamba fedha kidogo tunazozipata kutoka katika *Capital Development Grant* tunazielekeza kwa sehemu kubwa katika uchimbaji wa visima. Nataka nikuhakikishie na kulihakikishia Bunge lako Tukufu na Waziri wa Maji anajua hili kwamba tumejitahidi sana kuchimba visima vingi, tumekosa maji katika baadhi ya visima, lakini vingine tumepata maji na namshukuru kipekee Mheshimiwa Prof. Mark Mwandosya, kwa kushirikiana na Waziri Mkuu kwa kulitambua tatizo hilo na kutenga shilingi milioni 200 kwa ajili ya kutafuta maji katika mji wa Orkesmet. Nataka kusema tumefanikiwa kiasi, tumepata maji katika visima vichache pale Simanjiro Sekondari, kijiji cha Narosoito, tumepata maji Lormorijoi, Lakaiyanga na maeneo hayo yote yanahitaji miundombinu kwa maana ya *tank, cattle trough* na maeneo ya binadamu kuchotea maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini tumekwenda mbali zaidi, kwa kutumia fedha za *CDG*, tumechimba na kupata maji katika kijiji cha Loonderkes, tumepata maji Namalulu, Loswaki, Engonongoi, Nyorit, Mbuko, kote kule tumefanikiwa kupata maji. Tumepata maji katika eneo la Sekondari Loiboisoit, kwenye Kata ya Kijiji cha Ngage, tumepata maji Msitu wa Tembo, tumepata maji katika eneo lingine la Kata ya Loiborsiret ambapo tulichimbiwa na Kampuni moja ya Bundu Safari, lakini haina miundombinu. Nitumie nafasi hii kuiomba Serikali sasa isaidie kukamilisha miundombinu hiyo ya maji ili vijiji

vile ambavyo vinahama wakati wa mwezi wa Julai waendelee kuwa na anuani ya kudumu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lengo la Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ni ustawi wa Watanzania. Ili uweze kukamilisha lengo la ustawi wa Watanzania, ni lazima kuwepo na maendeleo yenye uwiano kati ya jamii moja na jamii nyingine katika sehemu moja ya nchi na sehemu nyingine ya nchi. Haiingii akilini wala huwezi kumshauri mtu mwenye akili zake kwamba mpaka leo baada ya miaka mingi ya uhuru kuna watu ambao wanachota maji kwa kutumia mifuko ya ngozi katika visima ambavyo watu wanapokezana kati ya watu sita, wanapokezana ndoo za maji ili zifike kwenye hori la ng'ombe ili na ng'ombe waweze kupata maji katika eneo au katika mahori ya kutengeneza kienyeji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni rai yangu kwa Serikali ya Chama changu kwamba katika Bunge hili Tukufu na hasa katika bajeti hii ya leo, Mheshimiwa Prof. Mwandosya, kwa niaba ya Serikali, atoe kauli itakayowafariji wananchi wa Simanjiro kuondokana na tatizo la maji. Mimi sio mwizi wa fadhila, natambua bwawa mlilonipa la Emboreet ambako tumeweka katika korongo la Namuke na maji tumeweza kuyapata. Nitumie nafasi hii pamoja na kukumbusha tatizo la maji na kuomba Serikali baadaye itoe maelezo na nichukue pia nafasi hiyo kuikumbisha Wizara ya Maji na Umwagiliaji kwamba pamoja na kwamba Simanjiro ni miongoni mwa maeneo ambayo ipo katika maeneo kame au nyanda kame, *semi arid land* lakini yako maeneo pia ya upande wa Mashariki ya Wilaya Simanjiro ambayo yana Mto Ruvu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuna maeneo mazuri kwa ajili ya umwagiliaji ambayo yangeweza kupunguza tatizo la chakula na kwamba kauli yetu ya Kilimo Kwanza katika eneo hili lingewezekana. Kijiji cha Ruvu-Remit, kijiji cha Ngage, Gunge, Lemkuna, Kiluwani, Kijiji cha Msitu wa Tembo na kijiji cha Kambi ya Chokaa, ni maeneo ambayo yana mto na yana maji kwa wakati wote lakini haina miundombinu bora ya umwagiliaji. Mheshimiwa Rais Jakaya Mrisho Kikwete alipita maeneo hayo na kuahidi kwamba mambo haya yatashughulikiwa. Nafikiri kwamba madhali upembuzi yakinifu umekamilika katika eneo la Malila na katika sehemu ya kijiji cha Ngage na katika maeneo mengine ya Lemkuna, ni rai yangu kwamba Wizara ya Maji na Umwagiliaji, sasa itenge fedha maalum kwa ajili ya kukamilisha miundombinu ya maeneo hayo niliyoyataja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa muungwana ahadi ni deni. Mheshimiwa Rais Kikwete aliahidi alipofanya ziara katika Wilaya ya Simanjiro kwamba mradi wa maji wa Orkesmet ungeanza kabla ya mchakato wa uchaguzi. Ni rai yangu kwamba wanaomsaidia Rais Kikwete, Mheshimiwa Prof. Mark Mwandosya, Naibu Waziri, Mheshimiwa Christopher Chiza na Waziri Mkuu ambaye ni mtu mwenye ahadi na ambaye kwa kweli analijua tatizo hili, wote mtakaa na Waziri wa Fedha, mtafute fedha kwa ajili ya mradi wa Orkesmet. Vinginevyo Waziri Mwandosya alishafika ameliona lile tatizo, Naibu wake aliona tatizo lililopo, Mheshimiwa Rais analijua na wananchi wa Simanjiro wanasubiri kauli ya faraja ili nao waweze kuwa na anuani ya kudumu.

Hatuwezi kuwaambia wafugaji waache kuhamahama kutoka sehemu moja ya nchi kwenda sehemu nyingine wakati hawana maji kwa ajili ya mifugo yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninamheshimu na nawaheshimu sana viongozi wanaoongoza Wizara hii. Namheshimu sana Waziri Mkuu wangu, naiheshimu sana Serikali ya Chama change lakini wananchi wa Simanjiro wataniona kama msanii nitakaposimama na hasa katika mwezi huu Juni nikasema naunga mkono kabla sijapata ufafanuzi. Mheshimiwa Waziri nategemea kauli yako ndiyo itakayonipa msimamo wa baadaye wa kuunga au kutokuunga mkono hoja yako. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa Christopher Ole-Sendeka. Sasa Waheshimiwa Wabunge, namwona Mheshimiwa Dkt. Zainab Gama ameingia, nitamruhusu lakini pamoja na hivyo namwomba Mheshimiwa Zabein Muhaji Mhita ajiandae pamoja na Mheshimiwa Dkt. Raphael Chegeni.

**MHE. DR. ZAINAB A. GAMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nikushukuru sana, ulipokuwa unaniita nilikuwa mlangoni, nakushukuru sana. Kwanza, naomba kusema naunga mkono hoja ya Wizara hii kwa asilimia mia kwa mia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niishukuru Wizara hii ya Maji na Umwagiliaji na Mawaziri wote walioingia katika Wizara hii, wamelisaidia Jimbo la Kibaha Mjini kwenye tatizo kubwa la maji. Naomba niwashukuru sana wote na Mheshimiwa Prof. Mark Mwandosya amenisaidia zaidi, naomba nimshukuru.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ndugu zangu, kabla sijasema nini kilichotendeka, nataka kusema hivi, ukimuona msichana umempenda na ukamsifia, usimtukanie wazazi wake, ukimtukania wazazi wake hustahili kuoa. Kuna baadhi ya wagombea wanataka kugombea kupitia CCM lakini wanasaidiana na watu ambao hawaipendi CCM kwa kusema Ilani haikutekelezwa, wanasema Mbunge hakufanya kitu chochote. Bahati mbaya ilikuwa nizungumze katika Ofisi ya Waziri Mkuu kwa sababu ni Wizara ya Maji inabidi niseme maji tu kwa hiyo mengine sitosema, nitasema maji tu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilipoinuka, nilitangaza Ilani na utekelezaji, kwa yeyote anayesema Mbunge hakufanya kitu maana yake unasema Chama cha Mapinduzi na Serikali yake haikufanya kitu, hao ni wasaliti, hao ni matapeli wanaojidai kuwadanganya wananchi. Chama cha Mapinduzi, Wilaya ya Kibaha imetekeleza Ilani kwa uhakika. Kila mwaka tukikaa hapa katika bajeti fedha zinawekwa ili kutekeleza Ilani. Yule anayesema Ilani haikutekelezwa eti kwa sababu Mbunge hakufanya kitu ni kwamba hizi fedha mnazozitoa nyinyi ni Mbunge na watu wake kule Watendaji na Madiwani wanakula, si sahihi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hivyo, naomba wananchi wangu muwaangalie hao wanaokuja, hawaishi Kibaha, hawaijui Kibaha, wanaishi Dar es Salaam, wameogopa kugombea Dar es Salaam wanakuja kugombea huku, kwa sasa naomba nizungumze.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, nawashukuru Mawaziri wote kwa sababu katika mradi wa *Quick Win,* sisi tuliwekwa Kibaha Kijijini na Kibaha Mjini na Kibaha Mjini tukapewa vijiji vinne kati ya vijiji 10 ambapo sita vilipewa Vijijini, nilipokwenda kubembeleza kila mwaka ilipokuwa *Quick Win,* nilipewa vijiji 10, naomba niwashukuru sana Wizara hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini naomba niwashukuru sana sasa hivi nikisema wananchi wataelewa, kwa sasa kuna mradi unaitwa mradi wa Wachina, najua sio wa Wachina isipokuwa *contractor* alikuwa Mchina, nani asiyeona Kibaha Mjini sehemu kubwa ya watu wamepata maji. Mita 50 wamepewa bure maana yake hawakugharamia hata ile *pipe* ya kwenda kwao, nani asiyeona hilo, huo sio utekelezaji wa Ilani? Kwa hiyo, nawaambia wananchi wangu hao matapeli wanaojidai Mbunge hakufanya kitu wana matatizo. Kwa hiyo, naomba niseme tu katika mradi huu na nilikuomba Waziri kwamba mtu mita 50 amepewa maji na mwingine anasema yuko tayari kuvuta kwa gharama yake kuendelea zaidi ya mita 50 wanasema haiwezekani. Sasa Waziri umeniahidi utazungumza na watendaji wako angalau haya maji watu watagharamia wenyewe kupeleka katika lile eneo *vicinity* ya maji yanayoweza kupatikana. Ningekuomba hilo kwa sababu wananchi wengi wameshakuja kwangu maana yake imekuwa nyumbani kwangu sasa ni kila siku mikutano nawapeleka kwa Mhandisi wa Maji, jibu kamili hajawapa, maji haya wao wanasema wako tayari kuvuta wao wenyewe kwa fedha, naomba muwasaidie hawa watu mita 50 hapo halafu mbele yake tu mtu anakosa maji, hilo nilikuwa naomba nisaidiwe sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri naomba anisaidie, Vikawe nisipoizungumzia inaniuma, kila mwaka nazungumzia Vikawe, Vikawe hawana maji hata ile *Quick Win* ilipokwenda kuchimba visima hawakupata maji. Vikawe wanachota maji ndoo shilingi 500/=. Nashukuru sasa hivi angalau kuna wenye *bulldozer*, wanaleta maji kutoka Dar es Salaam lakini ndoo shilingi 500/= zamani walikuwa wanakunywa maji machafu. Mheshimiwa Waziri, fedha tunazo, kwanza mlitupangia shilingi milioni 80, naomba niseme hii DAWASA, ika-*dillydally* na nini matokeo yake fedha ile ikatumika. Lakini mpaka sasa tumeweza kupata karibu shilingi 105 na wananchi pamoja na Mbunge wao yuko tayari kuchangia *any extra* kama ninyi Serikali hamna, wapate maji jamani na njia ya karibuni ya kupata maji ni kutoka Ruvu Chini Bagamoyo kwa sababu wako karibu na Bagamoyo. Ndugu zangu wahurumieni hawa watu, ni maskini lakini wanalipia ndoo shilingi 500/=. Wahurumieni sana Dar es Salaam mkikosa maji siku moja tu kelele, naomba mnisaidie.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niwashukuru *TASAF* imeongezea fedha katika ile fedha ya *Quick Win* niliyopewa, naomba unisaidie, DAWASA, sisi tumesema basi turuhusuni tutoboe, mnatukatalia, fedha tunayo tangu mwaka juzi, tumeiweka, wananchi wa Mbiswe wanateseka, naomba mfike pale.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana Waziri kutokana na Wizara yako imemtafuta mtaalamu kuja kufanya *investigation* na ninaamini itatusaidia. Lakini naomba pia nishukuru mradi mwingine wa *World Bank* ambapo wao watachangia shilingi milioni 90 kwa vijiji 10, Halmashauri shilingi milioni tano na wananchi shilingi milioni tano kwa kututengenezea kama ni visima au matenki. Mimi naomba nikushukuru sana Mheshimiwa Waziri. Ninachowaomba wananchi wangu shilingi milioni tano tusaidiane ili tuupate huu mradi ambao utatukimbia, hilo nilikuwa naomba nisaidiwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini nisaidieni maji Mtaa wa Zogowale na Kata ya Kibaha. Mtaa wa Zogowale kuna maji yameonekana kwamba yanaweza ku-*supply* Zogowale nzima, wamechimba kisima kirefu halafu maji yale mazuri na ni maji hayana chumvi. Kata ya Kibaha sehemu kubwa watu wanachimba *locally* visima virefu lakini kwa mkono maji yale hayana chumvi. Naomba tusaidiane na DAWASA ili haya maji tuyatoe na tuyasambaze, hilo nilikuwa nataka niombe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ni umwagiliaji, Kata ya sasa ambayo ni Kata ya Mbawa kulikuwa na mradi wa umwagiliaji mmetoa shilingi milioni 23 mkafanya *feasibility study* ambayo bahati mbaya mmefanya wenyewe lakini sisi hatukuweza kujua. Lakini mpaka leo ule mradi unangojewa, ndio utakaowaongezea kipato wananchi, hilo naomba mnisaidie sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hivyo, kwa kuwa nimesema ile miradi miwili muhimu sana nisaidieni. Watu wa Vikawe wamesema Mheshimiwa Gama hatukupi, wala Diwani wako hatuwezi kuwapa kura kama hatukupata maji, mimi ninawaelewa wanateseka. Mheshimiwa Waziri najua ananipenda sana, anaipenda Kibaha sana atatusaidia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hivyo, nimesema naunga mkono, ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa Dr. Zainab Gama, sasa namwita Mheshimiwa Zabein Muhaji Mhita atafuatiwa na Mheshimiwa Dr. Raphael Chegeni na Mheshimiwa Hamza Mwenegoha ajiandae.

**MHE. ZABEIN M. MHITA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii ili nami nichangie hoja iliyo mbele yetu. Awali ya yote, naomba kwa niaba ya wananchi wa Wilaya ya Kondoa…

**MWENYEKITI:** Kumradhi! Mheshimiwa Salum huwezi kupita katikati ya msemaji na Kiti, unavunja Kanuni za Bunge. Endelea Mheshimiwa Mhita.

**MHE. ZABEIN M. MHITA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote, kwa niaba ya wananchi wa Wilaya ya Kondoa, napenda kumshukuru kwa dhati kabisa Mheshimiwa Rais wetu, Dr. Jakaya Mrisho Kikwete, Waziri Mkuu, Mheshimiwa Mizengo Kayanza Peter Pinda na Mheshimiwa Celina Kombani, Waziri wa TAMISEMI,

kwa kutupatia Wilaya mpya ya Chemba. Ni matumaini yetu kuwa huduma mbalimbali sasa zitaweza kuwafikia wananchi kwa karibu zaidi. Vilevile naomba nimpongeze Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na watendaji wote wa Wizara ya Maji na Umwagiliaji, kwa kazi nzuri wanayoifanya kuwapatia wananchi maji na kwa Bajeti ambayo imeandaliwa kwa usayansi kabisa. Ninaamini kwa jinsi Bajeti hii ilivyoandaliwa na utekelezaji wake nao utakuwa hivyo hivyo kwa ufanisi mkubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitakuwa mwizi wa fadhila endapo sitawashukuru wananchi wa Jimbo la Kondoa Kaskazini, kwa ushirikiano wao mkubwa ambao wamekuwa wakinipa katika kipindi chote cha miaka minne na nusu katika masuala mbalimbali. Ni dhahiri kuwa ushirikiano na upendo wao umeniwezesha kutekeleza Ilani ya Uchaguzi kwa ufanisi mkubwa. Ninawashukuru sana wananchi wa Jimbo la Kondoa Kaskazini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa naomba nichangie tatizo la maji, kwa kweli Jimbo la Kondoa Kaskazini lina uhaba mkubwa wa maji. Wananchi wa Kondoa Kaskazini wanaopata majisafi na salama ni chini ya asilimia 30. Kuna vijiji vingi katika Jimbo la Kondoa Kaskazini ambavyo havipati maji kabisa. Kwa idhini yako, naomba nivitaje vichache tu. Vijiji hivyo ni Mwembeni, Kata ya Changaa, Sakami, Kata ya Thawi, Kikilo Kati, Kata ya Kikilo, Berabera, Kata ya Kikilo, Puhi, Kata ya Bereko, Salranka, Kata ya Bereko, Chubi, Kata ya Bumbuta, Humai, Kata ya Soera na Thawi Juu, Kata ya Thawi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi ni baadhi tu ya vijiji ambavyo kwa kweli havipati maji kabisa na wananchi katika vijiji hivi huwa wanachota maji makorongoni, wanachota maji mitoni. Wanaochota maji haya, ni wanawake na wasichana na wanatembea zaidi ya masaa matano kutafuta maji ambayo sio safi na wala si salama. Namwomba Mheshimiwa Waziri, wanaposhughulikia ugawaji wa miradi ya maji, namwomba atoe kipaumbele katika maeneo yenye uhaba mkubwa wa maji kwa mfano Jimbo la Kondoa Kaskazini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa katika Programu ya *WSDP*, Halmashauri imekwishasaini Mkataba na Mtaalam Mshauri tarehe 30/9/2009, ni mategemeo yetu kuwa fedha itatolewa ili vijiji ambavyo viko kwenye mradi huo, naomba nivitaje vijiji hivyo, Kirere cha Ng’ombe, Makirinya, Madisa, Choka na Sowera vipatiwe fedha ili viweze kupata maji. Baadhi ya vijiji hivyo havina havina kabisa maji. Aidha, kwa kuwa mradi wa skimu ya umwagiliaji wa Kisese umeshafanyiwa upembuzi yakinifu na usanifu wa kina, nao pia upatiwe fedha ili uweze kukamilika hasa tukizingatia kwamba eneo hilo ni eneo ambalo lina rutuba na kwa kukamilisha mradi huo wananchi wanaweza wakanufaika sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na mradi huo, miradi ya umwagiliaji inayotekelezwa kupitia *DIDF* ya Mongoroma na Kwamadebe, nayo ipatiwe fedha ili wananchi waweze kunufaika kwa kilimo cha umwagiliaji ambacho ndicho kilimo cha

uhakika zaidi hasa tukizingatia ukame mkubwa ambao uko katika Jimbo ka Kondoa Kaskazini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilipochangia Bajeti ya Maji katika Mkutano wa Kumi na Sita, tarehe 14/7/2009, nilimwomba Mheshimiwa Waziri kuwa Mtaro wa Ntomoko ambao ulijengwa mwaka 1973 na ukakamilika mwaka 1975, ufanyiwe ukarabati mkubwa kwa kuwa kwa sasa Mtaro huo hautoi maji kabisa kama ilivyokuwa imetegemewa. Mtaro huu, maeneo ambayo yalikuwa yapate maji hayapati maji kabisa. Naomba tena kwa mara nyingine nikumbushie na nimwombe Mheshimiwa Waziri Mtaro huu utengewe fedha ili uweze kufanyiwa ukarabati mkubwa na wanachi waweze kupata maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na uhaba mkubwa ambao uko katika Jimbo la Kondoa Kaskazini, naomba nichukue nafasi hii, nimshukuru sana Mheshimiwa Waziri wa Maji na Umwagiliaji, kwa kutupatia mradi pale Mjini Kondoa ambao wananchi wananufaika na maji hayo. Zamani ilikuwa ni jambo la kawaida kuwaona watu wanaenda kuchota maji kwenye chemchem na katika mifereji lakini sasa hivi adha hiyo imekwisha, watu wanafaidika na maji ambayo yanatoka majumbani mwao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia niliwahi kumwomba Mheshimiwa Waziri kwamba katika mradi huo kuna eneo la Tura ambapo maji hayakufika. Nilimwomba kwamba Wizara iangalie uwezekano wa kutenga fedha ili kuwezesha maji kufika eneo hilo na pia nazidi kukumbusha na nikiamini kwa uungwana wa Mheshimiwa Waziri na ninavyomfahamu jirani yangu mimi, naamini hataniangusha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba nimalize kwa kuunga mkono hoja hii ambayo iko mbele yetu kwa asilimia mia moja, nikiwa na matumaini makubwa sana kuwa maombi yangu yatapewa uzito unaostahili. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. DR. RAPHAEL M. CHEGENI**: Mheshimiwa Mwenyekiti, nami napenda kuanza kwa kusema naunga mkono hotuba hii ya bajeti ya Mheshimiwa Waziri Mwandosya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukisikiliza mazungumzo humu ndani, kila mmoja anayechangia anamsema Waziri Profesa Mwandosya ni muungwana, ni msikivu, ni mchapa kazi na mfano wa kuigwa na mimi naomba niseme kwamba na mimi naungana nao kusema kwamba kwa kweli kaka yangu Mheshimiwa Mwandosya ni mfano wa kuigwa kwa sababu ni mchapa kazi, ni msikivu na mfuatiliaji wa kile anachokisema na hana ahadi ya uongo hata siku moja na napenda nikwambie *Shikamoo* Kaka Mwandosya. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tufike mahali Watanzania sasa tuanze kuelewa kwamba mtu akifanya vizuri ni bora kumwendeleza na kuzidi kumpa moyo. Kwa misingi hiyo, napenda kutumia mfano wa Profesa Mwandosya kwamba katika Wizara hii na ningependa kushauri mamlaka inayohusika safari ijayo aendelee katika Wizara hii ili hii ndoto ya kuboresha Wizara ya Maji na Umwagiliaji iweze kufikika. Tumekuwa na tabia

ya kuacha vitu nusu nusu na matokeo yake tunaanza moja. Tumekuwa na mfano Wizara ya Ujenzi, Mheshimiwa Dr. Magufuli alianza na ndoto nzuri sana pengine tusingefika hapa tulipo sasa hivi kama asingekuwa mtu ambaye naye ni msikivu, mchapakazi, hajali kusikia ambayo anadhani hayamuhusu, ndiyo maana inafika mahali tuwe na watendaji ambao wana-*vision* na apewe kila aina ya msaada ndani ya Bunge hili. Napenda kusema kwamba namshukuru sana na nampongeza Mheshimiwa Profesa Mwandosya pamoja na Msaidizi wake, Injinia Christopher Chiza pamoja na timu yao. Wamejipanga vizuri na mimi nasema kwamba kwa kweli Mheshimiwa Rais alikuja Jimboni kwangu mwaka 2007 akaahidi kupata Mradi wa Maji katika Mji Mdogo wa Lamadi. Ahadi hiyo sasa imeanza kutekelezwa. Sasa nitasema nini zaidi ya hapo? Mheshimiwa Profesa Mwandosya aliahidi ndani ya Bunge hili na baada ya kuahidi akaja yeye mwenyewe kufuatilia na ninavyosema nasema basi kama ni tiki ya CCM, basi huko inaendelea vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna miradi mingi ambayo ipo nusu nusu, ningeshauri kwamba kuna haja ya kuingalia badala ya kuanza miradi mipya tukamilishe miradi ambayo bado haijakamilika ili kusudi wananchi waanze kuona matunda badala ya kuanza miradi mipya huku ya zamani tunakuwa hatujaikamilisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hivi si muda wa kuzungumza mambo mengi ya kitaifa makubwa makubwa, unajikita kidogo Jimboni. Naomba nielekeze kwanza pale na kipindi hiki ndicho cha kubembeleza kura. Kuna mradi wa Kalemela. Mradi huu toka mwaka 2002 tulifunga pampu mpya, baada ya kufunga pampu mpya tulikuwa tunajaribu kuboresha mtandao wa maji wa mabomba ambao mpaka leo hii hatujafanikisha. Ningeomba Mheshimiwa Waziri, kwa sababu wewe ni mchapa kazi na ninaimani kipindi kijacho pengine utaendelea kuwepo palepale, naomba mradi huu wewe na watendaji wako mjaribu kuupa kipaumbele kwa sababu unahudumia vijiji vingi sana na ambao ni rahisi sana kuutekeleza. Kwa mtu anayekaa Jimbo la Busega na Wilaya ya Magu kwa ujumla, Ziwa haliko mbali, kwa hiyo chanzo cha maji si tatizo. Tatizo ni kuboresha mfumo pamoja na mtandao wenyewe wa maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, kuna mradi wa maji Mwamanyiri. Mradi huu tumetumia zaidi ya shilingi milioni 250 kujenga birika pamoja na pampu ya maji na vilevile kujenga tanki la maji kwa ajili ya kusambazia maji hayo. Lakini kwa bahati mbaya sana, mtandao wa kuyapeleka maji kwa watumiaji bado haujakamilika mpaka leo. Kwa hiyo, ninaomba Mheshimiwa Waziri katika hili hebu tupia macho, jaribu kuona ni kwa namna gani tukamilishe ili kusudi wananchi wanaohusika waweze kupata huduma za maji kama inavyotakiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ziwa Victoria linahitaji kupata matumizi sahihi kwa sababu sasa hivi kumekuwa na tatizo moja ambalo unakuta kwamba watu wanaokaa kandokando kwenye mabonde ambayo yangeweza kutumika kwa ajili ya umwagiliaji, hayatumiki ipasavyo. Kwa hiyo, nadhani sekta ya umwagiliaji ingeainisha maeneo hayo na kuanzisha kilimo mkakati ambao utakuwa ni kielelezo cha namna ya kutumia mabonde yetu. Leo hii unapotoka Magu Mjini unakwenda mpaka sehemu za Lamadi, mkono wa kushoto, ni bonde zuri sana kwa kilimo cha umwagiliaji. Lakini miaka yote

unakuta ni kiangazi, watu wanalia njaa, hawaweze kufanya umwagiliaji na mimi ningeomba kuwe na angalau na kama maeneo darasa, yatumike kwa ajili ya kuanzisha kweli kilimo cha umwagiliaji na hii itasaidia sana hata dhana nzima ya Kilimo Kwanza iweze kufika vizuri na kueleweka kwa wananchi. Mimi siamini kwamba tusipatiwe maji ya Victoria ni kwa namna gani mwananchi ataondokana na umaskini? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kingine ambacho nataka kusema ni suala la uchimbaji wa mabwawa. Tunatumia fedha nyingi sana kuchimba mabwawa makubwa ambayo mimi siamini kwamba kwa sasa hivi tunayahitaji, pengine kuna baadhi ya sehemu lakini tungejielekeza kuchimba mabwawa madogo madogo ambayo haya yatazidi kukidhi haja na mahitaji ya wakulima na wafugaji kwa urahisi zaidi na gharama zake sio kubwa sana. Kwa lugha nyingine wanayaita Malambo au *charcoal dam*. Mimi nafikiri itasaidia sana ili kusudi kunapokuwa na hizi *charcoal dam*, itasaidia sana wananchi kupata huduma ya maji kwa urahisi zaidi. Kwa hiyo, naomba sana Wizara ilichukue suala hili kwa umakini na ilifanyie kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kingine ni suala zima la Halmashauri zetu, zina tatizo la watendaji wa Idara za Maji. Mimi sijui Halmashauri zingine lakini nyingi zina matatizo hayo. Ningeomba kuwe na Mkakati mahususi wa kupata watendaji wenye sifa kweli ya kufanya shughuli za uhandisi katika Idara za Maji vinginevyo fedha nyingi zitakuwa zinakwenda kwenye Halmashauri lakini matokeo yake hatuwezi kuyaona. Kwa hiyo, naomba sana Mheshimiwa Waziri, aweke mkakati wa makusudi, ikiwezekana hata kuwe na programu ya kufundisha vijana wasomee Uhandisi wa Maji ili kusudi tuweze kusaidia kuokoa fedha nyingi ambayo Serikali sasa hivi inapoteza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naipongeza sana Mamlaka ya Majisafi na Majitaka ya Mwanza. Kwa kweli sisi tulitembelea kama Kamati ya Mahesabu ya Mashirika ya Umma, tumejionea jinsi ambavyo wameweza kubadilisha sura na matumizi ya majitaka na majisafi katika Jiji la Mwanza. Hii ni kazi nzuri sana na ningependa Mamlaka zingine waende Mwanza wakaige. Mkurugenzi Mwendeshaji wa Mamlaka hii pamoja na timu yake, ameweza kuhakikisha wananchi wa Jiji la Mwanza wanaweza kunywa maji bila kuchemsha kwa asilimia 80. Haya ni mafanikio makubwa sana. Kwa hiyo, ninashauri kwamba kama ikiwezekana na Halmashauri zingine ziige jinsi ya Mamlaka ya Majisafi na Majitaka ya Mwanza inavyofanya kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la mwisho, Mheshimiwa Waziri, naomba tutekeleze miradi haraka. Unajua pale Lamadi wanahitaji kunywa maji haraka, sasa na kura zimekaribia najua tutakunywa kabla ya kura lakini ninaimani kwamba haya yote yatatekelezwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana na naunga tena mkono hotuba hii. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. HAMZA A. MWENEGOHA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru sana. Kwanza nianze kabisa kwa kuishukuru Serikali ya Awamu ya Nne ni sikivu, ina

ukweli lakini vilevile niwashukuru sana kwanza Mheshimiwa Prof. Mwandosya na Naibu wake na niseme kweli niwapongeze Wizara nzima, ni wasikivu hata ukiwasimamisha barabarani, watasimama na kukusikiliza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa bahati mbaya, nasema kwa bahati mbaya kwa sababu kila nikisimama hapa inabidi nizungumzie bwawa la Kidunda. Hii ni bahati mbaya kwa sababu gani? Kwa sababu bwawa la Kidunda linazungumzwa maneno. Limesimamisha maendeleo Kata nzima ya Selembala. Hakuna madarasa yanayojengwa, hakuna zahanati ya Kiborumo inayojengwa, hakuna nyumba zinajengwa, tukiambiwa bwawa la Kidunda linajengwa. Sasa naomba Mheshimiwa Waziri, kwa mara ya mwisho tafadhali sana hebu toa tamko utuambie ni lini bwawa hili litajengwa na kama halijengwi sasa hivi utupe ruhusa na sisi kufanya hatua za maendeleo. Hilo ni bwawa la Kidunda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niende bwawa la chini Tutumi. Tutumi pana matatizo makubwa sana ya maji lakini pana kituo cha afya na pana *ginnery*. Pale pana matatizo makubwa sana ya maji. Nilizungumza na Naibu Waziri labda angeweza kuja kuangalia jinsi ya kutusaidia kutengenezewa bwawa tu ambalo lingeweza kutupa maji ya kunywa na maji ya kumwagilia. Pale tuna *vegetable gardening* lakini hayo matatizo ya maji, lile bwawa la Tutumi tulitumie kwa kuchota maji chini sana. Naomba hilo mlitilie maanani kwa sababu sasa hivi kituo cha afya cha Tutumi kinahudumia wagonjwa wa kipindupindu kutoka Kisaki Station na Gomero na yenyewe haina maji. Sasa angalia hayo matatizo yalivyokuwa makubwa. Hili naomba mlitilie maanani mtusaidie. Kisaki Station haina maji kabisa na ndiyo maana nikataja pale kuna wagonjwa wanakwenda Gomero kwenda Kisaki Station.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna mradi wa Benki ya Dunia. Kila Injinia anapofanya na kutangaza tenda Benki ya Dunia inasema hiyo haifai, ni miaka, pesa zipo pale, kibali cha kujenga mradi ule Kisima na Tank na kuchukua maji kutoka kwenye mto wa Gomero, Benki ya Dunia haitoi Kibali. Kuna nini, huyu Injinia afanye nini? Ni binti mmoja anajitahidi sana lakini Benki ya Dunia inakwamisha mradi huu. Sasa kama hawataki pesa yao itumike, tunaomba basi Serikali mtusaidie, muwarudishie ile milioni kumi ya mwanzo, mtusaidie ninyi kwa sababu kutoa kibali, *no objection*, kila wakati inaumiza sana wakazi wa Kisaki na Kisaki Station na Nyarutanga na Mdokonyule pamoja na Kambi ya Matambwe ya Selous wote wanangoja mradi huu ili watu wapate maji. Wao wanasema *no objection* kila wakati, sasa hatujui tatizo ni nini. Tunaomba mtusaidie hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, watu wa Ngerengere wamenituma niwazungumzie maji. Lakini kwa bahati nzuri naomba niwaambie, watu wa Tarafa nzima ya Ngerengere na wale wanajeshi wa Ngerengere wanashukuru kwamba Wizara ya Maji imewakumbuka sana, Tarafa nzima inaletewa maji katika mradi wa Chalinze. Kwa hiyo, hapa kusema ukweli ninaipongeza sana Serikali ya Awamu ya Nne. Ninawapongeza CCM, nawapongeza sana kwa usikivu wao hawa Mawaziri wawili kwamba wameliona hili tatizo na kwa sababu waliwahi kwenda huko na wamesikia, sasa watu wa Ngerengere, mtapata maji kwa uhakika. Ila ningeomba tu katika mradi ule uendelezwe ufike Serengeti ‘A’ na Serengeti ‘B’ ambapo huko kuna uduni wa maji kupita kiasi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nizungumzie viongozi wa bwawa la Wami na bwawa la Ruvu, wamewapotosha hawa Mawaziri. Mara nyingi nimeomba Waziri na Naibu wake waje na wao kwa heshima hiyo wamekuja. Lakini badala ya kuwapeleka kule ambapo Kata nzima itahama bwawa la Kidunda litakapojengwa wamewapeleka Kata nyingine ya Mkurazi hawakuwapeleka Kata ya Serembala. Sasa nauliza, kwa nini? Kwa nini unaweza kumpotosha kiongozi mkubwa huyu wa Taifa unamwepusha kwenda kuzungumza na kupata maswali kwa wananchi ambao wote Kata nzima itahama, unampeleka kwenye Kata nyingine na huyu Mheshimiwa Waziri anapokuja wala hawatupi taarifa Wabunge kwamba Waziri anakuja au Naibu Waziri anakuja unashtukia tu Waziri amepita huku kwenye Kata nyingine wewe uko huku Jimboni kwako unasema, lakini mimi nilikuwa ninamngoja huku, kwa nini hakuletwa huku?

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa nadhani ni wao lakini sasa nimevua jukumu lile siyo wao. Wanaojua tatizo hilo kubwa ni Wami, Ruvu ambao wanashughulikia ambao mabwawa ya Wami, Ruvu wao ndiyo wanajua tatizo hilo na wao ndiyo wanajua wananchi wa Kata nzima ya Serembala kwamba watahama, kwa nini wamewapotosha Mawaziri? Naomba Mawaziri wawahoji watu hawa, kwa nini? Kuna nini? Wanaogopa kuulizwa maswali? Walituongopea kule mambo fulani wanaogopa watasemwa kwa nini imekuwa hivi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, mawaziri wawili wote wameongopewa, wamepitishwa Ngerengere wakaenda Mkurazi, wakaenda Kidunda wakarudi. Bwawa la Kidunda litakapojengwa waathirika siyo watu wa Mkurazi wala wa Kidunda, waathirika ni watu wa Kata ya Serembala. Kata nzima iliyokuwa nyuma bwawa linatakiwa lihame, sasa hawa ndiyo wenye maswali na hawa wanatakiwa kupata majibu hawakupata, hawakuuliza maswali kwasababu hawakupata nafasi ya kuwapata mawaziri. Sasa ninataka jibu, kwa nini viongozi wa bwawa la Ruvu Wami hawakuwaleta kwetu? Kwa nini hawakuwaleta na Mbunge yupo anaishi kwenye Kata hiyo? Atahama!

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini siyo suala la Mbunge ni la maendeleo. Maendeleo yamesimama. Naomba Mheshimiwa Waziri ajue taarifa hizo. Matatizo ya maji katika Jimbo la Morogoro Kusini yapo mengi sana utafikiria tuna mito mingi. Hatuna mito mingi, hatuna matatizo, lakini mito hiyo mingi haitoi maji safi na salama, matokeo yake maji yote yanayoporomoka yanatakiwa kukingwa na kuhudumia. Maji yote yanakuja Dar es Salaam katika mto Ruvu, mito yote hiyo inaingia Ruvu.

Tunataka mtusaidie kwa makusudi kabisa kupata maji safi na salama. Mabawawa yanaweza kujengwa kwenye milima, Kibogwa inahitaji maji safi na salama, Kibungo Juu inahitaji maji safi na salama, Twa inahitaji maji safi na salama, Lundi wanahitaji maji safi na salama. Bahati nzuri tu Matombo na Mtombozi wanayo maji safi na salama, hapa hakuna matatizo, tumekinga maji Matombo, tumekinga maji Mtombozi tunawapatia maji safi na salama, wale wanayo, tunashukuru sana na muda mrefu tunayo. Lakini hizi chache nilizozitaja hazina, kama Kasanga, Kaguna, Singisa na huko kunawezekana kabisa kupatikana maji. Ni kuyakinga, lakini uwezo ni fedha. Hatuna fedha za kutosha. Mtusaidie, Wizara hii inaweza kutusaidia kwa makusudi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MHE.ATHUMANI S. JANGUO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipatia nafasi na mimi nichangie katika hoja hii muhimu sana kwetu na kwa maisha ya binadamu. Namshukuru Mwenyezi Mungu kufikia hatua hii na kuweza kuingia kwenye orodha. Nianze tu kwa kusema kwamba Mwenyezi Mungu kawapa binadamu macho, lakini wengine hawaoni; kawapa masikio, lakini hawasikii na wale wote ambao wanasema Chama cha Mapinduzi hakikufanya kitu wala hakikuweza kutekeleza Ilani zake za Uchaguzi, nadhani wako katika makundi hayo. Leo asubuhi upande wa wenzetu, bahati mbaya msemaji mkuu wa upande wa upinzani hayupo, lakini ninamwona, wachache wapo watampelekea habari.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Msemaji Mkuu wa Kambi ya Upinzani amesema kwamba mwaka 1992 waliopata maji walikuwa asilimia 46, ilipofika mwaka 2001 wakapata asilimia 55. Hapo ni nyongeza ya 9%, lakini hawakuiona. Lakini kutoka mwaka 2001 mpaka 2007 kulipokuwa na kushuka kwa 3%, wanasema hatukufanya kitu. Lakini hawatuambii hivi idadi ya watu waliokuwepo mwaka 2001 ndiyo ile ile mpaka mwaka 2007? Mtu hahitaji kwenda shule, aseme haya. Kwa ufupi ninasema tu, yeyote ambaye anaona kwamba hatukutekeleza aje Kisarawe aone yaliyofanywa katika miundombinu, katika afya, kwenye elimu na hata kwenye masuala ya uchumi. Tulikuwa hatuna hata viwanda, sasa hivi tuna kiwanda kimoja ambacho kitatoa *cement* tani 365,000 kwa mwaka, tuna mashamba makubwa ya kibiashara ambayo zamani hayakuwepo na mengine na mengine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maji ni tataizo katika sehemu nyingi, lakini ninataka nimsifu sana ndugu yangu Professor Mwandosya na timu yake, wamejitahidi sana. Tumechimba visima vingi sana katika Wilaya, ila havikutusaidia kwa sababu ya ukame ulioendelea kwa muda mrefu na vingi vimekauka. Tukahamia kwenye malambo, Serikali ikasaidia tukachimba malambo manne chini ya fedha za Serikali na malambo manne tena kwa msaada ambao umepatikana kutoka kwa wahisani. Lakini kwasababu ukame umeendelea, haikusaidia kitu. Nasema na ninamsifu sana Mheshimiwa Mwandosya baada ya kumwambia matatizo yaliyokuwa pale Kisarawe mji mdogo, alikuja mwenyewe na timu yake akayaona. Hakuishia hapo, akaenda mpaka vijijini. Amefika kule Visiga na kijiji cha Ngongele. Namshuru sana Mheshimiwa Waziri, msafara wake ulifuatiwa na kutolewa fedha na nimhakikishie kwamba wananchi wa Ngongele na Visiga wamenituma nikwambie kuwa sasa wanapata maji safi na salama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri hukuishia hapo. Tuna matatizo ya maji kule Kata ya Tondoroni, lakini Serikali imetoa fedha na vilevile kwa msaada wa Serikali tumepata msaada wa kutoka kwa Wajapani katika *Japanese, Tanzania Counterpart Fund* ambao sasa hivi karibuni utawezesha yapatikane maji. Ni mradi mkubwa, lakini sasa hivi kwa jitihada za Wizara yako pamoja na Halmashauri, naamini kabisa kwamba Makandarasi ambao wako kwenye *site* wanamalizia sasa kutandika mambomba na matanki na umeme unafika mpaka kwenye chanzo cha maji. Ninaamini kuwa jitihada za sasa zinalenga maji yapatikane kabla ya Desemba. Kisarawe mjini maji

yatakuwa yamefika na matatizo ya pale yatakuwa historia. Niseme tu kwamba Kisarawe ni kubwa na bado ina mahitaji mengi. Sehemu nyingi sana bado hazijapata maji. Namshauri Mheshimiwa Waziri na timu yake, ule utaratibu wa Malambo uendelee, kwasababu angalau sasa mvua zinapatikana, kule kukauka malambo kutakuwa hakupo na sehemu nyingi zitapata maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nifanye maombi makubwa matatu. La kwanza, Mheshmiwa Waziri utakumbuka kwamba katika bajeti ya mwaka uliopita, nilikukumbusha suala la mradi wa maji wa Ruvu – Mzenga ambao ulibuniwa katika miaka ya 1980 na maji yaliwahi kutoka. Lakini mradi ule hivi sasa haufanyi kazi. Mawaziri wote waliotangulia waliahidi na sasa Waziri mwenyewe alisema alikuwa hauelewi, lakini atauliza kutoka kwa wenzake na akishauelewa atajitahidi kuujenga. Sina uhakika hizi Sh. 2,760,000,000/= zilizopangwa kwa ajili ya Mkoa wa Pwani kwa maji ya Vijijini kama mradi huu umo ndani yake. Kama haumo, basi ninashauri kwenye bajeti nyingine tafadhali sana Mheshimiwa Waziri hebu aangalie vizuri mradi wa Mzenga ili hii miradi inayokufa iendelee kuwepo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili, kuna mradi wa ujenzi wa mabwawa ya Gumba na Titu. Mabwawa haya vilevile nimeyasemea tena ilikuwa katika miaka ya 1970 siyo 1980, lakini yamesahauliwa. Nimweleze tu Mheshimiwa Waziri kwamba akiyajenga haya Mabwawa ya Gumba na Titu atakuwa amekomboa vijiji vingi sana. Kwa mfano, Gumba ilikuwa ipeleke maji Gumba kwenyewe, Masaki, Kisanga, Kazimzumbwi mpaka Kisarawe na pale Titu kuna Vijiji vya Kihale, Kisangile, Chole, Panga la Muingereza, Vikumbulu na kadhalika bado wanategemea sana akiweza kuikamilisha miradi hii hawa wao wote watapata maji.

La tatu Ndugu yangu hapa sasa hivi Mheshimiwa Mwenegoha amezungumzia habari ya bwawa la Kidunda. Bwawa lile linajengwa mpakani mwa Kisarawe na Morogoro Vijijini Kusini. Nilikwishasema siku zilizopita kwamba maji haya yakipatikana tusilenge kupeleka Dar es Salaam tu, watu wa maeneo yale ni lazima wafaidike.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pale ni maeneo mazuri sana ya kilimo. Suala la umwagiliaji litakuwa limeboreshwa sana na mchango wa kilimo katika pato la Taifa utakuwa umeongezeka sana iwapo bwawa hili litajengwa haraka kama alivyosema mwenzangu. Nimeshukuru kuwa katika hotuba ya Waziri amegusia kwa kusema kuwa mambo yameendelea, basi yakamilike ili tuweze kuhakikisha kwamba maeneo haya yanapata maji kwa njia ya matumizi na vilevile kwa umwagiliaji.

Mwisho, tunashukuru sana kwa mpango wa mkopo wa Benki ya Dunia. Lakini, kama walivyosema wengine, tabia ya Benki ya Dunia baada ya mikataba kusainiwa kama ulivyotuambia leo, ni kusuasua katika utekelezaji. Namwomba Mheshimiwa Waziri afuatailie kwa haraka ili zile *cluster* kumi ambazo zimeahidiwa kwa Wilaya ya Kisarawe ziwe zimeweza kuanza kutekelezwa, tumeshasaini mkataba na Mhandisi mshauri, kilichobaki ni utekelezaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MHE. LUCAS L. SELELII:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru na kwa kweli Mheshimiwa Waziri wa Maji pamoja na Naibu wake ni watu ambao ni wachapa kazi. Nami nachukua nafasi hii kuwapa pongezi kubwa sana na pia hata wafanyakazi katika Wizara yao, Katibu Mkuu na Wasaidizi wake nao pia ni watu ambao wanachapa kazi vizuri sana. Dunia hii katika *Sunday School* nilipokuwa nasoma nikiwa mdogo tulifundishwa kuwa Dunia ilipokuwa inaumbwa, Mungu mwenyewe alikaa juu ya uso wa maji kwa wale waendao Kanisani, ukisoma Biblia Mwanzo Sura ya pili utaona kuwa Mungu mwenyewe alikaa juu ya maji, ndiyo akaanza kuumba watu, akaumba miti, wadudu, akaumba anga, akaumba jua na hiyo inadhihirisha kuwa maji ni kitu muhimu, kitu cha msingi sana hata katika uumbaji wetu na ndiyo maana tukasema kwamba maji ni uhai.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, sekta hii kubwa ya maji mimi ninaamini kabisa kwa kazi ambayo wamepewa ndugu zetu hawa wawili *Professor* pamoja na *Engineer* ukiondoa ule msemo wetu wa Kiswahili unaosema kuwa mzigo mzito mpe Mnyamwezi, mimi nadhani mzigo huu wanastahili hawa ndugu kwasababu ni wachapakazi. Ninaamini kuwa wanaweza kuchapa kazi vizuri sana.

Mimi nilikuwa nina maoni yafuatayo kwenye sekta kubwa hii ya maji. Tatizo la maji hapa nchini kila mahali ni kubwa sana, na mimi napenda kutambua juhudi mbalimbali ambazo Serikali inafanya, kama vile kwa kupitia *Rural Water supply and Sanitation Projects RWSSP* kuna mpango ambao ni wa *World Bank*, kuna mpango mwingine wa *ASDP*, kuna mpango mwingine wa *Quick Wins*, mipango mbalimbali ambayo Wizara inafanya pamoja na Serikali naitambua kabisa, lakini uzito wa suala hili ni mkubwa sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na uzito wa suala hili na umuhimu wa maji na jinsi ambavyo Serikali inajitahidi kujaribu kutatua tatizo hili, mimi nilikuwa ninapendekeza kwamba Serikali ifanye hatua za makusudi kuamua kama ilivyoamua kwenye mpango wa Elimu ya Msingi tukaita MMEM, kama tulivyoamua kwenye Elimu ya Sekondari tukaita *MMES* na mpango wa maendeleo ya Afya ya Msingi tukaita *MMAM*, tukienda na mpango wa namna hiyo maalum kwa ajili ya maji naamini tunaweza tukafaidika tukaondoa hili tatizo kubwa na muhimu sana kwa wananchi. Tunaweza labda hata kuita *MMA* au Maji Vijijini au vyovyote, vile lakini uwepo mpango maalum kwa ajili ya kushughulikia suala la maji. Hivyo, pesa nyingi za kutosha ziweze kuwekwa na bajeti iwe kubwa kuliko bajeti ilivyo sasa hivi ambapo tunagawana kidogo kidogo kila mtu anataka kisima, kila mtu anataka maji ya bomba na ikielekea kwenye mpango huo naamini tutafanikiwa zaidi kuliko ilivyo hali ya sasa hivi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiangalia vilevile suala la maji lilivyo pamoja na maji ya kunywa, yaani maji ya binadamu, tunahitaji vilevile maji ya mifugo. Lakini cha msingi kuliko yote tunahitaji kwa ajili ya kilimo cha umwagiliaji. Ninampongeza sana Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa dhana hii ya sasa hivi ya kuanzisha dhana ya Kilimo

Kwanza, lakini ninaamini bila ya kuwezesha Idara au Wizara hii ya maji, kwa kuwa na kilimo cha umwagiliaji kwa maana ya kuchimba mabwawa mengi ya kutosha, kuchimba malambo ya kutosha, kuchimba hata visima kwa ajili ya umwagiliaji, Kilimo Kwanza kitakuwa kimekwama. Ningependa kutoa mfano katika maeneo ya Mikoa yetu ambayo mara kwa mara inapata ukame wa mara kwa mara na mara nyingi kunakuwa na upungufu wa chakula. Upo mto mkubwa ambao unahusisha Mikoa ya Mwanza, Shinyanga na Singida ambao unapitisha maji mengi sana hasa wakati wa masika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mto huo unapopitisha maji yale huwa yanakwenda na baadaye yanapotelea kwenye Ziwa Eyasi. Lakini laiti yale maji ambayo yanapita katika mto Manonga tungeweza kuyavuna kwa maana ya kuchimba malambo na mabwawa. Maji yale tukayavuna yakatumika katika kilimo cha umwagiliaji kwa juhudi ambazo wanazo wananchi wa Mikoa ya Shinyanga na Mkoa wa Tabora hususani Wilaya ya Kahama, Wilaya ya Shinyanga Vijijini, Wilaya ya Nzega kwa juhudi walizokuwanazo za kujituma kwenye kilimo, ninaamini suala la kuagiza mchele lingefikia ukomo. Kwa maana bonde lile lote la mto Manonga linazalisha mchele wa kutosha tena mchele safi. Hivyo, tungeibua chakula cha kutosha na hasa kwa mchele na wala tusingeagiza nje tena mchele kama tunavyofanya sasa hivi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa, bonde hilo linafaa kwa umwagiliaji na kwa kuwa bonde hilo maji mengi yanapita na yanapotea bure, ningependekeza malambo katika Wilaya za Kahama, Wilaya za Shinyanga vijijini, Wilaya za Nzega, Wilaya ya Igunga na Singida yaweze kujengwa ili bonde lile lote liweze kuwa ni bonde maalum kwa suala la umwagiliaji kwa ajili ya kilimo cha mpunga, umwagiliaji kwa ajili ya kilimo cha mazao mengine ambayo yanaweza kulimwa wakati mwingine wa kiangazi. Nasema hivyo kwasababu katika bajeti ambayo tunaifanya mwaka huu, pesa ambazo zimetengwa kwa ajili ya umwagiliaji kwa mwaka huu zimepungua mwaka jana 2009/2010 ambao tunamaliza. Sasa hivi zilitengwa jumla ya shilingi bilioni 17, mwaka huu zimetengwa jumla ya shilingi bilioni 15. Kwa maana hiyo, hata pesa ya umwagiliaji kwa mwaka huu imepungua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kusema kuwa kwasababu tunazungumza kilimo kwanza na bila kutenga pesa nyingi za kutosha kwenye suala la umwagiliaji, tutakuwa tunajidanganya kwa sababu maeneo mengi yanapata mvua kwa msimu na mvua sasa hivi zimekuwa haziaminiki. Hivyo, juhudi nyingi zingefanyika na pesa nyingi zingetengwa kwa ajili ya suala hili la umwagiliaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kurejea maombi ambayo nimeyatoa kwa muda mrefu, naamini kabisa Waziri wa Maji pamoja na Wasaidizi wake wanafahamu, lakini kabla sijasema hayo maombi... *(Hapa kengele ililia kuashira muda wa mzungumzaji kwisha)*

**MWENYEKITI:** Kengele ya pili, Mheshimiwa unga mkono hoja.

**MHE. LUCAS L. SELELII:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

## MICHANGO KWA MAANDISHI

**MHE.BERNADETA K. MUSHASHU**: Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kumpongeza Waziri wa Maji, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na Watendaji kwa kuandaa hotuba hii. Nawapongeza pia kwa kazi nzuri inayofanywa na Wizara hii ya Maji.

Ni kweli usiofichika kwamba katika kipindi hiki cha miaka mitano upatikanaji wa maji umeongezeka katika vijiji na mijini kutokana na visima, mabwawa, skimu za maji na uvunaji wa maji ya mvua. Hivi sasa wananchi vijijini wanaopata maji safi na salama ni asilimia 58.7 na miji upatikanaji umefikia asilimia 84. Nawapongeza kwa ongezeko hilo ila naishauri Serikali iendelee kutenga bajeti ya kutosha kusudi watu wengi zaidi waendele kupata maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kusimamia rasilimali maji, Bunge limetunga Sheria ya Usimamizi wa Rasilimali za Maji sheria Na. 11 ya mwaka 2009 na sheria Na. 12 ya mwaka 2009, Sheria ya Huduma za Maji na Usafi wa Mazingira, sheria hizi zinavipa vyama vya watumiaji maji, Bodi za maji za mabonde na Bodi ya Ushauri ya Kitaifa, halmashauri na kadhalika, nguvu ya kisheria ya kusimamia rasilimali hizi sheria zilitungwa tangu mwaka 2009. Kanuni za utekelezaji haijawafikia watekelezaji. Je, Serikali ina mpango gani wa kuhakikisha kanuni zote husika zinatungwa na zilizotungwa zinawafikia walengwa?

Mheshimiwa Mwenyekiti, naipongeza Serikali kwa hatua iliyofikia ya upatikanaji maji vijijini kupitia mradi wa vijiji 10 kila Wilaya, nimesikia na nimeona orodha ya Halmashauri zilizofikia katika mchakato wa kupata wataalam washauri, lakini huu mchakato wa tangu hili wazo litamkwe umekuwa mrefu takribiani miaka zaidi ya mitatu. Je, ni lini sasa wakazi wa Wilaya ya Bukoba vijijini na mijini Biharamulo, Ngara, Muleba, Chato, Karagwe na Missenyi mchakato huu ukafika mwisho wakapata maji?

Mheshimiwa Mwenyekiti, nawapongeza kwa skimu mbalimbali za umwagiliaji. Kitu kitakachoikomboa Tanzania ni kilimo. Kilimo chenye tija ni kile kinacholimwa kwa zana za kisasa, mashamba makubwa, mbegu bora na umwagiliaji. Bila umwagiliaji kama ulichukua mkopo wa kilimo ni tatizo kubwa. Ili tulime kilimo bora kilimo chenye tija inabidi tupange na kuongeza bajeti ya Wizara hii ili eneo la umwagiliaji liongezwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sehemu nyingi hapa Tanzania zina vipindi vya mvua na vya ukavu. Lakini ukipita kwenye kaya, shule, zahanati, hukuti matanki ya kuvunia maji. Je, Serikali haioni ingeanza *program* kabambe ya kuhakikisha matanki ya kuvunia maji kwa ukubwa tofauti tofauti yanajegwa kila kaya na taasisi zote?

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

**MHE.DR. FESTUS B. LIMBU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napongeza sana juhudi zinazofanyika katika Wizara, kazi ni nzuri sana, iendelee kwa kasi zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naipongeza Wizara kwa kugawa vitendea kazi kama *Computer, photocopier, fax mashine,* pikipiki na magari kwa kila Wilaya ya Magu tumepata. Watendaji huko chini wasiwe na visingizio wasimamiwe vizuri zaidi ili wachape kazi zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mhandisi wa Maji wa Wilaya ya Magu *(DWE)* ni jeuri na utaalamu wake unaacha mashaka makubwa juu ya elimu yake na uwezo wake wa kiutendaji, sijui iwapo alikotokea kuja Magu alihamishwa kwa kawaida ama alihamishwa kama adhabu. Kwa nini wana-magu tuadhibiwe? Mtendaji huyu hafai kuwa *DWE* (Mkuu wa Idara).

Mheshimiwa Mwenyekiti, maji katika mji wa Magu ni tatizo kubwa na Rais aliahidi maji yangepatikana kabla ya mwaka 2010. Katika hotuba ya bajeti ya Waziri sikuona mahali ambako kuna eneo la matumaini ya lini hasa wakazi wa mji mdogo wa Magu watapata maji salama na ya uhakika kwa kuwa wana-magu walimsikia Mheshimiwa Rais akitoa ahadi hiyo. Wana-Magu wanaamini kuwa mimi Mbunge wao nimezembea na kushindwa kufuatilia ili pesa za kutekeleza zipatikane na mradi utekelezwe. Hivyo Mheshimiwa Waziri naomba niandikiwe barua ya maelezo ya nini hasa kinaendelea kuhusiana na upatikanaji wa maji katika mji wa Magu hadi sasa na lini maji ya uhakika na salama yatapatikana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja mia kwa mia.

**MHE. SHALLY J. RAYMOND:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru. Kipekee ninamshukuru Mungu kwa baraka zake kwetu sote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba nichukue fursa hii nimpongeze sana Mheshimiwa Prof. Mwandosya - Waziri mhusika, Mheshimiwa Eng. Chiza - Naibu Waziri, Eng. Sayi Katibu - Mkuu na timu yote ya Watendaji. Pamoja nao, ninaipongeza sana Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Kilimo, Mifugo na Maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaunga mkono hoja kwa asilimia 100%. Yangu ni machache na ninaomba ufafanuzi au majibu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa upotevu wa maji katika miundombinu ya maji ni mkubwa na limekuwa tatizo sugu, Serikali ina mkakati gani wa kulimaliza? Fedha zinazopotea kupitia uvujaji wa mabomba na wizi ni nyingi sana. Kuweza kufikia 20% ni ndoto na inasikitisha sana.

Ninatoa pongezi kwa mamlaka zote za maji safi na taka zilizopata hati safi katika hesaabu za kipindi kilichopita. Hakika, nyingi zimekuwa mfano bora ikiwemo *MUWASA, DUWASA,* Arusha na nyinginezo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mnyonge mnyongeni lakini haki yake mpeni. *MD* wa *MUWASA* ni mfano wa kuigwa japo magazeti hayaishi kutoa taarifa hasa kuhusu mamlaka hiyo. Ukweli utajitokeza na wengi wataumbuka. Asilimia ya upatikanaji wa maji safi katika Manispaa ya Moshi inatia fora na ninashukuru kwa niamba ya wanawake

wa eneo husika kwani tatizo la maji hakuna. Elimu tumepatiwa na tutalipa ankara zetu bila usumbufu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatizo lingine linalosumbua ni taasisi za Serikali nchini kote kutokulipa ankara zake kwa wakati. Kwa kuwa kila Waziri angependa mafanikio ya kazi zake, hivi inashindikana vipi katika mazungumzo ya kawaida mkajadili kumaliza tatizo hili? Wizara husika ni Mambo ya Ndani, Afya na Elimu. Ninashauri mlimalize tatizo hili ili vitabu vya mamlaka viwe safi. Ninashauri Katibu Mkuu naye awasiliane na Makatibu Wakuu wenzake.

**MHE. ZAYNAB MATITU VULU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naipongeza Serikali na Wizara kupitia Mheshimiwa Waziri, Naibu waziri, Katibu Mkuu na Watendaji wote wa Wizara hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na pongezi, napenda pia nimshukuru Mheshimiwa Waziri na Wizara yake kwa juhudi zake zote katika kuhakikisha tatizo la maji kwa Mkoa wa Pwani wanalipatia ufumbuzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la maji ni muhimu katika maendeleo ya nchi hii. Je, ni kwa vipi wananchi wanapata ankara za kila mwezi wakidaiwa walipe maji ili hali maji yenyewe hawayapati kwa uhakika. Naomba nipatiwe maelezo ya fumbuzi wa suala hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia suala la uchimbaji visima uwe makini siyo baada ya kuchimba maji hayapatikani. Tatizo ni nini? Juhudi ziongezwe kwa Mkoa wa Pwani ambao una vyanzo vingi vya maji, lakini wenyewe hupata kwa shida.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya maelezo hayo, natarajia kupata majibu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

**MHE. ABDUL J. MAROMBWA**: Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote, napenda kuunga mkono hoja iliyotolewa na Waziri wa Maji na Umwagiliaji - Mheshimiwa Prof. Mwandosya. Hotuba hii ya leo kama itatekelezwa kwa ukamilifu, tatizo la upatikanaji wa maji pamoja na chakula kwa kiasi kikubwa litapungua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwa kuishukuru Serikali kwa kuupatia mji wa Kibiti mradi mkubwa wa maji wenye zaidi ya shilingi billion 4.6. Mradi huu unaendelea vizuri na unatarajia kukamilika muda sio mrefu. Ninaiomba Serikali izidi kumhimiza mkandarasi anayetekeleza mradi huu azidi kuongeza nguvu ili uweze kukamilika kwa wakati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la pili ni kwa mradi wa maji wa vijiji kumi kila Wilaya. Katika Wilaya ya Rufiji, vijiji hivi tayari vimetambuliwa na tayari mafunzo yamefanywa katika vijiji vyote. Jambo ambalo bado sijaelewa ni kuhusu lini sasa uchimbaji wa visima utaanza. Naiomba Serikali kuwa mpango huu tangu utangazwe

hadi sasa ni muda mrefu umepita bila kukamilika.  Ni vizuri basi awamu ya kwanza ya vijiji hivi kumi ikakamilika ili vijiji vingine navyo viweze kuchaguliwa ili viingizwe kwenye programu hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ni maji katika kijiji cha Jaribu Mpakani. Kijiji hiki kina wakazi zaidi ya 4,000.  Kwa muda mrefu wakazi wa kijiji hiki wanahangaika kutafuta maji.  Halmashauri ya Wilaya ya Rufiji kwa kushirikiana na Benki ya Dunia *(World Bank)* ilikipatia kijiji hiki mradi wa maji.  Mradi huu ulikuwa ni pamoja na uchimbaji wa visima na uwekaji wa mtandao wa mabomba katika kijiji hiki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, visima vilichimbwa, maji yalipatikana na pampu ikafungwa.  Tatizo lililojitokeza ni kuwa maji yalikuwa machache kiasi ambacho hata pampu ikashindwa kufanya kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya tatizo hilo kujitokeza, Halmashauri ya Wilaya ya Rufiji ilichimba kisima kirefu ambacho kina maji mengi. Kisima hiki kina tatizo la kukosa pampu kubwa *(submissive pump).*  Kutokana na makadirio yaliyotolewa, zinahitajika zaidi ya shilingi milioni 15.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Halmashauri ya Wilaya ya Rufiji kutokana na ufinyu wa bajeti imeshindwa kutenga fedha kwa ajili ya ununuzi wa pampu kwa mwaka huu wa 2010/2011.  Taarifa hii Mheshimiwa Waziri Prof. Mwandosya analifahamu vizuri na barua ya maombi ya kupewa fedha na Wizara ipo ofisini kwake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naiomba Serikali ijitahidi na kuyakubali maombi ya Wilaya ya Rufiji kukipatia kijiji hiki pampu katika mwaka huu wa fedha, ili miundombinu iliyowekwa isiharibike.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

**MHE. CHIRSTOPHER OLE-SENDEKA:**  Mheshimiwa Mwenyekiti, Baba wa Taifa, Hayati Mwalimu Julius K. Nyerere katika wosia wake wa kutaka viongozi kutembea na kutenda kwa kadri ya maneno yao au kupunguza ufa kati ya maneno na matendo yao aliwahi kusema, naomba kunukuu: “Mawazo yanaendelea kujengeka miongoni mwa Watanzania kwamba kati ya maneno ya viongozi na matendo yao kuna ufa unaozidi kupanuka.  Uzito wa matatizo yetu na  ugumu wa kuyatafutia ufumbuzi wa haraka vinaendeleza mawazo haya na mashaka haya.” JK Oktoba,1987 Dodoma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maneno haya ya busara ya Baba wa Taifa, Mwalimu Julius Kambarage Nyerere bado ni changamoto kubwa kwa viongozi wa Afrika ikiwemo nchi yetu (Tanzania) wa ngazi mbalimbali za uongozi. Pamoja na kutambua na kuthamini mchango mkubwa wa Waziri wa Maji na Umwagiliaji - Mheshimiwa  Prof. Mark Mwandosya, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na wataalam wa Wizara hususan shilingi milioni 200 kwa ajili ya utafiti wa maji Ockesumet.  Nichukue nafasi hii kuikumbusha Serikali, ahadi zake hususan ahadi ya Rais Benjamin Mkapa, ahadi ya Mheshimiwa

Jakaya Mrisho Kikwete na ahadi ya Mheshimiwa Mizengo Pinda Waziri Mkuu kuwa mradi kabambe wa maji ya kuvutwa kutoka ruvu hadi Ockesumet unatekekezwa haraka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, inasikitisha kuwa niliwasilisha ombi la kuanza mchakato wa kupeleka maji Ockesumet ambayo ni Makao Makuu ya Wilaya ya Simanjiro na Serikali ilikubali na kutenga shilingi bilion moja ambayo siyo tu ilitumika kukamilisha upembuzi yakinifu wa mradi huo, bali pia nusu yake ilitumika kukamilisha upembuzi yakinifu kwa mradi wa maji katika Wilaya za Same na Mwanga Mkoani Kilimanjaro.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sote tunakubaliana kwamba kupanga ni kuchagua, lakini Swali ambalo serikali yetu inapaswa kujiuliza, ni vigezo gani vimetumika kutenga fedha kwa ajili ya miradi ya maji mingi tu nchini kwa Wilaya ambazo hazina hali mbaya kwa kiwango cha Simanjiro?

Mheshimiwa Mwenyekiti, Waziri Mkuu, Mheshimiwa Mizengo Pinda aliliambia Bunge hili kuwa maeneo mengi ya nchi yetu yana matatizo ya maji, lakini Simanjiro inaongoza kwa kero hii kubwa ya maji. Swali lingine kwa kuwa Mheshimiwa Rais kwa kutambua uzito wa tatizo letu alitamka akiwa Ockesumet kuwa utekelezaji wa mradi huo ungeanza kabla ya uchaguzi, ni lini hasa ahadi hii itatekelezwa? Kwa bajeti ipi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, hakuna sababu yoyote ya msingi itakayokubalika na watu wenye akili zao kuwa utekelezaji wa mradi wa Ockesumet uendelee kusubiri eti hadi siku zijazo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, inasikitisha kuwa Serikali ya Chama changu cha Mapinduzi sasa inatenda kazi kwa namna ambayo kuna dalili zote za kupendelea majimbo ya Wabunge ambao ni Mawaziri wakubwa wa Awamu hii. Ninafahamu Makao Makuu ya Wilaya nyingi ambazo zimetengewa fedha wakati wao wana hali njema ukilinganisha na Simanjiro.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali yetu inafahamu zaidi ya asilimia 80 ya wananchi wa Simanjiro na mifugo yao katika msimu wa kiangazi kilichopita walilazimika kuhama makazi yao ya kawaida ikiwemo kuhamia Mikoa ya jirani. Hadi leo vipo vijiji ikiwemo Makao Makuu ya Wilaya ambayo ikifika mwezi wa Saba hulazimika kuhama makazi yao ya kudumu kufuata maji kwa ajili ya binadamu na mifugo. Hali hii inatisha na haikubaliki kwa Serikali ambayo lengo lake la msingi ni ustawi wa watu wake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vijiji vifuatavyo vimekuwa na tabia ya kulazimika kuhama kila mwaka mwezi wa Saba:- Loondeckes, Ockesumet, Narmalulu, Losokonoi, Lozbene, Londanai, Olchoro-Onyori, Langai, Endorujo-engiyape, Lozmozjoc, Olerumo, Lengurnumwa (Lemkuna), Kiliengare, Nadonjukir, Okutu, Loosoito (Moshie), Ocborkushu, Nyzue na Loibocsoct na kadhalika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatizo la maji Mererani ni tatizo kubwa na bahati mbaya visima vingi vilivyopo kwenye ukanda huo wa Kata ya Mererani, Nawinyai na Shambarai maji yake yameonekana kutokufaa kwa matumizi ya binadamu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali yetu sasa iwatazame wananchi wa Simanjiro kwa jicho na moyo wa huruma. Pamoja na maneno ya faraja ya Waziri Mkuu na matumaini ya ahadi ya Waziari wa Maji bado ombi langu liko pale pale. Serikali itenge fedha kwa ajili ya mradi wa maji wa Ockesumet. Aidha, Serikali isaidie uchimbaji wa visima vya kina kirefu, mabwawa na kukamilisha miundombinu katika visima ambavyo maji yamepatikana. Visima vinavyohitaji miundombinu ni Loondeckes, Ockesumet, Ockirang'irung, Namalulu, Nasosicto, Lorunorijoni, Engonongoc, Loswaki, Msitu wa Tembo, Ngage, Nyorit Mbuko, Simanjiro Sekondari, Naisenyai Sekondari na kadhalika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wana-Simanjiro na mimi Mbunge wao tunasubiri hatua na vitendo vya matumaini ya Serikali yetu leo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana.

**MHE. DR. IBRAHIM S. MSABAHA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mradi wa Benki ya Dunia *(WB)* pana maelezo kuwa katika mradi wa *World Bank* na kama visima vitakavyochimbwa havitakuwa na maji ya kutosha: Je, utakuwaje? Itawezekana kuchukua maji kutoka Mto Ruvu?

Mheshimiwa Mwenyekiti, wananchi ambao wameachwa na mradi wa Wachina, watahudumiwa na mradi gani?

Mheshimiwa Mwenyekiti, maeneo ambayo utekelezaji umeibua malalamiko ni Dengwa, Soga, Bomu – Soga, Janga – Mlandizi, Kaloleni – Mlandizi, Mlandizi kati na Mtambani – Mlandizi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, maeneo ya mradi wa *World Bank* yataanza lini kuwekewa maji? Maeneo hayo ni Mihande – Mlandizi, Misufini – Mlandizi, Disunyala – Mlandizi, Ruvu kwa Dosa – Mlandizi, Kipangege – Soga na Bokomunemula – Kata ya Soga.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

**MHE. MARTHA M. MLATA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nafurahi sana kwa kupata nafasi japo nichangie kwa maandishi katika wizara hii. Mchango wangu utakuwa ni kwa njia ya maswali. Hivyo kabla ya kuanza, naomba nami nitoe pongezi kubwa na za dhati kwa kuipongeza Wizara hii kwa namna ambavyo imefanikiwa kwa kiwango kikubwa katika kutekeleza Ilani ya Chama cha Mapinduzi. Nasema hivyo, kwa sababu

maji yaliyokuwa tatizo katika maeneo mengi hapa nchini hususani Mkoa wa Singida kwa kiasi kikubwa yamepatiwa ufumbuzi na yanapatikana. Niombe tu kasi zaidi iongezwe!

Mheshimiwa Mwenyekiti, nampongeza Waziri na timu yote wa Wizara hii. Naomba Mungu awajalie ili kipindi kinachokuja wawepo tena wote katika Wizara hii. Hivyo basi, baada ya hayo, naomba pia kujua yafuatayo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna utaratibu gani juu ya mradi wa Wachina wanaofunga mabomba katika Mji wa Dar es Salaam?

Je, ni kwa nini wamevuka baadhi ya maeneo kama Kiluvya?

Ni sababu zipi zilizopelekea Kiluvya kuondolewa bomba kubwa ambalo lilikuwa linaleta maji yaliyotosheleza wakazi wa Kiluvya?

Je, Serikali inawaambia nini Klava-Kiluvya? Tafadhali naomba jibu. Sipendi nisimame kwenye vifungu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Je, Wizara imeweka mikakati gani katika kutekeleza dhana ya Kilimo Kwanza? Kwani kilimo ni maji. Ni kitengo gani kinachowaunganisha na Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika?

Mheshimiwa Mwenyekiti, Je, Wizara imejipanga vipi katika kuhimiza wananchi kuvuna maji ya mvua?

Mheshimiwa Mwenyekiti, je, kuna fungu lililowekwa katika kujenga mabwawa katika Wilaya ya Manyoni kwenye mashamba yao ya umwagiliaji, kwenye majaluba *(PIDP)*, Chikuyu na kadhalika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, je, Wizara inafahamu kuwa, kuna mito ya majira mingi katika Wilaya ya Iramba na kunatakiwa kuwe na program ya mabwawa ya umwagiliaji?

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia, kwa nini kusiwe na program ya maji ya chini ya ardhi (visima) yatumike kwa *Drip Irrigation* ya Msoga, mazao ya biashara kama zabibu na pamba na kadhalika, kama anavyofanya mwekezaji mmoja pale Isuna Mkoani Singida?

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya hayo naunga mkono hoja.

**MHE. AL-SHAYMAA JOHN KWEGYIR:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naanza kwa kuipongeza Serikali ya Chama cha Mapinduzi kwa kuitekeleza Ilani kwa kiasi kikubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nawapongeza Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na Watendaji wote kwa kazi nzuri mliyoifanya kwa kipindi chote mlichofanya kazi kwenye Wizara hii. Hongera sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jitahada kubwa mmezifanya kuwawezesha wananchi mijini na vijijini kupata maji safi, salama na ya kutosha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pongezi kwa kukamilisha miradi mikubwa ya maji hasa ule wa kutoka Ziwa Victoria kwenda Wilaya za Shinyanga Mjini, Kahama, Nzega na Igunga. Mradi wa maji wa Chalinze katika Mkoa wa Pwani pamoja na mradi kabambe wa kufufua mifumo ya maji safi na majitaka katika Jiji la Dar es Salaam.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia napenda kuwapongeza katika sekta ya umwagiliaji ikiwa ni pamoja na kuandaa mifumo ya uvunaji wa maji ya mvua na kuchimba mabwawa ili kuimarisha kilimo cha umwagiliaji, kwani bila maji hakuna kilimo bora.

Mheshimiwa Mwenyekiti, dira ya Wizara tumeisikia na dhamira ya Wizara tumeisikia ili kuleta maisha bora kwa kila Mtanzania kwa kukuza uchumi na kupunguza umaskini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kinachosikitisha ni bajeti ya Wizara hii, imekuwa ikipungua, wakati mahitaji ya maji kwa matumizi ya binadamyu na mifugo yameongezeka na pia yanahitajika kwa kilimo cha umwagiliaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho nawatakia kila la kheri katika uchaguzi ujao. Nyote wawili mshinde kwa kishindo na mrudi kwenye Wizara hii ya Maji na Umwagiliaji.

**MHE. MWANTUMU B. MAHIZA**: Mheshimiwa Mwenyekiti, awali, napenda kutoa shukurani za dhati kwa Wizara hii kipekee kwa kuwezesha mradi wa maji Vijijini katika Wilaya ya Handeni, Kata ya Segera, Kijiji cha Mandera, kitongoji cha Mkwajuni hadi Mwananyamale. Wananchi wote wa maeneo hayo, wamenituma niwashukuru na kuwapongeza kwa ukarimu wenu. Hali imebadilika sana, maji yameleta sura mpya kwa eneo hilo, utulivu na amani sasa vitawezesha wananchi kujiletea maendeleo ya haraka kiuchumi na kijamii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa Serikali imefanikiwa kwa kiasi kikubwa kujenga shule za msingi na sekondari, mafanikio haya yameibua changamoto mpya ya upatikanaji wa maji na umuhimu wa maji kwa shule zote nchini. Ninapenda kuleta ombi rasmi kwa Wizara hii kutengeneza utaratibu mahsusi ambao utawezesha maji kupatikana shuleni. Maji ni chanzo kikubwa cha utulivu shuleni hivi sasa, kutokana na kukosa maji, wanafunzi wengi hutoroka, kuchelewa au mahudhurio hafifu kwa sababu ya ukosefu wa maji. Wasichana huathirika zaidi kutokana na shule kutokuwa na maji. Ninaiomba Wizara hii iandae mkakati endelevu na kutoa elimu kwa umma hususan kwa Serikali za Kata ili wapate utaalamu wa kuvuna maji ya mvua kwa Shule na Kata, kufanya hivyo kutasaidia upatikanaji wa maji na hivyo kuondoa kero hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uhifadhi wa maji ya mvua kwa kilimo, mwamko kwa wananchi juu ya Kilimo Kwanza, umekuwa mkubwa, wengi wanapenda kulima mboga kwa kutumia umwagiliaji binafsi. Naamini kuwa kilimo ndiyo njia pekee

itakayowaondoa wananchi katika umaskini uliokithiri. Napenda kuishauri Wizara hii iandae michoro ya malambo na mabwawa au kuanzisha kitengo maalum ambacho kitatoa elimu na utaalamu wa ujenzi wa malambo na mabwawa. Aidha, gharama za ujenzi huo ni vema zikaimarishwa. Matarajio yangu ni kwamba ujenzi wa aina hiyo ungeweza kupunguza kero ya maji kwa kiasi kikubwa na kwamba wengi wangeweza kumwagilia kwa kutumia vyanzo hivyo. Kwa hakika, malambo yangeweza kuhifadhi maji ya mvua katika maeneo mengi na pia kupunguza matumizi ya maji ya bomba kutumika katika umwagiliaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatizo la maji taka limekuwa kero kubwa katika miji mikubwa. Dar es Salaam ni mfano mbaya sana kwa tatizo hili la maji taka. Katikati ya jiji la Dar es salaam (Kariakoo), mitaro imeziba, majitaka hayaendi yananuka na kuzalisha vijidudu vinavyosababisha maradhi ya mlipuko. Je, nini matumizi ya fedha tunazokatwa katika ankra za maji kwa ajili ya huduma ya majitaka? Au ni nani mwenye dhamana ya kuondoa majitaka mjini? Naiarifu Wizara kuwa hali ni mbaya sana Dar es Salaam. Naomba Wizara ifanye kila iwezalo kwa kushirikiana na Jiji la Dar es Salaam kuhakikisha majitaka yanaondolewa kwa faida ya usalama wa wananchi wote kwa ujumla kwa vile maradhi ya mlipuko yakianza Dar es Salaam huenea nchi nzima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nawasilisha.

**MHE. HEMED MOHAMED HEMED**: Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote, nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijalia siku ya leo kuamka nikiwa mzima.

heshimiwa Mwenyekiti, ni vyema nimpongeze Mheshimiwa Waziri, Naibu wake pamoja na wataalamu wake, kwa hotuba yao iliyojaa matumaini hasa ukitilia maanani ili tuishi maji ni lazima, ili tuishi tunahitaji chakula na kupatikana kwa chakula ni lazima kilimo ambacho kinahitaji maji. Kwa kuzingatia kuwa Wizara inashughulikia maisha ya wanadamu wanyama pamoja na mimea, ni kusema iko haja ya bajeti yake kuongezwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla sijaendelea kutoa mawazo yangu, napenda kuiomba Wizara iwe na utaratibu maalum wa kuchungua visima vya watu binafsi hasa Mkoa wa Dar es Salaam, ili vikidhi haja ya maji safi na salama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nchi yetu ni kubwa pamoja na nia njema ya Wizara kunusuru maisha ya watu, bado hali ya huduma ya maji safi na salama haijawafikia wananchi wetu. Huduma hii haijawafikia wananchi walio wengi huko Vijijini, maji yanayotumiwa ni ya mito ama visima ambavyo haviko salama kwa matumizi ya mwanadamu ambaye amejitawala, anahitaji maisha bora kwa kila Mtanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu majitaka, mara nyingi maradhi yanatokana na maji ambayo hutuwama na kusababisha vijidudu kukaa. Mara nyingi kwa baadhi ya maeneo ikinyesha mvua huwa ni balaa kwa maji kutwaa. Hii ni wazi kwamba miundombinu ya maji sio sahihi. Naiomba Serikali suala hili ilishughulikie kwa haraka ili tunusuru maisha ya watu wetu. Hali hii mara nyingi hutokea Jijini Dar es Salaam, mji ambao haupungui, una wakazi wasiopungua milioni nne.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nchi yetu inahitaji kuwepo mabwawa mengi ili maji yakimbilie eneo maalum, kutofanya hivyo, mvua zitaathiri hata barabara zetu. Maendeleo endelevu ya nchi ni maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Dodoma ni Makao Makuu ya nchi. Ukiangalia mji wa Dodoma utaona "*Water Table*" iko juu sana. Hii ni alama tosha kuwa Mkoa huu hautakuwa na shida ya maji. La kusikitisha, ukitoka mjini utaona Vijiji vilivyo karibu na mji hukosa maji, je, ni kitu gani kinachopelekea wananchi wa Dodoma Vijiji kukosa maji safi na salama?

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya maelezo yangu haya, sina budi kumpongeza Mheshimiwa Waziri pamoja na Naibu wake, kwa umahiri wao katika kuiongoza Wizara hii ambayo inashughulikia maisha yetu. Ahsante.

**MHE. JOB. Y. NDUGAI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, natoa hongera na pongezi kwa Mheshimiwa Prof. Mark Mwandosya, Waziri wa Maji na Umwagiliaji, kwa kazi nzuri sana. Pia Naibu Waziri *Engineer* Christopher Chiza, wananchi wa Kongwa wanashukuru kwa miradi ya *Quick win* na *RWSSP*, mchango wangu ni huu ufuatao:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, miradi inayofadhiliwa na *WB*, inagharimu fedha nyingi sana *per project*; Vijiji vingi bado havina maji kabisa kwa visima (*Boreholes* na Matanki). Tungeweza kutumia fedha zipatikanazo kupata *mileage* kubwa zaidi. Kwa nini Wizara isinunue mtambo katika gari wa kuchimbia visima *(boreholes)* angalau mmoja kila Mkoa na hasa Mikoa ya Dodoma na Singida, ubabaishaji katika makampuni binafsi yanayochimba maji ni makubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, miradi ya Awamu ya Kwanza ya *RWSSP* ilikuwa na matatizo makubwa sana ya utekelezaji unaotokana na Wakandarasi na wasimamizi wabovu. Tunaomba sana *Phase II*, iwe tofauti kabisa, iende kwa wakati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunashukuru sana kwa kupatikana Mkandarasi mradi wa Kibaigwa. Tunaomba DUWASA wanaosimamia, wawe karibu na Halmashauri ya Kongwa ili tujue *progress* yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mradi wa *Quick Win*, ni muhimu sana kutatua matatizo madogo madogo ya huduma ya maji Vijijini. Mradi huo uendelezwe! Je, bado upo? Kama haupo nini mbadala wake?

Mheshimiwa Mwenyekiti, mafunzo yatolewe kwa vijana wanaokabidhiwa kuendesha miradi ya maji hasa *Technical Aspects*, namna ya kuendesha na kukarabati mashine, pampu, mabomba, matanki, *tapes* na kadhalika. Pia mafunzo ya namna ya kukusanya fedha, kuweka Benki na kutumia fedha za maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kule Dar es Salaam kuna Vyama vya Watumia Maji kama kile cha eneo la Salasala; bili wanazotozwa wateja ni *excessively higher* kuliko bili za umeme au *utilities* nyingine. Kama bili ya kawaida ya maji kwa nyumba moja ni

shilingi laki moja, kwa nini jambo hili linaendelea? *Unchecked* wakati hela wanayopewa Mamlaka ya Maji DAWASA, ni kidogo sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu umwagiliaji, tunaomba wataalamu wafike Kongwa kupembua na kusanifu ujenzi wa Bwawa kubwa la Maji. Eneo la milima ya "Ibwaga Kongwa", tukiweza ku-*capture* maji pale, yatakuwa mengi sana na yatafaa kwa matumizi ya binadamu, mifugo na umwagiliaji na uchumi wa watu wa Kongwa, utakuwa kwa kiwango kikubwa sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia kuna maeneo mawili yanayofaa kwa mabwawa makubwa ya umwagiliaji nayo ni Kijiji cha Mlanga na Kijiji Matongoro. Tunaomba wataalamu wapelekwe kufanya usanifu na upembuzi yakinifu wa miradi hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wataalamu katika Idara ya Maji, Halmashauri ya Kongwa, ni wachache sana. Pia Maafisa Umwagiliaji, *almost* hakuna. Wizara iongeze wanafunzi Vyuo vya Maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naishauri mwakani, sekta ya maji na umwagiliaji, ipewe fedha kwa kipaumbele cha kwanza katika bajeti. Ni wazi kabisa ni tatizo namba moja Vijijini na mijini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

**MHE. BASIL P. MRAMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono kwa kuipongeza Wizara, kwa kazi nzuri inayofanya kupunguza tatizo la maji nchini ikiwemo Wilaya ya Rombo. Naomba Wizara ishughulikie matatizo yafuatayo:-

(a) Upotevu wa maji kwenye bomba la zamani kwa asilimia 50%.

(b) Hatma ya *Kiliwater Company*, ina tatizo la *management* ngazi za Vijiji ambapo kuna malalamiko mengi ya usimamizi. Ili maji yapatikane kwa haki, kwa kuwa mkataba wa Meneja Mkuu wa *Kiliwater Company*, unakaribia kumalizika, tunaomba tupatiwe mtu mwenye uwezo mkubwa kitaalamu na kiuongozi. Lipo suala kama *Kiliwater Company* iwe mamlaka au vipi.

(b) Upungufu wa maji bado unaendelea hasa maeneo ya tambarare (Mashariki) na Tarafa za Mengwe na Tarakea. Uharakishaji wa mpango wa visima virefu na uvunaji wa maji ya mvua, utasaidia sana kupunguza tatizo hili. Naishukuru Wizara kwa kazi zinazoendelea katika maeneo haya.

(c) Suala la Ziwa Challa kuvunwa, limechukua muda mrefu mno. Binafsi nimetoa ushahidi kwa Waziri jinsi Kenya inavyoendelea na mpango wao wa kuvuna maji hayo ifikapo Oktoba 2010. Kenya ina haki ya 30% ya maji hayo ya pamoja. Naomba Serikali ichukue hatua si tu ya kudhibiti Kenya bali pia ya kuvuna maji hayo ambayo yako kwenye Ilani ya CCM 2010.

(d) Naona umuhimu wa kuona mbele kama Rombo itapata wapi maji miaka 10 ijayo. Vyanzo vyote vitakuwa vimekwishatumika, idadi ya watu itakuwa kubwa zaidi, ukame utaongezeka na Mlima Kilimanjaro kuwa na barafu finyu zaidi au hata kuyeyuka. Bonde la Pangani lingeanza kufikiria vyanzo vingine mfano toka mito ya bonde hilo au hata nchi ya Kenya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, natoa tena pongeza na kuunga mkono hoja hii.

**MHE. KHADIJA SALUM ALLY AL-QASSMY**: Mheshimiwa Mwenyekiti, namshukuru Mwenyezi Mungu, kwa kunijalia kuwa mzima na afya njema na kuweza kuchangia kwa kuandika hoja hii ilioko mbele yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wewe binafsi, Spika, Naibu Spika na Wenyeviti wote, mnajitahidi kuhakikisha kuwa Bunge hili linaendeshwa kwa viwango vya Kimataifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nampongeza Waziri, Naibu wake na watendaji wake wote, kwa jitihada zao za kuhakikisha yanapatikana maji safi na salama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile nampongeza sana Msemaji wa Kambi ya Upinzani, kwa hotuba yake nzuri, Mwenyezi Mungu amjalie aendelee kutuwakilisha zaidi, Amen.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na Serikali kupanga mikakati ya kupatikana majisafi na salama lakini bado hali si nzuri kutokana na sehemu nyingi kukosa huduma hiyo. Ukiangalia Jiji la Dar es Salaam bado taabu sana kupata majisafi na salama na hata sehemu yanapopatikana bado maji hayo mengi yana matope. Kwa hiyo, tunaiomba Serikali ijitahidi sana kwani bado hali sio nzuri hata kidogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sehemu nyingi wananchi wanatumia maji ya mito ambayo kwa kweli hali inatisha kwani maji hayo wanakunywa wao na mbwa na wanyama wengine. Hata hapa Dodoma unawakuta wananchi wanachota maji kwenye sehemu ambazo maji yanatuwama na si salama. Kwa hiyo, Serikali itekeleze ahadi zake zisiwe maneno kwenye makaratasi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu miundombinu ya majitaka, kwa kweli, mfumo wake si mzuri katika Jiji la Dar es Salaam hasa ukizingatia mfumo huo. Tangu Jiji lina watu kidogo mpaka sasa lina watu zaidi ya milioni nne, bado mfumo ni ule ule. Mji unafurika na gari hazipiti kwa usalama. Sehemu nyingine nyingi zinalalamikiwa na wananchi kutokana na majitaka hasa ukizingatia maji hatarishi kwa afya za binadamu kutokana na Serikali kutokuwa bajeti ndogo kwa Wizara hii itasababisha madhara na kutumia pesa nyingi kutibu wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashuruku sana.

**MHE. ALI KHAMIS SEIF**: Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiangalia hotuba ya Waziri, ukurasa 83, ameelezea juu ya mradi wa maji kutoka Ziwa Victoria hadi Kahama

– Shinyanga. Ieleweke kuwa katika ziwa hilo kuna uchafuzi mkubwa wa mazingira. Kama hatua madhubuti hazitachukuliwa juu ya uchafuzi huu wa mazingira, Ziwa hilo linaweza kuchafuka na maji hayo yakawa hayafai kwa matumizi ya binadamu na viumbe hai ikiwemo samaki kutoweka. Je, Wizara ina utaratibu gani katika suala zima la mazingira ya Ziwa hilo kwa vile suala la mazingira ni mtambuka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili nchi yetu iondoke kwenye kuleta maendeleo au mapinduzi yakinifu, ni lazima kilimo chetu kitegemee kilimo cha umwagiliaji. Kwa maelezo ya Waziri, ukurasa 36, nchi yetu ina jumla ya hekta milioni 29.4 zinazoweza kuendelezwa kwa kilimo cha umwagiliaji. Nchi yetu imekuwa na hekta 264,388 na mpaka June, 2010, hekta hizo za umwagiliaji zimeongezeka kufikia hekta 331,490. Kwa kasi ya ongezeko kama hilo kwa hekta 67,102 kwa mwaka, ni dhahiri Mapinduzi ya Kijani kwenye Kilimo Kwanza, kwa kutegemea kilimo cha umwagiliaji ni ndoto. Je, Serikali ina mpango gani kabambe katika suala la umwagiliaji?

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kadhia ya uvujaji wa kemikali katika Mgodi ya North Mara, ilibainika kuwa Mamlaka ya Bonde la Ziwa Victoria ilikuwa haielewi lolote juu ya tatizo hilo. Ni mpaka pale watendaji kutoka Makao Makuu ya Wizara inayohusika na Mazingira, Afya, Maji na Mifugo kutoka Dar es Salaam ndiyo Mamlaka ya Bonde la Ziwa Victoria nalo likashtuka. Huu si utendaji bora. Ipo haja Mamlaka ya Bonde la Ziwa la Victoria iwe mahiri kuzuia uchafuzi wa maji ya Ziwa Victoria kwa sababu unaweza ukasababisha maafa makubwa kwa wanaotumia maji hayo, ahsante.

**MHE. MOHAMED H. MISSANGA**: Mheshimiwa Mwenyekiti, nampongeza Mheshimiwa Waziri Mwandosya na Naibu wake, Mheshimiwa Chiza pamoja na Katibu Mkuu wa Wizara, kwa kazi nzuri wanayoifanya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Singida ni miongoni mwa Wilaya zinazohusika na mradi wa Benki ya Dunia kwa kutenga au kuteua Vijiji 10 kila mwaka. Mradi huu ni wa miaka mingi na baadhi ya Vijiji 10 vya kwanza kabisa havijaonja hayo maji na wananchi wa Vijiji husika wanalalamika sana kwani wamechangia kwenye mradi lakini zaidi ya miaka mitano hawajapata maji. Huu ni mradi dhaifu ingawa jina lake ni kubwa kwani unaenda polepole sana. Je, Vijiji vyote vya Singida Vijijini vitaenea lini maji safi na salama? Nashauri na kusisitiza kuwa bora kuwe na mradi mwingine wa kutupatia maji kwa vile mradi huu haukidhi haja. Wilaya nyingine mradi huu wanaufadhili sana kuliko sisi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la uvunaji maji, ni muhimu sana lakini halijapewa umuhimu unaostahili na Serikali yenyewe. Nashauri Serikali iwe *serious* juu ya suala hili kwa kuhakikisha kuwa shule zote zinakuwa na mfumo wa uvunaji maji. Aidha, nyumba mpya zote hasa mjini ziwe na mfumo wa uvunaji maji.

Mradi wa Man’gony, ni wa muda mrefu na nashukuru Serikali kwa kufufua skimu hii. Hata hivyo, fedha zinazotengwa kwa ajili ya skimu hii ni ndogo sana na ikiendelea hivi, skimu hii itachukua miaka 50. Naomba skimu hii itengewe fedha zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa *water table* ipo chini katika maeneo mengi, nashauri visima vitakavyochimbwa viwe ni virefu. Tuachane na visima vifupi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

**MHE. CHARLES M. KAJEGE**: Mheshimiwa Mwenyekiti, nafurahi kuchukuwa fursa hii, kumpongeza Waziri Mwandosya na Naibu Waziri Chiza, pamoja na watendaji wake wa Wizara ya Maji, kwa kazi yao nzuri wanayoifanya. Pongezi hizi za kipekee zinatokana na jinsi ambavyo wameweza kutekeleza baadhi ya miradi ya maji Jimboni Mwibara. Baadhi ya maeneo tatizo la maji limekuwa ni historia, limekwisha kabisa. Hongereni sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na pongezi hizi, nashauri Serikali iangalie jinsi ya kutekeleza miradi ya maji ya Vijiji 10 kila Wilaya ili maeneo husika yafaidike na huduma hii muhimu. Tatizo kubwa linaloikabilli miradi hii ni pamoja na wananchi wa maeneo husika kutakiwa kuchangia miradi hii. Je, ni mchango gani wa Serikali yetu kwa wananchi maskini kama wa Jimbo la Mwibara ambalo ndilo maskini zaidi ya yote Tanzania? Serikali itafute pesa ili miradi hii ifikie mwisho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana na mbarikiwe sana.

**MHE. EPHRAIM N. MADEJE**: Mheshimiwa Mwenyekiti, nyongeza kwa mchango wangu wa kuzungumza. DUWASA iongeze juhudi na kasi ya kutafuta vyanzo mbadala vya maji ya mji wa Dodoma kutokana na kuongezeka kwa kasi kubwa kwa idadi ya watu. Bwawa la Farkwa, liangaliwe upya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kijiji cha Ngh'onghonha, kipatiwe maji kwani ni jambo la aibu wananchi wake kuendelea kuhangaikia maji wakati majirani zao UDOM hawana shida hiyo. Kijiji kipo Bondeni na mtandao wa DUWASA uliopo UDOM unaweza kutumika kuwateremshia maji.

**MHE. DR. GUIDO G. SIGONDA**: Mheshimiwa Mwenyekiti, tunashukuru kwa jitihada za Wizara za kusambaza huduma ya maji Jimboni Songwe. Hata hivyo, kuna tatizo la msingi lifuatalo. Mwaka jana 2009, visima sita vilichimbwa kwenye Kata ya Mkwajuni (4) na Kapalala (2). Hivi sasa visima hivyo, pampu zake zote hazifanyi kazi, ni mbovu na hakuna hatua zozote zilizochukuliwa dhidi ya Mkandarasi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Programu ya Uendelezaji wa Mto Songwe, Mto Songwe upande wa mwisho, maji yanaingia na kumwaga kwenye Ziwa Rukwa. Sehemu hiyo ya mwisho ya Mto husababisha mafuriko kila mwaka kiasi cha kuharibu mazao. Je, utekelezaji wa program hiyo haiwezi ikahusisha pia mwisho wa mto huo?

Mheshimiwa Mwenyekiti, Bonde la Ziwa Rukwa, moja ya hadithi rejea ya Bonde la Ziwa Rukwa, ni kuhifadhi na kuendeleza ziwa hilo. Je, Serikali ina mpango wowote juu ya kuhifadhi Ziwa hilo hasa kutokana na kupungua kwa kina, kupungua kwa eneo la Ziwa *(Shrinking,* kupotea au kuadimika kwa aina ya samaki kama Kambale, Genge, Linapira na Kachinga hata dagaa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sekta ya umwagiliaji, kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Songwe, tunaishukuru sana Wizara kwa kuandaa mpango madhubuti wa umwagiliaji hasa kwenye eneo la Bonde la Songwe. Ni mategemeo yetu, mpango huo utakamilika kama inavyotarajiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

**MHE. SALIM HEMED KHAMIS**: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru wewe binafsi kwa kuliendesha Bunge letu kwa kiwango kikubwa. Namshukuru Waziri wa Maji na Umwagiliaji, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na watendajji wote wa Wizara ya Maji, kwa kazi nzuri wanayofanya kuhakikisha kuwa binadamu na wanyama wanapata maji lakini pia Watanzania wote wanakunywa maji safi na salama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na juhudi hiyo, bado Wizara inakabiliwa na changamoto nyingi ikiwemo upungufu mkubwa wa maji katika Jiji la Dar es salaam na mji mingine kama Gairo na kadhalika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukosefu wa maji Dar es Salam, ni kilio cha nchi. Haifurahishi kuona watu wanatangatanga na ndoo za maji wakitafuta maji. Watu wengi wa Dar es Salaam wamelazimika kuchimba visima vyao wenyewe kupunguza tatizo hata hivyo visima hivi havina ufuatiliaji ili kujua kama maji hayo yanafaa kwa matumizi ya binadamu. Naiomba Wizara ikazane kuhakikisha kuwa Jiji la Dar es Salaam linapata maji ya kutosha ili kuondoa aibu kwa Serikali ya Awamu ya Nne na kwa ajili ya kulinda afya za binadamu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ofisi za Mabonde, kama tujuavyo, nchi yetu imebahatika kuwa na mabonde saba kijiografia. Mabonde haya yana rasilimali kubwa ya maji ambayo ikitumika vyema, inaweza kusaidia sana umwagiliaji mashamba. Tatizo kubwa la ofisi za Mabonde, ni fedha za kuendesha shughuli zao. Kwa kuwa Serikali haiwezi kuzipatia ofisi hizi pesa za kutosha, nazishauri ofisi za Mabonde kukopa fedha kutoka taasisi mbalimbali za kifedha yakiwemo mabenki, ili kujenga miundombinu ya maji na baadaye kuikodisha kwa wakulima wadogo na wa kati. Haya yakifanikiwa, yatakisaidia sana kilimo chetu kukua na kuwa na tija.

Mheshimiwa Mwenyekiti, umwagiliaji maji ni pembejeo muhimu sana katika kilimo, tatizo tunaloliona ni ufinyu wa bajeti ya umwagiliaji kwa ujumla wake. Katika bajeti hii ambayo kauli mbiu ni Kilimo Kwanza, ufanisi wake unahitaji bajeti kubwa ya umwagiliaji. Hili ni tatizo kubwa sana na labda Wizara kubwa sana na labda Wizara itueleze ina mikakati gani kukabiliana na changamoto hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatizo lingine ninaloliona, ni kama Wizara ya Maji na Umwagiliaji, Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika, zinashirikiana kupanga maeneo ya umwagiliaji. Wasiwasi wangu unakuja pale mtakapotofautiana katika vipaumbele na wasiwasi niliopata Ruvu kwenye kilimo cha mpunga wa umwagiliaji kwa wastaafu. Hapa Wizara ya Kilimo ililima lakini Wizara ya Maji na Umwagiliaji haikuonekana na hivyo mpunga ulikufa.

**MHE. SAVELINA S. MWIJAGE**: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa mchango kuhusu Wizara hii kuhusu Mkoa wangu wa Kagera, Wilaya ya Karagwe, Bukoba Vijijini, Muleba Vijijini, Biharamuro na Ngara. Wilaya hizo zote zina matatizo ya maji. Ni aibu kubwa sana Mkoa kama Kagera, Wilaya pamoja na Vijiji hivyo kukosa maji, mvua ya kila mara, mito isiyokauka, ni kwa nini Wizara pamoja na Serikali haiwafundishi kuvuna maji au kuwatengenezea visima Bukoba?

Mradi wa kutengeneza visima au matanki walifurahia, mradi huu, kwa sasa matatizo ni makubwa, vimefanya mito ikauke. Kwa sasa wananchi wanalia na wanajuta kwa nini walikubali kujengewa Kisima katika Kijiji cha Mshambya, wanajuta. Naomba Wizara iwatolee ufafanuzi. Walitaka kuandamana wajue hatma yao, matatizo yanazidi na si Kata hiyo peke yake ni sehemu nyingi tu. Sasa tunaenda kwenye kilimo cha umwagiliaji, bila kuanza mapema kufundisha uvunaji maji, kuna Vijiji ambavyo hawatafaidika na kilimo cha umwagiliaji. Wizara ina mikakati gani kuwasaidia wananchi ili wafaidike na mvua inayonyesha mara kwa mara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna tatizo kubwa linalotokana na Wizara ya Ardhi wanaogawa viwanja vyanzo vya maji. Kwa mfano, Wilaya ya Bukoba Mjini, tuna mto wa Kanoni. Mto huo una historia ndefu usiokauka, watu wamepewa viwanja, mto huo umebananishwa na majengo, wamepanda miti, matokeo yake unakauka. Mvua ikinyesha inakuwa mafuriko. Wananchi waliojenga kando kando, kupanda miti na kulima mazao wanalalamika. Huo mto ungetusaidia kilimo cha umwagiliaji sasa tunabaki kulaumiana. Je, kilimo cha umwagiliaji tutakipataje? Je, Wizara au Serikali inatusaidiaje?

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati tulitembelea Bwawa la Manchira, tumeona mabwawa yanavyotengenezwa: Je, Kagera kuna matatizo gani watu wa Vijiji nilivyovitaja kutengenezewa mabwawa kama haya? Hii itasaidia wananchi kuondokana na tatizo la maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatizo la maji Mkoa wa Dar es Salaam, wananchi wanakata mabomba mitaa mingi, usiku wanaacha maji yanamwagika hivyo wanaolipa bili za maji hawapati maji kabisa. Kwa nini DAWASA wasiwe na *operation* au rushwa imetawala ambapo sehemu nyingi wanakunywa maji machafu kwa kuwa mabomba yanaingiliana na maji machafu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uuzaji wa maji, vijana wanaokota chupa na bomba za sindano na wanajaza maji kwenye chupa za UHAI, watu wanaugua kipindupindu. Naomba suala hili lishughulikiwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna Mikoa mingine yenye matatizo ya maji, wanakunywa maji ya madimbwini kwenye mazalio ya vyura, hawana jinsi ya kupata maji. Sio Kagera peke yake, tukiwa tunasafiri au kutembea Kikamati, tumeona sehemu nyingi maji wanayotumia ni kama maziwa. Unashindwa kuelewa kama ni maji ya kunywa au kufulia. Mikoa hiyo ni Dodoma Vijijini, Singida, Kigoma, ni Mikoa mingi sana huwezi kuitaja ukaimaliza. Watanzania wana shida ya maji kando kando ya barabara

ya Dar es Salaam - Dodoma. kuna madimbwi, wananchi ndio wanatumia kama maji ya kunywa, kufulia na ng'ombe kunywa: Je, huyo ni Mtanzania? Nilikuwa natoka Dar es Salaam nakuja Dodoma, watalii walikuwa wanapiga picha, niliona aibu. Nchi yetu iliyoendelea ambayo ina mali nyingi, ina ardhi ya kutosha hatuna maji? Tatizo hatuna bajeti na hatuna bajeti mbadala, hatuandai, mapema nchi yetu kubwa sana, tupange kulingana na nchi yetu ilivyo. Maji ni muhimu, maji ni uhai, bajeti ya Wizara hii iongezwe ili kupunguze magonjwa kwa wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wanaokusanya vyuma chakavu, wanachafua maji, wanamwaga kwenye mto au visima, wanaacha hivyo hivyo, wanaacha uchafu, kutu, wengine wanachota humo humo. Naomba nipatiwe majibu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha.

**MHE. JACOB D. SHIBILITI**: Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwa kukupongeza wewe kwa uongozi wako uliotukuka katika miaka yote nimefurahishwa na uongozi wako.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya wananchi wa Jimbo na Wilaya ya Misungwi sitakuwa nimewatendea haki kama sitampongeza Waziri wa Maji Prof. Mark Mwandosya kwa kazi kubwa na nzuri isiyosahaulika kwa Wanamisungwi kwa kusimamia mradi uliotelekezwa tangu 1987 na kuufufua kwa nguvu zote mwaka 2010, ni miaka 23 bila huduma ya kuridhisha katika Mji wa Misungwi, leo hii maji tayari kilichobaki ni Uzinduzi tu. Lakini maji wameshaanza kuyatumia hongera sana Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu, Wakurugenzi wote mnaosaidia Wizara katika shughuli nzima.

Shukrani pia ziwafikie timu nzima ya MWAUWASA Jijini Mwanza chini ya Dr. Eng Rwetabula ambaye amesimamia vizuri mradi wa maji kwa kuiwakilisha Wizara. Mwisho ni Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya na timu yake ya Wahandisi, Eng. Witike na Kiyenze ambao ushiriki wao umezaa matunda yanayoonekana kwa wakazi wa Wilaya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya wananchi kwa dhati kabisa wananchi watakachofanya ni kumwomba Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri kwa Mungu awajalie maisha marefu na baraka njema katika kila waombalo lifanikiwe, haya ndiyo maombi yao. Nimechukua muda mrefu kwa sababu kero ya hii ilikuwa kubwa sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, changamoto bado zipo, hata hivyo, Serikali inaendelea kuzitatua hatua kwa hatua. Moja ya kero au changamoto ni usambazaji wa maji hasa katika Kijiji cha Ihelele/Nyang'homango sehemu ambapo kuna chanzo cha maji ya kwenda Kahama na Shinyanga, sehemu hiyo haina maji hata katika uzinduzi wa mradi huo, Mheshimiwa Rais alilielezea suala hilo. Hadi sasa wananchi wa eneo hilio wanasubiri upatikanaji wa maji, kumbuka kuwa wananchi hao ndio walinzi wa chanzo cha maji ambacho ni muhimu sana. Niiombe sana Serikali kupitia kwa Katibu Mkuu ambaye anafahamu vizuri suala hilo sambamba na kijiji hicho, vipo baadhi ya vijiji

ambavyo katika upembuzi huo ni vyema vikahusishwa navyo ni Mahando, Mwamagili, Mwagiligili, Mwagimagi, Bulunda na Isesa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, shukrani zingine ni katika Mradi wa Maji wa Benki ya Dunia, tayari wa vijiji kumi na viwili, viko katika hatua za kuanza ni vyema wataalam wetu hao wakajitahidi ili huduma hiyo ianze katika vijiji hivyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la maji ni pamoja na umwagiliajim, nishukuru sana kwa hatua ya mradi wa umwagiliaji Mbarika kwa kuwa mradi huu umekuwa ukishughulikiwa na Wizara moja kwa moja, ningependa kufahamu ni hatua gani imekamilika na ni nini kimebaki kinachoihusu Wizara ili tuweze kushirikiana kwa karibu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, skimu zilizoanzishwa za Mabuki (Igongwa) Nyashidala eneo la Kasololo na Ndula. Miradi hii imekuwa ya wakati wa msimu wa mvua tu badala ya kuwa chanzo cha maji ya umwagiliaji. Ni vyema bajeti ikaongezwa ili yajengwe Malambo au Mabwawa kwa ajili ya kutunza maji pindi ukame unapojitokeza, maji haya yatumike katika kilimo kama nia ya mradi ilivyo kwa sasa sehemu hizo hazitofautiani na wale wasio na skimu hizo. Serikali imefanya mengi chini ya uongozi wa Waziri kwa muda wa miaka miwili ambayo Waziri amepewa Wizara hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mgawanyo wa fedha kidogo alizopewa katika bajeti hii umedhihirisha kuwa keki hiyo ndogo kila Mtanzania ameionja. Hotuba ya Waziri imepunguza kero za wananchi kwa ugawaji usio na upendeleo, Mheshimiwa Waziri na timu yake chini ya Katibu Mkuu, ugawaji wa aina hii uendelee kwa siku za usoni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nafurahi kupokea barua toka kwa Wizara ya Maji aliyoisaini Waziri Profesa Mwandosya ya tarehe 21/6/2010 ikinitaarifu kuwa Wizara imetoa fedha Tsh.230,000,000/= kwa ajili ya ukamilishaji wa mradi wa Nyakiti – Misungwi Mjini. Nimepokea kwa mikono miwili na niahidi tu kuwa mimi, Waheshimiwa, Madiwani na Mkurugenzi wa Halmashauri kuwa pesa hizo zinatumika vizuri kukamilisha pale patakapohitajika ili huduma iwafikie wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nafurahi kukuarifu kuwa naunga mkono hoja hii ili Waziri na Wizara kwa ujumla iweze kutekeleza mahitaji ya Watanzania. Kwa maana hiyo, Waziri apewe pesa zote alizoomba bila mabadiliko.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante na Bwana awe na timu nzima ya Wizara.

**MHE.NIMROD E. MKONO**: Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujua kwa nini ile miradi kumi ya maji tuliyoahidiwa Musoma vijijini haijatekelezwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mkandarasi wa ujenzi wa Wegero tarafa ya Kagata ametutapeli bwawa kubwa lililoahidiwa kuchimbwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pale shuleni Chief Wanzazi ilikoKata ya Butuguri halijachimbwa, je, Mheshimiwa Waziri anawaambiaje wananchi na wanafunzi katika shule hiyo ambayo ni ya kwanza jimboni humo?

Mheshimiwa Mwenyekiti, Shule ya Oswald Mang'ombe iliyoko Butuguri haina maji. Rais aliahidi angechimba bwawa kwa ajili ya shule hiyo ya Sayansi. Lakini mpaka sasa hakuna maji. Je, ahadi hiyo itatekelezwa lini? Butiama sasa imekuwa Wilaya hali ya maji Butiama ni mbaya sana, Mheshimiwa Waziri anasemaje kuhusu swala hili?

Mheshimiwa Mwenyekiti, Bugwema ni mradi wa umwagiliaji uliobuniwa miaka mingi sana hakuna chochote kinachoendelea hapa. Je, mradi huo umekufa? Kama ndivyo hivyo kwa nini Serikali isichukue hatua ya haraka sana ili wananchi wagawiwe ardhi hiyo walime kwa njia nyingine kama vile *Windmills* badala ya kuwatelekeza. Ningependa Mheshimiwa Waziri awahakikishie wananchi wa Bungwema kwamba hawatanyanganywa ardhi yao na kupewa wawekezaji bila kuwashirikisha wananchi wa eneo hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kupata maelezo ya kuridhisha nitaunga mkono hoja hii.

**MHE. MKIWA A. KIMWANGA**: Mheshimiwa Mwenyekiti, nami napenda kuchangia hoja iliyoko mbele yetu hasa nikizingatia kuwa maji ni uhai. Pili, napenda kumpongeza sana tena sana Waziri Mheshimiwa Mwandosya kwa umahiri wake na Naibu wake Mheshimiwa *Engineer* Chiza kwa kufanya kazi bila kuchoka wala kuchelewa pindi unapowaeleza tatizo. Tunaomba waendelee na mpango huo kwa ni ni mfano bora.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na sifa nilizozitoa naomba kusema kuwa, naiomba Wizara hii kufuatilia kwa karibu watendaji wao ili wasije wakawaangusha. Pia naiomba Wizara kuangalia sana Jiji la Mwanza kwani kuna maeneo ambayo hayana maji kabisa na kwa masikitiko makubwa ukizingatia katika Jiji la Mwanza ndiko hasa Ziwa Victoria ndiko lina eneo kubwa na hata baadhi ya maeneo ya Jiji kukosa maji kabisa. Hii inatia simanzi kwa baadhi ya wakazi wa Jiji.

Tazama mji au niseme Kata ya Sangabuye eneo la Kayenze bila shaka maji ya ziwa hayako zaidi ya mita mia nne, lakini watu hawa hawana maji ya uhakika na wengine hawajawahi kutumia maji safi na salama hata siku moja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, namshukuru Mheshimiwa Waziri kwa kutumia wataalam wa maji katika kufuatilia maji katika eneo la Nyasaka na hasa shule ya sekondari ya Kiislamu ya Nyasaka na maeneo jirani. Pamoja na tatizo kujulikana naomba kuongeza bidii kwenu ili kushirikiana na Wizara ya Nishati ili wananchi hawa waweze kupata maji safi na salama. Ni hatari kuwa na shule za bweni ambazo hazina maji pia kuzungukwa na maji lakini huna maji na ukiona maji hayo Shinyanga mpaka Kahama ni maumivu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naiomba Wizara ya Maji katika kazi ambazo zinaendelea katika Jiji la Mwanza la kutengeneza mabomba ya maji taka ambayo kwa kuchimba maeneo makubwa na wakati wanapojenga au wanapojengelea kukuza ujenzi wa mashimo kwa kwenda juu hadi kusababisha hata gari kushindwa kupita kwa vikuta kuwa juu zaidi ya barabara tukizingatia kuwa Serikali haina pesa za kutosha kurekebisha. Hili nimeliona katika maeneo ya Nyamanoro na hata Kata zingine. Pia kukata barabara za lami ni kushindwa kuzirejesha katika hali ya zamani, hii inaenda sambamba na kampuni iliyosambaza maji safi ya Maliwato ambayo imeacha bila kutengeneza barabara ambazo ilizikata na kutuharibia barabara za lami ambazo zilikuwa ni nzuri na hasa kuziacha mashimo mashimo. Naiomba Wizara isimamie vizuri makampuni ambayo yanapewa tenda kwani ni kero.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia tuliambiwa katika Mkoa wa Dodoma kuna maji mengi sana, cha ajabu katika maeneo ya kisasa (Nyumba za Magufuli) wakazi wa maeneo haya ni tabu sana upatikanaji wa maji, ikija *bill* ni kubwa sana lakini maji hayatoki. Mheshimiwa Waziri usione hivi hata Wabunge wenzio tunakuja hapa Bungeni wakati mwingine bila hata kuoga na wakati mwingine tunapikia maji ya kununua dukani, hii ni hatari.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia napenda kuuliza lile shamba la umwagiliaji la Kahangara sasa hivi linamilikiwa na nani? Je, bado kilimo cha umwagiliaji kinaendelea katika shamba hili?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante.

**MHE. MBARUK K. MWANDORO**: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwapongeza kwa dhati Waziri wa Maji na Umwagiliaji, Mheshimiwa Profesa Mark J. Mwandosya, Naibu Waziri, Katibu Mkuu pamoja na timu nzima ya Wizara ya Maji na Umwagiliaji kwa hotuba nzuri sana na kwa kazi nzuri sana ya utekelezaji wa Ilani ya CCM ya 2005 kupitia program ya maji na umwagiliaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wilaya ya Mkinga imefaidika sana na kwa niaba yao naipongeza na kuishukuru sana Wizara na Serikali ya Awamu ya Nne kwa kazi nzuri iliyofanyika kutekeleza Miradi ya Maji Wilayani humo. Hata hivyo, kero ya maji Wilayani humo bado ni kubwa. Bado Mji wa Kasera unahitaji Mradi wa Maji ambao ni muhimu sana kwa ujenzi wa Mji huo pamoja na maji safi na salama kwa wakazi wa Mji huo na vijiji vya karibu na mji huo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, miradi mingine mikubwa ya maji ni pamoja na mradi wa kuze kibago – Mhinduro, Magoti – Kichangani pamoja na mradi wa vijiji kumi chini ya ufadhili wa Benki ya Dunia wakati miradi hiyo miwili iliyotajwa awali na mingineyo iko katika hatua mbalimbali za kuidhinishwa.

Mradi wa maji kuwa vijiji kumi chini ya ufadhili wa Benki ya Dunia umeidhinishwa kwa utekelezaji, hata hivyo, kama ilivyo kwa Wilaya nyingine utekelezaji wa mradi huu unasuasua kutokana na wananchi kutakiwa kuchangia kiasi

kikubwa mno ambacho hawana uwezo nao, kuna hatari ya miradi hii kukwama endapo hapatapatikana namna ya kuwawezesha wananchi kuchangia kiasi hicho kikubwa au kuwepo namna ya kuwapunguzia mzigo huo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mtazamo wa muda mrefu matumaini pekee ya kutatua kero kubwa ya maji kwa Wilaya ya Mkinga ni kwa kuipatia Wilaya hizo mahitaji yake ya maji safi na salama kutoka Mto Zigi baada ya Bwawa la Mabazani, Pande ambapo Jiji la Tanga linapata maji yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunashukuru kwa hatua za awali za umwagiliaji Wilayani Mkinga, hivi sasa miradi ya umwagiliaji imo katika matengenezo katika bonde la Mto Umba kwa vijiji vya Mwakijembe na Mbuta. Maeneo mengine ambayo yamehamishwa kuwa na fursa nzuri ya umwagiliaji Wilayani Mkinga ni pamoja na Kata za Mhinduro na Daluni ni matumaini yangu kwamba Wizara itaendelea kutoa ushirikiano stahiki kuwezesha Wilaya ya Mkinga kujenga miundombinu ya umwagiliaji Kata za Mhinduro, Daluni na kwingineko kutakakobainika Wilayani Mkinga.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naishauri Wizara iendeleze teknolojia na elimu kuhusu uvunaji wa maji ya mvua sambamba na jitihada za kuhifadhi na kulinda vianzio vya maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti,naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja.

**MHE. LUCAS. L. SELELII**: Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja ya Waziri wa Maji na Umwagiliaji.  Pia nawapongeza kwa kazi kubwa ya kukabiliana na kutatua kero kubwa ya maji hapa nchini. Natambua juhudi za dhati za Wizara kutafuta kila aina ya mbinu katika haja ya kukabiliana na kuliondosha tatizo la upatikanaji wa uhakika wa maji safi na salama. Pamoja na juhudi hizo, naomba uwekwe mpango maalum kama ilivyokuwa MMEM/MMES/MMAM mpango maalum wa maji uitwe MMA (Mpango wa Maji).  Natambua mipango mingi mfano, *RWSSP/WB/Quick wins* na kadhalika. Natamani uwepo mipango mingine ya makusudi makubwa yenye pesa za kutosha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mafanikio ya kilimo kwa vyovyote vile ni lazima yahusishe kilimo cha umwagiliaji.  Ukame na uhaba wa mvua ya mara kwa mara unasababisha upungufu wa njaa katika maeneo kadhaa. Napendekeza nguvu ziwekwe hasa kwenye mabonde mfano, Bonde la Mto Manonga, Ruvu, Rufiji na kadhalika. Lakini pia maeneo mengi yana uwezekanano wa kujengwa malambo na mabwawa maalum kwa umwagiliaji. Nadhani kiasi kinachotengwa kwenye eneo la umwagiliaji napendelea pesa za kutosha ziongezwe ili maeneo mengi yawe ya kilimo cha umwagiliaji. Mji wa Nzega umeleta kwako mapendekezo ya maombi ya kupatiwa fedha kwa ajili ya kuongezea mtandao wa upatikanaji wa maji maeneo ya Ipuli, Nyasa, Kitongo na Ujenzi. Pamoja na umakini wa Wizara naamini ombi hili litapewa kipaumbele.

Hata hivyo, nashukuru sana kwa ujenzi wa mradi wa Bwawa la Mihama, ujenzi wa tuta na mtaro umekamilika bado miundombinu ya umwagiliaji. Shukrani hizo

zinaambatana na kukumbushia miradi niliyoomba muda mrefu ya Bwawa la Idudumo na bonde la Mirambo Itobo.

Je, katika mwaka 2010/2011, kwa ajili ya maji ya Ziwa Victoria ni shilingi ngapi zimetengewa mradi wa maji Nzega - Tabora?

**MHE.PROF. RAPHAEL MWALYOSI**: Mheshimiwa Mwenyekiti, Miradi ya umwagiliaji inayosimamiwa na kanda za umwagiliaji imeonekana kuwa na tija ndogo kutokana na urasimu na usimamizi duni. Mara nyingi miradi hiyo hutekelezwa na kanda bila kuzishirikisha Halmashauri na haiwi na uhusiano wa karibu na mipango ya Halmashauri mfano, imejitokeza kwenye miradi kama ule wa Lifua Wilayani Ludewa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, michango ya vijiji kwenye miradi ya maji yanayofadhiliwa na Mfuko wa Benki ya Duniani asilimia tano, ni mkubwa sana hasa kwa miradi inayopata maji kupata masafa marefu na maeneo ya milima milima. Viwango vya michango vya kufikia hadi sh.40 milioni haiwezekani kuwa vijiji kadha vya Wilaya maskini kama Ludewa katika mazingira hayo Serikali itasaidiaje ili maji yapatikane kwa wananchi.

Mradi wa umwagiliaji Manda (Ludewa) unangojewa kwa hamu sana na wananchi wa Manda ambao tayari wameunda Chama chao cha Ushirika na kukisajili. Eneo hilo ni kame (*semi–arid*) na hukabiliwa na njaa kila mwaka. Mradi huu utategemea sana ushirikiano wa Wizara za Maji na Umwagiliaji; Miundombinu, Kilimo na Chakula na Mikoa ya Iringa na Ruvuma. Mradi unategemea uwepo wa Daraja au Bwawa kwenye Mito Ruhuhu ambayo ni ahadi ya Mheshimiwa Rais ili kuondokana na kivuko kisichotosheleza mahitaji ya wananchi pamoja na umwagiliaji. Je, Serikali itahakikisha ujenzi wa Daraja au Bwawa (Ruhuhu) utaanza 2010/2011? Mbona kwenye bajeti hii haupo?

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mradi wa Masimavalafu (Ibumi) Wilayani utakuwa mkubwa zaidi ya hekta 3,000. Licha ya kutenga shs.50,000/= mwaka 2009/2010, fedha hiyo hadi leo hazijatumika je katika mwaka wa fedha 2010/2011, mradi huu umetengewe fedha kiasi gani na kwa ajili ya shughuli zipi?

**MHE. CHARLES N. MWERA**: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kupata nafasi kuchangia kwenye bajeti ya Wizara ya Maji na Umwagiliaji. Napenda kumpongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri na watendaji wote wa Wizara hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mji wa Tarime umekuwa na matatizo ya muda wa upungufu wa maji safi na salama licha ya kuwepo karibu na Ziwa Victoria. Serikali chini ya uongozi wa Rais wa Awamu ya Mheshimiwa Mkapa na Rais wa Awamu ya Nne, Mheshimiwa Dr. Jakaya Kikwete waliahidi kuwa nyakati tofauti kuleta maji kutoka Ziwa Victoria hapa Mji wa Tarime mpaka sasa wananchi wanasubiri mradi mkubwa wa kutoa maji Ziwa Victoria. Ni vema viongozi wanapotoa ahadi ziwe za kweli ili wananchi waendelee kuwa na imani na uongozi wao.

Mheshimiwa Spika, kumekuwa na tatizo kubwa la uchaguzi wa Mto Tigite ambao umechafuliwa na mgodi wa North Mara unaomilikiwa na kampuni ya Barrick. Wananchi wa Vijiji vya Nyakunguru, Nyarwana, Genkuru, Nyamwaga na maeneo mengi wamepata madhara makubwa kutokana na sumu ndani ya Mto Tigite, wananchi wengi wamepoteza maisha pamoja na mifugo na afya za wananchi zipo matatani, akinamama wanaendelea kupata madhara hasa ya kuharibika mimba, ng'ombe, kondoo, mbuzi magonjwa ya ngozi ni baadhi ya madhara ambayo yanawakabili wananchi kwa kutumia maji yenye sumu na ya Mto Tigite.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali ina mpango gani wa muda mfupi, muda wa kati na muda mrefu wa kuchimba visima au malambo kwa ajili ya matumizi ya binadamu na mifugo ili wananchi wasiendelee kupata madhara ambayo yanapelekea vifo? Pia ni lini Serikali itatoa matokeo ya sampuli ya maji iliyochukuliwa na kupelekwa maabara kwa uchuguzi itakamilika lini? Ni lini wananchi watalipwa fidia kutokana na madhara yaliyowapata baada ya kutumia maji yenye sumu ya mto Tigite.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa vile Serikali inatoa pesa nyingi kwa ajili ya miradi katika Halmashauri, ni vema Serikali iwapelekee (kuajiri) wataalam ambao watakuwa wanasimamia hiyo miradi. Serikali iwe inatoa fedha mapema ili miradi ikamilike kwa wakati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kupata nafasi na nimshukuru sana Waziri, Naibu Waziri, Watendaji wote kwa kazi nzuri, ni kweli "maji ni uhai".

Mungu ibariki Tanzania.

**MHE. PROF. PHILEMON M. SARUNGI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya wananchi wa Rorya napenda kutoa shukrani zangu za dhati kwa Mheshimiwa Profesa Mwandosya, Waziri; Naibu Waziri Mheshimiwa Chiza; Katibu Mkuu, Wakuu wa Idara, Watendaji wa Wizara, Mikoa na Wilaya kwa kazi nzuri, wanayofanya katika kutekeleza kwa mifano ya kuigwa Ilani ya CCM kuhusu uchaguzi mkuu wa 2005 -2010.

Napenda kutamka kuwa naunga mkono hoja. Wananchi wa Rorya hawatasahau jinsi Mheshimiwa Waziri alivyoshughulikia kero yao ya miaka 30 kuhusu ujenzi na ufunguzi wa Gati za Guta na Kinesi mwaka 2004, wanampongeza katika miradi ya ujenzi wa mabwawa, Malambo na Visima. Ahsante sana Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wananchi wa Rorya wamenituma niwafikishie maombi yao kwa Mheshimiwa Waziri wakiwa na imani kubwa watasikilizwa na matatizo yao kupatiwa ufumbuzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Vijiji vilivyoingizwa katika mradi inayofaidhiliwa na Benki ya dunia ni vifuatavyo:Utegi, Mika, Nyamkonge, Randa, Kinesi, Nyihara, Ngope, Kisumwa, Kirogo, Baraki, Makao Makuu ya Wilaya Ingiri juu na Nyarombo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wananchi wa vijiji hivyo wanauliza je uchimbaji wa visima na ujenzi wa miundombinu utaanza lini na kukamilika mwaka gani ?

Mheshimiwa Mwenyekiti, Miradi inayofadhiliwa na *JICA* ni vijiji sita kama ifuatavyo: Kisumwa - Visima 3; Nyamkonge – Visima 4; Masika – Visima 3; Bukama – Visima 4; Oliyo – Visima 4 na Tatwe – Visima 4. Je, visima vilivyotajwa bado vipo katika orodha ya *JICA*, na uchambuzi utaanza lini?

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika jedwali Na. (6) kuhusu maeneo yaliyofanyiwa upembuzi yakinifu na usanifu wa awali mwaka 2009/2010, ni pamoja na mradi wa umwagiliaji wa Bwawa la Cherecho Rorya, lenye eneo la hekta 120 inayo,imwa sasa. Hata hivyo, hekta inayofaa ni 250, hivyo upembuzi yakinifu na usanifu wa hekta 130 bado hazijafanyiwa upembuzi. Naomba upembuzi ufanywe katika kipindi cha mwaka 2010/2011.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Miradi mingine inafanya kazi lakini haikutajwa ni pamoja na Bwawa la Ochuna hekta 60; Bwawa la Baraki hekta 60 na Bwawa la Irienyi hekta 130.

Mheshimiwa Mwenyekiti, miradi mipya ni Mradi wa Rwangenyi hekta 120 na mradi wa Bonde la Nyathorogo hekta 400. Naomba miradi hii yote ifanyiwe upembuzi mwaka 2010/2011.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mradi wa Bwawa au Lambo la Kanyisambo mwaka 2008, Wizara iliwatuma wataalam wakiongozwa na ndugu Mnzava kufanya upembuzi yakinifu kuhusu eneo la kuchimba Bwawa la Kanyisambo lakini hadi sasa hakuna taarifa. Wananchi wanataka kujua, je, Bwawa la Kanyisamba mradi wake unaendelea?

Mheshimiwa Mwenyekiti, wananchi wanamshukuru Mheshimiwa Waziri kwa kuwapatia gari la mradi wa maji na kuongeza fedha mwaka 2010/2011 kwa ajili ya maji Ingri juu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kupatiwa majibu.

**MHE. PASCHAL C. DEGERA**: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kupata nafasi hii ili niweze kuchangia hotuba ya bajeti ya Wizara ya Maji na Umwagiliaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote nimpongeze Mheshimiwa Waziri kwa hotuba yake nzuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mkoa wa Dodoma hukabiliwa na ukame wa mara kwa mara na kusababisha upungufu wa chakula na umaskini kwa wananchi. Kwa niaba ya wananchi wa Mkoa wa Dodoma naishukuru sana Serikali kwa misaada yake ya chakula, hali hii inapojitokeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na misaada hiyo tatizo la msingi la mkulima wa Mkoa wa Dodoma bado halijafanyiwa kazi. Tatizo la msingi la mkulima wa Dodoma ni ukame.

Mheshimiwa Mwenyekiti, njia pekee ya kumsaidia mkulima wa Dodoma kujitosheleza kwa chakula na kuondoa umaskini ni kumsaidia Miundombinu ya Umwagiliaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niikumbushe tena Serikali kuhusu mradi wake wa *Far* kwa *Multipurpose Dam Scheme* uliobuniwa na ulioandaliwa na Serikali miaka ya 1980. Lengo la mradi huu lilikuwa ni kujenga Bwawa la Farkwa katika Mto Bubu Wilayani Kondoa kwa madhumuni ya:-

Kwanza, kuanzisha kilimo cha umwagiliaji wa hekta 10,000 eneo la xxpendo lenye uwezo wa kuzalisha mazao ya chakula jumla ya tani 24,678 kwa mwaka. Hatua hii ingeondoa njaa za mara kwa mara. Mkoani Dodoma.

Pili, kufikisha huduma ya maji Makao Makuu Dodoma hatua hii ingeondoa tatizo la maji Mjini Dodoma.

Tatu, kuzalisha umeme kwa kiwango cha MW20 kiwango hicho kingeongezwa kwenye grid ya Taifa.

Nne, kufuga samaki hatua hii ingeondoa au kupunguza umasikini wa wananchi wa Dodoma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa mradi huu ni ukombozi kwa wananchi wa Dodoma hivyo kwa niaba ya wananchi hao naomba mradi huu utekelezwe haraka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitumie nafasi hii kuiomba Wizara iharakishe utekelezaji wa miradi ya maji chini ya program ya maji na usafi wa mazingira vijijini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kuchangia haya machache nitamke kuwa, naunga mkono hoja hii.

**MHE. GAUDENCE C. KAYOMBO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza ni pongezi kwa Mheshimiwa Waziri na Mheshimia Naibu Waziri wake pamoja na Katibu Mkuu na wafanyakiazi wa Wizara kwa kazi nzuri wanazofanya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mchango wangu ni katika maendeleo ya maji katika Jimbo la Mbinga Mashariki, mambo ambayo nimeyazunguza mara kadhaa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahadi ya gari na *computer* kwa Mamlaka ya Maji Mbinga bado haijatekelezwa. Naomba itekekezwe ili muendelee kuaminika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maji katika Mji wa Mbinga. Mara kadhaa nimezunguza na Mheshimiwa Waziri na Naibu Waziri na niliahidiwa kwamba fedha zitatumwa Mbinga bado haijafanyika. Maji yanamwagika barabarani kwa kukosa tu mabomba ya kupeleka maji hayo mjini ili yakatumiwe na wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kupata shilingi milioni 273 ambazo ndizo zilisaidia kuboresha miundombinu ya maji katika mji huu. Sasa tumalizie kazi hiyo kama jambo la dharura. Nafahamu juu ya mradi mkubwa kwa ufadhili wa Benki ya Dunia lakini hii inachukua muda mrefu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vijiji vya Mbinga vina matatizo makubwa ya maji ingawa vyanzo vya maji vipo. Naiomba Wizara itume wataalam Mbinga ili wakashirikiane na halmashauri ili kupunguza kero hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba msaada zaidi kwa vijiji vya Kingoli, Litumbandyosi na Luhagara ambavyo maji ni tatizo kubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu umwagiliaji, Kata ya Litumbandyosi ina eneo kubwa sana la kulima mpunga. Halmashauri inajitahidi lakini msukumo wa Wizara unahitajika ili tupate mpunga. Jimbo langu lina mito mikubwa miwili ya Mngaka na Mnywamaji ambayo haikauki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napendekeza tujenge mabwawa mawili makubwa ili maji hayo yasiende tu Ziwa Nyasa lakini yatumike katika umwagiliaji, uzalishaji samaki lakini pia yanaweza kuhamasisha utalii. Naomba sana Wizara ilifanye kazi jambo hili. Maji ni kweli mengi lakini si lazima yawe mengi miaka yote hivyo ni lazima tuweke akiba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja hii na nawatakia kazi njema.

**MHE. TEDDY L. KASELLA-BANTU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na kuchangia kwa kusema, muda ni mdogo sana naomba nichangie haya kwa maandishi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maji ya kutoka Ziwa Victoria kwenda Kahama, naomba kukumbushia vijiji jirani upande wa Jimbo la Bukene, visiachwe kwani vitaleta kero mfano Sigili, Lyamalagwa, Igusule na kadhalika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna maji yaendayo Nzega/Igunga/Tabora, mtiririko huu haugusi jimbo la Bukene, pamoja kwamba ni Wilaya ya Nzega kwa misingi hiyo, naomba ule utaratibu wa maji toka Kahama kwenda Tabora kama tulivyoambiwa kwenye mkutano wa *RCC,* Tabora. Kwa misingi hiyo basi lile bomba likiwa linapeleka maji Tabora, litapita kwenye jimbo langu katika kata mbili kama ifuatavyo; Kata ya Semembela katika vijiji vya Itena Busalu, Mbooga, Nyangahe na Mhumbugu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kata ya Maambali, katika vijiji vya Ntumbili, Kikonoka na Maambali yenyewe. Vijiji hivi viwemo katika mradi huo ili tusiongeze kero tena.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nizungumzie kuhusu maji ya Dar es Salaam. Kama kamati tunapenda kukumbushia kwamba umalize tatizo hili la maji Dar es Salaam, ili na sisi yaani wajumbe wa kamati pamoja nanyi yaani Mheshimiwa Waziri na Mheshimiwa Naibu Waziri ni wajumbe pia. Tuweke kumbukumbu ya kamati yetu kumaliza kabisa tatizo la maji Dar es Salaam. Naamini ni watendaji mahodari, hivyo tutatimiza ahadi yetu na hivyo tukumbukwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *bill* za maji wengi wanalalamika kwamba wanapata *bill* za maji kubwa bila kupata maji, yaani maji hewa. Kuna wakati *bill* zinakuwa kubwa sababu ya kuvuja maji kwenye mabomba. Mtu anaandika barua za malamiko kuhusu hili, lakini hakuna *DAWASCO* kuja kuangalia na kusawazisha utaratibu, bali wanakuja kukata maji, kulikoni!!

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba hawa wafanyakazi wasiwe wazembe, kwani si haki kumkatia mtu maji bila kuangalia ubovu uko wapi, na kuweka *bill* halali. Mfano ni wangu mwenyewe, kwenye nyumba yangu ya Dar es Salaam – *IPTL* karibu na *Cornelius Girls Secondary School.* Nimefuatilia mwenyewe Boko na kuandika malalamiko, la kusikitisha wamekuja kukata maji na si mimi tu ni wengi tulikutana hapo Boko tukilalamika. Naomba watende haki nasi *(consumers)* wao tuko tayari kulipa iliyo haki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha na ninaunga mkono 100%.

**MHE. ELIETTA N. SWITI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mkoa wa Rukwa unahitaji maji safi na salama. Kwa mantiki hii nachukua fursa hii kuomba mradi wa uvunaji maji mkoani Rukwa kwa sababu maji mengi ya Rukwa huingia ardhini na mengine huenda mito mpaka katika maziwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, visima vya maji havitoshi mkoani Rukwa. Naomba Serikaliiongeze uchimbaji visima mkoa mzima wa Rukwa ili kupunguza maradhi ya homa ya matumbo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maendeleo ya Wanarukwa yanategemea kilimo endelevu ambacho ni umwagiliaji, kwa kuwa Rukwa ni mkoa wa kilimo, naomba kasi ya miradi ya umwagiliaji iendelee kwa mkoa mzima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba na elimu ya matumizi ya miradi hiyo iende sambamba na ujenzi wake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

**MHE. EUSTACE O. KATAGIRA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, pongezi nyingi kwa Mheshimiwa Waziri na watendaji wote kwa kuandaa hotuba nzuri ya Bajeti na pia

kuiwasilisha kwa umahiri.  Lakini zaidi nawapongeza kwa kazi nzuri mnayofanya kuendesha Wizara hii muhimu sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, umwagiliaji sasa ni muhimu, jinsi tunavyojielekeza katika *Agricultural Mechanizations*, ndivyo miundombinu ya umwagiliaji inavyozidi kuwa muhimu.  Itakuwa hasara kubwa kama tutalima mashamba makubwa kwa kutumia matrekta  halafu mashamba haya makubwa yakauke, hii itakuwa ni hasara kubwa. Naomba *agricultural mechanizations* iambatane na miundombinu ya umwagiliaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mijini watumiaji walipie maji.  Jitihada zifanywe ili watumiaji maji mijini walipe ankara zao na walipe kwa wakati na ankara ziwe sahihi. Wasilipe wachache.

**MHE. SIRAJU JUMA KABOYONGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuanza kwa kuwapongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu wake, Katibu Mkuu pamoja na watendaji wote wa Wizara kwa matayarisho mazuri ya Bajeti hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na kazi nzuri inayofanywa na Wizara hii, napenda kusisitiza haja ya Wizara kuongeza nguvu katika utekelezaji wa mradi wa maji mjini Tabora.  Mradi huu ambao unafadhiliwa kwa pamoja baina ya *SECO* ya Uswiss na Serikaliya Tanzania unasua sua sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mpaka sasa mradi ambao unahusisha ukarabati na upanuaji wa chujio katika bwawa la Igombe, ukarabati wa mtandao wa mabomba ya mjini pamoja na kuongeza wigo wa mtandao, ujenzi wa bomba kubwa la kupeleka maji toka Igombe mpaka *Kazeh Hill* pamoja na kuongeza tanki lingine la maji *Kazeh Hill*, ukarabati na upanuzi wa mtandao wa maji taka kwa pamoja unahitaji takribani shilingi milioni 24.5.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kukidhi mahitaji ya maji ya mji wa Tabora katika kipindi cha muda mfupi ni lazima Serikaliielekeze nguvu zake katika kupata maji kutoka vyanzo mbadala zaidi ya mabwawa ya Igombe na Kazima.  Hivyo naishauri Serikaliitenge fedha maalumu kwa ajili ya kuchimba visima virefu mjini Tabora.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naipongeza Serikalikwa kukubali kutenga fedha kwa ajili ya mradi wa umwagiliaji katika Kata ya Inala (Hekta 400).  Mradi huu utawawezesha wananchi wa Tabora nao kuwa na mradi wa kisasa wa umwagiliaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naishukuru Serikalipia kwa kuhakikisha kwamba mradi wa vijiji kumi chini ya ufadhili wa Benki ya Dunia unaendelea vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja hii 100%.

**MHE. BUJIKU P. SAKILA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote napenda kuchukua fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na watumishi wote katika Wizara hii kwa kazi nzuri yenye matumaini makubwa kwa Watanzania.  Kwa niaba yangu binafsi na kwa niaba ya wapiga kura wote wa jimbo la

Kwimba wote hao tunawatakia kheri na mafanikio katika kila walipangalo kwao, kwa familia zao na kwa Taifa hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Jimbo la Kwimba linayo matatizo makubwa matatu, matatizo ambayo yanalewesha sana maendeleo ya watu wa eneo hili. Matatizo hayo ni elimu duni, kwa wananchi wake wengi, ukosefu wa umeme na kubwa kuliko yote ni ukame uliokithiri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu elimu duni, wananchi wamekubali kusomesha watoto wao. Vijana nao wamekubali kusoma. Ni imani yangu baada ya muda mfupi tatizo hilo litatoweka lenyewe. Tunaishukuru sana Serikalikwa kuwekeza kwa nguvu katika sekta hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la ukosefu wa umeme, wananchi katika sehemu kubwa ya jimbo wamewekwa katika hali ya matumaini makubwa ya kufikishiwa umeme. Maelezo mbalimbali ya utekelezaji wa mradi huo yamewafikia wananchi wao sasa wamekubali kuwa na subira wakiwa na ufahamu kuwa umeme ni msingi wa maendeleo na wanasubiri kuupokea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu ukame uliokithiri, kilio kikubwa cha wananchi wa Kwimba ni ukame uliokithiri. Kuna ukame uliokithiri kwa matumizi ya watu na mifugo. Matokeo ya ukame huo ni watu kuhama kwa makundi na mifugo yao kwenda maeneo yaliyo na maji, maeneo yaliyo na mabonde yenye nyasi za malisho ya mifugo. Ni kilio cha miaka mingi. Mradi wa kupeleka maji Shinyanga na Kahama uliposanifiwa kwa mara ya kwanza, Wilaya ya Kwimba haikuwemo. Wananchi wakawa wakijiuliza imekuwaje Serikalikuuona ukame wa Shinyanga na Kahama kabla ya kuuona ukame wa Kwimba pamoja na kutambua ya kuwa iliwahi kuanzisha mradi wa Mwamashimba ambao haukuwa umefanikiwa? Kilio hicho kiifikie Serikalikupitia kwa mwakilishi wao Bungeni, na Serikali ikasikia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda nitumie fursa hii kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Kwimba kwa Serikali ya Awamu ya Tatu kulipokea ombi hilo na kuingiza Mwamashimba katika mradi huo. Aidha, tunaishukuru kwa dhati Serikali ya Awamu ya Nne kwa kukubali kutekeleza mradi huo kwa kusambaza maji katika vijiji kumi na saba kwa kuanzia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ombi langu ni kuwa usambazaji huo ufanywe haraka, mchakato ukianza wananchi watakuwa na imani. Mradi unavyozidi kuchelewa wanakumbuka yaliyowafika miaka ya 1975 mradi wa Runele – Mhalo – Mwamashimba uliotelekezwa bila watu kupewa taarifa yoyote, jambo lililopekekea wananchi kuanza kuhujumu miundombinu ambayo tayari ilikuwa imetandazwa tayari.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushauri wangu ni kuwa taarifa za mara kwa mara kwa wananchi ni vyema ziwe zikitolewa ili wawe wakiendelea kujua kinachoendelea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu vijiji kumi kwa kila wilaya, naipongeza Serikali kwa hatua zilizofikiwa. Jimbo langu lina vijiji saba, vimearifiwa mhandisi mshauri tayari yuko Ngudu, Makao Makuu ya Wilaya ya Kwimba kwa shughuli hiyo. Kinachotakiwa ni kuuharakisha mchakato huu ili hatimaye wananchi katika vijiji hivyo waweze kuondokana na tatizo hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ombi la ufafanuzi, lipo jambo ambalo sijafanikiwa kuelewa mantiki yake. Mamlaka ya maji Ngudu tumeomba msaada serikalini/wizarani ya TShs.200 mil. Kwa ajili ya kuweka upya mfumo wa maji wa mjini hapo na kutafuta vyanzo vipya. Serikali kimsingi imekubali ila itatoa fedha hiyo kwa awamu. Hivi sasa shilingi milioni kumi zimekwishatolewa. Fedha hiyo haitatumwa moja kwa moja kwa Mamlaka ya Maji Ngudu (mwombaji na mtumiaji) badala yake tayari fedha imetumwa Mamlaka ya Maji Jijini Mwanza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, halmashauri ya Kwimba kupitia mhandisi wa maji wake waliomba shilingi milioni 51. Kwa ajili ya kufufua sehemu ya mradi wa Mwamashimba kutoka Mwamashimba hadi Kijiji cha Milyungu. Tunashukuru pia Serikali imekubali kutoa fedha hiyo (japokuwa sijapata taarifa kama imetolewa na mwisho wa mwaka unakaribia kufika), kwa mujibu wa taarifa toka Wizarani fedha hiyo haitatumwa Halmashauri ya Kwimba (mwombaji na mtumiaji).

Mheshimiwa Mwenyekiti, badala yake fedha hiyo itatumwa Kashwassa (msimamizi wa utekelezaji wa mradi). Sina tatizo sana na fedha kupelekwa huko, tatizo langu ni mantiki yake. Je, watu wa Ngudu (Mamlaka) hawana uwezo au stahili ya kupokea fedha hiyo? Je, watu wa Halmashauri ya Kwimba kwa kuwa nao wako TAMISEMI, hawana stahili ya kupewa fedha hiyo moja kwa moja na kuitumia? Je, utaratibu huu unaotumika hauongezi urasimu? Naomba kufahamishwa kama je, utaratibu unaenda sawa na matakwa ya *D by D?* Naomba ufafanuzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

**MHE. MAGDALENA H. SAKAYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, pongezi kwa Waziri, Naibu Waziri na wataalam wote kwa kuandaa hotuba hii na kuileta hapa Bungeni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni jambo la busara kwamba Serikali imefuatilia uundwaji na usajili wa vyombo vya watumiaji maji. Ingekuwa vizuri Serikali ikatueleza watumiaji hawa wanashiiriki vipi kutumia vyanzo vya maji kwenye maeneo yao ili kuhakikisha maji endelevu. Kwa muda mrefu sana wenye viwanda ambao ni watumiaji wakubwa wa maji lakini ndio wanaoharibu vyanzo vya maji. Wapo wanaomwaga *chemicals,* maji machafu kwenye mito na hivyo kuchafua maji yanayotumiwa na wananchi wengine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano ni Kiwanda cha *Mtibwa Sugar Estate* wamekuwa wanafungulia maji machafu kwa kufungulia *chambers (collection chambers)*

muda wa usiku. Nimelifikisha hapa Bungeni miaka ya nyuma sasa wanaendelea tena kuumiza wananchi wanaoishi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu kukosekana kwa umakini, utaalam wa kutosha wakati wa kutekeleza miradi mikubwa ya maji maeneo mbalimbali, hili linapelekea fedha nyingi za wananchi kutumika bila tija lakini pia ni hasara kwa Taifa. Badala ya kumaliza tatizo la maji eneo fulani na kuhamia eneo lingine kwa fedha zetu kidogo tunabaki kupiga *mark time* (danadana) eneo lile lile, kwani kwa mwendo huu tutachukua miaka mingapi kuwapatia Watanzania wote maji? Hii ni aibu kwa Taifa.

Mheshimniwa Spika, mfano mradi mkubwa maji Kahama – Shinyanga imegharimu shilingi bilioni 252 *from World Bank.* Sote tuliongea lakini tukatulia kwamba wenzetu wapate maji, wengine kwa hatua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada tu ya kukamilika kwa mradi huu kiasi kikubwa sana cha maji kinapotea ardhini bila kutumiwa wakati huo huo wananchi wa maeneo hayo wanahangaika. Kila siku lita 40,000 zinapotea *MUWASA* wanapata hasara ya shilingi milioni 300 kwa mwezi kusafishia maji haya yanayopotea. Umakini gani ulitumika hapa kuunganisha mabomba mapya na mabomba ya tangu ukoloni?

Mheshimiwa Mwenyekiti, mradi wa Newala shilingi milioni 172 kujenga mabwawa na matanki 11, leo maji hayatoki wananchi wanaangaika hawana maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mradi wa Pwaga – Mpwapwa umegharimu shilingi milioni 600, mabwawa yamejengwa chini ya viwango na wananchi hawana maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mradi wa uchimbaji wa visima kumi kwa Wilaya ya Urambo unaenda taratibu sana wakati matatizo ya maji ni tatizo sugu. Wananchi wanapata mateso makubwa kutembea kilomita tatu hadi tano kufuata maji ya kisima mbali na anakokaa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, visima vichache vilivyochimbwa kupitia mradi huu ni vifupi sana na havikidhi mahitaji wakati wa ukame vinakauka, hakuna maji. Wananchi wamejichimbia maji yao wenyewe kwenye maeneo yao kwa matumizi ya kawaida, maji hayo kwa kuwa yako juu ya mwamba siyo salama kwa matumizi ya kunywa na kupikia. Kuendelea kwa tatizo hili la maji ni adha kubwa kwa wananchi hawa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati Serikali ikiwa kwenye mikakati mizuri ya kuhakikisha Mkoa wa Tabora na wilaya zake unapatiwa maji safi na salama tunaomba Serikali isaidie Manispaa ya Tabora kuweza kumudu gharama za usafishaji maji yanayotoka kwenye mabwawa ya Igombe (1958) na Kazima (1949). Maji ya mabwawa haya ni machafu sana na dawa za kuyatibu ili yafae kwa matumizi ni gharama kubwa hali inayosababisha wananchi kunywa maji yasiyo mazuri kwa matumizi ya binadamu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la Wachina kupewa kibali na Serikali cha kuchimba madini kwenye chanzo cha maji hapa Chunya, Mbeya ni fedheha kwa Taifa

hili.  Hivi kweli Serikali inaweza kutoa kibali kwa kampuni kuchimba madini bila kujua kampuni hiyo inakwenda kuchimba wapi?  Hili limekuwa shamba la bibi?  Dhamana tuliyopewa na wananchi ya kusimamia rasilimali zao iko wapi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kampuni hii ya Kichina imeleta uharibifu mkubwa sana ya vyanzo vya maji. Serikali imewasimamisha kuendelea na uchimbaji lakini haijasema kwenye barua kuhusu nani atarudisha hali ya mazingira yaliyoharibiwa, adhabu gani watapewa kwa kwenda kinyume na taratibu za nchi na nani karuhusu kampuni hiyo kufanya shughuli hapo.  Tunaomba Waziri ufafanue haya yote wakati anajibu hoja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati wa mvua za masika maji mengi yanapotea na hata kuleta maafa makubwa ya uharibifu wa miundombinu na hata kubomoa nyumba. Serikali ijenge miundombinu ya umwagiliaji na mabwawa ya kukusanya maji hayo yatumike kwenye kilimo wakati wa vuli. Ahsante.

**MHE. RUTH B. MSAFIRI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nampongeza mtoa hoja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaandika kuunga mkono hoja, kwani kazi nzuri imefanyika na Wizara hii chini ya Awamu ya Nne.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naishauri Wizara kuongeza jitihada maana miundombinu ya maji iliyoanzishwa zamani mingi imeharibiwa, kisha tulitegemea kusaidiwa na wafadhili jambo ambalo pia lilitudhoofisha pale wafadhili walipochelewesha misaada hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naishauri Serikali yetu kwa hali mbaya ya uharibifu mkubwa wa mazingira tangu kukata miti, kulima katika vyanzo vya maji, uchomaji ovyo wa moto, kupanda miti isiyotunza maji, ukame unaoletwa na mabadiliko ya hali ya hewa duniani na mengine yameathiri vyanzo vyetu vingi vya maji vya asili na maji ya chini ya ardhi kuteremka chini zaidi.  Kwa ujumla hali hii imeipa kazi kubwa ya ziada Wizara hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naishauri Wizara hii ishirikiane na Wizara zingine kudhibiti uharibifu mkubwa wa mazingira ili tupate maji ya wanadamu, wanyama, mimea na matumizi mengine muhimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nitoe shukrani kwa hatua japo chache za kuwezesha upatikanaji maji unaoendelea. Naishukuru Serikali, tumepata kisima katika Kata ya Muhutwe, kijiji cha Nyakashenye.  Hali kadhalika tumefanyiwa ukarabati maji bubujiko ya Kata Bulyakashaju.

Aidha, maji makao makuu ya tarafa ya Kamachumu yapo na yanaendelea vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naishukuru Serikali kwa mradi mkubwa unaoendelea katika vijiji vya Katoke na Izigo.  Nashukuru kwa hatua zote zinazoendelea, nawapongeza wananchi kwa kuelewa na kuchangia huduma hii muhimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashauri Serikali ihakikishe kila mahali inapoanzisha mradi iukamilishe, isirukeruke na kuuacha mradi huo bila kukamilika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda niseme masikitiko pia niliyonayo. Serikali imeweza kupeleka mradi mkubwa sana kwa kweli wa kihistoria kutoka Ziwa Victoria kwenda Mkoa wa Shinyanga, lakini Serikali haijatuangalia ipasavyo sisi tuliopakana na Ziwa hilo hilo kwamba tuna matatizo makubwa ya maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, imekuwa kama haieleweki ukasikia sisi tulio katika maeneo yenye vyanzo visivyokauka kama vile Ziwa Victoria na Mto Ngono trunakosa maji ya uhakika. Aidha, tunazo mvua nyingi tena za muda mrefu kila mwaka, lakini tuna shida kubwa sana ya maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naishauri Serikali katika zoezi hili la kujenga matanki kwa ajili ya kuvuna maji ya mvua, maeneo kama Jimbo la Muleba Kaskazini tukapewa kipaumbele. Watu wengi wamejenga nyumba za bati imara, naamini wako tayari kupokea huu mradi. Naishauri Serikali itupe kipaumbele basi katika hili, wakati tupate matanki ya kuvuna maji kwa watu binafsi na taasisi tulizonazo hasa shule zetu za sekondari tulizojenga kwenye kata huko vijijini, zahanati na kadhalika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru na ninawakaribisha Muleba Kaskazini kwa kuzifanyia kazi hoja nilizotoa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nawasilisha.

**MHE. CLEMENCE B. LYAMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, natoa pongezi kwa Waziri wa Maji na Umwagiliaji, Mheshimiwa Profesa Mark Mwandosya, kwa uwasilishaji mahiri wa hotuba yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naanza kwa kuunga mkono hoja hii. Pia namshukuaru sana Mheshimwa Waziri kwa ahadi aliyoitoa Julai, 2009 ya kutoa shilingi milioni 100 kwa ajili ya kuchimba kwa dharura visima vinne Mikumi.

Pamoja na kuunga mkono hoja, napenda Mheshimiwa Waziri wakati unahitimisha hoja hii alieleze Bunge lako Tukufu na wananchi wa Mikumi wamsikie ni lini visima virefu vinne alivyoniahidi kwa maandishi vitachimbwa katika Mji mdogo wa Mikumi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, wananchi wa Mikumi wameninunia kutokana na tatizo la uhaba mkubwa kuendelea kwa kipindi kirefu kinachozidi miaka 15 bila ufumbuzi. Wananchi wananiona nawapiga siasa ninapoeleza ahadi ya Mheshimiwa Waziri. Nimefuatilia sana suala hili kwa kufika Wizarani mara nyingi na nilisaidiwa kila mara na ndivyo nilivyowapa matumaini wananchi wa Mikumi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wananchi wanahitaji kunywa maji, siyo kunywa matumaini. Namuomba Mheshimiwa Waziri wa Maji achukue hatua zote

zitakazomuwezesha kutoa shilingi milioni 100 kadri ya barua yake Na. BA.30/544/01/136 ya tarehe 10 Julai, 2009 iliziwezesha kuchimba visima virefu vinne na kununua mabomba ya kusambaza maji na vifaa vingine ili kuharakisha maji kuwafikia wananchi wa Mikumi kabla ya Uchaguzi Mkuu ujao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa heshima zote namuomba Mheshimiwa Waziri anikubalie ombi hili ili kuilinda na kuienzi ahadi aliyoitoa Mheshimiwas Rais alipotembelea Mikumi mwezi Novemba, 2008.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu upatikanaji maji vijijini, naiomba Serikali iwe makini sana ku-*audit* au ku-*verify* takwimu za idadi ya visima vinavyoelezwa kuwepo katika ripoti za halmashauri. Kuna kila dalili za kuwepo takwimu zinazopikwa *(cooked)* kuonesha kuwepo idadi kubwa ya visima vinavyofanya kazi au vilivyokarabatiwa na hivyo kuonesha asilimia kubwa ya upatikanaji wa maji, wakati hali halisi ni pungufu mno kuliko ukweli ulivyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hali hii inawakanganya sana wanavijiji ambao wanakumbwa na uhaba mkubwa wa maji ambayo ndio hali halisi ambapo watendaji wanatoa ripoti kuwa upatikanaji wa maji unaridhisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo hili ni muhimu sana na nasisitiza Mheshimiwa Waziri alifanyie kazi na kuwaagiza halmashauri wazingatie kuwadhibiti wahandisi na kuhimiza watoe takwimu sahihi za visima na *status* yake, pamoja na mahitaji halisi ya visima vinavyohitajika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na umuhimu wa kutekeleza miradi ya maji ya kutumia manyumbani vijijini ambako kuna skimu za umwagiliaji, naishauri Wizara iangalie uwezekano wa ku-*intergrate* miradi ya umwagiliaji na miradi ya kuwapatia maji ya matumizi ya nyumbani kwa kutumia vyanzo vile vile, kwa kiwango kinachowezekana. Mahitaji ya ziada ndio yatokane na visima vifupi au virefu kadri hali itakavyoruhusu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mfano uliopo unaowezekana kutumika kufanya majaribio ya mapendekezo yangu ni mradi na umwagiliaji uliopo Kijiji cha Malolo ambako kuna vyanzo viwili vya maji ambapo chanzo kimoja tu ndicho kinachotumika kwa umwagiliaji. Hii ina maana kuwa, ingegharimu fedha chache zaidi, kama wakati mradi wa umwagiliaji unatekelezwa, mradi wa maji ya mtiririko kutoka chanzo cha pili ungetekelezwa kuliko kuitekeleza kwa nyakati tofauti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii ni kwa sababu gharama za *logistics* na *overheads* nyingi zingeokolewa na kuongeza tija.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya mchango huu, narejea tena kuunga mkono hoja hii.

**MHE. JUMA SAID OMAR:** Mheshimiwa Mwenyekiti, namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujaalia uzima na afya na hivyo kuweza kushiriki kikao cha leo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nampongeza Waziri, Naibu Waziri pamoja na watendaji wote wa Wizara kwa kuwasilisha hotuba hii ya Bajeti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maji ni uhai kwa hivyo ni rasilimali muhimu sana na ya lazima kwa viumbe vyote vyenye uhai. Serikali inapaswa kuwa na mikakati madhubuti ya kusimamia rasilimali za maji kwa maslahi ya wananchi wote pamoja na viumbe vingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sekta za maji ni muhimu sana katika suala zima la kilimo cha umwagiliaji hasa katika maeneo ambayo kuna mito na maziwa ambayo hayakauki kwa mwaka mzima. Serikali ina mipango gani ya kushirikiana na Wizara nyingine kama vile Viwanda, Miundombinu, Maliasili na kadhalika ili kuhakikisha kwamba Kilimo Kwanza kinafanikiwa ili kukuza kipato kwa wakulima pamoja na kukuza uchumi wa nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa binadamu, wanyama na viumbe vingine vinategemea maji kwa maishi yao, je, Serikali ina mipango gani ya utunzaji na udhibiti wa rasilimali za maji ili kuhakikisha vyanzo mbalimbali vya maji hapa nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na juhudi kubwa inayochukuliwa na Wizara ili kuwapatia wananchi maji yaliyo safi na salama lakini bado kuna maeneo ya mijini na vijijini ambako maji wanayasikia tu. Serikali unawaambia nini wananchi hao?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na umuhimu wa maji Serikali inapaswa kutafuta vyanzo vingine vya mapato ndani ya nchi badala ya kutegemea sana wafadhili ambao hawana uhakika wa kupatikana kwao. Hii itasaidia kupunguza tatizo la upatikanaji wa maji hapa nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa mahitaji ya maji yanaongezeka siku hadi siku kutokana na sababu mbalimbali za matumizi ya maji Bajeti ya Wizara ya Maji na Umwagiliaji inapaswa iongezeke badala ya kupungua kama inavyoonekana hivi sasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali Kuu isimamie miradi yote ya maji nchini badala ya kuziachia halmashauri ambazo hazina wataalamu wa kutosha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Jiji la Dar es Salaam lina matatizo makubwa ya upatikanaji wa maji. Serikali inapaswa kuliangalia tatizo hili kwa umakini zaidi hasa ukizingatiwa kuwa Dar es Salaam ni kioo cha nchi.

**MHE. GEORGE B. SIMBACHAWENE:** Mheshimiwa Mwenyekiti nina mambo mawili. Kwanza ni kuhusu utekelezaji wa miradi ya *quick wins.* Baadhi ya halmashauri ufanisi haukufikiwa kwa sababu miradi hasa ya visima virefu havikutoa maji ya kutosha wakati *pump* na mabomba yametandazwa lakini maji hamna.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushauri, miundombinu ya maji isianze kujengwa kabla ya utafiti wa kiwango cha maji haujakamilika, mfano wa tatizo hili ni Wilaya ya Kiteto.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mabwawa makubwa yalijengwa na Serikali miaka ya zamani na sasa yamebomoka au kuharibika. Jimboni kwangu Kibakwe kuna bwawa kubwa lililokuwa linaitwa Wiyenzele liko tarafa ya Rudi, lilikuwa muhimu sana miaka hiyo kwa matumizi ya binadamu, mifugo na kilimo cha umwagiliaji. Eneo lile bado linatunzwa hadi leo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushauri wangu ni kuwa mabwawa yote ya zamani yafanyiwe mkakati kwa programu maalumu ili yafufuliwe. Najua yako mengi nchini hususani sehemu inakopita reli ya kati na ndiyo sababu hata ya kasi ya mafuriko.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante, naunga mkono hoja.

**MHE. DR. REPHAEL M. CHEGENI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hotuba ya Waziri wa Maji na Umwagiliaji, ambayo ameiwasilisha Bajeti hii licha ya changamoto nyingi za KiBajeti na vipaumbele. Sambamba na changamoto hizi, naomba tu Wizarainisaidie kufafanua pamoja na kuwajulisha wananchi juu ya yafuatayo:-

Kuhusu kukamilisha ahadi ya Mheshimiwa Rais ya kuwapatia maji wananchi wa Mji mdogo wa Lamadi na Lukungu katika Wilaya ya Magu. Mradi huu pia umekuwa ukiahidiwa kutekelezwa na Wizarahii, na kwamba Mheshimiwa Waziri alikwishawahi kufika na kuzungumza na wananchi juu ya utekelezaji wa mradi huu. Naomba kufahamu ni lini mradi huu utaanza na ni kiasi gani cha fedha zimetengwa katika Bajeti hii.

Kuhusu Mradi wa Maji wa Mwamanjili – Magu, mradi huu ulishaanza kutekelezwa lakini umekwama kwa ukosefu wa fedha kidogo kwa ajili ya msambazaji (mtandao) wa maji mara baada ya chanzo cha maji kufungwa pampu na tanki la maji kukamilika. Naomba kupata maelezo ni lini mradi huu sasa utakamilika ili uweze kuwapatia wananchi huduma ya maji na hasa vijiji vya Mwamanyili, Nyasho, Jineri na Mwanangi. Kuhusu mradi wa maji wa Kalemera - Mkula mradi huu umekuwa kwa muda mrefu bila ya kuwa ni kiasi kidogo tu cha fedha kilihitajika ili uweze kukamilika. Mara baada ya pampu mpya ya maji kufungwa mwaka 2002. Kinachokosekana ni mtandao (kukarabati) wa mabomba na hasa kutokea Kalemera kwenda Mkula.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashauri Wizara ijielekeze katika kukamilisha miradi hii ili kuwawezesha wananchi kupata huduma ya maji na hasa kwa kuzingatia kuwa Ziwa Victoria haliko mbali na ni chanzo muhimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja hii.

**MHE. JOHN P. LWANJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, maeneo ya juu ya Wilaya ya Manyoni hususan Tarafa ya Itigi – kata zote za Idodyandole, Aghondi, Ipande,

Sanjaranda, Itigi, Mgandu, Mitandu, Mwanagembe na Rungwa (ni maeneo ya *plateau*), uchimbaji wa maji ni mgumu kwa sababu visima ni vya kina kirefu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja hapa ni kwamba fedha nyingi sana zimekuwa zikitumika katika kutafiti wapi visima vichimbwe na kwamba visima vinapochimbwa maji hukosekana, wanaotafiti na kubaini maji chini ya ardhi ni wataalam wa maji (Serikali) lakini wachimbaji ni makandarasi. Wananchi hushangaa wanapokuta makandarasi hao wanapochimba hawapati maji na maeneo husika kuachwa na kilio kile kile cha kiu ya maji. Mbaya zaidi wananchi huachwa na hisia kwamba kuna mchezo unaochezwa baina ya watafiti na makandarasi kujipatia fedha kwa njia haramu na kuwaacha wananchi solemba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napendekeza kwamba fedha za kutafiti maji na za kuchimba zitolewe moja kwa moja kwa vijiji husika ili Serikali ziendeshe mchakato huo zenyewe kwa ushirikiano na wataalam. Mvaa kiatu ndiye anajua ni sehemu ipi panaumia. Wao wanauchungu wa fedha hizo za kutafuta maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali iwatambue wataalam wa jadi wanaopima maeneo yenye maji kwa njia ya *water dousing system.* Hawa huwa na uhakika zaidi kuliko hata *machine* zinazotafiti maji ardhini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wananchi wengi wanajichimbia visima vyao na hivyo kusaidia Serikali kuteka majukumu yake *(core activity)* ya kuwapatia wananchi maji ya kunywa na matumizi ya mifugo na umwagiliaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napendekeza kuwa kila mwananchi anayefanikiwa kuchimba kisima ambacho kitahudumia na wananchi wengine wanaomzunguka Serikali iweke mkono wake kwa kumpatia mwananchi huyo pampu/*machine* ya kuvuta maji. Visima hivi vina tija zaidi katika kuwapatia wananchi maji na ndiyo ufumbuzi wa haraka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, natarajia kuwasilisha Serikalini orodha ya majina ya wananchi wote wenye visima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mradi wa kusambaza maji ya Ziwa Victoria kutoka Shinyanga/Kahama uendelezwa. Usambaze maji kupitia Mkoa wa Tabora (Igunga), kuingia Mkoa wa Singida (Iramba, Singida na Manyoni) na hatimaye kufika Dodoma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hatua hizi ndizo zitakazoleta ukombozi wa tatizo la maji katika maeneo yetu kame.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naipongeza sana Serikali ya Tanzania kwa kuwa na msimamo dhabiti juu ya matumizi ya maji ya Ziwa Victoria kwa maendeleo ya wananchi wake kwamba maji hayo ni haki ya nchi ya Misri na Sudan pekee ni ukoloni mamboleo na ubaguzi. Naiomba Serikali iendelee na msimamo huo wa kuyatumia maji hayo bila kujali vitisho hivyo ili hutuletea maendeleo ya haraka. Nawapongeza sana waasisi wa mradi huu muhimu sana kwa Taifa letu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali iendelee kutenga fedha za kutosha katika kuchimba malambo na mabwawa maeneo yenye ukame na yenye mifugo mingi kama vile Manyoni na Singida ili kuwapa wananchi ahueni ya kutafuta maji ya kunywesha mifugo na kilimo cha umwagiliaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napendekeza malambo/mabwawa kwa vijiji vifuatavyo, Sanjaranda, Kitaraka, Gurungu, Kitopeni, Dorito, Idodyandole, Kashangu, Leje, Madibila, Aghundi, Njiri, Mabondeni, Itagata, Lulanga, Mgandu na Mitundu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nawatakia kila la kheri katika kuiendesha Wizara hii muhimu sana kwani maji ni uhai.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Waziri Mkuu alipotembelea mji mdogo wa Itigi Mei 13, 2010 Naibu Waziri wa Maji na Umwagiliaji alifuatana nae. Ilitolewa ahadi na Waziri Mkuu pale Itigi kuwa Serikali itahakikisha inaongeza *Distribution Points (DPs)* za maji ili kusambaza maji mji huo. Ahadi hii ilitokana na wananchi kumweleza Waziri Mkuu kero yao ya maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujua ni lini ahadi hiyo ya Mheshimiwa Waziri Mkuu itaanza kutekelezwa na shilingi ngapi zimetengwa kwa mradi huo?

**MHE. SAMUEL M. CHITALILO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nachukua nafasi hii ya kwanza kabisa kumshukuru Waziri na Naibu pamoja na watendaji wa Wizara wote kwa kuandaa hotuba nzuri ambayo imesheheni mambo muhimu kwa manufaa ya Watanzania wote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru Wizara kwa kutenga pesa kwa ajili ya halmashauri zote kupata pikipiki na *photocopy machine* hiyo itarahisisha utendaji wa kazi katika idara husika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, je, kuna mpango gani au mikakati gani ya kuhakikisha kila palipo na jimbo la uchaguzi kunakuwa na mradi wa umwagiliaji kama mradi wa mfano?

Mheshimiwa Mwenyekiti, je, Wizara ina mkakati upi wa kuhakikisha Jimbo la Buchosa linapata visima kwa ajili ya kuwasaidia wananchi wanoishi mbali na maji ya karibu yalipo?

Mheshimiwa Mwenyekiti, je, Wizara inaweza kuwa inatoa dawa za kuua wadudu katika visima vya kienyeji ambavyo hutumiwa na wenyeji kujipatia maji ya kunywa na wenyeji kujipatia maji ya kunywa? Ili kunusuru maisha ya wapiga kura wangu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vinginevyo sina zaidi budi nazidi kuipongeza Wizara kwa kuandaa hotuba ambayo haina ubishi kwa mtu yeyote labda awe na sababu binafsi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja kwa asilimia mia kwa mia.

**MHE. DR. LUKA J. SIYAME:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nichukue fursa hii kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Mbozi Magharibi kumpongeza Mheshimiwa Waziri kwa hotuba yake iliyotayarishwa kwa weledi mkubwa ikibainisha kwa mapana utekelezaji wa Wizara yake na Ilani Uchaguzi Mkuu ya Chama cha Mapinduzi ya mwaka 2005, na mipango mikakati ya mwaka wa fedha 2010/2011 na baadaye.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kumpongeza Naibu Waziri, *Engineer* Christopher Chiza, ambaye utendaji wake wa kazi unastahili tuzo ya kipekee kwani anatekeleza majukumu yake bila kuchoka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda nimpongeze sana Katibu Mkuu wa Wizara hii *Engineer* Christopher Sayi, ambaye kwa hakika ameonesha ufanisi mkubwa katika kuhakikisha Wizara hii inatekeleza mipango yake kama ilivyopangwa. Utaaalamu na uzoefu wake katika Wizara hii umekuwa mhimili wa mafanikio ya Wizara yake.

Napenda nichukue fursa hii tena kutoa shukrani na pongezi zangu kwa Wakurugenzi na watendaji wote wa Wizara ya Maji na Umwagiliaji na taasisi zote zilizo chini yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wananchi wa Wilaya ya Mbozi hususani wale wa Jimbo la Mbozi Magharibi wanayo kila sababu ya kuipongeza Wizara ya Maji na Umwagiliaji na kuunga mkono hoja kwa sababu zifuatazo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, miaka mitano iliyopiata Jimbo la Mbozi Magharibi – uwanda wa juu na hata uwanda wa Bonde la Ufa, lillikuwa likikumbwa na kiu kali na magonjwa yaambatanayo na kutooga kama upele, kutokana na ukame mkubwa uliokuwa ukitokea kati ya mwezi Juni na Novemba kila mwaka. Pia kati ya mwezi Desemba na Mei kila mwaka, lilikuwa likikumbwa na magonjwa ya milipuko hususan kipindupindu, homa ya matumbo na kuhara damu kutokana na kunywa maji yasiyo safi wala salama. Katika kipindi cha mwaka 2007 – 2010 wananchi wa Jimbo langu wanapata miradi mbalimbali ya maji safi na salama kwa njia ya visima vya kati na virefu na pia vyanzo vingine kama mito na kuwasambazia wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kusema hivi sasa mpango wa kupeleka maji katika vijiji kumi kila Wilaya utapunguza sana tatizo la maji jimboni kwangu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, miaka mitano iliyopita tatizo la maji katika mji wa Tunduma lilikuwa limekithiri kiasi cha kufikia kiwango cha *political crisis*, kwa maana kasi ya ukuaji wake na upatikanaji wa maji haukuwa na uwiano. Hali hii ilisababisha watu kuvuka mpaka na mikokoteni iliyobeba magudulia kwenda Nakonde nchini Zambia kuchota maji. Suala hili wakati mwingine lilifuatiwa na udhalilishaji mkubwa. Pia kutokana na ukosefu huo wa maji magonjwa ya milipuko kama kipindupindu, homa ya matumbo, kuhara na upele yalichukua mkondo wake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kwa heshima na taadhima, kwa hivi sasa kutokana na kuchimba visima virefu vinne mjini hapa, tatizo la maji limepungua sana na hivyo tena shukrani nyingi ziiendee Wizara hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wananchi wa Jimbo la Mbozi Magharibi kwa heshima na taadhima wanaishukiuru na kuipongeza sana Wizara kwa kuwapatia fedha za miradi ya umwagiliaji ya skimu za Nanung'ongo na Iyendwe kwa mwaka wa fedha 2009/2010.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mradi wa umwagiliaji wa skimu ya Naning'ongo ambao ulikuwa umegharimu Serikali na wananchi ulisombwa na mafuriko tarehe 24 Desemba, 2006 siku tano tu kabla ya kukabidhiwa Serikali kutoka kwa mkandarasi. Serikali yetu iliitikia haraka sana kilio cha wananchi kwa kufanya tathmini ya uharibifu, kufuatiwa na upembuzi yakinifu wa ujenzi upya wa mradi huo na kuanza kugharamia ujenzi mpya mwaka wa fedha 2008/2009. Mradi huu unategemewa kugharaimu shilingi bilioni 5.6 utakapokamilika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mradi wa umwagiliaji wa skimu ya Iyandwa, ulikuwa umesimama ujenzi wake toka mwaka 2005 lakini kwa kuthamini sera ya kilimo cha umwagiliaji kwa kuanza tena Serikali katika mwaka wa fedha 2009/2010 ilitoa shilingi milioni 400. Mimi binafsi na wananchi wa Jimbo la Mbozi Magharibi tunashukuru sana. Pongezi pia, zinatolewa kwa Wizara kwa kutoa shilingi milioni 50 ili kupunguza tatizo la maji Tunduma wiki hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna maeneo machache ambayo wananchi wa Mbozi Magharibi wanaomba Wizara ya Maji na Umwagiliaji iwasaidie ili kuweza kuwaongezea mafanikio yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuendelea kuongezea fedha kwa ajili ya mradi wa maji Tunduma ili maji ambayo sasa hivi hayasukumiwi kutoka kwenye visiwa yaweze kusambazwa maeneo mbalimbali ya mji kwa mtandao wa mabomba. Pamoja na ombi hili, tunashukuru sana Wizara kutenga shilingi milioni 50 na kuzipeleka kwa dharura wiki hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia kuendelea na mpango wa kusambaza maji wa vijiji kumi Jimboni kwangu ili kumaliza kabisa tatizo la upatikanaji maji safi na salama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kufanya marekebisho katika kasoro zilizojitokeza kwenye visima na mfumo wa kusukuma maji hususan kwenye vijiji vya Kata za Kamsamba, Ivuna na Chilulumo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Jimbo la Mbozi Magharibi mbali na miradi ya umwagiliaji ya Naming'ongo na Iyendwa, ina mradi wa Chilangu ambao bahati mbaya umesimama. Tunaomba ufufuliwe.

**MHE. DEVOTA M. LIKOKOLA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napongeza hotuba ya Mheshimiwa Waziri na kazi nzuri inayofanywa na Wizara hii.

Nashauri ushirikiano wa Wizara na sekta binafsi na *NGOs, CBOs* na kadhalika uongezeke hasa kwa sekta zenye wadau na utendaji katika maji.

Nashauri pia Serikali kutambua na kushirikisha zaidi wadau wa maji mfano miradi mikubwa na mizuri ya Shipo Njombe. Nashauri pia kusaidia na kutambua wabunifu wadogo wadogo kama Mzee Pwagu wa Njombe anayesambaza sana maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashauri pia Serikali iangalie uwezekano wa kuweka ruzuku kwa wananchi vijijini wanaotaka kuweka pampu za mkono walipe 20% na 80% litolewa ruzuku ya Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, natoa pongezi kwa uundaji vikundi vya watumiaji maji vijijini, itasaidia kuwezesha gharama za maji endapo kuna vikundi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu umwagiliaji, Waziri Mkuu aliahidi *scheme* ya umwagiliaji ya Bonde la Mto Ruvuma katika eneo ya Londoni, Lizaboni, Songea litatengewa fedha, je, hilo limetekelezwa? Tunaomba *scheme* hiyo iwe katika mpango wa mwaka huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja. Ahsante.

**MHE. CASTOR R. LIGALLAMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote napenda kumpongeza Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na Wakurugenzi wote kwa hotuba nzuri.

Mchango wangu utahusu utekelezaji wa miradi ya maji katika miji ya Ifikara na Mlimba katika wilaya yangu ya Kilombero. Niliwahi kuuliza hapa Bungeni juu ya mradi wa maji wa mtiririko *(gravity water)* kutoka chanzo cha Mto Lumemo kwa mji wa Ifakara na chanzo cha Mto Mpango kwa mji mdogo wa Mlimba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika majibu yake, Waziri alikiri kutambua miradi hiyo na kueleza hatua iliyofikiwa katika utekelezaji kwa kuwapata wataalamu washauri kwa ajili ya usanifu wa miradi hii, cha kushangaza ni kwamba wananchi wa mji mdogo wa Mlimba wamenieleza kuwa mradi wao umegeuzwa kuwa wa visima badala ya kuwa wa maji ya mtiririko kutoka Mto Mpango.

Naomba ufafanuzi juu ya mabadiliko hayo kwa miradi yote miwili ya Ifakara na Mlimba kwa sababu kuna tofauti katika maelezo yaliyotolewa wakati Waziri akijibu swali langu nililoliuliza hapa Bungeni tarehe 5 Februari, 2009.

**MHE. ARCHT. FUYA G. KIMBITA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nampongeza kwa dhati Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu, pamoja na watendaji wengine wote wa Wizara hii, hongereni sana. Naipongeza sana Serikali kupitia Wizara hii kwa kutuunga mkono katika mipango yetu ya maji safi na salama na miradi ya umwagiliaji kule wilayani Hai, tunashukuru sana.

Nashukuru sana kwa kutupatia pesa kwa ajili ya banio la maji kule Mijongweni pamoja na mifereji/miundombinu mingine ya umwagiliaji katika ukanda wa tambarare. Tunashukuru pia kwa mradi wa maji safi na mazingira unaondelea kule wilayani kwetu.

Baada ya pongezi na shukrani hizo naomba niweke mbele yenu maombi machache yafuatayo, kwanza pesa zaidi kwa ajili ya miradi ya umwagiliaji kule tambarare. Pia pesa kwa ajili ya kuboresha vyanzo vya maji maeneo ya milimani ikiwa ni pamoja na kupata uwezo wa kujenga sehemu za magawio katika mifereji yetu ya asili huko huko maeneo ya milimani ili kuepuka upotevu wa maji unaondelea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa msisitizo mkubwa sana ni ombi langu la kujengewa mabwawa madogo madogo na bwawa kubwa la Kwamamasawa ambalo litasaidia sana haswa nyakati za kiangazi kwa ukanda mkubwa sana huko wilayani kwetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga hoja mkono na kuendelea kuwaombeeni kila la kheri.

**MHE. DR SAMSON F. MPANDA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote naunga mkono hoja asilimia mia kwa mia, ila yafuatayo napendekeza yangetiliwa mkazo.

Kwanza kwa kuwa kila Mbunge kwa namna yake ana matatizo makubwa ya maji na kwa kutegemea maji ya mvua kwa mkono wangu naona hayakidhi haja ya Wabunge hao hivyo napendekeza uchimbaji wa visima kwa kutumia Wakala wa Serikali *(DDCA)* naona ndio ingekuwa suluhisho muafaka. Inasikitisha hata kazi za serikali za uchimbaji wa visiwa na ujenzi wa mabwawa, hawapewi kipaumbele na hata Bodi ya *DDCA* bado haijazinduliwa na Waziri, sijui Waziri anakigugumizi gani wakati vifaa na wataalamu wanao wa kutosha.

Napendekeza kila Mkuu wa Wilaya katika malengo yake ya kazi suala la upatikanaji maji ingekuwa ndio kipimo cha utendaji bora wa kazi yake, nafikiri ni wakati muafaka sasa kuchimba mabwawa madogo madogo *(Chaco - Dams)* ingekuwa ndio suluhisho zuri kuliko kutegemea mabwawa makubwa na yenye gharama kubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kitengo cha utafiti wa maji chini ya ardhi ambayo makao yake makuu yapo hapa Dodoma naona inafifia sana wakati zamani walikuwa watoa mchango mkubwa katika kutatua matatizo ya maji.

Napendekeza kwa mfano njia iliyokuwa inatumika zamani kupitisha watumwa kutoka Kigoma (Bara) hadi Bagamoyo (Pwani) wangechimba visima vingi njiani ingekuwa kivutio kikubwa cha kitalii na hata wanyama wauzwao Dar es Salaam kutoka Bara wangeweza kupita humo humo kwenye njia hizo.

Kwa kuwa Mto Rufiji na Ruvu pale maeneo ya Morogoro yangeunganishwa ili kuhakikisha Mto Ruvu haupungui maji wapi na vipi endapo kama nisingekuwa mwanasiasa, ningechukulia hiyo kama moja ya *project* yangu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Jimbo la Kilwa Kaskazini kwa kweli tatizo la maji ya kunywa ni moja kati ya matatizo makuu hata *programme* ya *quick wing* ya visima kumi haijaanza kutoa matokeo yoyote hadi sasa sijui kulikoni!

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kilimo Kwanza haina maana kama hatutaweka mabwawa makubwa katika mito mikubwa kama vile Mto wa Matandu, Kilwa, kilimo cha umwagiliaji kingefanikiwa sana. Kauli mbiu ya maji ni uhai inapungua umaana wake, maana kila sehemu tatizo la maji lipo, karibu Tanzania nzima au tuanze tena kufikiria neno lingine la kisiasa la kusema maji ni uhai?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni lini pampu ya Kipatimu itakarabatiwa ili kujaza tanki linaloota kutu?

**MHE. DR. JAMES A. MSEKELA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwa kumpongeza *Engineer* Profesa Mark Mwandosya, Waziri wa Maji na Umwagiliaji pamoja na *Engineer* Mheshimiwa Christopher Chiza, Naibu Waziri kwa kazi kubwa na ya mafanikio kwa kutekeleza Ilani ya Uchaguzi katika miaka hii mitano. Hakika wahandishi hawa wakisaidiwa na wahandishi wengine wa Wizara chini ya Katibu Mkuu wa Wizara, *Engineer* Sayi, wamefanya kazi nzuri sana na kujenga utaratibu katika kufikisha huduma ya maji kwa wananchi katika sehemu mbalimbali za nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na uchimbaji wa visima virefu katika jimbo la Tabora Kaskazini nashauri Wizara ione umuhimu wa kusaidia kujenga malambo kwa kukinga maji mengi ya mvua ambayo hupotea bure katika maeneo mengi ya jimbo la Tabora Kaskazini. Malambo haya ni vyema yakawa madogo madogo yakiwa yamesambaa kwa kuyaweka karibu na *settlement* za wanavijiji, utaratibu huu tunao na umekuwa wa msaada mkubwa katika maeneo husika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja ya Mheshimiwa Waziri.

**MHE. FELIX N. KIJIKO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa napenda kusema kuwa naunga mkono hoja na Bajeti ya Wizara hii kwa kiasi kikubwa cha asilimia mia kwa mia.

Pamoja na maelezo mazuri ya Waziri katika kuwasilisha hotuba yake, napenda kujua utelekezaji na siyo mpango wa kuwapatia maji ya kuaminika wananchi wa mjini Kibondo. Mji wa Kibondo unao wakazi wapatao 27,000 ambao wanaishi ama wanatakiwa kuishi kwa kupata huduma muhimu ya maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kusema kuwa wananchi hawa ambao wamekuwa wakiishi maisha yasiyo na uhakika kutokana na Wizara hiyo kutokuwatendea haki tangu Uhuru hadi leo, wamepangiwa nini katika Bajeti hii ambayo hoja yake

imeletwa mbele yetu? Napenda kwa niaba ya wananchi wa Kibondo, nimshukuru Mheshimiwa Rais kwa msaada mkubwa wa kuwaonea imani kwa kuwapatia kisima kimoja kinachotumia *solar* ambacho sasa kinafanya kazi. Naomba kwa mfano huo huo wa Mheshimiwa Rais wa kuwaonea huruma wananchi hao, Wizara nayo ifumbe macho na kuwaonea huruma, hao viumbe.

Natoa kilio hiki kwa masikitiko makubwa kwa Wizara inaweza kabisa kuwapatia wananchi hawa maji yenye uhakika kutoka kwenye chanzo cha maji cha iliyokuwa kambi ya wakimbizi ya Nduta ambayo iko umbali wa kilomita nane tu. Chanzo hiki cha maji kilikuwa kinao uwezo wa kuwapatia maji ya kutosha wakimbizi 60,000 waliokuwapo kwenye kambi hiyo ukilinganisha na idadi ya watu 27,000 tu waishio Kibonzo mjini na vijiji vyake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

**MHE. DR. MARY M. NAGU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda nimpongeze na kumshukuru Mheshimiwa Waziri, Prof. Mark Mwandosya, pamoja na Naibu Waziri Dr. Chiza.

Pia nawapongeza watendaji wote na wataalam katika Wizara wanayoongozwa na *Engineer* Sayi.

Naomba nikumbushe umuhimu wa Wilaya ya Hanang kuchimbiwa Lambo kutokana na matatizo makubwa ya maji, kwani Wilaya yetu haina vyanzo vingi vya maji hasa Kata ya Gidahababieg.

Wilaya ya Hanang kwa maeneo mengi ina madini ya *Floride* katika maji, hivyo tunaiomba Wizara itusaidie kutushauri nini la kufanya ili tuwe na maji yasiyo na *Floride* ambayo si salama kwa afya ya watu.

Narudia tena pongezi zangu kwenu nyote na ninaunga mkono hoja hii.

**MHE. MWANAWETU SAID ZARAFI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Bunge hili la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania niliwahi kuuliza, nini hatima ya mradi wa maji ambao ulifadhiliwa na Serikali ya Finland miaka kadhaa ya nyuma, mradi ambao upo katika kijiji cha Nipara Wilaya ya Kilwa.

Mradi huu ulibakia asilimia chache ukamilike kwani ulishakamilisha *Tank* la Maji, Visima vidogo vidogo (*channel* za kuunganisha maji hayo) vile vile hata nguzo za umeme ziliwekwa.

Inasemekana kuwa tatizo ni umeme na hivi sasa umeme upo, ni lini mradi huu utamalizika ili wananchi wa maeneo niliyoyataja waweze kupata maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana.

**MHE. JANETH M. MASSABURI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nimpongeze Waziri wa Maji na Umwagiliaji, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na Watendaji wote waliochini ya Wizara hii kwa kazi nzuri sana wanayoifanya ya kuboresha Sekta ya Maji na pia kwa kutayarisha/kuandaa hotuba hii ya bajeti 2010.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa ni maoni au ushauri. Kuwepo na takwimu sahihi ya visima ambavyo vinatoa huduma ya maji katika mitaa yote ya Mkoa wa Dar es Salaam ili kujua uhalisia wa idadi kamili na kujua ni idadi gani ya visisma vilivyochimbwa kwa gharama kubwa lakini havitoi maji na sababu zake.

Eneo la Chanika na Msongola liongezewe visima kwani ukame na ukosefu wa maji umeathiri sana hali ya Wananchi wa eneo hilo na ikizingatiwa kuna idadi kubwa ya watu wanaohamia huko pembeni mwa Mkoa wa Dar es Salaam.

Mpango kabambe wa kutandaza mabomba katika Mkoa wa Dar es Salaam ufike katika maeneo yote yakiwemo eneo la Chanika, Pugu na Msongola ili wakati maji yatakapo patikana wananchi wa huko wafaidike na maji hayo.

Kuwepo na Programu itakayosimamia Miundombinu ya Kilimo cha Umwagiliaji cha kutumia dripu *(Drip Irrigation System)* kwa Mikoa ya Dar es Salaam, Pwani na kwingineko. Hii itasaidia Wakulima na Mboga mboga na Matunda kuzalisha mazao kwa mwaka mzima mfululizo na kuleta tija kwa wananchi wenyewe na Taifa zima. Kuwe na utaratibu wa kujenga Makinga Maji katika maeneo mengi ya nchi yetu na Elimu juu ya kujifunza ukingaji na uvunaji wa maji itolewe.

Mwisho, napenda tena kumpongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na Watumishi wote kwa kazi njema yenye vikwazo vingi na kuiweza.

**MHE. BAKAR SHAMIS FAKI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nachukua nafasi hii kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipa uzima na kuniwezesha kuchangia juu ya mada niliyoitaja hapo juu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Maji ni muhimu sana katika uhai sio tu wa Wanadamu lakini hata maisha ya miti, wanyama, mimea na kadhalika. Kwa kuzingatia hilo ni lazima na ni jukumu la kila Serikali hasa iliyo makini kuhakikisha kwamba maji yanapatikana kwa wingi na yaliyo safi. Swali, ni jitihada gani ya ziada inayochukuliwa na Serikali katika kuhakikisha kwamba maji safi yanapatikana nchi nzima bila matatizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa kuna malalamiko mengi kuhusu matatizo ya maji, daima sote ni mashahidi hapa Bungeni kwamba Wabunge wengi wanalalamikia suala hili la maji ndani ya majimbo yao. Je, Serikali inao mpango gani wa makusudi wa uchimbaji wa visisma vya maji nchini ili kuondokana na shida hii ya maji?

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inasemaje kuhusu ile miradi ya maji ambayo imechukua muda mrefu kukamilika. Hivi ni kwa sababu ilipoanzishwa miradi hiyo

Serikali ilikuwa haijajipanga vizuri au ni sababu zipi za msingi zinazopelekea miradi hiyo kuchelewa sana kukamilika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sera ya umwagiliaji ina malengo mazuri pindi itatekelezwa kama ilivyo ili kuweza kutoa tija na hivyo kusaidia katika utekelezaji wa dhana ya Taifa ya kilimo kwanza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Nchi yetu inayo maeneo mengi sana yanayofaa kwa umwagiliaji, kasoro iliyopo ni vipi Serikali itajipanga katika kutumia fursa hii aliyotujalia Mungu.

Swali, hivi Serikali inao mpango gani mahususi na wa muda mrefu wa jinsi ya kuyatumia maeneo haya yanayofaa kwa umwagiliaji hapa nchini. Ahsante sana.

**MHE. DR. MZERU O. NIBUKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza naomba kuunga mkono hoja x 100%.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa napenda kumpongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri kwa umahili wao katika kutekeleza majukumu yao, pia napenda pia kmpongeza Katibu Mkuu na Watendaji wengine katika Wizara hii nyeti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Maji ndiyo uhai wa mwanadamu yeyote hasa ukizingatia kwamba maji ni asilimia 75% ya uzito wa mwanadamu yeyote aliye na afya njema.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu kilimo ambacho ndiyo uti wa mgongo, ni vizuri hivi sasa tukajikita kwenye kilimo cha umwagiliaji lakini kwa vile kilimo hicho ni cha gharama kubwa mno, hivyo ningeshauri kuyalenga maeneo machache ambayo yanayo maji ya kutosha kama vile Mkoa wa Morogoro, Pwani na kadhalika. Ili kusudi miradi hiyo iweze kumalizika katika muda muafaka ili iweze kuleta tija iliyokusudiwa na tupate mazao ya kutosha na kuondokana na shida ya chakula pia na kufanya biashara kitakachobaki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini tukizigawa hizo fedha kidogo tulizonazo kwenye miradi mingi matokeo yake miradi hiyo haitaisha na badala yake fedha zinapotea bure, na kurudi nyuma katika maendeleo yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili ni kuanzisha mpango wa kuvuna maji ya mvua, kwa vile maji hayo yanapotea bure ambayo ni zawadi kutoka kwa Mungu. Baadhi ya nchi nyingi duniani zinatumia mpango huu ili kupunguza shida ya maji hasa wakati wa ukame. Na pia, jambo hili litahitaji muda lakini naamini ni muhimu sana kwa maendeleo ya nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho nawatakia kheri wale wote wanaohusika katika maandalizi ya Bajeti ya Wizara hii muhimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja 100%.

**MHE. HALIMA O. KIMBAU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa napenda kupongeza hotuba hii nzuri. Nawapongeza wewe Mwenyewe Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na Watendaji wote walioshiriki kuandaa hotuba hii. Hivyo basi sina sababu ya kunifanya nisite kuunga mkono, nasema naunga mkono hoja kwa 100%.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo ninayo machache ya kurudia kushauri kwanza kuona jinsi gani mtatumia Mkoa wa Pwani kwenye kilimo cha Umwagiliaji. Mto Rufiji, Wami na Ruvu yote ni Maji ya uhakika yaliyo tayari kutumiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, narudia tena kusema hebu tuone jinsi gani ya kutumia hii mikopo ya Wakulima kuunda Kambi za Vijana za kilimo. Maana yangu ni hivi hawa vijana wawekwe kwenye makundi ya hata ishirini ishirini, wakopeshwe pembejeo na chakula cha miezi kadhaa na baada ya mavuno waanze kulipa. Mheshimiwa Spika, maeneo yapo mengi tu. Kwetu Mkoa wa Pwani iwe basi mfano wa tendo hili. Mimi naamini jambo hili litatoa ajira kwa vijana na pia itasaidia kuongeza chakula na mazao ya biashara. Mimi niko tayari kushirikiana nanyi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho naomba sana tena sana hilo dirisha la mikopo ya Wakulima liwaangalie sana Wakulima wadogo wadogo na hasa wanawake mmoja mmoja na vikundi. Chonde tusifanye kosa la kutoa fedha hizi kwa wakubwa tu. Kilimo kwanza kisaidie kuwatoa pia maskini Wakulima wa vijembe vya mkono vijijini nao wapige hatua. Hawa ni wengi nao wana haki ya kufaidika na mikopo hii.

Narudia kupongeza wewe Mheshimiwa Mwenyekiti, Spika na Naibu Spika, wenyeviti wengine na nawatakia kheri kwa Mwenyezi Mungu awawezeshe kushinda na kurudi tena Bungeni humu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja, ahsante sana.

**MHE. ATHUMANI S. M. JANGUO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakupongeza kwa dhati kabisa pamoja na Spika na Naibu Spika. Aidha nampongeza Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na Wasaidizi wake kwa:-

(a) Kazi nzuri.
(b) Hotuba safi na uwasilishaji fasaha.
(c) Kwa jinsi ulivyo shughulikia matatizo ya maji katika Wilaya ya Kisarawe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nizungumzie tatizo la Maji Kisarawe Mjini. Kama walivyo fuatilia waliokutangulia wana Kisarawe tunakushukuru binafsi kwa kuruhusu shs. 319 millioni zitumike tena nje ya Bajeti ili kuukamilisha mradi. Hivi sasa Makandarasi wanamalizia uunganishaji umeme, utandikaji mabomba na ujenzi wa matanki. Upo ucheleweshaji kidogo kwa sababu *Plan International* wamechelewa

kidogo kuingiza mchango wao wa shs. 182 millioni. Hata hivyo yapo matumaini ya maji kufika mjini mwishoni mwaka huu.

Sasa ni Maji Vijijini. Umefika mwenyewe kuona matatizo ya vijiji vya miradi ya maji katika vijiji vya Msanga, Visiga na Ngongele. Baada ya wewe mwenyewe na Maafisa wako kutembelea Kisarawe mjini na vijiji vya Visaga na Ngongele, ulielekeza na zikatolewa Shs. 105.6 ambazo zimetumika, miradi imekamilika sasa wananchi wanapata maji safi na salama. Tunakushukuru sana.

Katika Kata ya Kiluvya kwa juhudi za Wizara yako, tumepokea Shs. 158 milioni kutoka mfuko wa *Tanzania/Japanese Counterpart Fund* na hivi karibu mradi utakamilika. Tunazishukuru, Wizara, Serikali za Tanzania na Japan.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ombi. Mradi wa Bomba wa Ruvu Mzenga ni wa siku nyingi na nimeuombea sana fedha tangu nilipoingia Bungeni mwaka 1995. Mawaziri wote waliopita waliahidi sana kuutekeleza mradi huu pindi fedha ikipatikana. Wewe mwenyewe mwaka huu 2009/2010 ulitoa udhuru wa kutokuujua mradi huu na ukashauri kujielimisha kutoka kwa Maofisa wako kisha utaushughulikia. Bila shaka hivi sasa unauelewa vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa naomba yafuatayo:-

Je, sasa umeuandaliaje mradi huo?

Kama haumo kati Shs. 2.7 bilioni za Maji Vijijini Mkoa wa pwani, basi uwekwe kwenye Bajeti ya 2011/2012.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nampongeza sana Mheshimiwa Waziri na naunga mkono hoja hii.

**MHE. GODFREY W. ZAMBI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuchukua nafasi hii kumshukuru sana Mheshimiwa Profesa Mark James Mwandosya, Waziri wa Maji na Umwagiliaji, Naibu Waziri, Mheshimiwa Mhandisi Christopher Chizza, Katibu Mkuu na Wataalam wote waliohusika katika maandalizi ya Bajeti hii nzuri. Hata hivyo nina mambo machache ya kuchangia kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mradi wa Maji – Mlowo. Hadi sasa Mlowo ni Kijiji pamoja na kwamba kijiji hicho kina Maendeleo makubwa sana ukilinganisha na baadhi ya miji. Kijiji hicho kwa sasa kinakadiriwa kuwa na watu zaidi ya 20,000. ni kijiji cha kibiashara ambacho idadi ya watu wanaotembelea eneo hilo kwa mchana kwa ajili ya shughuli za kibiashara inafikia watu karibu laki moja (100,000).

Bahati mbaya sana tuna tatizo la maji, tatizo ambalo baada ya kufikishwa Wizarani lilipewa kipaumbele. Wizara ilikubali kugharimia mradi huo kwa kutoa Tshs. 400,000,000/=. Tunashukuru Mheshimiwa Mwandosya ambaye mara baada ya kusikia kilio cha wana Mlowo alikubali kwa dhati kabisa kuwasaidia mradi huo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nataka kujua ni lini hasa mradi huo utakamilika ili kuwaondolea wana Mlowo tatizo la Maji ambalo ni la muda mrefu sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mradi wa Maji wa *Lukulubu Group.* Nampongeza pia Mheshimiwa Mwandosya kwa kukubali kuuingiza mradi wa maji wa Lukulubu kwenye mipango ya Wizara. Hata hivyo nataka kujua nini maendeleo ya mradi. Aidha napenda kujua mradi huo umetengewa kiasi gani cha fedha kwa mwaka wa fedha wa 2010/2011.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mipango ya Maji – Mji wa Viwawa. Mji wa Viwawa wenye idadi ya Wakazi zaidi ya 40,000 bado hauna huduma ya maji inayoeleweka. Mji huo unategemea maji ya kutega ambayo wakati wa mvua huwa machafu sana.

Pamoja na mipango mizuri ya Wizara kuupatia mji wa Viwawa maji ya kuaminika (uhakika), nataka kujua utekelezaji wa mipango hiyo itaanza kutekelezwa lini?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaunga mkono hoja.

**MHE. MWADINI ABBAS JECHA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nichukuwe nafasi hii kuwapongeza Mheshimiwa Waziri Mheshimiwa Mwandosya, Naibu wake Mheshimiwa Chiza pamoja na Watendaji wa Wizara hii kwa juhudi ambazo wanazichukuwa kuwaondolea wananchi shida ya Maji. Juhudi hizo zinaonekana pamoja na kwamba fedha ambazo zinatengwa kwa matumizi ya shughuli za Maendeleo hazitoshi kuweza kuzikabili changamoto zinazoikabili Wizara hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na changamoto hiyo ninaishauri Serikali hususan Wizara hii ichukue hatua za ziada kuomba misaada kutoka kwa wadau wa Maendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la maji taka hasa katika miji mikubwa kama Dar es Salaam, miundombinu iliyopo kukabiliana na tatizo hilo haitoshelezi kukidhi mahitaji. Aidha wananchi ambao wameunganishwa na mtandao wa kudhibiti maji taka ni wachache mno. Hakuna juhudi za makusudi zinazochukuliwa kuona kwamba wananchi wengi wanaoishi katika miji hiyo wanajiunga na mtandao wa maji taka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, inawezekana kabisa kwamba wananchi wetu waliowengi hawafahamu umuhimu wa kujiunga na mtandao wa majitaka. Aidha suala zima la udhibiti wa maji taka halijapewa umuhimu unaostahili ikiwa ni pamoja na kutotungiwa Kanuni madhubuti zinazomlazimisha mwananchi kujiunga na mtandao wa maji taka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nichukuwe nafasi hii kuishauri Serikali kwamba juhudi za makusudi zichukuliwe kuandaa kanuni madhubuti zitazopelekea kila mwananchi ambaye ataanzisha ujenzi mahali ambapo huduma za kudhibiti maji taka kwamba ni lazima ajiunge na mtandao wa maji taka katika eneo hilo.

Aidha, wale wananchi ambao bado hawajiungi iwe ni lazima kwao kujiunga na mtandao huo. Tukifanya hivyo tutaweza kudhibiti maji taka katika miji yetu katika hiyo tutaweza kuimarisha usafi wa miji na kudhibiti magonjwa ya milipuko pamoja na malaria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kilimo cha umwagiliaji hapa nchini kimekuwa kinapigiwa kelele sana kwamba bado hakijapiga hatua inayostahili. Eneo kubwa la nchi hii ambalo linafaa kwa kilimo cha umwagiliaji bado halijafanyiwa kazi. Ni ukweli usio shaka kwamba kutokana na mabadiliko ya tabia nchi kumeathiri sana upatikanaji wa mvua hapa nchini hali inayopelekea kuathiri pia kilimo na upatikanaji wa maji.

Lakini ni ukweli kwamba nchi yetu imejaliwa kuwa na mito mingi isiyokauka kwa mwaka mzima ambayo hadi sasa mito hiyo haijatumika ipasavyo kuimarisha kilimo cha umwagiliaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa nchi yetu sasa haiwezi kutegemea mvua kuzalisha mazao ya kilimo ni lazima Serikali ielekeze nguvu zake kubwa katika kilimo cha umwagiliaji.

Hivyo hapana budi Wizara hii kuimarisha Ofisi zote za Mabonde kuweza kusimamia ipasavyo rasilimali maji ikiwa ni pamoja na vyanzo vya asili vya maji. Kadhalika Wizara isimamie ipasavyo skimu za Umwagiliaji kwa kuzigatia fedha za kutosha kukidhi mahitaji yao. Ikiwa ni pamoja na kuanzisha mfuko maalum wa uendelezaji wa skimu za umwagiliaji ili ziweze kufanyakazi zake kwa ufanisi mkubwa.

**MHE. DIANA M. CHILOLO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, utangulizi. Ninapenda kutumia nafasi hii kwa njia ya maandishi kuwapongeza Waziri wa maji na umwagiliaji, Mheshimiwa Prof. Mark Mwandosya, Naibu Waziri wa Maji na Umwagiliaji, Mheshimiwa Christopher Kajoro Chiza, Katibu Mkuu, pamoja na Watendaji wote walioshiriki kuandaa Bajeti hii yenye mwelekeo thabiti wa kuboresha huduma ya maji pamoja na Kilimo cha Umwagiliaji. Ninawaombea afya, nguvu na mshikamano ili watekeleze mpango kazi wao kama walivyouandaa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mpango wa kuvuna maji ya mvua. Ninaipongeza Serikali kwa kutambua kuwa maji ya mvua ni muhimu sana kukusanywa kwa njia za kisasa. Utaratibu au njia inayotumika ni nzuri lakini bado jitihada hizo ni ndogo kwa vile fedha zinazopelekwa kwenye Halmashauri zetu ni ndogo sana.

Ombi, ninaomba Serikali kutupatia fedha za kutosha kwa ajili ya kilimo cha umwagiliaji kwenye mabonde mengi yaliyoainishwa kwa kilimo cha umwagiliaji. Vile vile wananchi wafundishwe kuvuna maji ya mvua kwenye nyumba zao za bati kwani wengi wao wanayaacha yanamwagika na kuleta mmomonyoko wa udongo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uharibifu wa vyanzo vya maji. Nakumbuka Serikali ilitoa tamko kuwa miti ya aina ya mikaratusi ikatwe kwani inanyonya maji kwa kiasi

kikubwa sana, lakini hadi leo hii miti hii bado ipo tena mingi sana mfano Manispaa ya Singida eneo la Kinyeto, Mandewa na kadhalika.

Agizo hili la kata mti na panda mti limetekelezwa kwa kiwango gani na hii miti inayoua vyanzo vya maji itaisha lini pamoja na kuacha tabia ya kujenga nyumba ama kutenga maeneo ya malisho kwenye mabonde yenye vyanzo vya maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa ni kuhusu kuongezwa kwa wataalamu wa maji. Ninaipongeza Serikali ya awamu ya tatu kupitia Waziri Mkuu Mstaafu Mheshimiwa Edward Ngoyai Lowassa, kwa kutupelekea maji mji mdogo wa Shelui ambayo ni mengi na ya kutosha, ingawa vituo vya maji yaani vioski ni vichache sana.

Ninaiomba Serikali kupeleka mtaalam wa maji mji mdogo wa Shelui ili wakazi wa Shelui ambao wengi wao wamejenga nyumba za kisasa na kuweka vyoo ndani vya kuvuta waweze kupelekewa maji kwenye nyumba zao kwani fedha wanazo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mfumo wa maji katika Jiji la Dar es Salaam. Ninapenda kukiri kuwa juhudi za Serikali kutengeneza mfumo wa maji upya katika Jiji la Dar es Salaam zinaonekana katika maeneo mbalimbali.

Ninaiomba Serikali ifanye hima kutengeneza mfumo wa maji Magomeni Mikumi Mtaa wa Muhuto ikiwemo nyumba No. 7 ambayo ni miongoni mwa nyumba zenye adha kubwa ya maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Malambo kwa ajili ya Mifugo. Vile vile ninakila sababu kuipongeza Serikali kwa kuchimba mabwawa ya kunyweshea mifugo mkoani Singida.

Ninaiomba Serikali kutenga fedha kila Bajeti za kukarabati mabwawa kwani mara nyingi huingia udongo na kupunguza kina na kufanya maji yapungue sana. Je, Serikali imetenga fedha kiasi gani kukarabati mabwawa ya Halmashauri ya Iramba, Singida vijijini na Halmashauri ya Manyoni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la mfumo wa majitaka (maji machafu) Manispaa ya Dodoma upo lakini umekuwa ukiziba mara kwa mara hasa *Area D* ingawa Bunge hili tatizo hilo sijaliona. Ninaiomba Serikali kufuatilia mfumo huo kwani mara nyingi ulikuwa unaziba na kutishia afya za wakazi wa maeneo hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nasikitika kuiarifu Serikali kuwa kuna haja ya kutenga fedha za kutosha kwa ajili ya kununua gari la majitaka katika Manispaa ya Singida, ambalo litasaidia pia Halmashauri zote za Mkoa huo. Ninaomba Serikali itoe matumaini wakati waziri anajibu hoja za Waheshimiwa Wabunge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, ninapenda kumalizia mchango wangu kwa kuunga mkono hoja kwa moyo mkunjufu mia kwa mia.

**MHE. JUMA H. KILLIMBAH:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nimpongeze Prof. Mark Mwandosya, Waziri wa Maji na Umwajiliaji, Mheshimiwa Eng. Christopher Chiza, Naibu Waziri wa Maji na Umwagiliaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niwapongeze Katibu Mkuu wa Wizara ya Maji na Umwagiliaji na Watendaji wote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maji ni uhai, usafi wa mazingira ni utu.

Mheshimiwa Mwemyekiti, kauli mbiu hii ni nzuri sana na ni kauli yenye kuthibitisha kwamba bila maji uhai wa viumbe na utendaji wa masuala mbalimbali haiwezekani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mchango wangu ni katika maeneo yafuatayo:-

Miradi ya umwagiliaji banio la Mlandala, ukarabati wa banio hili uko vipi? Kwa nini wizara imekuwa na ahadi zisizotekelezeka?

Kwa nini kiwango kikubwa cha fedha zilizotumika awali kwa kutengeneza mradi huu ziteketee bila tija yoyote ya uzalishaji? Naomba maelezo ya kina kuhusu mradi huu. Sambamba na hili pia miradi ya Masimba na Tyeme/Masasi wizara inasema nini kuhusu miradi hii mbali na taarifa kuandikwa vitabuni bila utekelezaji, miradi hii inaonekana kama kiini macho kwa wananchi ambao ni wakulima waliopo maeneo hayo.

Miradi ya maji maarufu kwa jina la *Quick wins,* ile ya visima vifupi nashukuru serikali kubuni mradi hii, lakini tatizo lipo ni pale elimu ya kutosha juu ya uendelezaji wa mirdi hii hasa wananchi kukosa mbinu ya kuilinda kiufundi miradi hii, kwanini wizara isiandaye wataalam katika maeneo yenye miradi hii ili wafundishwe na wawe na mbinu za kiufundi pindipo hitilafu inapojitokeza hatua zichukuliwe. Nasema hivyo kutokana na hali halisi kwani miradi mingi ya aina hii iliyopo jimboni kwangu (Iramba Magharibi) imekufa na sasa hakuna hatua zozote zinazochukuliwa kuifufua miradi hii.

Mradi wa maji wa maporomoko ya Mto Wembere, naomba maelezo kuhusu mradi huu uliotumika miaka ya 1975 – 1980 kwa kusambaza maji kwa Kijiji cha Wembere na Nselembwe (Shelui) na Kijiji cha Mseko.

Mheshimiwa Mwenyekiti, iweje wananchi wa vijiji vya Wembere kuendelea kukosa maji wakati maji ya Maporormoko haya yanapotea bure? Naomba wizara sasa ifufue mradi huu kwa kusambaza maji kwa vijiji vya Wembere, Tintigulu, Mgongo, Kizonzo, Mseko na Malendi. Inasikitisha kuacha mradi kama huu maji yapotee bure wakati wananchi wanateseka kwa kuhitaji maji kwa matumizi.

Miradi ya mabwawa ya umwagiliaji na matumizi mengine. Kwa kuwa mahitaji ya matumizi ya maji kwa shughuli mbali mbali hasa shughuli za kilimo na kutekeleza kilimo kwanza na kwa kuwa maeneo ya jimbo la Iramba Magharibi ni kame na ya msimu mmoja wa kilimo.

Naomba wizara itilie mkazo ujenzi wa mabwawa kwa maeneo ya maporomoko ya Kijiji cha Kikonge, bonde la Shelui na maeneo mengine yenye taswira hiyo.

Naomba wizara pia kuona umuhimu wa kujenga mabwawa kwa ajili ya mifugo kwa vijiji vya Msansao na Ujungu ili wafugaji wa maeneo hayo kuondokewa na wafugaji wa maeneo ya mifugo.

Naipongeza serikali kwa miradi ya maji ya mpango wa Benki ya Dunia. Naomba utekelezaji wa miradi ya awamu ya pili uharakishwe ile ya Ujungu, Mlandala, Mgungia, Ng'anguli, Nguvumali na Mingela.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja, ahsante sana.

**MWENYEKITI**: Waheshimiwa Wabunge, sasa nitamwita Naibu Waziri wa Wizara ya Maji na Umwagiliaji ili naye aje atoe mchango wake ambao kwa sehemu nyingine utakuwa unajibu baadhi ya hoja za Waheshimiwa Wabunge. Mheshimiwa Chiza Tafadhali.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nami naomba nichangie hoja hii kwa dakika zangu hizi kumi nilizopata kwa haraka haraka. Kwanza kabisa naunga mkono hoja iliyopo mbele yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kwanza nitumie nafasi hii kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunifikisha salama katika Mkutano huu wa Ishirini ambao ni Mkutano wa mwisho katika awamu hii ya Bunge lako Tukufu. Nachukua pia nafasi hii kumshukuru Mheshimiwa Rais Jakaya Mrisho Kikwete, kwa imani yake kwangu kwa kuwa ameniteua mara mbili katika awamu hii. Kwanza kama Naibu Waziri wa Kilimo Chakula na Ushirika na baadaye Naibu Waziri wa Maji na Umwagiliaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nawashukuru pia viongozi wangu wa Chama Tawala na Serikali katika ngazi zote kwa ushirikiano na ushauri mkubwa walionipa hususan Makamu wa Rais - Mheshimiwa Dr. Ali Mohammed Shein, Waziri Mkuu - Mheshimiwa Mizengo Pinda, Mheshimiwa Spika, Naibu Spika, Wenyeviti wote kwa kazi nzuri ambayo mmeifanya hapa ndani kwa umahiri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kipekee kwa niaba ya wapigakura wangu wa Buyungu, namshukuru Mheshimiwa Rais kwa kukubali kuanzishwa kwa Wilaya mpya ya Kakonko na Tarafa mpya ya Nyaronga na kwa sababu hiyo Umoja wa Vijana wa Kakonko kupitia kwa Ndugu Masoud Ramadhani wameniomba nimpongeze Mheshimiwa Kikwete na kumwahidi kwamba baada ya kuchukua fomu wataendelea kumuunga mkono. Namshukuru sana kaka yangu Profesa Mark Mwandosya kwa jinsi anavyoendelea kuniongoza tangu tumekuwa pamoja. Kwa kweli kama mlivyosema, ninyi wote ni mfano wa kuigwa. Nawashukuru pia na watendaji wote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, namshukuru pia kipekee mke wangu Elisafina na watoto wetu, kwa uvumilivu wao, huko waliko najua wananiangalia, nasema poleni kwa kuni-*miss* kwa muda wote huu ninapokuwa huku. *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho lakini siyo kwa umuhimu, nawashukuru sana tena Wapigakura wangu pamoja na Madiwani wote wa Kata Tisa wa Jimbo la Buyungu. Kwa kweli mmenisaidia sana na ninaamini wote tutarejea tena katika ngwe inayofuata.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sasa kwa haraka niende katika hoja chache za Waheshimiwa Wabunge. Haitawezekana kabisa nikawataja Mbunge mmoja baada ya mwingine kama mnavyojua muda ni mfupi, lakini naomba nizungumze kwa ujumla na hoja nitakazozungumza sio zile tu ambazo zimechangiwa na Wabunge waliochangia siku ya leo. Mimi nitaangalia kwa ujumla waliochangia katika Bajeti ya Serikali, Hotuba ya Waziri Mkuu, Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika na leo kwa ujumla wake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka niahidi kwamba mawazo yote mazuri tumeyapokea na ushauri tutaufanyia kazi. Kwa ujumla, naomba nizungumzie uwezo au kujenga uwezo wa kitaasisi katika sekta zote mbili za Maji na Umwagiliaji. Jambo hili pia dakika chache zilizopita Mheshimiwa Dr. Chegeni amelizungumzia na mimi naomba nirudie kwa namna hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunatekeleza dhana ya *D by D* kwa maana ya kusogeza maendeleo na kusogeza madaraka katika ngazi za chini. Ni lazima tukubali kwamba uwezo uliopo pale tunahitaji kuujenga na lazima tuwe na mahali pa kuanzia. Kwa sababu hiyo, sisi katika sekta za Maji na Umwagiliaji kama ilivyo katika sekta nyingine tumeangalia ni mambo gani ya muhimu ambayo tunatakiwa tuyafanye ili kuwajengea wenzetu katika ngazi hasa ile ya Wilaya na Mkoa ili waweze kutekeleza miradi hii na pesa hizi ambazo tunapeleka kila mwaka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitaje mambo machache. Katika sekta ya maji kuanzia mwaka 2006 tuliamua kuajiri kila Halmashauri ya Wilaya ipate Mhandisi mmoja. Lengo lilikuwa ni kuhakikisha kwamba Halmashauri hizi zinapata watalaam ambao wanaweza kutusaidia katika kutekeleza miradi hii ambayo tunasukuma fedha nyingi kupeleka katika ngazi ya Wilaya. Lakini pia kama vile haitoshi, tumeamua kwamba ofisi zetu za Mabonde ambazo wote mnazijua, tuchukue mafundi sanifu 198, tuwaondoe katika ofisi hizi tuwapeleke kusaidia kusukuma kazi katika Halmashauri zetu zile za Wilaya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile tumeamua kwamba tuandae ikama ili kila Halmashauri ya Wilaya ipate nafasi ya kuajiri watalaam wengine 28. Kwa maana nyingine tunataka kila Halmashauri iwe na uwezo wa kuwa na watalaam 28. Hapa ni katika kujenga uwezo wao. Baadaye tumeona Wabunge wengi wamekuwa wakihoji kwamba kwa nini Idara ya Maji haina nafasi katika ngazi hiyo, naomba niseme kwa ufupi tu kwamba suala hili lipo mikononi mwa Wizara ya Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa inazishughulikia na ninaamini baada ya muda sio mrefu Idara hii itapewa hadhi katika ngazi ya Halmashauri ya Wilaya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kimkoa pia kama mnavyojua tumekuwa na Watendaji. Watendaji hawa wapo katika sekretariati, lakini tumeamua kwamba mara nyingi tumekuwa na Mtendaji mmoja katika Mkoa, kwa hiyo, tumeona afadhali tuongeze watu hawa wawe watatu ili tuwe na nguvu kidogo ya watendaji katika ngazi hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wote mmeshuhudia siku za karibuni kwamba Halmashauri zetu tumezipatia vitendea kazi, tumezipatia magari, vifaa vya ofisini na Halmashauri 61 tayari zimeshapewa magari yale ambayo yameandikwa Programu za maji na nyingine zilizobaki zote tunatarajia mwisho wa Mwezi huu zitapata kwa sababu tayari yapo Wizarani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sekta ya Umwagiliaji. Tuna upungufu mkubwa wa vitendea kazi. Wanaotakiwa katika sekta hii ya Umwagiliaji ni Watumishi 706, waliopo ni Watumishi 162. Bado tunahitaji watumishi 544. Tumeangalia mifano katika nchi nyingine kama India wao walichofanya ni kubadili mitaala katika Vyuo vyao, na sisi tunataka tufanye hivyo katika Vyuo vyetu vya ndani na Vyuo Vikuu. Chuo chetu kwa mfano cha Arusha, tunataka kibadili mitaala kiweze kutoa Wahandisi wa Umwagiliaji, Chuo cha Maendeleo na Usimamizi wa Maji nacho kifanye hivyo na kwa upande wa Mafundi Sanifu, pia Chuo chetu cha Kilimo cha Igurusi kitaendelea kutoa watalaam kama kilivyokuwa kinafanya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa ufinyu wa muda, naomba niende mbio. Naomba nizungumzie suala ambalo navutwa tu kulisema ambalo Waheshimiwa Wabunge wamelizungumzia katika hotuba zilizopita kuhusu sera ya umwagiliaji. Hata leo asubuhi niliona Msemaji wa Kambi ya Upinzani, sijui ni Waziri Kivuli, naye alitaka kulisema lakini baada ya kujua kwamba nimeshalisema alikwepakwepa.

Ndugu zangu tumepitisha sera hii na Serikali pamoja na Bunge tulifanya Semina tukaipitisha mwezi wa pili, lakini katika Taarifa ya Kambi ya Upinzani wamesema tumeendesha bila sera. Sijui maana yake ni nini, lakini naomba mrejee basi. Pengine mimi nilisema kwamba labda huu ni ubishi tu lakini baada ya msemaji kusema amekubali kwamba kweli sera ipo, amebadili tu akasema imechelewa kuja. Basi kawia ufike, tumekwishafika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilitaka niseme kwamba suala la Umwagiliaji kufikia ekari laki sita ambayo imezungumziwa sana, mimi naomba niliseme hivi kitaalamu, ukifikisha ekari laki sita kwa *cropping intensity* ya mara mbili tu utapata ekari milioni moja na laki mbili. Kwa hiyo, unakuwa umevuka, hatuangalii tu ile *horizontal development* kwenda mbele ekari milioni moja, ukishafika ekari laki tatu ukilima mara mbili tayari umeshafika hapa kwa hiyo, ile nyingine inakuwa ni ziada. Hii inajibu zile hoja chache ambazo wenzetu walikuwa kidogo wakizibeza kwamba tunakwenda bila kuwa na malengo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niseme mafanikio kidogo ambayo tayari tumekwishayapata. Kama nilivyosema, lengo siyo kuongeza tu maeneo ni pamoja na kuongeza tija katika uzalishaji. Ipo mifano mizuri katika miradi kadhaa ya umwagiliaji na

niseme tu kwa mfano Mpunga umeongezeka kutoka tani mbili mpaka tano katika *scheme* za umwagiliaji za huko Katengera, *Lower* Moshi, Igomero, Mbarari na kwingineko. *(Hapa kengele ililia kuashiria muda wa mzungumzaji kwisha)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, umenidhulumu, lakini naomba niseme naunga mkono hoja hii na mengine Waziri ataendelea kuyafafanua jinsi tutakavyoendelea, na mengine tutayajibu kwa maandishi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI**: Ahsante sana Naibu Waziri wa Maji na Umwagiliaji - Mheshimiwa Cristopher Chiza. Sasa naomba nimwite Mtoa hoja, Mheshimiwa Waziri wa Maji na Umwagiliaji Profesa Mark James Mwandosya.

**WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwa kutoa salamu za rambirambi kwa wananchi wa Wilaya ya Kyela. Wana-CCM wa Wilaya ya Kyela, hivi majuzi tulipotelewa na Mwenyekiti wa CCM wa Wilaya ya Kyela aliyefariki baada ya kuugua, naye sio Mwingine bali ni Ndugu yetu Japhet Mwakasumi. Nachukua nafasi hii kutoa pole kwa familia yake, Ndugu na kama nilivyosema wananchi pamoja na wana-CCM.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile jana tumepokea taarifa ya kifo cha Katibu wa CCM wa Wilaya ya Mbarali ambaye kwa jina maarufu tunamwita kwa Ba' George, kimetushtusha. Nawapa pole familia, ndugu na marafiki zake na wanachama wa CCM wa Mbarari, Kyela na Mbeya. Nimepokea vile vile kwa mshituko taarifa za kifo cha Mke wa rafiki yangu Emily Luyangi ambaye mke wake mpendwa amefariki baada ya kuugua. Natoa pole kwake, kwa familia yake, ndugu na marafiki wote. Mwenyezi Mungu azirehemu roho za Marehemu. Amen.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nawashukuru tena wananchi wa Rungwe Mashariki kwa kunichagua bila kupingwa mara mbili mfululizo. Ni heshima ambayo sikuitegemea. Ni heshima kubwa na kila wakati nimeipokea kwa unyenyekevu mkubwa, nimeahidi kwamba kwa kadri Mwenyezi Mungu atakavyonijalia afya njema, nitakuwa tayari kufanya kazi nao ili tuweze kuendeleza Rungwe, Mbeya na Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wengi waliofika Jimboni wamesema Jimbo limepiga hatua kubwa sana pamoja na Wilaya, tumekua kimaendeleo. Lakini niseme sifa hiyo siyo ya kwangu hata kidogo, ni sifa ya wananchi wa Rungwe Mashariki na ni sifa ya wananchi wa Wilaya ya Rungwe. Kwa upande wa Rungwe Mashariki wananchi hao wote ni kutoka Mpunguti mpaka Kapolampunguti, kutoka Ngeleka mpaka Bujingijira. Ninawashukuru sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nawashukuru tena familia yangu, watoto na wajukuu. Kama nilivyosema hapo awali, ni muhimili mkubwa katika maisha yangu ya kila siku na katika juhudi zangu za kulitumikia Taifa langu. Nashukuru ushirikiano mkubwa nilioupata kutoka kwa Waheshimiwa Wabunge, nilipokutana na Watendaji wenzangu

niliwaambia sifa zote ambazo Waheshimiwa Wabunge wametupatia na wanaendelea kutupatia sio zangu na Naibu Waziri.

Niliwaambia hizo sifa ni zenu Watendaji kwa sababu bila wao kwa kweli sisi tusingeweza kupata hizo sifa. Lakini nikawaambia vile vile kwamba moja ya sifa ya uongozi ni kuchukua lawama na kubeba mizigo. Nikawaambia lawama zote zinazotokana na utendaji ambao hauridhishi wa sekta ya Maji na Umwagiliaji, basi mimi na Naibu Waziri tunaubeba. Nawashukuru sana Waheshimiwa Wabunge. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama ilivyo ada na ninaomba saa isimame niwataje waliochangia katika hotuba hii. Nianze na wale ambao wamechangia kwa kuongea hapa Bungeni ambao walikuwa zaidi ya 21 nao sio wengine bali ni Mheshimiwa Janeth Z. Mbene kwa niaba ya Mwenyekiti wa Kamati ya Kilimo, Mifugo na Maji, Mheshimiwa Mhonga Said Ruhwanya - Msemaji Mkuu wa Kambi ya Upinzani, Mheshimiwa Ephraim Madeje, Mheshimiwa Peter Serukamba na Mheshimiwa Teddy Kasela-Bantu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wengine waliochangia kwa maandishi ni Mheshimiwa Ibrahim Msabaha, Mheshimiwa Ramadhani Maneno, Mheshimiwa Elieta Switi, Mheshimiwa Benito Malangalila, Mheshimiwa Felister Bura, Mheshimiwa Benson Mpesya, Mheshimiwa Prof. Raphael Mwalyosi, Mheshimiwa Magdalena Sakaya, Mheshimiwa Christopher Ole Sendeka, Mheshimiwa Dr. Zainab Gama, Mheshimiwa Zabein Mhita, Mheshimiwa Dr. Raphael Chegeni, Mheshimiwa Hamza Mwenegoha, Mheshimiwa kaka yangu Athumani Janguo, Mheshimiwa Lucas Selelii na Mheshimiwa Mhandisi Christopher Chiza. Nawashukuru sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, waliochangia kwa maandishi ni wengi pia, kwa kweli inaelekea kama rekodi za *Hansard* itakuwa ni kitabu kabisa cha Maji na Mwongozo wa Maji Tanzania. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, waliochangia kwa maandishi wapo 68, nitawataja wote kama ifuatavyo:- Mheshimiwa Magale John Shibuda, Mheshimiwa Dr. Mary Nagu, Mheshimiwa Mwanawetu Said Zarafi, Mheshimiwa Janeth Massaburi, Mheshimiwa Bakari Shamis Faki, Mheshimiwa Dr. Omar Mzeru Nibuka, Mheshimiwa Halima Kimbau, Mheshimiwa Athuman Janguo, Mheshimiwa Godfrey Zambi, Mheshimiwa Mwadini Abbas Jecha, Mheshimiwa Diana Mkumbo Chilolo, Mheshimiwa Dr. Luka Siyame, Mheshimiwa Dr. Samsoni Mpanda, Mheshimiwa Dr. James Msekela, Mheshimiwa Felix Kijiko, Mheshimiwa Jacob Shibiliti, Mheshimiwa Nimrod Mkono, Mheshimiwa Mkiwa Kimwanga, Mheshimiwa Lucas Lumambo Selelii na Mheshimiwa Mbarouk Kassim Mwandoro. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wengine ni Mheshimiwa Prof. Raphael Mwalyosi, Mheshimiwa Charles Mwera, Mheshimiwa Prof. Philemon Sarungi, Mheshimiwa Paschal Degera, Mheshimiwa Mwantumu Mahiza, Mheshimiwa Hemed Mohammed Hemed, Mheshimiwa Job Yustino Ndugai, Mheshimiwa Basil Mramba, Mheshimiwa Khadija Salum Ally-Qassmy, Mheshimiwa Ali Khamis Seif, Mheshimiwa Mohammed Missanga, Mheshimiwa Charles Kajege, Mheshimiwa Ephraim Madeje, Mheshimiwa Dr. Guido Sigonda, Mheshimiwa Salim Hemed Khamis, Mheshimiwa Bernadeta Mshashu,

Mheshimiwa Dr. Festus Bulugu Limbu, Mheshimiwa Shally Raymond, Mheshimiwa Zaynab Vullu, Mheshimiwa Sevelina Mwijage, Mheshimiwa Katagira, Mheshimiwa Elietta Switi, Mheshimiwa Teddy Kasella-Bantu, Mheshimiwa Christopher Ole-Sendeka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wengine ni Mheshimiwa Abdul Jabir Marombwa, Mheshimiwa Siraju Kaboyonga, Mheshimiwa Bujiku Sakila, Mheshimiwa Magdalena Sakaya, Mheshimiwa Ruth Msafiri, Mheshimiwa Clemance Lyamba, Mheshimiwa Gaudance Kayombo, Mheshimiwa Al-Shaymaa John Kwegyir, Mheshimiwa Martha Mlata, Mheshimiwa Dr. Ibrahim Msabaha, Mheshimiwa Paul Lwanji, Mheshimiwa Halima Kimbau, Mheshimiwa Juma Killimbah, Mheshimiwa Dr. Raphael Chegeni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wengine ni Mheshimiwa Samwel Chitalilo, Mheshimiwa Devota Likokola, Mheshimiwa Castor Ligallama, Mheshimiwa Archt. Fuya Kimbita, Mheshimiwa Wilson Masilingi, Mheshimiwa Ania Said Chaurembo, Mheshimiwa Juma Said Omar, Mheshimiwa Prof. Maghembe, Mheshimiwa Sijapata Nkayamba, Mheshimiwa George Simbachawene, Mheshimiwa Juma Said Omar, Mheshimiwa Gaudentia Kabaka na Mheshimiwa Mathias Chikawe wa mwisho lakini si kwa umuhimu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba vile vile kama iwapo nitakuwa nimemsahau Mbunge yeyote itakuwa ni kwa bahati mbaya. Wakati nikiendelea kufanya majumuisho, naomba yale majina ambayo sijataja waniwie radhi, lakini nikipata nafasi nitawataja hapa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, muda ni mfupi kama tulivyojipangia sisi wenyewe. Kwa hiyo, nitafanya majumuisho yangu katika maeneo makubwa matatu kama yalivyo kwenye *program* ya maendeleo ya sekta ya maji, raslimali za maji vijijini na maji mijini. Lakini yote haya kwa kweli ni utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi.

Badala ya kumjibu Mheshimiwa Mhonga Ruhwanya kwa yale aliyoyasema, nimeona niorodheshe mambo 21 ambayo kwa kweli ni mafanikio yaliyopatikana katika utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi wa Chama cha Mapinduzi. Nitataja machache. Lakini yaliyobaki nitaomba yaandikwe katika *Hansard* kama rekodi ya kikao hiki kwa sababu ya muda.

Kwa upande wa huduma ya maji safi na salama, imeongezeka kutoka asilimia 53.7 mwaka 2005 mpaka asilimia 58.7. Kwa upande wa mijini asilimia 78 hadi asilimia 84. Kwa upande wa visima tumechimba visima 2,871, tumeweza kuchimba mabwawa 25 ambayo tumejenga na tumekarabati mabwawa 15. Kamati za Maji zimefikia 12,000, fedha za Mfuko wa Maji zimeongezeka za wananchi wenyewe kufikia bilioni tatu; Bodi za Maji zimetoka 67 mpaka 86; vyombo vya watumiaji maji vimetoka 121 mpaka 235; vikundi vya watumiaji maji vimeongezeka kutoka 7,200 mpaka 11,600; ujenzi wa mradi mkubwa wa maji wa Ziwa Victoria, Kahama umekamilika na unaendelezwa, ujenzi wa awamu ya pili ya Chalinze ambao utahusu vijiji vingine 48 umeanza, mradi wa

uboreshaji wa maji safi na maji taka Jijini Dar es Salaam Awamu ya Kwanza umekamilika, mabomba tumelaza zaidi ya kilomita 1,200.

Magati jumla ya 490, Dar es Salaam tumejenga vituo vya kuchotea maji na tumeunganisha wateja zaidi ya 65,000. Mabomba ya majitaka umbali wa kilomita 46.7. Miradi 322 ya kuvuna maji tumetekeleza katika Wilaya 22. Tumepitisha sheria za raslimali maji za maji na vile vile sheria za huduma za maji na usafi wa mazingira. Tumeongeza fedha za umwagiliaji kutoka shilingi bilioni 6.7 mwaka 2005 mpaka shilingi bilioni 54.4 mwaka huu. Eneo la umwagiliaji limeongezeka kutoka 264,000 kufikia 331,000.

Tumeandaa Sera ya Taifa ya Umwagiliaji, wakulima 2800 wamepewa mafunzo ya kilimo cha umwagiliaji. Wataalam 250 wamejifunza mafunzo ya umwagiliaji. Vituo 25 vya kuhamasisha teknolojia mpya za umwagiliaji vimeanzishwa. Jumla ya vikundi 210 vya umwagiliaji vimeundwa na uzalishaji wa mazao umeongezeka kama alivyoeleza Mheshimiwa Naibu Waziri. Katika umwagiliaji katika kipindi cha miaka mitano tumejenga mabwawa makubwa 24 ya umwagiliaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningekuwa na muda wa kutosha ningeeleza zaidi. Kwa hiyo, badala ya kwenda kuzungumzia kuhusu takwimu, nimeona nitoe haya mafanikio ya utekelezaji wa Ilani ya Chama cha Mapinduzi. *(Makofi)*

Lakini pamoja na hayo, namshukuru Waziri Kivuli, amejitahidi sana kufafanua yale waliyoyaona na kwa kweli aliwasilisha hoja yake kwa ufasaha sana. Kwa hiyo, hatutayapuuza yale yaliyomo tutayazingatia mbele ya safari yale ambayo tunayaona yana kitu ndani yake kama ilivyo kawaida yetu. Hatujawapuuza hata kidogo. Kwa hiyo, nimeona nianzie na hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu raslimali za maji, maji ni uhai na ili uhai uwe endelevu, basi tutunze vyanzo, hili limesisitizwa. Tuvitunze dhidi ya uhalibifu wa mazingira na uchafuzi. Hilo tutaendelea kuwajibika kama Serikali. Lakini vile vile kila mwananchi anawajibika kutunza maji. Hilo ni wajibu wake wa kiuraia. Lakini vile vile nasema ni wajibu wa kiroho maana yake maji ni uhai. Wajibu mkubwa wa vyama vya watumiaji maji Serikali, Uongozi wa Kata na Halmashauri sehemu zote nchini ni kutunza vyanzo vya maji.

Viwanda visiwe wachafuzi wa maji. Sheria za raslimali maji na sheria za mazingira zinawahusu sana. Mchafuzi hulipia gharama katika dhana ya *polluter pays* hiyo ni dhana muhimu sana ya msingi. Basi niseme tu kwamba haya ndiyo yaliyojitokeza kwenye raslimali za maji hayakuwa mengi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye upande wa maji Vijijini nipitie haraka haraka tu ule mradi wa Vijiji kumi. Mimi nasema hapa na nasisitiza mradi umeanza. Lakini kama nilivyosema, kuanza kwa mradi matayarisho ndiyo magumu. Lakini kutekeleza kuchimba mitaro ni kutengeneza matanki, hiyo ndiyo kazi rahisi ya utekelezaji wa miradi. Lakini maandalizi awali ni makubwa na yamefanyika. Halmashauri 129 kati ya 132 tayari zimepata ridhaa ya Benki ya Dunia kusaini mikataba. Halmashauri tatu

zilizobaki, mbili hizo ni Singida na Kilosa ambazo karibu Benki ya Dunia itatoa maamuzi.

Lakini Halmashauri ya Manispaa ya Musoma vile vile Vijiji vyake vimeingizwa katika kutekelezwa programu ya maji mjini ya Musoma. Kwa hiyo, tumekamilisha karibu asilimia 100. Kati ya hizo, sita Halmashauri ziko katika hatua za awali za utafutaji wa vyanzo vya maji. Tayari 12 zimepokea ripoti za awali, 45 zimeainisha kazi za kufanya, Halmashauri 19 zimeandaa zabuni za uchimbaji wa visima vya majaribio. Halmashauri 17 zimetenga tayari, zimeshatangaza zabuni. Wote mnaona kwenye magazeti siku hizi zabuni za uchimbaji visima. 13 tayari zimeshapata wazabuni na wakandarasi wameanza kazi. Karibu Halmashauri mbili za Hai na Babati wenyewe tayari hata michoro ya usanifu imeshafanyika, zabuni zimetangazwa na ujenzi unaanza. Kwa hiyo, huu mradi wa Vijiji kumi umeshaanza jamani. Jumla ya Vijiji itakuwa ni 1517 na vitahusu watu tukitekeleza watu milioni 5.4 watapata maji salama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini maeneo mahususi yaliyochangiwa na Waheshimiwa Wabunge hapa ndani ni haya yafuatayo:- Kuhusu Kijiji cha Pwaga maji yapo, mradi unafanya kazi. Ujenzi na ukarabati wa tanki moja na ujenzi wa matanki mawili mapya. Vile vile mfumo wa usambazaji maji. Leo hii tumecheki na Wilaya ya Mpwapwa maji yapo.

Kuhusu Kashwasa kulikuwa na uharibifu, yaani ule mradi wa Kahama – Shinyanga kulikuwa na uharibifu, yaani ule mradi wa Kahama – Shinyanga kulikuwa na uharibifu katika Vijiji. Ilikuwa ni hujuma. Lakini hizi fedha ambazo zinasemekana zimepotea, sisi kwa rekodi ni milioni 58. Lakini hizi milioni 600 hatujui hata hizo takwimu zimetoka wapi.

Kuhusu Mto Tigite, naomba kusema kwamba bado hatujatoa kibali cha kutupa majitaka kwenye mto. Bado tumekataa hatujaridhika. Kwa hiyo, bado mpaka waturidhishe, wale watu wa mgodi. Tumepima ubora wa maji wa Mto Tigite umerejea katika hali yake ya kawaida. Vyanzo vya maji vipya tumevitafuta na tumevibaini. Kazi inayofanyika sasa ni upimaji na usanifu wa miradi kama ifuatavyo:- kuboresha chemichemi nne, kujenga malambo saba, miradi saba ya maji ya mtiririko na kuchimba visima virefu 17 katika maeneo hayo kwa gharama ya shilingi bilioni 4.7. Tumeanza utekelezaji wake na tunaanza na uchimbaji wa visima virefu 17.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu Mzenga katika hotuba yangu Mheshimiwa Athumani Janguo naomba kueleza kwamba tumezingatia ushauri wako wa mwaka jana na mwaka huu. Tutakavyoendelea ni kama ifuatavyo:- Kuna Vijiji zaidi ya sita ambavyo viko katika baadhi ya Vijiji kumi katika uendelezaji wa Vijiji kumi. Tutaendelea kuchimba na uchimbaji wa maji chini ya ardhi kwa ajili ya kuvipatia Vijiji hivyo. Lakini Vijiji vingine tutakamilisha uchimbaji wa maji. Lakini sambamba na hilo tutaufufua huu mradi kwa kuanzia na kufanya usanifu kwa sababu uliharibika kabisa, nao tutautekeleza. Kwa hiyo, maeneo yale yatakuwa na maji chini ya ardhi. Lakini vile vile tutaanzisha mradi wa Mzenga tutaufufua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu maji Mufindi Kusini Mheshimiwa Benito Malangalila, ambaye ni Mhandisi, namshukuru sana, lakini vile vile ni mwanafunzi wangu Kitivo cha Uhandisi Chuo Kikuu cha Dar es Salaam. Kwa hiyo, huwa namsikiliza sana. Tumepokea ushauri tutashirikiana naye na Halmashauri ya Wilaya ya Mufindi na vile vile Halmashauri ya Wilaya ya Njombe kwa yale yote aliyoyasema.

Kuhusu maji mjini, tunawashukuru Wabunge, maana mmeainisha changamoto zifuatazo:- Upotevu wa maji, umuhimu wa ukarabati kuzuia upotevu huo, umuhimu wa dira na masuala mahususi yaliyojitokeza kuhusu Kahama Shinyanga, niseme tu kwamba nimeshaeleza kwamba hujuma iliyotokea imetugharimu shilingi milioni 58, wala siyo milioni 600. Lakini pamoja na hilo, tumelifanyia kazi hilo suala. Asilimia 45 ya mfumo wa usambazaji wa Shinyanga sasa ndiyo sehemu mpya. Kwa hiyo, bado tuna asilimia 65 ya mfumo wa zamani. Mradi mpya unahitajika, gharama yake itakuwa shilingi bilioni 14 tutatekeleza mradi huu kupitia Mpango wa Maendeleo wa Sekta ya Maji.

Kuhusu Maji Soga namshukuru sana ndugu yangu Dr. Ibrahim Msabaha, nawashukuru wananchi Soga kwa mapokezi waliyonipa na kushirikiana na mimi nilipofanya ziara. Niseme kwamba tumebaini katika Kijiji cha Dengwa kwamba itabidi tutoe maji kwa kaya 25. Mheshimiwa Dr. Ibrahim Msabaha, asiwe na wasiwasi alale na moyo mkunjufu atulie tu. Dengwa tunapeleka maji, tumeanza leo hii, itachukua wiki moja kila mtu pamoja na yeye watapata maji. *(Makofi)*

Kuhusu mradi wa Wachina uliozungumzwa na yeye lakini vile vile na Mheshimiwa Dr. Zainab Gama hasa tulianzia na mita 30. Mheshimiwa Dr. Ibrahim Msabaha tunashukuru na wananchi wanamshukuru akasema ongezeni mita 20 tukaongeza. Sasa anataka tuongeze mita 20 nyingine 70 tumeishiwa hela. Niseme tu kwamba katika yale maeneo ambayo yamo katika mita 50 lakini hawajapata maji, haya yataangaliwa kutoka eneo mpaka eneo. Katika maeneo ambayo yako nje mita 50 na hili linaoana na suala lile kwamba nje ya mita hizo sehemu nyingi hazijapimwa. Kwa hiyo, inakuwa ngumu sana kuweka mabomba makubwa ya maji. Lakini hatutawasahau, tutajenga magati kuwapatia wananchi maji ndiyo jukumu letu. Fedha tunazo kupitia mfuko wa kuunganisha wateja wapya. Mfuko huo unasimamiwa na *DAWASA* na *DAWASCO*. Kwa hiyo, naomba watulie tu sisi maji tutawapelekea wananchi hao, wala hatujawabagua. *(Makofi)*

Kuhusu Vikawe tutatekeleza mradi wa kupeleka maji Vikawe mwaka 2010/2011 kupitia mradi wa *MCC,* tunauita sisi ni *package number 2(f)* zabuni itatangazwa mwezi Julai.

Kuhusu Moshi maji mjini upande wa Upinzani umezungumzia kuhusu kesi iliyo mahakamani kwa hiyo, sitakwenda kwa undani kuhusu kesi yenyewe inayomhusu Mkurugenzi Mtendaji wa Mamlaka hiyo. Lakini niseme tu, Bodi ndiyo mamlaka ya nidhamu. Imetumia mamlaka iliyonayo chini ya Sheria ya *Employment and Labour Relations Act* baada ya kuridhika kwamba kuendelea kuwepo kwake hapo hakutaathiri uendeshaji wa shirika. Hayo ni mamlaka waliyonayo ndani ya sheria mpya. Sheria ya zamani ilikuwa inasema ilimradi kesi imefikishwa Mahakamani, basi wasimamishe.

Lakini sheria mpya ilikuja badala yake imeipa *discretion* Bodi na mamlaka ya nidhamu. Kwa hiyo, hakuna lililopotea hapa.

Kuhusu Mbeya, Mheshimiwa Benson Mpesya tumezingatia ushauri wako kuhusu eneo la Vijiji vya Itagano na Ihango Mbeya Mjini na Mbeya Vijijini. Usanifu umezingatia huo ushauri, chanzo ni kimoja, bomba kuu litakuwa moja, matoleo yatakuwa mawili kwenda kwenye sehemu ya Kijiji kimoja na upande wa pili na utekelezaji utatekelezwa na wakandarasi wawili tofauti. Lakini maadam chanzo ni kimoja na bomba kuu moja, basi tunauchukulia ule mradi kama ni mradi mmoja. Kwa hiyo, tunamshukuru sana kwa ushauri huo. *(Makofi)*

Kuhusu dira kwa wale wanaotumia maji kwa ajili ya biashara hasa matofali, napenda kumhakikishia Mheshimiwa Benson Mpesya kwamba hakuna mtu ambaye ataambiwa atoe fedha *flat rate* kwa ajili ya matumizi ya kutumia maji kwa ajili biashara kama ana dira. Dira yenyewe ni kidhibiti kinafaa kabisa. Kwa hiyo, hilo nataka kusisitiza tena haitawezekana na kama yupo mtu ambaye ameambiwa ana dira na atoe fedha, basi tunaomba tupate taarifa hizo ili tuweze tukazifanyia kazi. Kama nilivyosema dira yenyewe ni udhibiti, kinachobadilika ni *tariff* tu. Tukiona kwamba huyo mtu anafanya biashara, basi gharama zake zitakuwa kubwa. Kwa hiyo, hilo ndiyo tutakalolifanya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakubaliana na Mheshimiwa Serukamba kuhusu maji Kigoma, tumekubaliana siku nyingi wote inatuuma sana hasa sisi watu wa maji. Kwa maji yapo pale Kigoma lakini wananchi wanakosa maji. Ni ile Waingereza wanasema *is an iron,* lakini kwa kweli ni changamoto kwetu sisi ya maendeleo. Ametulinganisha sisi na nishati. Mimi ningekuwa na jenereta moja inatengeneza maji safi, kazi yangu ni kuinunua tu kuipeleka Kigoma na kuitengenezea *base* au kitako na kuwapa watu maji, ningefanya hivyo. Lakini maji ni tofauti kidogo na umeme. Lakini tunakwenda sambamba. Tunaendaje? Mpango wa muda mfupi unahusu marekebisho yatakayoleta matokeo ya haraka, ununuzi wa pampu, ununuzi wa *transformer* yote haya tunayatekeleza. Hivi juzi tu tumepeleka fedha kwa ajili ya ununuzi wa *transformer* ya *KV KVA* 1500 hasa baada ya huu mradi mpya wa umeme. Mpango wa muda wa kati kwa Kigoma tunautekeleza kupitia mpango wa maendeleo ya sekta ya maji. Tutajenga chujio pale Kigoma, tutafanya ukarabati mkubwa, tutapanua mtandao, Mhandisi Mshauri ameshateuliwa Saureka. Mradi utagharimu shilingi bilioni 10, utatekelezwa kwa muda mfupi, lakini utakidhi mahitaji ya Kigoma baada ya miaka 2015. Zabuni hii karibu tunaitangaza. Mradi wa muda mrefu wa Kigoma uko kwenye *ACPEU Water Facility* wa Miji saba ambayo ni pamoja na Kigoma, Sumbawanga, Mtwara, Lindi, Babati, Bukoba na Musoma. Kwa ajili ya mahitaji ya Kigoma mpaka mwaka 2030 tayari Mhandisi Mwelekezi amepatikana Polly Mjerumani kuhusu mradi wa Maji Safi, Maji Taka, usanifu utaufanya na vile vile atatayarisha zabuni kwa ajili ya utekelezaji. Mradi wa ziwa Tanganyika wa Hifadhi na Usimamizi na Mazingira nao umetenga fedha kwa ajili ya Maji Taka kwa ajili ya Kigoma. Kwa hiyo, Kigoma hatujaisahau.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu Simanjiro, Mheshimiwa Ole – Sendeka nimefika. Mheshimiwa Waziri Mkuu amefika, unaposhuka kwenda chini kule ambako wananchi na mifugo wanapata maji huwezi ukashindwa kuguswa na suala la maji

Simanjaro. Labda sijui uwe na moyo mgumu namna gani. Kwa hiyo, tuko na wewe pamoja na wananchi wa Simanjiro. Tulikubaliana mwaka jana tukatoa shilingi milioni 200, visima vitatu vimepatikana. Tutatangaza zabuni ya miundombinu kama alivyoomba mwanzo wa mwezi Julai kwa ajili ya mfumo wa upatikanaji maji, matanki na mfumo wa usambazaji pamoja na *viosk*. Kwa hili, pamoja na vile vile eneo la Mbauti au eneo la maji kwa ajili ya mifugo.

Kazi hizo zitahusu vile vile kutafuta maeneo ya kuchimba visima vya ziada. Lakini mradi mkubwa tutautekeleza, nathibitisha hivyo. Mradi mkubwa ni wa kuchukua maji kutoka Mto Pangani. Usanifu umekamilika, gharama zake zinakisiwa kuwa shilingi bilioni 23. Michoro tayari iliyobaki ni kutangaza zabuni. Tutatangaza zabuni wakati tukiendelea kutekeleza huu mradi wa kati hapa. Tumefanya mambo mawili, *BADEA* wametuomba tupeleke miradi ya ziada ya maji na huu ni mmoja wa miradi ambayo tumeipeleka. Lakini umo vile vile katika Mpango wa Maendeleo ya Sekta ya Maji. Kwa hiyo, naomba kuthibitisha kwamba tutatekeleza huu mradi pamoja pamoja na utekelezaji wa mradi wa dharura huu wa kuwapatia maji wananchi wa Simanjiro. Nathitibisha tena kwa hilo.

Tutafanya hivyo, tunajua suala la Simanjiro na Kibaya linafanana sana. Kibaya tutakachofanya siyo kitu kibaya, hapana kwa ajili ya Mji wa Kibaya tutakachofanya ni kuwa na zabuni kama ya Simanjiro na tutaitoa karibu mwezi mmoja, mwezi ujao ili kuweza kuangalia yale maeneo ambayo tunaweza tukaleta matokeo ya haraka na ya dharura. Fedha tunazo, fedha tumezipanga tutatekeleza kwa maana ya *encasement* pamoja na Kibaya.

Mheshimiwa Dr. Raphael Chegeni yote aliyoyazungumza tutayazingatia, Mheshimiwa Lucas Selelii tutayazingatia na naahidi hivyo. Sasa muda wenyewe hautoshi waliozungumza ni wengi na ni mambo mengi sana, ninachoweza kuahidi ni kwamba yote haya tutayatolea maelezo na kuweka pamoja katika kitabu ambacho tutakisambaza kabla hatujamaliza mkutano huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuhitimisha nimepata nukuu zifuatazo za hekima kutoka kwa Waheshimiwa Wabunge kama fedha zinazotengwa katika sekta ya maji na umwagiliaji ziongezwe, tuelekeze nguvu zetu katika fedha zetu za ndani, maji Dar es Salaam ni muhimu, hakuna kilimo bila maji, tuchimbe mabwawa mengi madogo madogo yenye gharama nafuu, tuimarishe utaalamu na utendaji wa ofisi za maji Halmashauri, maeneo yenye ukame yapewe kipaombele na maji tunayapata kwa taabu yasiishie njiani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimalizie kwa maneno ya matumaini aliyoyatoa Mheshimiwa Rais juzi alipokuwa akichukua fomu, hakuzungumzia Bajeti ya sekta yoyote ile isipokuwa alizungumzia maji siku ile na akatoa ahadi kwa wananchi kwamba katika kipindi chake cha awamu ya pili anasema kuanzia mwaka 2011/2012, Bajeti ya sekta ya maji kwa maana ya maji na umwagiliaji itapanda maradufu, amewaambia wananchi hadharani. *(Makofi)*

Nilipokuwa katika ziara ya kikazi Ikwiriri nilipitia kwenye mradi mkubwa wa umwagiliaji ambao tulitekeleza kwa msaada ya Serikali ya Iran sasa hauendelei. Niliahidi tutaufufua na tumeuingiza katika programu ya mwaka 2010/2011, tumetenga shilingi milioni 250, Ikwiriri. Taratibu zitaanza mwaka huu kwa maana ya utekelezaji, lakini mimeutaja mradi huu kutokana na maneno ya msingi sana, mimi nasema ni maneno ya kiroho kuhusu maji, sasa yaliandikwa kwa kiarabu kwa hiyo, mimi naamini ninukuu ya Msahafu Mtakatifu lakini chini yake kuna maneno ya Kiswahili yafuatayo na nanukuu; “Tumefanya kila kitu kuwa hai kutokana na maji.” Mwisho wa kunukuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naafiki. *(Makofi)*

*(Hoja iliamulia na Kuafikiwa)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana, Mheshimiwa Waziri wa Maji na Umwagiliaji, hoja imetolewa na imeungwa mkono, sasa kwa hatua inayofuata. Katibu.

## KAMATI YA MATUMIZI

## MATUMIZI YA KAWAIDA

### Fungu 49- Wizara ya Maji na Umwagiliaji

Kifungu 1001- *Administration and General*… … sh. 2,722,196,000/=

**MHE. MICHAEL L. LAIZER:** Mheshimiwa Mwenyekiti, *program 10, sub-vote 1001*, mshahara wa Waziri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilitaka tu kupata ufafanuzi katika hotuba yake ukurasa wa 13 alizungumzia mabwawa 24 ambayo ni ya umwagiliaji, akataja na bwawa la Kisirian ambalo ndio la kwanza, Kisirian - Longido.

Hilo bwawa ni kweli lipo lakini halijakamilika, limechimbwa na kuna vifusi vikubwa vilivyoko ndani ya bwawa, hakuna miundombinu ya kuonesha kwamba ni bwawa la umwagiliaji, sasa nilitaka kupata ufafanuzi, *Engineer* Chiza analifahamu vizuri sana hilo bwawa kwamba halijakamilika, ningependa kupata ufafanuzi, je, hilo bwawa litaachwa hivyo hivyo au litakamilishwa na Mheshimiwa Waziri sikusikia akitaja Longido na Longido ni moja kati ya maeneo kame ambayo yana shida ya maji kuliko vijiji vyote Tanzania.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Laizer tulizungumza takribani siku mbili zilizopita kuhusu bwawa hili la Kisirian na mimi mwenyewe nalifahamu vizuri, najua yako mambo machache sana yamebaki hasa hayo ya kusawazisha hivyo vichuguu na nimemuahidi Mheshimiwa labda nisisitize tu kwamba nimeshamwambia Mhandisi wa Kanda waende waangalie hizo kazi

zilizobaki wala hazina hata haja kusema tungoje, tutatafuta Bajeti ya mwaka mwingine tutaangalia tutekeleze.

**MHE. WILSON M. MASILINGI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana, programu namba 10, *sub vote 1001*, mshahara wa Waziri, sihitaji mshahara wa Waziri ni utaratibu wa Kibunge tu kuutaja ni halali yake ataupata. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninachoomba ni ufafanuzi kuhusu suala la kisera ambalo sisi kwa tafsiri yetu huko Muleba ya Kusini na katika mchango wangu wa maandishi nimetoa mfano wa miradi ya Nshamba ambayo zamani ilikuwa inakarabatiwa, Kashalunga na Kibanga. Katika taratibu ambazo unakuta wataalamu wanang'oa mabomba, wanatoa kitongoji kimoja kupeleka kingine, wanabomoa hapa wanamimina hapa, sasa hatujui tatizo ni utaalamu au ubadhilifu na ninavyofahamu Wizara ya Maji na Umwagiliaji ina wataalamu wazuri sana hata Katibu Mkuu ni Mhandisi, Waziri mwenyewe Mhandisi, sasa mimi tangu nilipoeleza suala hili la matatizo ya huko na namshukuru Mheshimiwa Waziri alifika Nshamba siku ya Maji ya Kitaifa akawafurahisha wananchi kwa kuonesha kwamba hadanganyiki na ikaelekea kwamba naye ameona ubabaishaji.

Sasa karibu miezi kama mitano inapita, sasa nilikuwa naomba kama ni TAMISEMI, Mheshimiwa Waziri Mkuu yuko hapa, Waziri Kombani yuko hapa, kama tatizo ni nani asimamie la kisera wanipe ufafanuzi, nani atakwenda? Nimetoka huko jana mchana nimewahi Dodoma hapa kusema haya ya wananchi na wananisikiliza. Sio mbali hawawezi kwenda kabla mwisho wa mwezi huu wakaangalie kulikoni, nani anaagiza kusafirisha mabomba, hili tatizo ni wahandisi au ni kandarasi au huyu *contractor* au nini? Nilitaka tu ufafanuzi, aseme neno moja tu na watu wa kule na wenyewe wafurahi maana yake nimeona hotuba zake zinafurahisha watu hapa. Lakini mimi sijafurahi hata kidogo. *(Makofi)*

**WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, neno moja ni kwamba tumemsikia, neno la pili tutazingatia, neno la tatu kwa kiingereza wanasema *the backs stops here* maana yake *the backs stops the Ministry of Water and Irrigation*. Kwa hiyo, pamoja na utekelezaji ngazi ya Halmashauri lakini tunaoguswa nikitaja maji basi mahali penyewe ni Wizara ya Maji. Kwa hiyo, tutazingatia hayo na tutafuatilia kwa ajili ya utekelezaji, ahsante. *(Makofi)*

**MHE. CHRISTOPHER O. OLE-SENDEKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, niko kwenye *vote* hiyo hiyo na programu hiyo hiyo iliyotajwa na kwa maana hiyo kwanza nitumie nafasi hii kusema bayana kwamba baada ya maelezo ya Mheshimiwa Waziri wa Maji, Mheshimiwa Profesa Mark Mwandosya kuhusu kutambua tatizo la maji Wilayani Simanjiro na haswa Orkesmet na kutueleza sasa kwamba hatua iliyofikiwa ni kutangaza zabuni ili kuweza kupata mzabuni wa kuvuta maji kutoka Ruvu kupitia Loiborsiret kuja Orkesmet na kwamba wewe kama ninavyojua tulikaa mimi, wewe na Waziri Mkuu mkaelewa tatizo langu la kupata fedha za dharula kwa ajili ya maji ya maeneo yale.

Sasa kwanza nibainishe wazi nina unga mkono hoja yako ambayo nilikuwa sijaiunga mwanzoni, lakini la pili baada ya kuunga mkono hoja niseme bayana kwamba

nimuulize Mheshimiwa Waziri kwa kuwa tatizo hili la maji la Wilaya ya Simanjiro linafahamika kwa upana wake na sio maeneo tu ya Orkesmet ukizingatia kwamba kuna eneo maarufu sana la Mererani ambalo kuna maji pale *Kilimanjaro International Airport* ambayo yangeweza kuvutwa, kuna kisima cha maji ambacho kimechimbwa pale Naisinyai kwa ajili ya kijiji cha Mishe na Losoito ambayo kazi yake ni kuweka *pipe* na kupeleka huko juu nyuma ya migodi.

Je, Mheshimiwa Waziri atakubaliana kwamba imefika wakati wa kufanya utafiti wa kutosha ili kuwafanya Watanzania hawa walioko Simanjiro waweze kuwa na makazi ya kudumu kwa muda wote wa mwaka kwa kuhakikisha kwamba tatizo lao linafahamika na wataalamu na mpango mahususi unaandaliwa kwa ajili ya kupunguza adha hii ya maji. Nilitaka Mheshimiwa Waziri atubainishie kama jambo hili linaweza likafanyiwa utafiti na Wizara yake inaweza ikasaidia kuondoa adha hii baada ya kwamba ameelekeza kwamba kuna fedha kidogo atakayotusaidia kwa ajili ya miradi ile ambayo tunapata maji lakini miundombinu yake bado?

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana. *(Makofi)*

**WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyosema wakati wa majumuisho labda uwe mtu wa aina gani sijui ushindwe kuguswa na matatizo ya maji ya eneo lolote ambalo zamani lilikuwa linaitwa *Masai Step* kuanzia Longido, Ngorongoro mpaka Simanjiro mpaka maeneo haya karibu na Kongwa huku ni jambo linalokugusa. Kwa hiyo, anayosema ni kitu ambacho tumekichukua na sisi ndio kazi yetu na tutafurahi kuifanya hivyo kuwa na mpango kabambe wa maji Simanjiro na Kibaya na vile vijiji katika hizi Wilaya mbili. Kwa hiyo, tutalifanya hilo na tutazingatia vile vile maji katika eneo lenye wakazi wengi sana, eneo la machimbo ya Mererani. *(Makofi)*

**MHE. LUCAS L. SELELII:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Kwanza mimi nina malalamiko, makatibu wako pale wamenipunja dakika zangu, mimi nimeanza kuzungumza saa 11.49 jioni, saa 12.00 jioni wamenigongea kengelele, nangoja hasa…*(Makofi/Kicheko)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Selelii, unakamata mshahara wa Waziri kwa saa ya Katibu? Twende kwenye hoja tafadhali. *(Makofi)*

**MHE. LUCAS L. SELELII:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kifungu hicho hicho 1001, mshahara wa Waziri.

Katika mchango wangu niliozungumza na hata kwenye maandishi nimeeleza bayana na kukubali na kutamba juhudi ambazo Serikali wanazifanya kukabiliana na tatizo la maji lilivyo kubwa. Kwa mfano, mradi mkubwa wanaoufanya sasa hivi ni wa *World Bank* ambao unachukua vijiji kumi kwa kila Wilaya. Wilaya ya Nzega ina vijiji 150 kwa hiyo, ukichukua vijiji 10 kwa kila Wilaya, kwangu Nzega, kwa Wilaya ya Nzega itachukua miaka kumi na tano kuondoa hili tatizo. *(Makofi)*

Sasa mimi nimependekeza kwa nini tusifanye kama tulivyofanya kwenye elimu ya msingi, kwenye elimu ya sekondari na kwenye afya tukawa na mpango maalum, tuuite MMA ili hili tatizo hili la maji liweze kuondoka, Waziri bahati mbaya hakupata muda wa kueleza basi ningependa kupata maelezo kwamba je, hili linakubalika kwa kiwango gani ili tatizo hili tuweze kuliondoa kwa haraka na mapema.

**WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nianze kwa kumshukuru Mheshimiwa Lucas Selelii kwa maana ya maji Nzega tumefanya nae kazi kwa karibu sana mjini pamoja na vijijini, ni kweli kazi inayotungoja ni kubwa sana, vijiji ni vingi sana lakini kama nilivyosema pamoja na hilo huu mpango wa vijiji kumi ambao kama nilivyosema ni vijiji zaidi ya 1,500 ni mpango mkubwa ambao haujawahi kutekelezwa Kusini mwa Sahara. Hili wametutibitishia Benki ya Dunia hivi juzi tulivyokuwa tunajaribu kupata taarifa za utekelezaji wa mradi huo kwamba ni mradi mkubwa kweli na wao kama Benki ya Dunia hawajawahi kutoa fedha kwa nchi yoyote ile kwa fedha kiasi hiki kwa ajili ya utekelezaji wa maji vijijini, sasa nchi ni kubwa lakini niseme tu kwamba pamoja na wafadhili hawa na mpango wa vijiji kumi, fedha nyingi zaidi zinatekelezwa nje ya vijiji kumi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukisikia kwa mfano upande wa Kisarawe kwa Mheshimiwa Athumani Janguo kuna *Plan International* ambayo inatekeleza miradi mingi sana, basi ukienda utakuta kuna *Caritas, World Vison,* kuna wafadhili wengi sana, madhehebu ya dini kila aina. Ni mradi mkubwa tena utekelezaji wake fedha nyingi zaidi kuliko hizi za miradi kumi.

Kwa hiyo, naomba tu twende pamoja, sisi tunauchukulia utekelezaji nje ya vijiji kumi kama sehemu ya utekelezaji wa mpango wa sekta ya maji. Kwa hiyo, mpango tunao ila hatuna neno la kifupi kama *MEM* au *MES*, sisi kwa kiingereza tunaita *WSDP*, sasa kwa Kiswahili tukasema Mpango wa Maendeleo ya Sekta ya Maji tulishindwa kupata kifupi chake lakini Mheshimiwa Selelii mpango huo tunao. Ahsante. *(Makofi)*

**MHE. MARTHA M. MLATA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Na mimi pia niko kwenye *sub –vote* hiyo ya 1001 kifungu kile cha mshahara wa Waziri

**MWENYEKITI:** Nenda moja kwa moja kwenye hoja, najua mmesimamia hiyo.

**MHE. MARTHA M. MLATA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati nachangia kwa maandishi nilikuwa nimeiuliza Serikali kwamba ina mpango gani sasa hasa katika Wilaya ya Iramba pamoja na Wilaya mpya ya Mkalama kwamba kuna mito mingi ambayo hii mito ni ya majira na kwamba kuwe na programu ya mabwawa ya umwagiliaji katika maeneo haya ili kuwasaidia wananchi waweze kuwa na kilimo cha umwagilaji kwa msimu wote na pia nikawa nimeomba kwamba katika maeneo yale ya Chikuyu, Wilaya ya Manyoni na maeneo mengine ambayo yana kilimo cha umwagiliaji kuyajengea mabwawa kwa sababu yanakuwa ni ya msimu mmoja tu na tunahitaji kwamba walime kwa wakati wote, lakini sikupata majibu. Nilikuwa naomba ufafanuzi. Ahsante. *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, labda niseme tu kwamba hatukupata muda kwa kweli, muda ulikuwa mfupi kama mlivyoona mpaka nikasema Mwenyekiti umenidhulumu lakini sikuwa na maana hiyo ya kunidhulumu. Lakini ilivyo ni kwamba mimi mwenyewe nimepita huko Iramba, Mkoa wote wa Singida huko Kina Mpanda na kila mahali na hiyo mito anayoizungumza nimeiona, ukija kwenye maeneo haya ya Chikuyu, Chilonwa, Chimenderi, Chikopero, Manyoni, Chipanga, kote huko anakosema Mheshimiwa Martha Mlata anapajua. Lengo letu ni kwamba maeneo haya ambayo wanavuna maji kwa njia ya majaruba tutafute fedha, tuwajengee mabwawa ili wakati mvua inapokatika basi waweze kupata maji ya kumwagilia na kama alivyosema Mheshimiwa Waziri kwenye Fungu lile la mfuko wa kuendeleza umwagiliaji katika ngazi ya Wilaya *(DIDF)* tumeongeza kiwango kutoka shilingi milioni 500 mpaka shilingi milioni 800. *(Makofi)*

Kwa hiyo, sasa tumeelekezana na Wahandisi na Mkoani, mimi nimekwenda kule Singida wataandaa programu nzuri kwa ajili ya miradi hiyo. Naomba Mheshimiwa Martha Mlata anielewe hivyo. Tutatekeleza kama alivyoomba. *(Makofi)*

**MHE. SULEIMAN O. KUMCHAYA:** Ahsante Mheshimiwa Mwenyekiti, kifungu hicho hicho programu 10, *sub-vote 1001*.

**MWENYEKITI:** Nenda kwenye hoja tu moja kwa moja ili kuokoa muda.

**MHE. SULEIMAN O. KUMCHANYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninasimama hapa kwa tatizo la maji katika Jimbo la Lulindi ambalo ni la muda mrefu tangu Waziri akiwa Mheshimiwa Shukuru Kawambwa, Mheshimiwa Shemsa Mwangunga na leo Mheshimiwa Profesa Mark Mwandosya, ninalizungumza katika Bunge hili na hata mazungumzo ya kawaida kati yangu mimi na Mawaziri hawa yamekuwa yakiendelea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatizo la maji katika Jimbo la Lulindi ni kubwa. Vyanzo vya maji vipo, hasa Chiwambo. Mheshimiwa Profesa Mwandosya alinishauri nini cha kufanya ili chanzo cha maji cha Chiwambo kianze kufanya kazi na kitoe maji kwa ajili ya Lulindi, Sindano, Chiungutwa, Mchauri na maeneo mengine. Juzi nilipokuwa nachangia hapa hotuba ya Waziri Mkuu niligusia hili na nikasema mradi wa maji wa Chiwambo utasaidia sana kupunguza tatizo la maji ama utaongeza nguvu katika mradi wa maji wa Mbwinji. Lakini nimesoma katika hotuba yake hii ukurasa wa 86 Nachingwea - Masasi sijaona kitu chochote kuhusu Chiwambo pamoja na ahadi ya mwenyewe Mheshimiwa Waziri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuwaonee huruma wale watu wanapata taabu sana. Naomba Mheshimiwa Waziri alitolee kauli ili wananchi wale wawe na matumaini. Wamepata taabu sana kwa muda mrefu sana. Ahsante sana Mheshimiwa Mwenyekiti. *(Makofi)*

**WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, inasaidia sana kutembea nchini kwa sababu vijiji vyote alivyovitaja nimevipitia. Kwa hiyo, ninalifahamu, na naelewa tatizo la maji. Kuhusu chanzo cha maji cha Chiwambo

tumezungumza na ninathibitisha Mheshimiwa amelifuatilia sana. Sasa naomba nimrejeshe kwenye hotuba yangu lakini siyo kwenye mradi wa Nachingwea – Masasi, lakini kwenye eneo la sehemu ya maji vijijini. Nilipokuwa nataja maeneo ambayo Serikali itasaidia Halmashauri katika kusanifu na kutekeleza miradi ya maji vijijini nje ya vijiji kumi, leo asubuhi nimeitaja Chiwambo. Tumeitengea fedha kwa mwaka 2010/2011. Namshukuru Mheshimiwa Mbunge. *(Makofi)*

**MHE. CLEMENCE B. LYAMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi. Kwa mtiririko ule ule wa *vote* na kifungu.

Napenda kutoa maelezo kwamba katika mchango wangu wa maandishi nilimwomba Mheshimiwa Waziri atoe ufafanuzi na kueleza ili wananchi wa Jimbo la Mikumi, Mji mdogo wa Mikumi waamini kauli kwamba Mheshimiwa Waziri aliahidi kutoa shilingi milioni 100 kwa dharura kuchimba visima virefu vinne katika mji mdogo wa Mikumi. Kwa kipindi kirefu katika mikutano nimekuwa nikiwapa matumaini wananchi kuhusu ahadi hii na ni kweli katika mwezi wa kwanza wa mwaka huu wataalam watatu walitumwa Mikumi kufanya utafiti wa uchimbaji wa visima vinne. Lakini pamoja na hayo wananchi wanaona kama ni matumaini ya kisiasa na wao hawawezi kunywa matumaini wanataka kunywa maji. Kwa hiyo, namwomba Mheshimiwa Waziri atoe kauli madhubuti kuhusiana na lini visima vinne vilivyoahidiwa vitachimbwa? Ahsante Mwenyekiti. *(Makofi)*

**WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahadi ya Serikali na kauli ya Waziri ndani ya Bunge na kwa Mheshimiwa Mbunge ni kitu ambacho naweza kukiita kwa Kiingereza *sacrow sancta.* Huwezi ukakifanya kwa kubabaisha tu, ni cha kutekelezwa, kama hatuwezi kutekeleza hatusemi, ndiyo maana tumewatuma wataalam Mikumi. Ripoti yao tutaiangalia mimi binafsi haijanifikia. Lakini kwa sababu mimi mwenyewe niliahidi na maadam bado nipo angalau hata baada ya Bunge kuahirishwa. Nadhani Baraza la Mawaziri linakuwepo kuwepo. Kwa hiyo, bado nina miezi michache ya utekelezaji na nitahakikisha kwamba visima hivyo vinachimbwa. Ahsante. *(Makofi)*

**MHE. MWANAWETU S. ZARAFI:** Ahsante Mheshimiwa Mwenyekiti. Katika swali langu la maandishi nilikuwa nimeuliza Serikali ina mpango gani kuhusu mradi wa maji ambao uko Kijiji cha Mpara. Mradi ambao kijiji cha Mpara, Wilaya ya Kilwa, mradi ambao umetelekezwa kwa muda wa miaka zaidi ya 10 ulikuwa unaendeshwa na wafadhili kutoka Finland. Mradi ambao chanzo chake cha maji kipo hapo Mpara na kina uwezo wa kutoa maji ya kutosha katika maeneo ya kijiji cha Mpara chenyewe, Kilwa Kivinje na kijiji cha Singino. Lakini hadi leo hii mradi huu haujakamilika. Kwa hiyo, mimi ningetaka kujua Serikali ina mpango gani hadi leo mradi huu haujakamiliki na ulikuwa umefikia karibu asilimia 80 kwa utekelezaji wake kwamba matanki yalikuwepo na mabomba yalishatandazwa. Tatizo lilikuwa ni umeme ambao nguzo pia ziliwekwa. Kwa hiyo, nataka tamko la Serikali kuhusu mradi huu. *(Makofi)*

**WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kama hauko katika vijiji 10 basi tutaangalia uwezekano wa kuufufua.

**MHE. SIRAJU J. KABOYONGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kifungu kile kile naomba ufafanuzi ufuatao. Matatizo ya maji ya Tabora yanahitaji kuongeza uzalishaji, kurekebisha mtandao kwa maana ya usambazaji na kuupanua. Halafu kujenga tanki lingine kubwa kule *Kaze Hill* na kurekebisha na kupanua mtandao wa maji taka, huu ndiyo mradi wa Tabora. Kwa ujumla unahitaji takribani dola milioni 25. *SEKO* wa Uswiss wameshabakiza dola milioni tano tu kwa ajili ya huu mradi mkubwa. Kwa hiyo, tuna pengo la takribani dola milioni 20, bila Serikali kuelezea namna gani hizi pesa zitapatikana, mradi wa kurekebisha matatizo ya maji Tabora ni *none starter*. Kwa hiyo, hizi dola milioni tano za Uswiss hazitoshi kurekebisha mfumo wa chujio kule Igombe peke yake wala hazitoshi kutengeneza mtandao ulioharibika. Ni lazima kuwe na pesa nyingine za kurekebisha kwenye mtandao na nyingine za kuboresha uzalishaji. Naomba ufafanuzi. *(Makofi)*

**WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Siraju Kaboyonga amesimamia suala la maji Tabora kwa nguvu zake zote. Sisi tunampongeza na analifahamu kwa dhati kabisa kwa sababu au ndiyo sababu tulimwomba awepo kwenye Bodi yetu ya Mamlaka ya Maji Tabora Mjini, tunamshukuru pia kwa hilo. Kuhusu utekelezaji wa mradi wa maji Tabora, tuna hatua tatu. Hatua ya kwanza ni kuendelea kutekeleza mradi unaoleta matokeo ya haraka pale inapobidi ambao unakwenda kwenye gharama ya shilingi milioni 100, milioni 200 kutatua tatizo la hapa na pale mambo yaendelee, kuchimba visima kuunga mkono juhudi zake za uchimbaji wa visima, tunamshukuru. *(Makofi)*

Pili, ni huo mradi aliousema ambao sisi tunasema ni wa muda wa kati. Ni wa muda wa kati wa kurekebisha mfumo wa maji Tabora na vile vile chanzo cha Igombe, *Kaze Hill* huko, tanki na mfumo wenyewe pale wa mabomba Tabora Mjini. Sasa tunajua kwamba hela za *circle* hazitoshi. Lakini tumuahidi kwamba popote ambapo tuna fedha za nje basi tuna sababu kubwa ya kutumia fedha zetu kuongezea pale ambapo zimekosekana. Kwa hiyo, sisi kwa maana ya utekelezaji wa Bajeti ya Wizara na programu ya maendeleo ya sekta ya maji sisi haitakuwa jambo kubwa sana kwa kuongezea fedha angalau twende kwenye kitu kimoja, tutekeleze sehemu ya chanzo ili fedha zetu zote za *circle* na za kwetu ziweze zikafanya kazi inayoonekana. La pili ni kuangalia zinazobaki tunakwendaje katika kufumua mfumo wa maji pale Tabora. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini la mwisho ambalo ni muhimu ni ahadi ya Mheshimiwa Rais kwa wananchi wa Tabora na Watanzania alipolihutubia Taifa kutoka Tabora siku ya Wanawake Duniani. Hapo alisema kwamba anatupa maelekezo tuangalie uwezekano wa kuleta maji Tabora kutoka mradi wa Kahama - Shinyanga kutoka Ziwa Victoria. Mimi huo nauona kama ni mradi wa kutatua la Tabora kwa miaka yote inayokuja, miaka niseme 50 au 100. Hili tutalitekeleza kwa dhati kabisa. *(Makofi)*

**MHE. JOHN P. LWANJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Mimi ningeomba nipate ufafanuzi kwamba katikati ya mwezi Mei Mheshimiwa Waziri Mkuu alitutembelea, alifika mji mdogo wa Itigi akiambatana na Mheshimwia Naibu Waziri wa Maji. Sasa pale aliahidi kwamba watafanya mpango wa kuweza kusambaza maji katika mji huo ili kuondoa hiyo kero. Ningependa kupata ufafanuzi kama ahadi hii ipo katika mpango wa Bajeti hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, halafu la pili, kwa muda mrefu, nafikiri miaka miwili tulipeleka maombi katika Wizara husika baada ya kushauriana kwa karibu sana kuhusu kuchimba mabwawa kijiji cha Sajaranda na Ngurungo na nikaambiwa nipeleke barua na barua hizo tulipeleka kama maombi. Ningependa kujua maombi hayo yamefikia wapi? Ahsante sana Mheshimiwa Mwenyekiti. *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli niliambatana na Mheshimiwa Waziri Mkuu, tulikwenda pale Manyoni. Mheshimiwa Waziri Mkuu alitoa maelekezo na hayo anayosema Mheshimiwa John Lwanji ndiyo maelekezo ambayo alitoa Mheshimiwa Waziri Mkuu. Sasa mahali ambapo Serikali yenyewe imesema Waziri Mkuu kwamba angalieni uwezekano wa kutatua matatizo haya basi sisi tuliyachukua hayo kwamba tunayafanyia kazi. Nataka nimhakikishie Mheshimiwa John Lwanji kwamba sisi kazi yetu sasa ni kutekeleza maelekezo yale aliyotupa Mheshimiwa Waziri Mkuu siku ile na mimi nilikuwepo na tutaendelea kuyafuatilia pamoja na wale walioko kule katika ngazi ile. *(Makofi)*

**MHE. PROF. RAPHAEL B. MWALYOSI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niwasilishe masikitiko yangu na kutokuridhika kwangu kuhusu ufanisi wa *Scheme* ya Umwagiliaji Maji Rifua, Ludewa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ufanisi wa mradi ule ambao ulikuwa ni mdogo tu ulikuwa uwe umeshakwisha. Lakini umechukua muda mrefu sana na mpaka leo haujakamilika kwa sababu ya ufanisi mdogo *(technical problem). Designs* zinaelekea zilikuwa na matatizo na nimelieleza hili kwa Mheshimiwa Profesa Mark Mwandosya na kwa Mheshimiwa *Engineer* Christopher Chiza, *no action* na sioni matokeo yoyote. Nimewaalika watembelee wakaone kule, hawajakwenda. Nataka maelezo. Lakini vile vile naamini tija ndogo inatokana na kwamba huu utaratibu wa kuwa Kanda. Katika Kanda wako Mbeya wanakuja kufanya kazi Ludewa, mbali sana. Lakini Bajeti ya Halmshauri na Bajeti ya Kanda hazioani, *project in take* iko porini kule. Kunatakiwa kuwe na *access road. Access road* ni kazi ya Halmashauri. Lakini ujenzi wa *in take* pale na mradi ni kazi ya Kanda. Unaoanishaje bajeti hizi mbili zioane kwamba barabara iwepo. Ndiyo maana Mheshimiwa Makamu wa Rais alipokuja alishindwa kwenda kuangalia mradi ule kwa sababu barabara ilikuwa haipitiki kwenda kwenye *in take.*

Mimi nauliza kwa nini fedha hizi zinazotengwa kupitia Kanda zisipelekwe moja kwa moja kwenye Halmashauri, Halmashauri zipewe wataalam wasimamie watu wa Halmashauri, wakipewa wataalam fedha yote ikae kule. Kwa nini inakaa mbali iletwe mpaka kule kwenye Halmashauri wakati hakuna uhusiano kati ya Taasisi hizo mbili. Ahsante sana.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la Lifua, kwanza naomba nikiri kwamba tumelizungumza kwa mara nyingi tu na Mheshimiwa Profesa Mwalyosi. Nakiri kwamba amenialika mimi mwenyewe na Mheshimiwa Profesa Mwandosya. Lakini pia kutokana na muda kubanana na ratiba hizi, mimi nakiri kwamba hatujapata nafasi ya kwenda pale. Lakini hiyo siyo sababu, kwa sababu pamoja na kukosa huo muda wa kufika pale niliweza kuagiza watendaji katika Wizara, wahandisi wamekwenda pale na nilimuahidi kwamba wangenipa taarifa kwamba ni nini hasa kilichotokea katika mradi huo. Wameshaniambia kwamba kulikuwa na matatizo katika *design* na ni matatizo ambayo yanarekebika na jana nilikuwa naongea na Mhandisi wa Kanda wa Umwagiliaji, *Engineer* Kweka, kwa sababu nilitarajia Profesa utaniuliza na amenihakikishia kabisa kwamba wamekwishaangalia yale yote, mapungufu yaliyokuwepo katika mradi ule, yatarekebishwa na yatafanyiwa kazi. *(Makofi)*

Lakini tukija kwenye fedha, huu usimamizi wa miradi ya umwagiliaji nilieleza hapa ni muda tu nilikosa. Nimesema tunajaribu kujenga uwezo katika ngazi, kwa kweli hatuna Wahandisi wengi wala siyo wengi, hatuna Wahandisi katika ngazi ya Wilaya, tuna wataalam wachache sana, wengine ni mafundi sanifu. Kazi za Uhandisi zinataka Mhandisi asimamie *design* na asimie *construction.* Huwezi ku-*delegate* kazi za Uhandisi kwa mtu ambaye wa fani ile. Sasa hicho ndicho kinatufanya sisi tuweze kufanya kazi kwa utaratibu huo, vinginevyo tungependa kabisa Wahandisi hawa tuwapeleke mpaka ngazi ile. Ndiyo maana nimetamka katika maelezo yangu ya awali kwamba tuna upungufu wa wataalam na tunafanya sasa utaratibu kuhakikisha kwamba vyuo vyetu vya ndani viwasomeshe Wahandisi ili tu-*bridge* hiyo *gap.* *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, la mwisho kuhusu hizi barabara, mimi nataka niseme hivi *farm to markets to roads*, hizi ni sehemu za mradi, ni *package* ya mradi. Kwa kawaida tuki-*design* mradi mkubwa kama ule *farm to market to road* ni sehemu ya mradi na kama haikuwekwa basi ni kama *oversight* tu. Ni mambo ambayo tunatakiwa kuyarekebisha. Kwa hiyo, naomba niendelee kumhakikishia kwamba yale yote yaliyojitokeza kama mapungufu, tumeyaona na tutajitahidi kuyarekebisha. *(Makofi)*

**MHE. NIMROD E. MKONO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kuniona. Katika mchango wa kimaandishi nilisema siridhiki kabisa na utendaji wa kazi upande wa maji kuhusu ahadi kubwa tatu alizofanya Mheshimiwa Rais wakati wa kugombea. Miradi hiyo mmoja wao ni Wegelo. Lambo la Wegelo ambalo liko sehemu ya Kiagata sehemu ambayo kwa kweli hakuna maji. Limejengwa kwa kulipuliwa lipuliwa hivi tu mpaka sasa ukienda huko wananchi wanatukana, hawaridhiki kabisa na utendaji wa kazi pale. Hilo lambo la Wegelo kwa nini Mheshimiwa Waziri angalau apite pale aone walivyotapeli?

La pili ni kuhusu mradi wa siku nyingi sana wa kule Butiama, Mheshimiwa Waziri amekuwa anatembelea sehemu hizi, mara nyingi anaona pale kijijini hamna maji, hospitali haina maji, wanajeshi wanaokaa pale pia hawana maji, lakini sioni chochote kinachoendelea. La mwisho kabisa ni sehemu ya Bugwema, kwa miaka 40 au 35 hivi walichimba wakaweka mtambo wa kumwagilia maji, eneo kubwa. Hiyo mitambo bado

ipo, wanajeshi wakaenda pale, baadaye wameondoka, inaonekana watu wamepewa tena mashamba pale, Serikali imekimbia imeacha wazi. Hakuna maji, hakuna shamba, hawa wananchi tuwaambiaje?

**WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, namshukuru sana kaka yangu na ndugu yangu, yeye anajua undugu wetu, Mheshimiwa Komredi Nimrod Mkono, kwa kufuatilia kwa karibu sana maendeleo ya Musoma Vijijini, Mara na Tanzania nzima. Kuhusu bwawa la Wegelo, tunakiri mapungufu lakini ni mradi unaoendelea, ujenzi haswa umeanza mwaka 2009/2010, bado katika Bajeti ya mwaka 2010/2011 Tumeuweka na matarajio yetu ni kwamba tutaukamilisha katika kipindi cha fedha cha mwaka 2010/2011. Tutazingatia yote ambayo ameyasema tunapoendelea kufanikisha ujenzi huo kabla hatujauzindua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu Bugwema, bahati nzuri nimetembelea hapo mahali na ni miundombinu ambayo kwa kweli imesanifiwa vizuri sana wakati ule wa Mwalimu na ninachoweza tu kumuahidi ni kwamba Bugwema, mradi ule tutaufufua na juhudi hizo zitaanza katika mwaka 2010/2011. Amezungumzia kuhusu matatizo ya maji katika baadhi ya maeneo ambayo nilimsikiliza kwa makini lakini sikuweza kupata vile vijiji vyenyewe. Lakini Mheshimiwa Mkono, unajua kwamba sisi akitueleza kwa kweli tutazingatia na kama hatuwezi sisi wenyewe kwenda. Lakini naomba kwa sababu hivi karibuni tunakwenda, Mheshimiwa Rais, atazindua bwawa la Manchira na mradi wa maji wa Mugumu na njia mojawapo ya kufika huko ni kupitia Jimbo lake, basi namuomba baada ya hapa anipe hayo maeneo. Nadhani Mwenyezi Mungu akitujaalia na nafasi ikipatikana, ni mambo ambayo naweza nikayafanya wakati ninakwenda kwenye kuhudhuria uzinduzi huo kabla au baada. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba apokee hilo kama ni jibu la yale aliyoyasema. Ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Kifungu hicho kinakubaliwa?

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

Kifungu 1002 *Finance and Accounts*………………sh. 896,354,000/=
Kifungu 1003 *Policy and Planning*…………………sh. 1,447,285,000/=
Kifungu 1004 *Information, Education and*
Communication……......................................................sh. 159,854,000/=
Kifungu 1005 *Legal Services Unit*……………………sh. 276,112,000/=
Kifungu 1006 *Procurement Management Unit*…sh. 566,571,000/=
Kifungu 1007 *Management Information System*...sh. 251,071,000/=
Kifungu 1008 *Internal Audit Unit*……….……………sh. 217,192,000/=
Kifungu 2001 *Water Resources Assessment &*
*Exploration*……...............................................................sh. 3,408,721,000/=
Kifungu 2002 *Central Stores*…………….…………sh. 190,452,000/=
Kifungu 2003 *Water Laboratory*…………………..…sh. 764,235,000/=
Kifungu 2004 *Directorate of Irrigation and*

*Techn. Services* …......................................................sh. 2,572,830,000/=
Kifungu 3001 *Urban Water Supply and Sewerage*………..sh. 2,045,846,000/=

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

Kifungu 4001 *Rural Water Supply*…………………sh. 1,993,389,000/=

**MHE. MAGDALENA H. SAKAYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, *sub-vote* hiyo 4001, kifungu kidogo cha 410700, *Feasibility Study, Project Preparation and Design;* kifungu kinahusu usambazaji wa maji vijijini na bado tunajua kuna miradi mingi ambayo inaendelea na mingine ambayo inatakiwa ianzishwe ili wananchi wa vijijini waweze kupata maji, lakini mwishoni hapa mwaka juzi ilikuwa ni shilingi milioni 58, mwaka jana ni shilingi milioni 75 na mwaka huu ni shilingi milioni nne. Tunaomba tuulize ni kwa nini imepungua sana wakati mahitaji bado ni makubwa?

**WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, hicho ni kifungu ambacho kinatusaidia sisi Wizara, pale ambapo tunaombwa na Halmashauri kuweza kuwasaidia katika kurekebisha michoro, kufanya masahihisho ya usanifu na mambo ya namna hiyo. Ni kweli tulikuwa na shilingi milioni 75 mwaka uliopita, lakini mwaka huu kuna miradi mingi ambayo tulikuwa tunaisaidia kwa maana ya usanifu kwa mwaka ule, sasa iko katika hatua ya utekelezaji. Ni ile miradi mingi niliyoitaja, kwa hiyo, matarajio yetu ni kwamba sasa tutaelekeza nguvu zetu kutafuta fedha za kukamilisha yale ambayo tumetoa usanifu kupitia kile kifungu kuzisaidia Halmashauri. Kwa hiyo, ni kiasi cha kuelekeza nguvu zetu huko kwa sasa, lakini hizi milioni nne bado kifungu kinabaki na tunatarajia kwamba iwapo Halmashauri moja inaweza ikatuomba msaada, basi tunaweza tukawasaidia kwa kutumia kifungu hicho. *(Makofi)*

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

Kifungu 5001 *Water development and*
*Management Inst.* ………........................................…sh. 465,338,000/=
Kifungu 6001 *Drilling and Dam Construction*
*Agency*.……..............................................................…….sh. 465,339,000/=

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**MATUMIZI YA MAENDELEO**

**Fungu 49 – Wizara ya Maji na Umwagiliaji**

Kifungu 1001 *Administration and General*………sh. 7,107,664,000/=
Kifungu 1003 *Policy and Planning*…………………sh. 4,684,080,000/=
Kifungu 2001 *Water Resource Assessment &*

*Exploration*……......................................................…sh. 12,431,086,000/=
Kifungu 2003 *Water Laboratory*………....……….sh. 5,165,917,000/=

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

Kifungu 2004 *Directorate of Irrigation and*
*Techn. Services* ….....................................................sh. 16,890,898,000/=

**MHE. PROF. RAPHAEL B. MWALYOSI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mchango wangu wa maandishi, nilizungumzia juu ya mradi ambao sisi Ludewa tunauona ni wa muhimu sana…

**MWENYEKITI:** Kifungu tafadhali.

**MHE. ROF. RAPHAEL B. MWALYOSI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kifungu kipo kimoja tu, 4486, *Directorate of Irrigation and Technical Services.* Sasa nilielezea kwamba mradi ule ni muhimu sana kwetu, lakini unahusisha *about* hekta 1,000 za *irrigation* kwenye *semi-arid area* ambako kila wakati watu wana njaa. Matumaini ya kutatua tatizo hilo wapate *irrigation project.* Lakini kupata kibanio, ni lazima kuweka bwawa kwenye Mto Ruhuhu, ambapo kuna kivuko ambacho hakifanyi kazi *most of the time*. Kwa hiyo, tuliamua kujenga daraja kubwa ambalo vilevile litakuwa ni kibanio na Mheshimiwa Rais, alipotembelea kule Mbinga, tulikuwa pale kwenye kivuko na aliahidi kwamba kwenye Ilani ijayo hii ni lazima itekelezwe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilitaka kujua *progress* kwa sababu niliandika barua kwenye Wizara hii, niliandika barua kwenye Wizara ya Miundombinu, washirikiane na Wizara hizi mbili pamoja na mikoa miwili ya Ruvuma na Iringa wafanye haraka, wajenge daraja lile, zipatikane fedha wajenge. Sasa nataka kujua *progress to date* tumefikia wapi? Kwa sababu tunahitaji huu mradi uanze mara moja. Ahsante.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, hili daraja kwenye Mto Ruhuhu na bwawa analolisema Mheshimiwa Mbunge, linahusisha Wizara takribani mbili kiutendaji, Wizara ya Maji na Umwagiliaji na Wizara ya Miundombinu. Baada ya kuwa Mheshimiwa Rais, alitoa maelekezo kwamba mradi huu utekelezwe, Wizara zote mbili tumekaa pamoja ili kuangalia sasa ni mambo gani ya kiuhandisi yanatakiwa yafanyike, maana mradi ule ni mkubwa si mdogo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hatua tuliyoifikia sasa tumeandaa hadidu za rejea kwa ajili ya mtaalamu atakayeangalia usanifu wa shughuli nzima. Kwa hiyo, kazi hiyo sio kwamba imesimama, tunaingalia kwa pamoja sisi Wizara ya Maji na Umwagiliaji na Wizara ya Miundombinu. Naomba labda kwenye wakati muafaka mimi mwenyewe ikiwezekana tukae na Mheshimiwa Profesa Mwalyosi, tuweze kumuelewesha ni wapi tumefikia sisi Wizara mbili. *(Makofi)*

**MHE. JUMA H. KILLIMBAH:** Mheshimiwa Mwenyekiti, na mimi nipo katika *sub-vote* hiyo hiyo ya 2004, *item number 4486.* Katika *item* hii inazungumzia juu ya miradi ya *ASDP* na kwa bahati nzuri tunapozungumzia hii Kurugenzi ya Umwagiliaji, kule Jimboni kwangu kuna miradi mitatu ile ya Ndandala, mradi wa Masimba na mradi wa Timemasagi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, historia ya miradi hii na ninaamini Mheshimiwa Waziri anajua na hasa Naibu Waziri, atakuwa na uelewa zaidi juu ya miradi hii.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa tusaidie upate ufafanuzi, usitupe historia, kwa sababu muda utakuwa hauruhusu.

**MHE. JUMA H. KILLIMBAH:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ningeomba kwa sababu bado nina dakika na bila kujenga hii bado hawezi kupata picha kamili. Kwa hiyo, kwa sababu nina dakika, ungeniacha ili niweze kuelekeza vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa ninachotaka kusema ni kwamba katika miradi hii mitatu niliyoizungumza na hapa ninaona kuna fedha zilizotajwa, hizi shilingi bilioni 16 na miradi hii imeshatumia pesa nyingi sana na kuna ahadi nyingi ambazo Serikali imeshaahidi kwamba miradi hii itakamilika. Je, sasa Waziri anataka kunipa ufafanuzi gani kuhusiana na miradi hii ambayo nimeitaja? Ahsante.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, miradi hii ya umwagiliaji, yote anayoisema ya Mlandala, Timemasagi na ule mwingine yote ni ya umwagiliaji. Kilichojitokeza katika miradi hii ya mkoa wa Singida, ni kwamba wao hawakuwa wametumia fursa ile ya fedha zinazotokana na mfuko ule wa umwagiliaji katika ngazi ya wilaya *(District Irrigation Development Fund)* na mwaka uliopita nilipowatembelea, nilipata muda wa kuongea na uongozi wa mkoa, nikawashauri, nikawaambia sasa ni lazima watumie fursa hii. Na kwa kweli mwaka huu wamejitahidi, miradi yote hii wameiweka katika mpango na wameiombea fedha. Sasa unapoomba fedha ambayo hukuwahi kuiomba mapema, huwezi kutarajia itengewe fungu wakati huo huo na fedha hizi zinatolewa na zile Wizara kiongozi za sekta ya kilimo, ambazo si Wizara moja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini nina uhakika kabisa kwa kazi ambayo imeshafanywa na mkoa wa Singida, sasa hivi miradi hii inayo nafasi na itapata fedha kwenye *DIDF* na ikizidi zaidi zitaingizwa kwenye *NIDF.*

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

Kifungu 3001 *Urban Water*
*Supply and Sewerage*…..........................................sh.111,610,391,000/=

**MWENYEKITI:** Nawaona Mheshimiwa Dr. Raphael Chegeni, Mheshimiwa Omari Kwaangw' na Mheshimiwa Hamza Mwenegoha, lakini labda kabla sijampa mchangiji wa mwanzo, itabidi nitumie kifungu cha Kanuni ya 104(1), ili tutumie muda.

Tunaweza tukafika saa 1.45 usiku tukawa bado hatujamaliza hizi shughuli, kwa hiyo, nitazidisha muda usiozidi nusu saa ili mpaka tutakapomaliza hizi shughuli tunazoendelea nazo. Sasa Mheshimiwa Chegeni, unaweza ukaendelea.

**MHE. DR. RAPHAEL M. CHEGENI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi naomba ufafanuzi kidogo sana. Katika jiji la Mwanza, kuna Mto Mirongo; mto huu unakuwa unaleta taka ngumu na taka nyingine ambayo inatoka mlimani inakwenda kwenye Ziwa Victoria, matokeo yake inaleta uchafuzi mkubwa sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilitaka kufahamu tu kwamba pengine kupitia Bajeti hii, Serikali ina mpango gani wa kudhibiti taka ngumu kuingia kwenye Ziwa Victoria na kutoendelea kuchafua mazingira na maji ya Ziwa Victoria.

**WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la kuzuia uchafuzi wa maji machafu yanayoingia Ziwa Victoria pamoja na taka ngumu, ni suala mtambuka ambalo tunalishughulikia sisi kama Wizara ya Maji kwa maana ya usimamizi wa Ziwa Victoria na mito, lakini vilevile viwanda kwa maana ya kuhakikisha kwamba maji taka kutoka viwandani yanakidhi viwango ambavyo vinatolewa na sisi sekta ya maji. Lakini vilevile na mazingira, Ofisi ya Makamu wa Rais Mazingira kupitia *NEMC,* kuhakikisha kwamba hizo taka hazifiki kabisa katika Ziwa Victoria. Tuna mradi wa *LEVEMP* ambao ni mradi wa hifadhi ya mazingira ya Bonde la Ziwa Victoria ambao sasa awamu ya pili imeanza na masuala yote haya tunayashughulikia kupitia Jumuiya ya Afrika Mashariki, hasa Kamisheni ya Ziwa Victoria. Kwa hiyo, hilo tunalizingatia na tutaendelea kulizingatia na huo mto tutaufuatilia. Ahsante.

**MHE. OMARI S. KWAANGW':** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye *sub-vote* hiyo hiyo ya 3001, Kifungu kidogo cha 3306, ukurasa wa 102 pale, *Rehabilitation and Expansion of Urban Water Supply.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilitaka tu Mheshimiwa Waziri, anipe ufafanuzi kwamba kwenye miradi hii tunaona fedha ipo na hata mwaka jana kulikuwa na fedha za kutosha kutoka kwa wafadhili na mwaka huu vilevile zipo za kutosha, kuna karibu shilingi bilioni 57 pale. Sasa nilitaka kuuliza tu kwamba wakati tunapopita kwenye miradi, nilipokuwa natembelea miradi pale babati wakandarasi wanalalamika kwamba hawalipwi fedha kwa wakati; na nina uhakika bila ya shaka fedha zitakuwa ni hizi hizi, sijui labda ataniambia nini? Lakini nataka ufafanuzi kwamba hawa wakandarasi, tunapowacheleweshea fedha zao, basi na miradi ndio inachelewa na mimi nimeona, nashukuru hapa kwenye Bajeti kwa Mji wa Babati, wanampongeza Waziri, kwenye ukurasa wa 77 ametaja vizuri na miradi inaendelea vizuri; lakini wakandarasi wanalalamika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hebu tupate *position* ya hizi fedha za kigeni, hizi ambazo zinatoka kwa wahisani, tatizo lake ni nini? Ahsante.

**WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI:** Sijui kama nitamridhisha ndugu yangu Mheshimiwa Omari Kwaangw' kwamba kudaiwa vilevile ni kiashiria cha kigezo

cha maendeleo kwa sababu usipodaiwa maana yake hutekelezi miradi ukadaiwa maana yake unatekeleza miradi mingi, shilingi bilioni 50 hazitatosha kutekeleza na kulipa madeni. Kwa hiyo, tuendelee hivyo hivyo wasikilize, watie moyo, tukipata tunawapa ili mradi tunakamilisha miradi yetu, lakini kwamba tutaweza kupata hela zote tunazozihitaji kwa wakati ule lakini naomba tuvumilie, wakandarasi wametuvumilia na yeye awe balozi wetu huko awatie moyo kwamba kidogo kidogo fedha zinakuja. Ahsante.

**MHE. HAMZA A. MWENEGOHA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru mimi naomba *sub vote 3001, item 3438, Kidunda Dam Construction* mwaka huu umepata *forex Tanzanian shillings three billion*, lakini katika mchango wangu niliyemuomba Waziri atupe maelezo maana yake hata hii shillingi bilioni tatu itafanya kazi gani na muda mrefu tulikuwa tunaomba maelezo hatupati, sasa labda msingekuwa na haja najua ameshindwa kupata muda kunipa maelezo hapa lakini sasa hii nafasi yangu naomba atoe maelezo niliyoyaomba katika mchango wangu.

**WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Hamza Mwenegoha kwanza namuomba atuwie radhi kwamba tumekwenda katika jimbo lake na kukagua miradi yeye mwenyewe hakuwepo, ilikuwa ni mawasiliano kati ya ofisi zetu, hatuwezi kuwalaumu wale walio chini ni kwamba tulitegemea kwamba mawasiliano haya yangekufikia ama kupitia mkoa au wilaya ambao lazima unapata ziara za Waziri au moja kwa moja toka ofisi zetu lakini kwa bahati mbaya hazikufika. Zuri ni kwamba na sisi tumefika kwenye eneo hili na tumepita na bahati nzuri tukakagua na vijiji vyote ambayo vinatekeleza mradi wa maji wa awamu ya pili ya mradi wa Chalinze lililo katika jimbo lake kwa hiyo, tumefaidika labda tungepita eneo lingine tusingeweza kuona hiyo miradi. Kwa hiyo, ni kama tulifanya kazi mbili kwa wakati mmoja.

La pili ni kuhusu kusema kwa uhakika kuhusu mradi wa Kidunda ili wananchi wa Morogoro watusikie, ni kwamba tayari tumeshampata mhandisi mshauri, sasa tumempata amesha-*mobilize* yuko kazini tulitarajia kazi zake zingechukua miezi tisa lakini tunafikiri Kidunda ni kazi kubwa, matarajio yetu ni kwamba kazi ya usanifu michoro na kuandaa zabuni pamoja na tathimini ya athari kwa mazingira na kijamii yote haya yatachukua karibu mwaka mzima wa 2010/2011. Pamoja na hiyo wataandaa na makabrasha ya zabuni na utekelezaji matarajio yetu ni kwamba utaanza mwaka 2011/2012 kwa uhakika. *(Makofi)*

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

Kifungu 4001 *Rural Water Supply*………………….sh. 75,502,571,000/=

**MHE. GEORGE B. SIMBACHAWENE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa nataka tu niombe ufafanuzi mdogo kutoka kwenye Fungu hili nakumbuka mwaka 2008/2009 wakati wa Bajeti ya Wizara hii nilielezea sana juu ya mkakati wa Serikali juu ya kufufua mabwawa yale makubwa yaliyojengwa enzi za zamani za mkoloni ambayo yalikuwa ni vyanzo muhimu sana vya maji katika shughuli za kilimo na matumizi ya

binadamu na wanyama. Lakini katika *vote* hii hapa imezungumziwa habari ya *borehole drilling and dams construction* na shughuli zake nadhani ni za jumla, nilitaka kufahamu tu kama Mheshimiwa Waziri atanipa ufafanuzi juu ya suala kama inahusisha na lile bwawa la Uyezele lililoko katika jimbo la Kibwake Tarafa ya Ludi ili niweze kufahamu ni shughuli gani itafanyika kwa sababu bwawa lile ni muhimu sana kwa ajili ya ukombozi ukizingatia Dodoma tuna hali ngumu sana ya uchache wa mvua, mimi naamini kabisa bwawa lile kwa sababu ya ukubwa kama litatumika kama lilivyotumika zamani basi lingeweza kutusaidia sana, naomba sana ufafanuzi kama katika mpango huu na katika fedha hizi linaweza likaangaliwa bwawa la Uyezele lililoko jimbo la Kibakwe. *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nadhani Mheshimiwa Mbunge hapa kidogo anachanganya mambo, hili Fungu la *Management Support to Local Government Authorities* ni Fungu la ku-*support local government authorities*. Sasa bwawa la Uyezele analolizungumzia ni bwawa lililoko hapa Mpwapwa na mimi nalifahamu lilibomoka, tulijenga zamani miaka ya 1970 likabomoka, sasa hilo linataka kuingizwa katika programu ya ujenzi wa mabwawa sidhani kama ni mahali pake hapa.

Kwa hiyo, naomba labda nimjibu tu kwamba katika miradi ambayo inaandaliwa sasa ni vyema mradi huu ukaingizwa na hasa hasa mimi naona nafasi nzuri kabisa katika miradi ya *ASDP* na *DIDF* ambayo ni endelevu yaani inaendelea tu kila wakati wakiibua hata kama mwaka unaendelea bado miradi hii inaweza ikaletwa, naomba alilete katika sehemu hiyo, hapa sidhani kama ni mahali pake. *(Makofi)*

**MHE. KILONTSI M. MPOROGOMYI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana katika mkoa wa Kigoma *sub vote 4001,* halafu 3216 na 3223, katika mkoa wa Kigoma kuna uhaba mkubwa sana wa maji na katika vijiji vya Nyakimwe, Mnanila na Mwayaya kulikuwa na mradi na *NORAD* ambao ulitandaza mabomba hayo ambayo hayakuwahi kutoa maji. Je, Mheshimiwa Waziri anaweza kunifafanulia kwamba sasa ni wakati muafaka ambao wanaweza wakafanya *expansion and rehabilitation* ya *rural water supply* katika sehemu hii ili ikaweza kutoa maji.

La pili katika wilaya ya Kasulu, wilaya ya Buigwe kijiji cha Nyamgali na Bulimanyi na kijiji cha Mganga wamepewa mradi wa benki ya dunia, jumla ya mradi mmoja ni shilingi milioni 400 na wanatakiwa wachangie 2.5% ya mradi kwa ajili ya *maintenance* ya mradi huo. Je, Waziri anaweza kuwaeleza watu wale kwa sababu hili jambo nilikuwa nimeshamweleza anaweza kuwaeleza sasa kufafanua hii 2.5% ni ya kitu gani na wao wanatakiwa kuipata namna gani maana kama kijiji kimoja wanatakiwa walipe shilingi milioni 11 na shilingi milioni 11 kwa kijiji ni hela nyingi sana. Mheshimiwa Waziri naomba unifafanulie. *(Makofi)*

**WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu vijiji alivyovitaja ambavyo vilikuwa na mpango wa mradi wa maji ambao unahitaji kufufuliwa au kuangaliwa upya namhakikishia kwamba Wizara itashirikiana na

Halmashauri ya Wilaya ya Kasulu kuliangalia hili suala na tuone jinsi gani tunaweza tukalifanikisha. *(Makofi)*

La pili kuhusu asilimia 2.5 kama mchango wa wananchi katika mradi wa vijiji kumi au niseme mradi wowote ule unaotekelezwa vijijini faida yake au maana yake ni kwamba kwanza unakuwa ni mradi wao kwa sababu wameshatenga fedha zao na wanaona kitu chao katika mradi ule. Kwa hiyo, inasaidia sana kufanya miradi hii iwe endelevu.

Lakini la pili ni kwamba kwa ufafanuzi ni kwamba ni mchanganyiko wa fedha taslimu lakini vilevile ni mchanganyiko wa nguvu kazi ambazo kijiji kinaweza kuchanga katika utekelezaji wa mradi kwa hiyo, si kwamba asilimia zote lazima zichangwe katika fedha taslimu. Lakini inasaidia kwa sababu zile fedha haziendi katika utekelezaji wa miradi, zinabaki katika shughuli za kufufua au kufufua mradi au kutengeneza mradi unapoharibika kwa hiyo, bado ni fedha zao zinabakia pale pale kijijini. Lakini ambapo hatuwezi kufikisha kifedha asilimia 2.5 basi nguvu kazi nayo inaweza ikahesabiwa kama ni mchango wa wananchi kufikia hiyo asilimia 2.5. *(Makofi)*

**MHE. CHARLES M. KAJEGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante *sub vote* hiyo hiyo ya 4001, kifungu kidogo cha 3280 *Rural Water Supply and Sanitation Project.* Katika jimbo la Mwibara tuna miradi chini ya programu hii katika vijijini vinne ambavyo ni Kibala, Buramba, Karukeke na Magunga, lakini utekelezaji wake umekuwa unasuasua na mojawapo ya sababu ambazo zimetajwa ni ukosefu wa pesa. Sasa nilikuwa nataka Mheshimiwa Waziri anihakikishie kwamba katika pesa ambazo zimetolewa hapa vilevile zitakuwa ni kwa ajili ya kutekeleza miradi hiyo ambayo nimeitaja.

**WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, iwapo vijiji hivyo alivyovitaja viko katika vile vijiji kumi vya wilaya ya Bunda basi fedha hizo zitatumika katika utekelezaji wake. Iwapo viko nje basi kwa kweli ni Halmashauri kutafuta fedha, vyanzo vingine au kwa wao wenyewe au kwa kushirikiana na Wizara, lakini nia yetu kwa kweli hatimaye ni kuwapatia wananchi maji safi na salama. *(Makofi)*

**MHE. NIMROD E. MKONO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante na mimi ni pale pale *sub vote 4001* sehemu ya kwanza na ya pili, *expansion and rehabilitation rural water*, katika eneo fulani la Busegwe, kuna shule ya wasichana ambayo waliombewa fedha kupitia *quick win*, tunakumbuka tuliongea na Mheshimiwa Waziri aliyekutangulia na wewe pia kuona kwamba baada ya uchimbaji ama *survey* ya hawa *agency* ya *drilling* walitambua sehemu fulani ya kuweka maji ili wa *supply* kwa shule ya wasichana ya Busegwa, nataka kujua kama hizi fedha zilizotengewa shlingi bilioni 12 ni kukamilisha ujenzi wa eneo hilo ama la, na kama ndiyo hivyo nataka kujua kama huu mradi umekufa ama bado upo?

**WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, namheshimu sana Mheshimiwa Mkono, mawazo yake siku zote tunayazingatia, narudia tena kusema nia yetu sisi ni kuwapatia wananchi maji. Kwa maana mahususi huo mradi alioutaja wa kupeleka katika shule ya sekondari na najua akisema hilo anamgusa mtoa

hoja ambaye vilevile ni mwalimu anajua tutashirikiana katika kufanikisha hili jambo, naomba tuendelee kuwasiliana. *(Makofi)*

**MHE. BASILI P. MRAMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nimesimama tu kuomba ufafanmuzi kuhusu kifungu hicho hicho, sehemu zile zinazoshughulikia *borehole drilling and dams* kwangu hizi *dams* nazihitaji, *rain water harvesting essentially* na suala la *kili water* na *lecturer* ambayo yote Mheshimiwa Waziri anayafahamu hasa hili la *lecturer* uhusiano wetu na Kenya.

Kwa kuwa hata pale kwenye ibara ya 70 ya Waziri chini ya Bonde la Pangani, Rombo haitajwi kabisa wala hakuna *indication effect*, Pangani inatajwa pale kama ni awamu ya tatu. Je, Waziri anaweza kunihakikishia kwamba yale yanayoendelea kwenye wilaya yangu hayatasimama kwa sababu hayakutajwa na haonyeshi vizuri ni wapi fedha hizi zitatoka?

Je, anaweza akanijibu kwa sababu mambo haya niliyasema kwa maandishi anaweza akanipa *favour* ya kunijibu kutokana na ile *contribution* yangu ya maandishi ili liwe na kitu cha kupepea ama cha kubeba wakati huu wa kiangazi ambao ndiyo sasa unaanza?

**WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa yale maeneo ambayo tumeyataja katika hotuba na yale ambayo tumemuahidi Mheshimiwa Basil Mramba kwamba tutayatekeleza yawe ya visima, yawe ya maji ya mtiririko tunajua matatizo ya Rombo ni makubwa lakini tunajua vilevile uwezekano mwingine ni wa matumizi ya maji ya Ziwa Chala ambalo hata wafanye nini wenzetu bado itabidi washirikiane na sisi, naomba sana lisimtishe lile la kwamba wametangaza zabuni ya utekelezaji wa maeneo ya maji kutoka Chala hasa watu wa *Castor Development Authority* ya Kenya lakini katika matangazo yale kipengele kimoja kipo kwamba utekelezaji wake lazima tutashirikiana na Tanzania na kama sisi vilevile tutakavyoshirikiana na Kenya kuhusu maji ya Ziwa Chala, ambalo jimbo la Mheshimiwa Mramba limo. Kuhusu barua ya kupeperusha wakati wa kiangazi Mheshimiwa Mramba, kaka yangu, kiongozi wangu, mkoa wa Mbeya Waziri mwenzangu nitaanguka, nitatia saini nitapeperusha.

**MHE. DR. SAMSON F. MPANDA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante *sub vote* hiyo, *item* 3216 nimeandika kwenye mchango wangu wa maandishi kuhusu ile *pump* ya Kipatimu ambayo imehamishwa kwa matengenezo lakini hadi leo haijarudishwa na *tank* lake linaota popo tu.

**WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, niseme kwamba sisi binadamu Mwenyezi Mungu ametupa mali na kushughulikia maisha yetu wenyewe ni kuangalia viumbe kwa hiyo kuwepo kwa popo vilevile ni usimamizi wa maeneo ambayo Mwenyezi Mungu ametupa tuwasimamie. La pili ni kwamba kwa kweli ni mradi mahususi sana wa Kilwa lakini sisi tumeuchukua yaani kama nilivyosema suala lolote linalohusu maji liwe la kata, kijiji maadamu limetaja maji *the backs stops here* ni la

Waziri wa Maji, basi tutalichukua, tutalifuatilia tutaona nini cha kufanya. Ahsante. *(Makofi)*

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

Kifungu 6001 *Drilling and Dam Construction Agency*…………sh. 0/=

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

*(Bunge lilirudia)*

**WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla sijatoa ripoti au taarifa naomba uniruhusu nifanye yafuatayo. Kwanza ni kusahihisha niliposema kwamba nilipita jimbo la Mheshimiwa Hamza Mwenegoha, maeneo yale ya Ngerengere, amenikumbusha kwamba hilo ni jimbo la Mheshimiwa Sameer Lotto. Lakini nimkumbushe kwamba Morogoro ni moja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili ni kwamba amenikumbusha Mheshimiwa Godfrey Zambi, kwamba sikuzungumza kuhusu Lukululu katika majumuisho yangu. Lakini huu ni mradi ambao ameusimamia kwa karibu sana, tutaendelea kuutekeleza katika mwaka huu wa fedha na mradi wa Mlowo. Nafikiri nimeutaja ambao nao ameusimamia kwa karibu sana, ametusaidia sana ambao vilevile nimesema tutauzindua mwezi Julai, 2010. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya hayo niseme vilevile kwamba kwa kweli kwa yote haya yaliyotendeka humu ndani namshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa amani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sasa kutoa taarifa kwamba Kamati ya Matumizi baada ya kujadili taarifa ya Makadirio na Matumizi ya Fedha ya Wizara yangu kwa mwaka 2010/2011 kwa kifungu kwa kifungu imeyapitisha bila mabadiliko, hivyo basi naomba sasa Bunge lako Tukufu liyakubali Makadirio haya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyosema Msaafu Mtakatifu unasema tumefanya kila kitu kuwa hai kutokana na maji kwa heshima kubwa naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Waziri hoja imetolewa na imeungwa mkono, sasa nachukua nafasi hii kuwahoji wale wote ambao wanakubaliana kwamba Bajeti ya Wizara ya Maji na Umwagiliaji imepita. *(Makofi)*

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*
*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

*(Makadirio ya Matumizi ya Wizara ya Maji na Umwagiliaji kwa mwaka wa fedha 2010/2011 yalipitishwa na Bunge)*

**MWENYEKITI:** Kwa bahati nzuri sana wote wameikubali, Bajeti imekubaliwa na watu wote bila kutokea hata mmoja ambaye anaikataa au kuipinga, nachukua nafasi hii kumpongeza sana Mheshimiwa Waziri, Mheshimiwa Naibu Waziri kwa wakati ambao walikuwa nao wakijaribu kujibu hoja pamoja na kwamba wakati ulikuwa hautoshi, lakini kwa kadri mlivyopata nafasi ya kuzungumza na kujibu hoja za Waheshimiwa Wabunge karibu wote wameridhika na ndiyo maana wote wamepitisha bila kupinga kwa hiyo nakupongeza sana kwa kuweza kuipitisha Bajeti.

Waheshimiwa Wabunge, kwa sababu muda umeshakwenda sana baada ya hayo machache napenda kuchukua nafasi hii kusema kwamba niliahirisha Bunge mpaka kesho saa tatu asubuhi. *(Makofi)*

*(Saa 2.04 usiku Bunge liliahirishwa mpaka siku ya Alhamisi, Tarehe 24 Juni, 2010 saa tatu asubuhi)*